

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TAZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao Cha Ishirini na Tatu – Tarehe 14 Julai, 2008

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:

Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii kuhusu utekekelezaji wa Wizara ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadrio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2008/2009.

MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Taarifa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

MASWALI NA MAJIBU

Hitaji la Kuundwa kwa Wilaya ya Kilwa

MHE. DR. FERDINAND S. MPANDA aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Kilwa ni kubwa sana na kwa kuwa, Jimbo la Kilwa Kaskazini limekuwa kama yatima kwa kukosa huduma muhimu kama Kituo cha Polisi, Hospitali, Benki, Makao Makuu ya Mbunge na kadhalika.

Je, ni lini tutapewa Wilaya ya Kilwa Kaskazini ili tupate huduma hizo kwa karibu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Ferdinand Samson Mpanda, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilwa yenyе idadi ya watu wapatao 181,341 kwa sasa ni miongoni mwa Wilaya zenyе maeneo makubwa hapa nchini. eneo lote la Wilaya ya Kilwa ni jumla ya kilometa za mraba 13,958, kati ya hizo kilometa za mraba 807 ndizo zinatumika kwa makazi ya watu na shughuli za kiuchumi kama vile kilimo. Eneo lililobaki kwa sehemu kubwa ni Hifadhi ya Taifa ya Seluu (kilometa za mraba 29) na Misitu ya Asili.

Aidha, Wilaya ya Kilwa kwa ujumla wake ina Tarafa 6, Kata 20 na Vijiji 96. Wilaya pia ina Majimbo mawili ya Uchaguzi kwa maana ya Jimbo la Kilwa Kusini lenye Tarafa tatu za Pwani, Nanjilinji na Pande; Jimbo la Kilwa Kaskazini analoliwakilisha Mheshimiwa Dr. Mpanda pia lina Tarafa tatu za Miteja, Njinjo na Kipatimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatudhani kwamba Jimbo la Kilwa Kaskazini limeachwa yatima kama Mheshimiwa Mbunge anavyoliweka. Wilaya ya Kilwa inayo Halmashauri ya Wilaya ambayo pamoja na mambo mengine inalo jukumu la kutoa huduma na kuratibu utekelezaji wa Shughuli mbalimbali za Kisekta na miradi ya Maendeleo.

Mantiki iliyopo hapa ni kwamba Wilaya za Kiutawala siyo ngazi za utoaji huduma. Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa inafanya kazi nzuri katika kutoa huduma bila kujali eneo au jimbo la uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kudhihirisha kwamba Jimbo la Kilwa Kaskazini halijaachwa yatima naomba kutoa takwimu chache. Kuhusu Huduma za Afya kuna Hospitali moja ya Shirika la Dini, kuna Vituo vya Afya viwili, Zahanati kumi na tisa

ikilinganishwa na Zahanati 18 zilizopo Jimbo la Kilwa Kusini. Kituo cha Polisi kinajengwa pale Somanga (Hakijakamilika).

Shule za Msingi zilizopo ni 54 zenye wanafunzi 21,090 ikilinganishwa na shule 56 zenye wanafunzi 19,414 za Jimbo la Kilwa Kusini. Shule za Sekondari ni 13 zenye wanafunzi 2,290 ikilinganishwa na shule 11 zenye wanafunzi 1,906 zilizopo Jimbo la Kilwa Kusini. Mtandao wa barabara Kilwa Kaskazini ni kilomita 200 barabara za Mkoa ni km 190 barabara za Wilaya ni km. 210, barabara za Vijijini ikilinganishwa na mtandao wa Kilwa Kusini yeny km. 86, barabara za Mkoa km.200, Barabara za Wilaya km. 109 barabara za Vijijini. Fedha za uwezeshaji wananchi (*JK. Fund*) kwa mwaka 2007/2008 jumla ya shilingi milioni 42 zilitolewa kwa SACCOS nne ambazo ni CHUMO, UWAKOTI, ALANJE na MWANZO MGUMU (NJINJO) zilizopo Jimbo la Kilwa Kaskazini. Jimbo la Kilwa Kusini lilipata shilingi milioni 32 tu kwa SACCOS tatu. Miradi ya Maji imesambazwa katika vijiji vya Kipatimu, Kandawale, Mingumbi, Namayuni na Njia Nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwa na Wilaya ya Kilwa Kaskazini, Serikali kwa sasa haina mpango wa kugawa Wilaya hapa nchini kama ambavyo tumeshaeleza hapa Bungeni wakati wa wa kujibu hoja za Wabunge tulipojadili hotuba ya Bajeti ya 2008/2009 ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kazi kubwa iliyopo ni kukamilisha miundombinu katika Wilaya mpya ambazo zimeshaanzishwa. Hivyo, wakati utakapofika kwa Serikali kugawa Wilaya mpya Wilaya ya Kilwa itafikiriwa kama itakidhi vigezo vilivyowekwa.

MHE. DR. FERDINAND S. MPANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kuuliza kama Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba Vita Kuu ya Majimaji ilianza Kilwa Kaskazini pale Nandete Kipatimu na kwamba ingekuwa busara kwa Serikali kuiwekea Wilaya Kibata Kipatimu.

Swali la pili, ni kwamba hizo huduma zingine zinazosemwa kama zitapatikana ni lini zitapatikana kwa hivi karibuni?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dr. Mpanda, Mbunge wa Kilwa Kaskazini kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kwamba Vita vya Majimaji vilipiganwa mwaka 1905 – 1907 na ninajua kwamba vilikuwa katika eneo la Kilwa katika eneo la Kipatimu ambapo anapazungumzia na hili jambo ni jambo kubwa sana katika historia ya nchi yetu lakini bado hilo tu haliwezi kuwa ndiyo sababu itakayowezesha kuanzisha Wilaya nyingine ya Kilwa kama nilivyoleza kwa sababu vigezo tulivieleza katika majibu yetu tuliyotoa huko nyuma.

La pili kuhusu huduma ni kwamba ni lini zitapatikana, hiki Kituo cha Polisi ambacho nimekizungumzia hapa kipo katika hali ya kwamba sasa kinaendelea

kutayarishwa katika maana ya kwamba kitaanza kutumika. Pia huduma nyingine ambazo zinatolewa katika wilaya ile nimeeleza hapa na tunaendelea kuziimarisha kufuatana na hali halisi itakavyokuwa kibajeti.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba Serikali haina mpango wa kugawa Wilaya. Je, kwa Tarafa ambazo ni kubwa kwa mfano Tarafa ya Mpwapwa ina watu zaidi ya 150,000. Je, kuhusu Tarafa Serikali ina maelezo gani?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo;

Nifafanue tu hapa kwamba si kwamba zoezi la kuanzisha Wilaya mpya limesimamishwa kabisa, tulichofanya hapa ni kuahirisha mpango mzima kwa ajili ya kuhakikisha kwamba zile Wilaya ambazo zimeanzishwa zinapatiwa miundombinu inayofaa na kuhakikisha kwamba zinakwenda kama utaratibu unavyotutaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la Tarafa lipo katika mchakato sasa hivi hapa tunazungumzia habari ya Tarafa, Kata na Vijiji kwa ujumla wake kwa hiyo kama kuna Tarafa ambazo wanafikiria kwamba zinahitaji kufanyiwa hivyo ni lazima kwanza zije katika Makao Makuu ili tuweze kuona kwamba tunafanya hivyo ikiwemo Wilaya ya Mpwapwa ambayo ameizungumzia Mheshimiwa Mbunge.

MHE. FAUSTINE K. RWILOMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, katika jibu lake la msingi anasema Serikali haina mpango wa kugawa Wilaya, lakini kuna Wilaya nyingine zenye matatizo kama Kilwa hasa Wilaya ya Geita ambayo ina watu sasa hivi wapatao milioni moja na kwa sababu ya miundombinu kuna tatizo kubwa sana linalojitokeza. Kwa mfano, leo kituo cha Katoro kimevamiwa na Askari wamelala kwa sababu ni wachache pale.

Je, kuna mpango gani wa kugawa Wilaya hiyo kuipa kipaumbele wakati zingine zinasubiriwa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Faustine K. Rwilomba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesema kwamba siyo kwamba Serikali haina mpango kabisa wa kugawa maeneo mapya, tunachosema kwa Bajeti ya mwaka huu kama tulivyoipitisha hapa Bungeni tumeanza kwanza kumaliza Wilaya zote na sehemu zote za kiutawala ambazo ziligawanywa katika awamu ya tatu. Sasa hivi awamu ya nne tuko katika mchakato wa kuangalia maeneo haya na Wilaya ya Geita ikiwa mojawapo.

Mwaka huu tumesema kwamba mpaka mwezi Desemba mgawanyo wa Vijiji na Kata utakuwa tayari kwa ajili ya Uchaguzi wa mwaka ujao.

Kwa hiyo, maeneo mengine ya kiutawala tutayagawa baada ya kumaliza hayo maeneo ambayo tumekwisha yatengea fedha nyingi tu kwa mwaka huu na tuna uhakika kwamba yatakuwa yamemalizika. (*Makofii*)

Na. 203

Ubora wa Mabasi ya Abiria

MHE. SAID AMOUR ARFI aliuliza:-

Katika kupunguza vifo vinavyosababishwa na ajali za barabarani, Je, ni nani anayesimamia na kuthibitisha ubora wa mabodi ya mabasi yanayosafirisha abiria?

NAIBU WA FEDHA NA UCHUMI – MHE. OMAR YUSSUF MZEE alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Viwango Tanzania (*Tanzania Bureau of Standards (TBS)*) ndilo lenye jukumu la kuthibitisha ubora wa bidhaa mbalimbali nchini zikiwemo bodi za magari yanayosafirisha abiria. Shirika la Viwango Tanzania limeweka kiwango cha kitaifa cha bodi za mabasi TSZ 598: 1999 *Automotive Engineering- Bus Body Building -Code of Practise* mtengenezaji au muagizaji wa bodi za mabasi anatakiwa kuzingatia kiwango hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango hicho kinaainisha matakwa muhimu ya kuzingatiwa kama ifuatavyo:-

- (i) Muundo wa basi kwa kuzingatia usalama wa basi lenyewe, ulindaji wa mazingira na afya ya watumishi (abiria);
- (ii) Aina za maligafi (*materials*) za kutengeneza sakafu, kuta, paa, ufungaji na vipimo vinavyotakiwa;
- (iii) Kuwepo kwa madirisha, milango ya kuingilia na milango ya dharura kulingana na vipimo vya ukubwa, aina za viooo vinavyotumika na ufungaji wake;
- (iv) Ukubwa wa viti, ufungaji wake na nafasi za kupita na kuwekea miguu;

- (v) Mikanda ya Usalama;
- (vi) Idadi ya abiria wanaouruhusiwa kukaa na kusimama; na
- (vii) Vifaa vya zimamoto na huduma ya kwanza.

Katika kusimamia utekelezaji wa masharti ya ubora, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, Shirika la Viwango Tanzania hushirikiana na taasisi nyingine zilizopewa mamlaka ya usimamizi wa usalama barabarani kama mamlaka ya Uthibiti wa huduma za Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) na Jeshi la Polisi, Kitengo cha Usalama Barabarani (*Traffic Police*).

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

Kuwepo na viwango kama Mheshimiwa Waziri alivyoeleza katika majibu yake ni suala moja na kusimamia ni suala lingine. Je, Waziri anaweza kunieleza kwa nini mabasi yanapofanya ajali yanakatika vipande viwili, yaani kipande cha juu kinakwenda peke yake na inabakia chesesi na viti na idadi kubwa ya watu wanakuwa?

La pili, je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba vyuma vinavyotumika kwa ajili ya kujenga mabodi ya basi ni vyuma hafifu ili mabodi yaye mapesi ili wenye mabasi wasitozwe gharama kwenye mizani, matokeo yake maisha ya watu wetu tunayaweka hatarini ni vema sasa wakaangalia vyuma vinavyotumika katika kujenga mabodi ya basi yaye imara au mabasi yasamehewe kwenye mizani?

NAIBU WA FEDHA NA UCHUMI – MHE. OMAR YUSSUF MZEE: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Said Amour Arfi, kama ifuatavyo:-

Kwanza nakubaliana naye kwamba hilo tatizo lipo lakini la msingi limetokana zaidi na Sheria ambayo iliyoweka *TBS*, Sheria hii haina meno. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira ili tutakapoleta marekebisho ya Sheria hiyo ataona meno ambayo tutaipa Sheria hiyo na mabasi ambayo yatatokea kwamba viwango vile havijakamilika yataweza kuondoshwa katika safari zinazohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni suala la vyuma kweli nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba vyuma vinavyotengeneza mabasi hayo ni vyepesi, sasa tulichokifanya ni kwamba tumejaribu kutoa mafunzo kwa Askari wa Barabarani kwa kushirikiana na *SUMATRA* pamoja na *TBS* kuangalia hali nzima ya *standard* ya vyuma hivyo ili mabodi yatakayotengeneza yazingatie *standard* ya vyuma vilivyowekwa.

MHE. ELIATA N. SWITI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa mabasi yanayosemekana kuwa na chesesi za lori husababisha adha kubwa kwa wasafiri hasa pale anapofika katika mizani na kupimwa kuonekana kuwa na uzito zaidi. Je, Serikali inatamka nini kuhusu mabasi hayo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Eliata N. Switi kama ifuatavyo:-

Mwezi *August, 2007* umefanyika upembuzi Serikali imegundua kwamba kuna mabasi karibu 198 yana chesesi ya lori. Serikali inatamka kwamba kuanzia mwezi huu itakaa iandae mpango ili kuweza kuona kwamba mabasi haya haya naanza kuondoshwa katika barabara kwa awamu kwa sababu yana matatizo mojawapo ni hili ambalo Mheshimiwa amelizungumza. Naomba Mheshimiwa avute subira kikao kitakaa mwezi huu ili kuweza kuandaa utaratibu wa kuya *phase out* mabasi hayo.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudzi za kupunguza vifo vinavyosababishwa na ajali za barabarani Serikali iliagiza kuwa mabasi yote ya abiria yawe na milango ya nyuma ili iwe rahisi kwa abiria kutoka wakati wa ajali.

Je, suala hili limefikia wapi?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, kama ifuatavyo:-

Serikali ilitoa tamko kwamba mabasi yote ya abiria yawe na milango ya dharura, hatua hiyo ni nzuri sasa hivi mabasi yote yana milango ya dharura na kama lipo basi ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliona kwamba halina mlango wa dharura naomba atufahamishe ili tuweze kuyafanyia kazi.

NAIBU SPIKA: Anasema yapo mengi tu!, Wizara ya Miundombinu, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama.

Na. 204

Kujenga Barabara ya Wino – Ifinga

MHE. JENISTA J. MHAGAMA aliuliza:-

Kwa kuwa, muda mrefu sasa Wizara imekuwa ikisaidiana na Halmashauri ya Wilaya ya Songea kujenga barabara ya Wino – Ifinga, na kwa kuwa, eneo lililobaki sasa ni wastani wa kilometra 12 tu.

Je, Serikali iko tayari sasa kutoa fedha za kumalizia eneo hilo ili kuwaokoa wananchi wa Ifinga ambao bado wanatembea kwa miguu na hawajui kuona Kiongozi wa Kitaifa wala Mwenge wa Uhuru kutokana na ubovu wa barabara hiyo?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba barabara hii iliyotajwa imekuwa ikifanyiwa matengenezo kwa pamoja kati ya Wakala wa Barabara (TANROADS) Ruvuma na Halmashauri ya Wilaya ya Songea. Vilevile ni kweli kwamba hadi sasa zimebaki jumla ya kilometa 12 ambazo hazijatengenezwa ili kukamilisha jumla ya kilomita 46 kutoka Wino hadi Ifinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Halmashauri ya Wilaya ya Songea ilitangaza Zabuni na kumpata Mkandarasi kwa matengenezo ya jumla ya kilometa 5 kati ya hizo kilomita 12. Vilevile Wizara ya Miundombinu katika Bajeti yake ya mwaka 2008/2009 imepanga kufanya matengenezo kilometa 7 zilizosalia na hivyo kukamilisha kilometa 12 zilizokuwa bado kutengenezwa.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba sasa Wizara imegundua tatizo la barabara hiyo na imeamua kutenga fedha za kumaliza matengenezo. Na kwa kuwa, mwaka jana tulipitisha Sheria mpya ya barabara ambapo Halmashauri yetu iliomba barabara hiyo sasa ipande daraja kutoka Daraja la Halmashauri kwenda Daraja la Mkoa.

Je, Mheshimiwa Waziri katika marekebisho ya Sheria hiyo sasa yuko tayari kuipandisha hadhi barabara hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa historia katika makazi ya wale wananchi kule katika Kata ya Ifinga kutokuona Kiongozi yeoyote wa Kitaifa wala Mwenye isipokuwa tu Mbunge wao wakiwemo viongozi wa Mkoa, Ma-RC na wewe mwenyewe peke yake ulishawahi kufika huko na Viongozi wa Halmashauri. Je, barabara hii itakapokamilika anakubali sasa kuwa mgeni rasmi wa kwanza wa kutembelea eneo hilo ili wananchi waanze kupata moyo kwamba maendeleo yamefika katika eneo lao?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri anataka ukakwamie hukohuko. Majibu tafadhali!

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu maswali mawili madogo ya Mheshimiwa Jenista J. Mhagama Mbunge wa Peramiho kama ifuatavyo:-

Kuhusu kupandishwa hadhi kwa Barabara ya Wino – Ifinga, mwaka jana Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria namba 13 ya barabara ambayo sasa Serikali iko katika mchakato wa kuandaa Kanuni ambazo zitaweka bayana na kwa njia nadhifu taratibu

ambazo zitafuatwa ili kupandisha daraja barabara kadhaa ambazo Waheshimiwa katika Majimbo mbalimbali wameziombea zipandishwe daraja.

Ni muda sasa tangu Serikali imeanza kuzishughulikia lakini nilihakikishie tu Bunge hili kwamba tutaweka juhudu kubwa kuhakikisha kwamba hizi Kanuni zinakuwa kamili na mara tu zitakapokuwa kamili mchakato utakamilishwa kupandishwa barabara zote zile ambazo zimeombwa kufanyiwa hivyo.

Kuhusu swali la pili la kuwa mgeni rasmi wakati wa ufunguzi wa barabara ya Wino – Ifinga niko tayari na nitapata faraja sana kufanya hivyo.

NAIBU SPIKA: Lakini Mawazi wanapossema wanafika hatupewi taarifa kama wamefika kweli. Tunaendelea na swali linalofuata ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura.

Na. 205

Fidia kwa Mahujaji wa Tanzania Mwaka 2007

MHE. MTUTURA A. MTUTURA aliuliza:-

Kwa kuwa Shirika la Ndege la Taifa (ATC) ndilo lililowachelewsa Mahujaji wa mwaka 2007 kufika Madina kuanza ibada ya Hijja kwa muda wa siku nne, na kwa kuwa, ATC ilikubali kulipa fidia ya dola za Kimarekani 200 kwa kila Hujaji kuititia Taasisi zao ili waweze kukamilisha ibada ya Hijja; na kwa kuwa baadhi ya taasisi kama vile **TAIBHA** iliwalipa Mahujaji wake malazi ya siku mbili tu badala ya siku nane:-

(a)Je, kwa vile fidia ile ililengwa kwa Mahujaji Serikali inatoa tamko gani kulinda maslahi ya waliolengwa ?

(b)Je, kama ikidhihirika kuwa, kuna taasisi zilizowadhulumu Mahujaji, Serikali itakuwa tayari kupokea pendekezo la kuzifuta kabisa taasisi hizo zisishiriki kusafirisha Mahujaji?

(c)Je, Serikali iko tayari kuwasaidia Mahujaji waliodhulumiwa kupata marejesho ya fidia hizo kutoka kwa taasisi zilizodhulumu?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU alijibu:

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mbunge wa Tunduru, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Kampuni ya Ndege Tanzania (*ATCL*), ilihusika katika kuchelewa kwa Mahujaji wa mwaka 2007 kufika Madina ili kuanza Ibada ya Hijja kama inavyotakiwa.

Ni kweli pia kwamba *ATCL* ililipa kwa wastani Dola za Marekeni zipatazo 200 kwa kila Hujaji kama Fidia kutokana na gharama zitokanazo na vyumba vya kulala ambavyo taasisi mbalimbali zilizokuwa zinaratibus safari za Hijja ziliwuwa zimeshalipia fedha hizo kutorudishwa kutokana na masharti ya Mikataba yao na wenye nyumba au mahoteli ambayo Mahujaji walikuwa wafikie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kueleza kwamba fedha za fidia ambazo kampuni ya Ndege ya Tanzania ililipa hazikulengwa moja kwa moja kwa mahujaji bali zililipwa kwa Taasisi ambazo ziliratibus safari za Mahujaji kwani ndizo *ATCL* ilikuwa imeingia mkataba nazo.

Lengo la malipo hayo lilikuwa ni kuhakikisha kwamba Mahujaji hawapati usumbufo kutoka kwa wenye nyumba au hoteli ambazo walikuwa wamefikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna baadhi ya Taasisi ambazo ziliwadhulumu Mahujaji kama Mheshimiwa Mbunge anavyodai, Serikali inashauri mkondo wa Sheria ufuatwe kulingana na makubaliano ama mikataba ambayo ilisainiwa kati ya Mahujaji na Taasisi husika ili haki iweze kutendeka.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa taasisi hizo hazikuanzishwa mahusuni kwa ajili ya kuratibus safari za Mahujaji, ni vigumu Serikali kufuta taasisi hizo moja kwa moja kwa vile tu zilishindwa kukidhi matarajio ya Mahujaji kwani kwa kufanya hivyo itakuwa ni kinyume na Sheria na Taratibus za uanzishwaji wa Taasisi hizo. Kufutwa au kutofutwa kwa taasisi hizo hapana budi kuendana na Sheria zilizozianzisha.

Hata hivyo, tunashauri Mahujaji waepuke kuingia mikataba ya Hijja na Taasisi ambazo kwa ujumla wake zinaonekana kutokuwa na uwezo wa utalaalamu wa masuala ya Hijja.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa taasisi hizi za *Hijja* ziliingia mkataba na ATC kwa niaba ya Mahujaji na ATC iliingia mkataba na taasisi zile kwa niaba ya Serikali na kwa kuwa lengo la malipo yale yaliyotolewa na Serikali kupitia ATC ilikuwa ni kuondoa usumbufu kwa Mahujaji, lengo ambalo halikuweza kutimia.

Je, Serikali haioni kwamba fedha za umma ambazo zimetumiwa na taasisi zile ambazo hazikuwafikia walengwa, zimetumika kinyume cha utaratibu na ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Serikali bila kuingilia kati mzozo huu kati ya Mahujaji na zile taasisi haioni kwamba inawatelekeza Waislam amba walikwenda *Hijja* mwaka ule? Nashukuru sana.

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la swali la msingi, Serikali haina taarifa mpaka sasa ya wale amba wamedhulumiwa na hizi taasisi lakini ni muhimu sana kwa sababu Mahujaji walikuwa na mikataba na makubaliano maalum na taasisi hizi, basi pale ambapo makubaliano yale yamekiukwa Mahujaji wachukue hatua za kisheria na itakapokuwa kuna tatizo lolote au mgogoro wowote ndani ya hilo basi Serikali ipo tayari kushirikiana na Mahujaji hawa amba wamekosa haki yao hata kupitia taratibu za kisheria.

Serikali inajali sana na itaendelea kulifuatilia jambo hili kwa ukamilifu ili kusije kutokea tena matatizo kama hayo ndani ya mwaka huu wa *Hijja*.

MHE. DR. WILBORD P. SLAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Shirika la Ndege la Tanzania ni chombo cha biashara na kwa kuwa fedha zilizotumika kulipa fidia ni pamoja na dola za Marekani milioni moja zilizotoka Tume ya Taifa ya Mawasiliano kwa maagizo ya Serikali na kwa kuwa *Hijja* ni shughuli za kidini na haina uhusiano na Tume ya Mawasiliano.

Je, Serikali inatoa kauli gani kutumia fedha za umma kwa jambo ambalo si la umma wote wa Tanzania?

NAIBU SPIKA: Ilikuwa ni kwa sababu ya usumbufu si sababu ya dini.

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la ATCL lililipa jumla ya dola za Marekani laki mbili na elfu sitini na mia nne na hamsini kwa ajili ya usumbufu amba Mahujaji walikuwa wameupata. ATCL ni shirika linalomilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia mia moja. Kwa maana hiyo fedha zozote ambazo zinatumika na shirika hilo ni fedha za mwenye mali ambaye ni Serikali. (*Makofii*)

Mawasiliano ya Simu za Mkononi

MHE. MASOLWA C. MASOLWA aliuliza:-

Kwa kuwa mawasiliano ya simu za mkononi yanazidi kuongezeka kila siku lakini hakuna utaratibu mzuri wa uuzaji hasa wa kadi za simu (*sim cards*) hizo na hivyo kusababisha baadhi ya watu kutumia vibaya mawasiliano hayo kama vile kuwasiliana kwa mipango ya kuhujumu, wizi, kutukana viongozi na kadhalika:-

Je, Serikali kupitia *TCRA* ina mikakati gani ya baadaye ya kuweka utaratibu mzuri zaidi wa uuzaji wa simu za mkononi, kadi na *line* zake kwa wafanyabiashara ili kuweza kuwatambua wenye majina na namba za simu wanaotumia vibaya mawasiliano na kuwakamata?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa pamoja na manufaa makubwa ya huduma za simu katika kuharakisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi, simu hizo zinapotumika isivyo sahihi huweza kusababisha athari kubwa na hivyo kuhatarisha utulivu. Serikali imeliona hilo na hatua zimeanza kuchukuliwa za kuboresha mfumo wa matumizi ya simu hizi hususan kurejea utaratibu wa sasa wa kuuza na kusambaza holela laini za simu (*sim cards*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) iliunda Kamati ya Kitaifa iliyojumuisha Makampuni yote ya Simu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Ofisi ya Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Ofisi ya Uhamiaji, Ofisi ya Mamlaka ya Mapato na Idara mbalimbali ndani ya Mamlaka ya Mawasiliano kuweza kuangalia kwa undani njia muafaka zitakazowenza kupata na kutunza kumbukumbu za majina na anuani za watumiaji wote wa simu za mkononi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hiyo inahusisha ufungaji wa mitambo husika ya kutunza kumbukumbu za wateja wa simu za mkononi. Pia kutahitajika mabadiliko ya sheria mbalimbali ili kuhakikisha ukiukwaji wa taratibu zitakazowekwa utadhibitiwa kwa mujibu wa sheria. Kazi hii ilianza mwaka jana 2007 na inatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka huu 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mapendekezo ya Kamati hiyo ni pamoja na kuunda mfumo wa kusajili simu zote za mkononi nchini na watumiaji wake kwa kutumia

njia mbalimbali zinazotumika duniani na wenzetu, kufanya uchunguzi wa kina kuhusu wizi wa simu za mkononi pamoja na kununua mtambo utakaosajili simu zote nchini ili kudhibiti wizi huo, kubuni sheria mbalimbali za kudhibiti watumiaji wa simu kwa kulazimika kuzisajili simu na laini zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kudhibiti usajili wa laini na simu, Kamati ilipendekezo kununuliwa kwa mtambo wa kusajili na kubaini laini za simu na matumizi yake kwa lugha ya kitaalam “*Central Equipment Identity Register*” (*CEIR*) ambao utamiliikiwa na mwendeshaji binafsi ili kutokuwa na maslahi binafsi baina yake na kampuni ya simu. Serikali hivi sasa inayaangalia mapendekezo haya ili yafanyiwe kazi mara moja ili kudhibiti tabia hii iliyojitekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itahakikisha utekelezaji wa suala hili unafanyika mapema iwezekanavyo baada ya mapendekezo ya kuongeza vipengele vyta sheria kuwekwa katika sheria za kudhibiti mawasiliano nchini.

MHE. MASOLWA C. MASOLWA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Serikali itadhibiti vipi kwa Makampuni ambayo yanafanya *roaming* ili kuepuka matumizi mabaya ya simu hizi kwa mfano *CELTEL*?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya *roaming* ni huduma ya kawaida ambayo inatakiwa kuwepo katika shughuli za mawasiliano ya simu na huduma hii inasaidia sana wasafiri kama sisi na wenzetu wanapotoka hapa wanapata nafasi ya kupata mawasiliano popote walipo.

Huduma ya *roaming* kawaida huwa hupati bila kuwa na *registration* ya kutosha na kulipia hapa hapa ulipo kabla hujakwenda huko unakokuwa lakini kama kutakuwa na vitendo vyta ukiukwaji tutaomba Kamati iliangularie suala hili.

MHE. ZUBEIR ALI MAULID: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwenye swali la msingi mwulizaji aliuliza kuhusiana na utambuzi wa namba, kuna baadhi ya nchi huwezi kununua *sim card* mpaka utoe kitambulisho chako ili uweze kujulikana na uweze kuondoa kabisa tatizo ambalo linatokea la usumbufu na ujambazi pamoja na hili la viongozi kutukanwa kwenye simu.

Sasa je, utaratibu huu kwa vile tayari Serikali imeshapanga na nadhani Sheria ipo, lini utaanza kutumika rasmi ili kuondoa matatizo yanayojitekeza ya watumiaji wanaotumia kwa lengo baya?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye kwamba sehemu nyingine ukitaka kununua *sim card* ni lazima uwe na kitambulisho na hicho ndiyo kinachofanywa sasa hivi na hiyo Kamati, ni lazima upeleke picha zako na *identity card* aidha inaweza kuwa *passport*, *utility bill* au kitu chochote ambacho kitakufanya ujulikane.

Laiti tungekuwa na vitambulisho vya uraia ambavyo viro tayari kazi hii ingekuwa ni nyepesi zaidi lakini hilo nalo namhakikishia Mheshimiwa Maulid kwamba linashughulikiwa na sheria hizi tatu tulizonazo ni lazima ziunganishwe pamoja ili sheria iwe na nguvu ya kumdhibiti yule ambaye anatenda uhalifu huu.

Na. 207

Mawasiliano ya Simu Mikononi

MHE. FATMA A. MIKIDADI (K.n.y. MHE. HASNAIN G. DEWJI) aliuliza:-

Kwa kuwa Vijiji vya Nanjilinji, Likawage, Makangaga, Waihokwi hawana mawasiliano ya simu za mkononi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuvipatia vijiji hivyo mawasiliano hayo?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikiyahimiza Makampuni ya Simu kupeleka huduma za mawasiliano katika maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na maeneo ya Kilwa Kusini na Makampuni hayo yamekuwa yakifanya hivyo kulingana na mwelekeo wao kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya ZANTEL kwa sasa imefikisha mawasiliano katika maeneo ya Nangurukuru na Kilwa Masoko. Aidha, Kampuni hiyo imeyaweka katika mipango yake ijayo maeneo ya Liwale na maeneo jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya CELTEL inaendelea kufanya utafiti wa masoko katika Vijiji vya Nanjilinji, Likawage, Makangaga na Waihokwi huko Kilwa Kusini ili kuweza kufikisha mawasiliano katika maeneo hayo ifikapo Julai, 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *VODACOM* imebaini maeneo husika ya Nanjilinji, Likawage, Makangaga na Waihokwi pamoja na maeneo mengine yaliyo jirani yenye shughuli za kibiashara. Mwezi Januari, 2008 tathmini ya kiufundi imefanyika kwa ajili ya kuweka mitambo ili kukidhi mahitaji ya mawasiliano kwa wakazi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *TIGO* inakusudia kuyaweka maeneo hayo katika mipango yake mwaka 2009 ili yaweze kufanyiwa utafiti kwa ajili ya kuweka minara ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika juhud zote hizi ni kuhakikisha kwamba Kilwa inapata mawasiliano ipasavyo. (*Makofi*)

MHE. FATMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuku. Je, utakubaliana nami kwamba katika Mkoa huo huo wa Lindi *CELTEL* waliweka mnara tangu mwaka 2007 lakini mpaka leo haujafunguliwa hapo hapo karibu na Kilwa, je Mheshimiwa Waziri atatusaidiaje?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nitafuatilia ni kwa nini mnara huo upo mpaka leo na haujafanya kazi lakini ninavyojua minara mingine huwa ni ya kupokelea mawimbi lakini kuna na mradi mmoja amba ni Sweden hasa kule Kusini kunahitajika minara kama mitano au sita kwa pamoja imalizike na *transmission* kama nilivyojibu katika jibu lililopita ili mawasiliano yale yaweze kufikishwa katika maeneo husika. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, suala hilo nitalifuatilia kwa karibu zaidi.

MHE. MANJU S. O. MSAMBYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa matatizo au hoja ya Kilwa Kusini haina tofauti na hoja ya Kigoma Kusini na kwa kuwa Vijiji anavyovitaja Mheshimiwa Dewji vinahitaji huduma ya mawasiliano kama Vijiji vya Sunuka, Sigunga, Kalya na Igalula na ambako suala la kibiashara si tatizo lakini vilevile lipo tatizo la hujuma wanayofanyiwa wavuvi wa maeneo hayo.

Je, Mheshimiwa Waziri anatuambia nini kuhusu kutusaidia huduma ya mawasiliano katika maeneo haya hasa ikitiliwa maanani kwamba tayari kwenye makampuni yao ya simu maombi yalikwishawasilishwa?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika Mheshimiwa Msambya atakubaliana nami kwamba huduma za mawasiliano ya simu zimeboreka sana hivi sasa katika Jimbo lake na ni kwa sababu tulichukua juhud za makusudi kabisa kwa ajili ya kumfikishia mawasiliano hayo katika maeneo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba vijiji alivyovitaja Sumuka, Kaje, Igalula nina hakika Makampuni haya ya Simu kutokana na mipango yao ya kibiashara muda muafaka ukifika mawasiliano yatafika hasa kwa sababu tayari tulishapeleka

maombi ya Mheshimiwa Mbunge kwa wanaohusika. Naomba avute subira na nina hakika wananchi wake wanamsikia kwamba anawahudumia vizuri na anataka mawasiliano ili wavuvi wasiweze kuhujumiwa na sisi tuko pamoja naye katika suala hili. (*Makofî*)

Na. 208

Uhitaji wa Kituo Kipyä cha Polisi – Wilayani Mbozi

MHE. GODFREY W. ZAMBI aliuliza:-

Kwa kuwa Kituo cha Polisi Vwawa Wilayani Mbozi kilijengwa mwanzoni mwa miaka ya 1960 na sasa majengo ya Ofisi na nyumba za askari na kituo hicho ni chakavu sana:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga jengo lingine la ofisi lenye hadhi sawa na uchumi wa Wilaya hiyo ikiwa ni pamoja na kukarabati nyumba za askari?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwenye Bajeti ya mwaka 2008/2009 kwa ajili ya ujenzi huo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, azma ya Serikali ni kuhakikisha kwamba vituo vyote vya Polisi hapa nchini vinakuwa na hadhi na huduma muhimu ya miundombinu ya umeme, maji, usafiri na vitendea kazi vingine ili kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma nzuri na askari wanafanya kazi katika mazingira mazuri. (*Makofî*)

Aidha, ni lengo la Serikali pia kuona kwamba, makazi ya Askari Polisi yanaboreshwu ikiwemo kuongeza makazi hayo pamoja na kukarabati nyumba chakavu zilizopo. Pamoja na azma hiyo nzuri ya Serikali, imekuwa ni vigumu kufikia malengo hayo kutokana na mahitaji mengi ya Jeshi la Polisi kulinganisha na uwezo wa Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na sababu nilizozieleza hapo juu katika Bajeti yetu ya Wizara kwa mwaka 2008/2009, Jeshi la Polisi halikutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi Vwawa na ukarabati wa nyumba za askari.

Hata hivyo, Serikali itaendelea kutenga fedha katika Bajeti yake ya Maendeleo ya miaka ijayo kadri hali ya fedha itakavyoruhusu pamoja na kutumia rasilimali watu na rasilimali chache tulizonazo kuitia mpango wa kushirikisha Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza kukarabati na kujenga nyumba za askari wetu hatua kwa hatua.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majibu yasiyordhisha sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa fedha 2006/2007 niliuliza swali juu ya kituo hicho hicho na majibu yalikuwa kwamba kituo hicho kipo kwenye program ya miaka mitano ya kukarabatiwa au kujengwa lakini mwaka 2007/2008 ambao umekwisha hakukuwa na kitu chochote, mwaka 2008/2009, Waziri anasema hakuna chochote kwa ajili ya kituo hicho.

Je, anataka kusema kauli ya Serikali iliyotolewa mwaka 2006/2007 ilikuwa ya uongo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa nyumba wanazoishi askari katika kituo cha Vwawa Wilayani Mbozi ambayo ndiyo Makao Makuu ya Wilaya kwa kweli ni chakavu sana na hazifai kwa watu wazima kuishi.

Je, Waziri atakuwa tayari kukitembelea kituo hicho ili aone haya tunayoyazungumza na kwa maana hiyo aone umuhimu wa kuzikarabati nyumba za askari hao?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, hakika kauli ya Serikali haijabadilika. Kama alivyozungumza yeze mwenyewe Mheshimiwa Mbunge ni kwamba hii ni program ya miaka mitano nami katika jibu langu la msingi nimesema kwamba tunafanya ukarabati na tunajenga na hii itakwenda hatua kwa hatua. Napenda tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tatizo hili si kituo chake au mahali anapotoka yeze, ni tatizo la Taifa zima na tunao mpango huo lakini tutafanya kufuatana na fedha tulizokuwa nazo au kulingana na Bajeti tuliyokuwa nayo. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba kauli ya Serikali bado ipo palepale lakini tutakwenda hatua kwa hatua, awamu kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kituo niko tayari na namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutazungumza na nitakwenda kukitembelea kituo hicho. Nimekuwa natambelea vituo kadhaa na najua hali ya vituo vingi na tunasikitika na hali hiyo na tutafanya jitihada za kuhakikisha kwamba nyumba hizi zitajengwa lakini itakuwa awamu kwa awamu au hatua kwa hatua kulingana na jinsi tutakavyokuwa tunapata fedha. Ahsante sana.

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Dibaji askari wanafanya kazi nyeti....

NAIBU SPIKA: Hakuna dibaji uliza swali tafadhali (*Kicheko*)

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Kwa sababu ya unyeti wa kazi ya askari makazi yao kwa maana wanakoishi hakulingani na kazi nzito wanayofanya hususan askari wa Tabora Mjini. Nyumba zile zilijengwa miaka ya 1960 mpaka leo zipo hoi bin taaban. Serikali inasema haina uwezo, juzi ilipata msaada kutoka *NSSF*. Kwa kutumia ubunifu wa kujenga nyumba kwa matofali ya kupanga wangeweza kujenga nyumba nyingi zaidi kuliko zile wanazojenga sasa. Naomba Serikali itumie vizuri mkopo wa *NSSF* ili nyumba nyingi za askari jeshi zijengwe.

NAIBU SPIKA: Huo ni ushauri. Mheshimiwa Waziri unashauri hivyo.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuupokea ushauri wa Mheshimiwa Kaboyonga na tutaufanyia kazi na kuuzingatia. Ahsante.

Na. 209

Uraia wa Nchi Mbili

MHE. MWADINI ABBAS JECHA aliuliza:-

Kwa kuwa Watanzania wengi wanaoishi nje ya nchi wanalazimika kuukana uraia wa nchi yao na kuomba uraia wa nchi wanazoishi kwa sababu nchi yetu bado haijaruhusu Uraia wa nchi mbili na kwa kuwa suala hili limesemwa sana hapa Bungeni lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa dhidi ya tatizo hilo:-

(a)Je, ni lini Serikali italeta Muswada wa Sheria Bungeni wa kuruhusu Uraia wa nchi mbili?

(b)Je, Serikali inaweza kueleza ni hasara gani tunazoweza kuzipata kwa kutokuwa na sheria hiyo ya kuruhusu Uraia wa nchi mbili?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mbunge wa Wete, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Uraia ni suala la Muungano kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 4(3). Aidha, Katiba inalipa Bunge mamlaka ya kutunga na kuweka masharti yanayoweza kuzuia raia asipige kura kama ana Uraia wa nchi nyingine (Ibara ya 5(2)). Kutokana na umuhimu

huu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ile ya Mapinduzi ya Zanzibar, zipo katika mchakato wa kuliangalia jambo hili kwa umakini na umuhimu wake. Pindi mchakato huo utakapokwisha Wizara yangu italeta Muswada wa Sheria hapa Bungeni kwa maamuzi ya mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukosekana kwa sheria hii kunawalazimu Watanzania wanaopata Uraia wa nchi nyingine kupoteza Uraia wa kuzaliwa. Aidha, watoto ambao huzaliwa nje ya nchi ambapo mmoja wa mzazi si raia wa Tanzania wanapofikisha umri wa miaka kumi na nane hutakiwa kuukana uraia wa mmojawapo wa mzazi wake.

Utaratibu huu haufahamiki vizuri kwa wananchi wetu, hivyo wakati mwingine watoto hao waliofikisha umri huo wa miaka kumi na nane hupata ugumu wa kupata huduma hususan hati ya kusafiria, nafasi ya masomo ya elimu ya juu chini ya udhamini wa Serikali na kadhalika.

MHE. MWADINI ABBAS JECHA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na ile ya Zanzibar inafanya huo mchakato wa kuliangalia suala hili hatimaye iweze kuleta Muswada hapa Bungeni na kwa kuwa Muswada wa Sheria mara nyingi haufafanui kila kitu katika maudhui yake. Je, Serikali inaweza kutueleza kidogo kwa maneno machache kwamba ni faida gani ambazo hupatikana tukipitisha sheria hii hapa Bungeni?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwa kuwa mchakato wa suala hili unaendelea na hatujaelezwa ukomo wake na kwa kuwa ngoja ngoja inaumiza matumbo.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutueleza ni hatua gani za dharura ambazo atazichukua kuhakikisha kwamba Muswada huu unafika Bungeni haraka na mapema iwezekanavyo ili sheria iweze kupita mapema?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu faida ambazo zinaweza kupatikana kutokana na Muswada huu kuleta hapa Bungeni, ningomba kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba itakuwa ni mapema mno kwa sababu nikishatamka itakuwa Serikali imetamka na kwa kuwa tupo katika mchakato tumepata maoni ya wadau mbalimbali, tumepata ya Serikali na sasa hivi tunapata ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na tupo katika mazungumzo, ningomba kwamba tusitamke nini itakuwa faida au hasara mpaka tutakapomiliza shughuli yote na wakati Muswada utakapokuwa unatengenezwa nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaeleza na itafahamika vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu lini Muswada utaletwa hapa nataka nimhakikishie kwamba tupo katika hatua za mwisho za mazungumzo kwa sababu ni suala la Muungano lazima lichukue sehemu zote mbili Bara na Visiwani na kweli ngoja ngoja huumiza matumbo lakini pia wakati mwingine haraka haraka haina baraka. Kwa hiyo, tunaomba atuvumilie tutauleta. Ahsante. (*Makofsi*)

Mgawanyo wa Mapato Yatokanayo na Shughuli za Uwindaji

MHE. CASTOR R. LIGALAMA aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali huchukua sehemu kubwa ya mapato yatokanayo na shughuli za uwindaji kuliko walinzi wa wanyama hao amba ni wananchi waishio maeneo yanayozunguka mbuga za hifadhi kama vile Serengeti na *Selous Game Reserves* kama inavyoelekezwa katika dhana ya “*Wildlife Management Area*” (WMA):-

(a)Je, Serikali haioni kuwa, wakati umefika sasa wa kupeleka fedha hizo katika vijiji vinavyozunguka mbuga hizo au vitalu vyta kuwindia katika mbuga hizo kama mchango wa Serikali kwa vijiji vinavyofanya shughuli hiyo ya ulinzi?

(b)Je, Serikali itakuwa tayari kufanya semina kwa viongozi wa Serikali za Vijiji vinavyozunguka maeneo hayo ili kuwezesha dhana ya WMA kueleweka kwa wananchi wa maeneo hayo?

(c)Je, katika Wilaya ya Kilombero, ni vijiji gani vimewahi kupata fedha kutokana na shughuli za uwindaji kwa miaka mitano iliyopita na kiasi gani cha fedha walipata kila kijiji?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Castor Raphael Ligalama, Mbunge wa Kilombero, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu hupeleka mgawo wa asilimia ishirini na tano ya mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii kwa Halmashauri za Wilaya ambapo uwindaji huo hufanyika. Fedha, hizi hupelekwa kwenye Halmashauri hizo kwa kuwa ndiyo huratibu shughuli za uwindaji huo katika Wilaya na ndizo zenye uwezo (watalam) wa kutunza, kujadili na kuamua matumizi ya fedha hizo.

Aidha, Wizara hutoa maelekezo kwamba asilimia sitini ya fedha hizo zitumike kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya wananchi waishio katika vijiji vinavyopakana na maeneo ya uwindaji na asilimia arobaini inayobaki itumike kwenye Halmashauri kwa ajili ya kugharamia shughuli za uhifadhi wanyamapori katika Wilaya husika.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekuwa ikitoa elimu ya uanzishaji WMA na iko tayari kuendelea kutoa elimu hiyo katika sehemu mbalimbali nchini ikiwa ni pamoa na maeneo ya vijiji vilivyoko kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero.

Wizara yangu iko tayari kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero kutoa semina kwa vijiji vilivyo tayari kuanzisha maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori kulingana na Mwongozo wa kutenga maeneo ya *WMA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka mitano 2002/2003 – 2007/2008, Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero imepata jumla ya Sh. 169,444,262/= zikiwa ni mgawo wa asilimia ishirini na tano ya mapato ya uwindaji wa kitalii. Mgawo wa fedha hizi kimradi na kimaeneo ya utawala (vijiji) ni orodha ndefu ambayo naomba nimpatie Mheshimiwa Mbunge baadaye.

MHE. CASTOR R. LIGALLAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu yasiyordhisha sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa swali langu la msingi lilihusu Serikali kuchukua kiwango kikubwa cha mapato kutoka na uwindaji wa Kitalii na nilipenda kusema kwamba, asilimia ishirini na tano tunayopewa ni ndogo.

Je, Serikali itakuwa tayari kutoa kwenye Halmashauri hizo zinazozunguka mbuga za hifadhi asilimia hamsini na kuendelea?

Mheshimiwa Naibu Spika, swal la pili, kwa vile masuala ya vitalu siku hizi yamechukua karibu maeneo mengi ya hifadhi za wanyamapori hata sehemu ambazo zilikuwa zinawindwa wanyama msimu wa kuwinda kuanzia Julai mpaka Desemba.

Je, Serikali inatuambia nini kuhusu mwananchi wa kawaida mwenye bunduki na leseni ambaye anapenda kuwinda kwa ajili ya kupata kitoweo katika msimu wa kuwinda Julai mpaka Desemba, atawinda wapi?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 25 kwamba ni ndogo inaweza ikawa ni kweli, lakini nini kifanyike ni suala la mjadala. Lakini ikumbukwe asilimia 75 inayobaki ni kwa ajili ya Watanzania au kwa ajili yetu sote ndiyo hiyo asilimia 75 tunayotumia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kugharamia miradi mingine ya kitaifa. Lakini kama asilimia 25 ni kidogo ni suala ambalo tuko tayari kulijadili na Waheshimiwa Wabunge, kufuatana na Kanuni zilizopo. Lakini si rahisi kiujumla jumla hapa. Kwa hiyo, namkaribisha Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine tuone kama asilimia 25 ni kidogo na nini kifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu wa kuwinda kwa ajili ya kitoweo utaratibu ni kwamba kila Halmashauri ya Wilaya kuna Afisa wa Wanyamapori ambaye kazi yake ni pamoja na mambo mengine ni kuratibu utoaji wa leseni kwa wawindaji wanaowinda kienyeji kwa ajili ya kitoweo. Karibu kila eneo la Halmashauri ambako kuna wanyamapori kuna *open areas* ambazo zinaruhusiwa kuwindwa kwa wananchi.

Kwa hiyo, ninamshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Afisa Wanyamaporini wa Wilaya ambaye yeye jukumu lake ni kutoa vibali hivyo. (*Makofî*)

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vijiji wanavyoishi kuzunguka meneo ya wanyamaporini ndiyo hasa za hifadhi za wanayama hao na ndiyo hasa wanaopata adha kubwa kutokana na usumbufu wa wanyama ambao wanaingia kwenye mashamba yao mara kwa mara; na kwa kuwa, hii asilimia 25 imekuwa haiwafikii kwa sababu inaingia Wilayani na Wilaya inapanga matumizi mengine. Je, Serikali sasa haioni sababu ya kutoa mwongozo kuhakikisha kwamba vile vijiji vinavyolengwa vinapata kiasi fulani cha asilimia hii 25 ili waweze kuona kwamba kazi wanayoifanya ina matunda?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi maana yake ni karibu yale yale.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 25 kwamba ipelekwe wapi kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ni kwamba mwongozo ulisema tulipeleke kwenye Halmashauri kwa kuamini kwamba huko ndiko uongozi wa Serikali za Mitaa ulipo. Huko ndiko kuna Baraza la Madiwani. Lakini pia tumesema asilimia 60 ya fedha hizo zinakwenda kwenye vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba kuna maeneo mengine wanapenda ziende kwenye Halmashauri. Hivi juzi tumejibu hapa swali la Mkoa wa Kilimanjaro, wakisema fedha zinazotolewa na *TANAPA* za ujirani mwema ambazo huenda kwenye vijiji hawapendi wanapenda ziende kwenye Halmashauri.

Kwa hiyo, kuna maeneo wanasema ziende kwenye Halmashauri na kuna maeneo wanasema ziende kwenye vijiji. Mimi nafikiri utaratibu wa kugawa asilimia 60 ziende kwenye vijiji moja kwa moja unafaa. Lakini kama bado una matatizo basi tunaweza tukaujadili. Lakini sisi kwa sasa tulikuwa tunaona unafaa sana kwa sababu huko ndiko waliko viongozi wa *Local Government*. (*Makofî*)

Na. 211

Gawio la Mapato ya Mlima Kilimanjaro

MHE. FUYA G. KIMBITA aliuliza:-

Kwa kuwa, Halmashauri zilizopo jirani na Hifadhi ya Taifa hupata gawio rasmi la asilimia 25 ya mapato yatokanayo na shughuli za utalii, na kwa kuwa Mlima Kilimanjaro kwa mwaka hutuingizia takriban shilingi bilioni 23:-

- (a) Je, mchango wa kuutunza na kuuhifadhi huo Mlima Kilimanjaro unaotolewa na wananchi wauzungukao Mlima huo unathaminiwa vipi?
- (b) Je, kwa nini kusiwepo na ‘*Gentleman Agreement*’ ya kuzipatia gawio rasmi Halmashauri za wananchi hao badala ya utaratibu uliopo hivi sasa wa hisani/maombi?
- (c) Je, utaratibu wa gawio kwa njia ya asilimia utaanza kutumika lini kwa mapato ya Mlima huo?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la rafiki yangu Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, Mbunge wa Hai, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inathamini mchango wa wananchi katika kutunza hifadhi za Taifa. Hivyo, hutenga kiasi cha fedha kwa ajili ya miradi ya ujirani mwema. Miradi inayohusika kwenye utaratibu huu ni ujenzi wa miundombinu na huduma za kijamii pamoja na shughuli nyingine zinazolenga uboreshaji wa shughuli za uhifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika swali namba 79 la tarehe 23/06/2008 liloulizwa na Mheshimiwa Fuya Kimbita (Mbunge), kwa kutumia utaratibu huu wa ujirani mwema, kwa mwaka 2007/2008 Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro ilitenga jumla ya shilingi 406,050,000/= kwa ajili ya miradi mbalimbali ya jamii inayozunguka mlima huu. Katika mpango huu, jumla ya miradi kumi ya ujenzi wa madarasa, ununuza wa samani za shule za msingi na sekondari na uanzishwaji wa vitalu vya miti yenye thamani ya shilingi 225,550,000/= imekamilika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia mpango wake wa ujirani mwema ulioko katika kila hifadhi huchangia moja kwa moaj kwenye miradi ya huduma za kijamii pamoja na kutoa elimu ya uhifadhi mazingira kwa vijiji vinavyozunguka hifadhi hizo. Kwa sasa utaratibu huu umeonekana kuwa unafurahiwa sana na wanavijiji kwani fedha nyingi hutumika kwenye miradi moja kwa moja.

Hata hivyo, kama Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Kilimanjaro wanapenda fedha hizi zипитie Halmashauri za Wilaya, Wizara yangu iko tayari kukaa na kuzungumza na Halmashauri ili kuona kama kuna uwezekano wa kuweka utaratibu mwingine unaofaa na kukubalika kwa wadau wote.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa, Wizara yangu kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa (*TANAPA*) hutenga asilimia 7.5 - 10 ya Bajeti ya matumizi ya kawaida ya hifadhi ya Kilimanjaro, kwa ajili ya kusaidia shughuli za Maendeleo ya Kijamii.

Pamoja na kukaribisha majadiliano kuhusu utaratibu wa kupeleka fedha hizi kwa wananchi kama nilivyojibu sehemu (b) Wizara yangu kupitia *TANAPA*, itaendelea kuongeza Bajeti ya miradi ya ujirani mwema kadri uwezo wa kifedha wa shirika unavyoongezeka.

MHE. FUYA G. KIMBITA: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake yenyе kuleta matumaini. Lakini naomba nimwulize maswali kama ifuatavyo:-(a)Kwa kuwa, Halmashauri ni chombo cha wananchi na sisi Wabunge ni wawakilishi wa wananchi. Je, Mheshimiwa Waziri haoni sasa hakuna sababu tena ya kuendelea kupoteza muda zaidi kwenda kufanya mazungumzo na Halmashauri na badala yake kilichobakia ni utekelezaji tu? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa hifadhi ya Mlima Kilimanjaro kwa maana ya *KINAPA* Bajeti yake ni ndogo siyo kubwa kutokana na shughuli zake kuwa siyo nyingi. Je, Wizara haioni kwamba umefika wakati muafaka sasa hivi ili iweze kuongeza kile kiasi cha ujirani mwema ili kile kitakachokuwa kinapelekwa sasa kwenye Halmashauri kiweze kuwa na *impact*?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pendekezo lake kwamba twende moja kwa moja kwenye utekelezaji kwa maana kwamba hizi fedha tuzipeleke moja kwa moja kwenye Halmashauri, nimesema tunapenda kufanya mazungumzo na viongozi wa maeneo haya. Lengo ni kupata muafaka wa pamoja. Ikumbukwe kwamba ziko Halmashauri nyingi ambazo zinazunguka hifadhi ile, si Halmashauri ya Hai peke yake, kwa maana hiyo, sidhani kama wengine katika Halmashauri ya Rombo na zingine zinaweza zikawa na mtazamo huo huo.

Kwa hiyo, tulifikiri tukikaa tukajadili na hili ni pamoja na swalı la pili analozungumzia kuhusu kuongeza kiwango. Kimsingi tumekubaliana kwamba kiwango tutakiongeza kwa sababu ni kweli hifadhi hiyo, inatoa mchango mkubwa. Ndiyo maana tumepanga kwamba baada ya muda si mrefu Shirika la *TANAPA* watacaa na viongozi wote kwa maana ya Mkurugenzi, Mwenyekiti wa Halmashauri na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wanazunguka Hifadhi ile wajadili kwa pamoja utaratibu mzuri ambao utakubalika na wadau wote. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda umekwisha. Hata hivyo tuliongeza kidogo kwa sababu tulianza na kuwasilisha mezani nyaraka. Leo swalı lililozidi sana muda na swalı lililokwenda mpaka dakika 9, lingine dakika 8, na lingine dakika 7. Kwa hiyo, bado tunahitaji wauliza maswali wawe *straight*, Mawaziri wawe *straight* na majibu yawe mafupi tunaweza kuwa na wachangiaji wengi.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni, leo Wizara hii ina wageni wengi, wako kama 400 uwezo wa ukumbi huu ni watu 180 kwa hiyo, wengi tumeweka *basement* hapo waweze kuangalia kwenye TV. Kwa hiyo, nitawatambulisha wachache na wengi wote wanakaribishwa.

Kwanza, nina wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu hiki ni chama cha UMATI , ni Chama cha Uzazi na Malezi Bora Tanzania kinaongozwa na Bibi Benedetha Ndunguru, Mwenyekiti wa Chama hicho. Mheshimiwa Benedetha Ndunguru naomba usimame ulipo. Na wale wajumbe wengine naomba wasimame. Karibuni sana. Hawa ni Wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Nina wageni wengine, wageni wa Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Waziri wa Elimu na Mafunzo, wanaongozwa na Katibu Mkuu Profesa Hamis Dihenga na Ndugu Oliver Mhaiki Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu na Mafunzo naomba wasimame. Ahsante sana. (*Makofi*)

Pia washiriki katika Maendeleo *development partners* sekta ya elimu wako wengi hao, tuna wageni wengi yuko Bwana Andesi Franken Beld, Mwenyekiti wa Washiriki katika Maendeleo *you are welcome*. Yuko Mary J. Ayekuze, tuna Pantaleo Kapichi, kuna Savelina Mwishema, kuna Wilbrod Kamgamba, siyo Slaa huyu ni *World Food Programme*, ahsante. Kuna Elizebeth Misokia mwakilishi wa Haki Elimu. Ahsante sana. (*Makofi*)

Tuna viongozi wa Chama cha Walimu Tanzania CWT wakiongozwa na Gracian Mkoba, Rais wa Chama cha Walimu Tanzania, yuko Honoratha Chitanda, Makamu wa Rais wa Chama cha Walimu Tanzania. Karibuni sana. (*Makofi*)

Halafu tuna Yahya Msulwa Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania, tuna Mohamed Utalii yeeye ni mweka hazina wa chama hicho na tuna Leonard Haule, Mkuu wa Idara ya Elimu na Utetezi wa Chama cha Walimu. Wote mnakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge, tuna Wenyeviti na Makamu Wakuu wa Vyuo Vikuu, hapa nchini. Kuna Balozi Kuhanga, Mwenyekiti wa Baraza la SUA, kuna Profesa Maboko Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kuna Profesa Monela SUA, kuna profesa Kamuzora Chuo Kikuu, Mzumbe, kuna Profesa Kusiluka Chuo Kikuu Huria, kuna Profesa Palanjo Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi ya Afya Muhimbili, kuna profesa Mshoro Chuo Kikuu Ardhi, kuna Profesa Kikula, Chuo Kikuu cha Dodoma, kuna profesa Chambo Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara Moshi.

Kuna profesa Misana Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, kuna Profesa Mushi, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa, kuna Profesa Mshimba Chuo Kikuu cha Zanzibar, kuna Profesa Shayo Chuo Kikuu cha Tumaini. (*Makofi*)

Halafu kuna watendaji wakuu Profesa Mkunya Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, tuna Bwana Nyatega, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu, kuna Eng. Zebedayo Moshi, Mkurugenzi Mkuu VETA, halafu kuna familia ya Mheshimiwa Waziri Mrs. Maghembe karibu sana mama. Yuko Dr. Mwanamkuu Maghembe mtoto wake ambaye ni Daktari yuko mwaka wa *internship*. Halafu yuko Namcheja Maghembe mtoto wake ambaye yuko mwaka wa pili Chuo Kikuu. Watakuwa maprofesa kama baba yao. Naomba wote wasimame. (*Makofi*)

Halafu kuna wageni wa Mheshimiwa Dr. Kamala, Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, yuko Dr. Mary Consolata Banda, Dr. Paul H. halafu Mrs. Jane Hipbell naomba wote wasimame, Anne Linchi, yuko Joha G. yuko Mrs. Anastazia Rwechengura, yuko Christian Banda na yuko Gen Banda. Wageni hawa wanatoka USA, Masasi *JET* na kupitia Taasisi yao ya *Jambo Tanzania* wanasaidia Jimbo la Nkenge Kata ya Gera, karibuni sana. (*Makofi*)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na Wabunge wote wa Mkoa wa Lindi ambaa ni wajumbe wa Baraza la Watoto Wilaya ya Lindi kama ifuatavyo: Yupo Katibu Mkuu wa Baraza Wilaya ya Lindi kama ifuatavyo:- Yupo katibu Mkuu wa Baraza la Watoto Wilaya ya Lindi Ndugu Ndondi, kuna Mjumbe wa Kamati Kuu Baraza la Watoto Wilaya ya Lindi Ndugu Jamila Juma Lulida, yuko Mwenyekiti wa Baraza la Watoto Kata ya Mtama Ndugu Mchora. Halafu kuna Afisa Maendeleo ya Jamii Msaidizi *Save Children* Ofisi ya Lindi Ndugu Rose Beatus. Halafu kuna Meneja wa Programu ya Ushiriki wa Ulinzi wa Mtoto yupo Derick Mbelwa. Ahsanteni sana kwa kazi hiyo ya kuwalinda watoto. (*Makofi*)

Tuna wageni kutoka Taasisi ya Elimu Mkoani Dodoma ambaa wanajumuisha walimu wakuu wa shule naomba walimu wakuu wote wasimame, wakae. Waratibu wa Elimu, kuna Wakuu wa Vyuo vya Walimu, kuna Wakaguzi na Makatibu wa Chama cha Walimu Tanzania jumla ni kama wapo watu 82 nadhani wengine wapo kwenye *basement*.

Wageni kutoka Taasisi mbalimbali za Elimu kama ifuatavyo na wengine watakuwa huko chini kwenye *basement*. Wanachuo 13 kutoka Chuo cha Ardhi Dar es Salaam. Kuna wanafunzi watano kutoka *Save the Children* ndiyo hao tulikuwa nao. Kuna wanafunzi kumi kutoka *Central Secondary School Dodoma*. Kuna wanafunzi nane kutoka *Makole Secondary School Dodoma* na kuna wanafunzi 21 kutoka Chuo cha Ualimu Mpwapwa.

Kuna wageni 25 kutoka Shirika la Vyama la Watu wenye Ulemavu Tanzania, kama wapo humu ndani wasimame. Karibuni sana wageni wanaotoka kwenye Vyama vya watu wenye ulemavu. Wamewakilisha kwa sababu wapo wengi, wengine wapo kule chini *basement*. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kuna jumla ya marais 40 kutoka Serikali za wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu Nchini ambaa wanaongozwa na mwenyeji wao Andrew Nkamba, Rais wa

CBE Dodoma, kama wachache wapo humu ndani wasimame. Ohoo karibuni sana. Kwa hiyo, tulikuwa na tatizo la nafasi ndiyo maana wengine hawapo hapo.

Waheshimiwa Wabunge, shughuli zingine. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali *PAC* Mheshimiwa John Cheyo anawaomba Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo tarehe 14/7/2008 saa 7.00 mchana wakutane katika chumba Namba 231. Wajumbe wa Kamati ya *PAC*.

Sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji Mheshimiwa Gideon Cheyo yeeye anawaomba wajumbe wake wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji wakutane leo saa 7.00 mchana katika chumba 219. Kwa hiyo, msije mkachanganya vyumba. Wajumbe wa *PAC* chumba 231na Wajumbe wa Kilimo, Mifugo na Maji chumba 219 saa 7.00 mchana.

Waheshimiwa Wabunge, jana naona kulikuwa na lile shindano la mpira nililotangaza siku ile ya Ijumaa kwamba lilikuwa kati ya Timu ya Bunge na Viongozi wa Dini. Matokeo yalikuwa hivi, ingawa kwenye Redio sijui kama walitangaza. Lakini hayakutangazwa. Waheshimiwa Wabunge waliwashinda wale viongozi wa Dini kwa mabao manne kwa bila au ziro. Hili lilikuwa uoneaji. Kwa hiyo, naomba kuwapongeza sana wale wachezaji wetu wa mpira, najua wanapata mafunzo ya kutosha. Kwa hiyo, waendelee kuwa hivyo hivyo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunaendelea na shughuli inayofuata. Katibu endelea na *Order Paper*.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mtoa Hoja Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii, Prof. Jumanne Maghembe.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, kutohana na taarifa iliyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii iliyochambua Makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kuitisha Makadirio ya Matumizi ya kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Nchi za Afrika. Kuteuliwa kwake kumeleta heshima kubwa sana kwa nchi yetu. Aidha, naomba nichukue fursa hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa kunithea kuiongoza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufund. Nitaendelea kushirikiana kwa dhati na Waheshimiwa Wabunge pamoja na Wadau wengine ili kuhakikisha utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Omari Shaban Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini, kwa kuchambua, kujadili na hatimaye kuitisha makadirio ya Wizara yangu. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara yangu imezingatia mapendekezo yaliyotolewa na Kamati na itaendelea kupokea mapendekezo ya ziada ya kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge ili kuongeza ufanisi na ubora wa elimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki kwa kuteuliwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nawapongeza pia Mawaziri na Naibu Mawaziri wapya walioteuliuwa hivi karibuni. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Benedict Ngalamu Ole Nangoro kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Kiteto, Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude Lwakatare na Mheshimiwa Dr. Christine Ishengoma kwa kuteuliwa kuwa Wabunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vilevile kumshukuru Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta (Mb) aliyekuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufund na Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla (Mb) aliyekuwa Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuongoza Wizara hii mpaka Machi, 2008. Nimejifunza mengi kutoka kwao ambayo yananisaidia katika kuiongoza Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa Naibu Mawaziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufund, Mheshimiwa Mwantumu Bakari Mahiza, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Tanga na Mheshimiwa Gaudentia Mugosi Kabaka, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mara, kwa ushirikiano, uaminifu na uadilifu mkubwa, kwa viongozi wetu Wakuu Serikalini na kwa watumishi wote Wizarani.

Aidha, nawashukuru Katibu Mkoo wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufund, Profesa Hamisi O. Dihenga, Naibu Katibu Mkoo Ndugu Oliver P. Mhaiki, pamoja na Kaimu Afisa Elimu Kiongozi Ndugu Leonard P. R. Musaroche kwa ushirikiano walionipa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nichukue fursa hii ya pekee kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Mwanga kwa ushikiriano wao mkubwa katika kutekeleza miradi ya maendeleo yetu, na kwa kuniunga mkono kwa dhati.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda nimshukuru sana Mke wangu Kudra Maghembe na watoto wangu Ngwali Maghembe, Dr. Mwanamkuu Maghembe, Namcheja Maghembe na Namghuma Maghembe, kwa upendo na misaada ya kila aina wanayonipa kila siku. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii, kwa niaba ya Wizara yangu kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kutokana na kifo cha Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia aliyekuwa Naibu na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Mheshimiwa Benedict Losurutia aliyekuwa Mbunge wa Kiteto. Mchango wao katika ujenzi wa taifa letu utakumbukwa daima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hotuba yangu imegawanyika katika sehemu kuu nne. Sehemu ya Kwanza ni Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2007/2008 na Malengo ya mwaka 2008/2009. Sehemu ya Pili ni changamoto katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Sehemu ya Tatu ni maamuzi muhimu yatakayopewa kipaumbele katika mwaka 2008/2009 na Sehemu ya Nne ni Makadirio ya Bajeti kwa mwaka 2008/2009.

Maelezo yaliyotolewa katika sehemu zote nne yamezingatia Sera na Sheria zinazoongoza utoaji wa elimu nchini na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2005. Majukumu ya Wizara. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundzi ina majukumu yafuatayo:-

(a) Kutunga Sera, kusimamia utekelezaji wake, kuratibu, kufuatalia na kutathimini mipango ya elimu katika ngazi za:-

- (i) Elimu ya Awali;
 - (ii) Elimu ya Msingi;
 - (iii) Elimu ya Sekondari Kidato cha 1 - 6;
 - (iv) Elimu itolewayo kwa wenye mahitaji maalumu;
 - (v) Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi;
 - (vi) Elimu ya Ualimu Daraja A na Stashahada;
 - (vii) Elimu na Mafunzo ya Ufundzi; na
 - (viii) Elimu ya Juu.
- (b) Kuandaa na kusimamia mitaala ya shule, vyuo vya ualimu na ufundi;
- (c) Kuhakiki na kupima ubora wa elimu katika ngazi zote;

(d) Kutunga na kuendesha mitihani ya kitaifa ya Darasa la IV, VII, Kidato cha 2, 4 na 6 na mitihani ya Elimu ya Ualimu; na

(e) Kutoa miongozo ya uendeshaji na kusimamia shughuli za Taasisi, Bodi, Asasi, Tume, Mabaraza na Vyuo vilivyo chini ya Wizara ambavyo ni:-

- (i) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;
- (ii)Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo;
- (iii)Chuo Kikuu Mzumbe;
- (iv)Chuo Kikuu Huria cha Tanzania;
- (v)Chuo Kikuu Dodoma;
- (vi)Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi za Afya Muhimbili;
- (vii)Chuo Kikuu Ardhi;
- (viii)Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam;
- (ix)Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara Moshi;
- (x)Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa;
- (xi)Chuo cha Kumbumbu ya Mwalimu Nyerere;
- (xii)Chuo cha Ufundı Arusha;
- (xiii)Taasisi ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma;
- (xiv)Baraza la Mitihani Tanzania;
- (xv)Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania;
- (xvi)Kituo cha Maendeleo Dakawa;
- (xvii)Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı Stadi;
- (xviii)Taasisi ya Elimu Tanzania;
- (xix)Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima;
- (xx)Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (*ADEM*);
- (xxi)Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu;
- (xxii)Mamlaka ya Elimu Tanzania;
- (xxiii)Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania;
- (xxiv)Elimu kwa Njia ya Posta;
- (xxv)Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundı; na
- (xxvi)Tume ya Taifa ya *UNESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kusimamia na kutekeleza majukumu yake, Wizara inaongozwa na:-

- (a)Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, Sera ya Elimu ya Juu ya mwaka1999 na Sera ya Elimu ya Ufundı na Mafunzo ya mwaka 1996;
- (b)Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na rekebisheso Na. 10la mwaka 1995 na Na. 2 la mwaka 1998;
- (c)Sheria Na. 1 ya Mafunzo ya Ufundı Stadi ya mwaka 1994;
- (d)Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025;
- (e)Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA); na
- (f)Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005.

Utekelezaji wa Mipango ya Mwaka 2007/2008 na Malengo ya mwaka 2008/2009. Sasa naomba niwasilishe Utekelezaji na Mafanikio ya mwaka 2007/2008 pamoja na Malengo ya Wizara kwa mwaka 2008/2009. Idara ya Elimu ya Msingi. Elimu ya Awali na Elimu ya Msingi ndiyo chimbuko na chemchem ya kutoa fursa sawa ya elimu kwa watoto wote. Idara ya Elimu ya Msingi ina jukumu la kuratibu utoaji wa Elimu ya Awali na Elimu ya Msingi iliyo bora. Aidha, Wizara yangu inafanya ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kuona utekelezaji wa Sera na Miongozo ya Elimu katika Halmashauri zote, kwa lengo la kutoa ushauri wa kitaalam na hatimaye kuinua ubora wa elimu itolewayo kwa wanafunzi.

Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 ilielekeza serikali kuongeza kasi ya upanuzi wa elimu ya awali, kuongeza kiwango cha ubora wa elimu ya msingi, kuandikisha watoto wote wa rika lengwa wenyе umri wa miaka 7-13, kuongeza uandikishaji wa watoto wenyе mahitaji maalumu, kuongeza idadi ya wanafunzi watakaoendelea na elimu ya sekondari na kujenga nyumba za walimu, madarasa na vyoo. Katika shule za Serikali na zisizo za serikali, wanafunzi wa elimu ya awali wameongezeka kutoka 638,591 mwaka 2005 (wasichana 319,974) kufikia 873,981 mwaka 2008 (wasichana 438,025) wakiwemo wanafunzi 2,146 wenyе mahitaji maalumu, wanafunzi katika elimu ya msingi wameongezeka kutoka 7,541,208 mwaka 2005 (wasichana 3,685,496) kufikia 8,410,094 mwaka 2008 (wasichana 4,148,263) wakiwemo wanafunzi 34,661 wenyе mahitaji maalumu, walimu wa elimu ya awali wameongezeka kutoka 11,148 mwaka 2005 kufikia 16,597 mwaka 2008, walimu wa elimu ya msingi wameongezeka kutoka 135,013 mwaka 2005 kufikia 154,895 mwaka 2008. Aidha, idadi ya madarasa ya elimu ya awali imeongezeka kutoka 21,607 mwaka 2005 kufikia 28,048 mwaka 2008 na shule za msingi zimeongezeka kutoka 14,257 mwaka 2005 kufikia 15,673 mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kutayarisha na kusimamia tekelezaji wa Mtihani wa darasa la IV. Mtihani huu utaendelea kutolewa wa lengo la kupima maendeleo ya wanafunzi, kudumisha nidhamu ya wanafunzi, kuwawezesha wanafunzi kuzoea mchakato wa mitihani ya kitaifa na kubaini wanafunzi wanaostahili mafunzo rekebishi. Aidha, mtihani huu utaendelea kuwa kipimo cha kupima utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Msingi, Ufundishaji na Maendeleo ya wanafunzi kitaaluma. Hivyo badala ya kuwafanya wanafunzi watakaoshindwa mtihani huu hawataruhusiwa kukariri darasa la IV bali msisitizo utawekwa katika kutoa mafunzo rekebishi wa wanafunzi hao ili kuwawezesha kuendelea na masomo na hivyo kuhitimi elimu ya msingi ambayo ni haki ya msingi ya kila mtoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ili kuyafikia malengo ya utoaji wa elimu bora, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) 2002 – 2006 ulianzishwa ukiwa na malengo yafuatayo; kuongeza uandikishaji; kuinua ubora wa Elimu itolewayo; kujenga uwezo wa watendaji; kuimarisha taratibu za kitaasisi; na kuimarisha elimu ya masuala mtambuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio makubwa yamepatikana kutokana na utekelezaji wa MMEM awamu ya kwanza. Mafanikio hayo ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi walioandikishwa katika shule za msingi kutoka wanafunzi 4,845,185 mwaka 2001 hadi kufikia 7,959,884 mwaka 2006, kuimari kwa vigezo vya kupimia maendeleo ya Elimu kama *Gross Enrolment Ratio* (GER) na *Net Enrolment Ratio* (NER) kutoka asilimia 84.4 na 66.0 mwaka 2001 kufikia asilimia 112.7 na 96.1 mwaka 2006, kuimari kwa uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi kufikia 1:3 mwaka 2006 kutoka 1:20 mwaka 2001, kuongezeka kwa shule za msingi kutoka 11,873 mwaka 2001 na kufikia 14,700 mwaka 2006 na kuboresha Mtaala wa elimu ya msingi ili kuwawezesha walengwa kukabiliana na changamoto za kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza MMEM awamu ya kwanza, changamoto mbalimbali zilijitokeza zikiwemo upungufu wa miundombinu kukidhi mahitaji makubwa yaliyopo hasa kwa madarasa, madawati, vyoo na nyumba za walimu; mafunzo kwa walimu waliopo kazini; uhaba wa walimu wenyewe sifa kwa shule za awali na msingi; na miundombinu duni ya shule inayoshindwa kukidhi mahitaji ya wanafunzi wenyewe ulemavu na wanafunzi wa kike na mapungufu katika kuimari mifumo wa upimaji na utahini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza awamu ya kwanza ya MMEM (2002-2006), na kuyafikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia ya Elimu kwa Wote, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis kwa kushirikiana na TAMISEMI, ilianzisha awamu ya pili ya MMEM (2007/2011). Maeneo yaliyozingatiwa katika awamu hii ni pamoja na upanuzi wa uandikishaji wa watoto wote wakiwemo wenyewe ulemavu katika ngazi ya elimu ya awali na elimu ya msingi ambapo lengo ni kuandikisha watoto 7,162,353 wa elimu ya awali wenyewe miaka 5 na watoto 6,299,995 wa elimu ya msingi kati ya mwaka 2007 na 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji huu unaenda na mikakati ya mafunzo na ajira ya walimu 52,088, ujenzi wa vyumba vya madarasa 45,315 na ujenzi wa nyumba 89,927 za walimu. Aidha, maeneo mengine yaliyozingatiwa ni pamoja na kuimari ubora wa elimu itolewayo kwa kuendelea kutoa mafunzo kwa walimu kazini; kufanya tafiti za kielimu, kufanya ufuutiliaji na tathmini na kuimari ukaguzi wa shule; kujenga uwezo wa watendaji, wataalam na wasimamizi katika kuongoza na kusimamia utoaji bora wa elimu; kuimari elimu ya masuala mtambuka yakiwemo; elimu dhidi ya UKIMWI/VVU, Mazingira na Jinsia na kuimari mifumo ya usimamizi na utoaji elimu kwa kuainisha wajibu na majukumu ya wadau wa ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa malengo ya mwaka 2007/2008. Mwaka 2007/2008 ulikuwa mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa awamu ya pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM II) 2007-2011. Utekelezaji wa Mpango huu unahuishisha Mradi wa Lishe Shuleni, Kukomesha Ajira Mbaya kwa Watoto na Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA). Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilitekeleza kazi zifuatazo:-

- (a) kufanya mapitio na kusambaza Miongozo ya Utekelezaji wa MMEM II kwa Halmashauri zote nchini na wadau;
- (b) kutoa mafunzo ya kujenga uwezo wa usimamizi wa MMEM II kwa watendaji na wasimamizi wa elimu 2,332 katika ngazi ya Mkoa na Halmashauri;
- (c) kuandikisha wanafunzi 853,893 wa Elimu ya Awali wenyi miaka 5-6 sawa na asilimia 82.7 ya lengo (wavulana 425,791 na wasichana 428,102) na wanafunzi 1,355,950 wa darasa la kwanza ambao kati yao, wenyi umri wa miaka 7 ni 1,022,551 wakiwemo wavulana 512,178 na wasichana 510,373;
- (d) kufanya ukarabati wa majengo na miundombinu ya shule maalum ya serikali inayotumia lugha ya Kiingereza “Arusha School”;
- (e) kuratibu, kufuatalia na kutathmini utekelezaji wa Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA) katika Halmashauri za Magu, Hai, Temeke, Mtwara (V), Makete na Bagamoyo. Aidha, ilibainika kuwa wastani wa asilimia 80 ya wanafunzi wa MEMKWA wamefaulu mtihani wa Darasa la IV na VII, kati yao 228 sawa na asilimia 66 walijiunga na Elimu ya Sekondari;
- (f) kufuatalia matumizi ya Ruzuku ya Uendeshaji wa shule na utekelezaji wa mtaala ulioboreshwa katika Halmashauri zote nchini kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI;
- (g) kutekeleza mpango wa shule zenyi mazingira yanayomjali mtoto katika Halmashauri za Hai, Magu, Makete, Bagamoyo, Mtwara(V) na Temeke kwa kushirikiana na UNICEF;
- (h) kuratibu, kufuatalia na kutathimini Mradi wa Lishe Shuleni unaoendeshwa kwa ushirikiano na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) katika Halmashauri 13 za Bahi, Longido, Chamwino, Karatu, Kiteto, Kondo, Iramba, Manyoni, Singida (V), Simanjiro, Ngorongoro, Monduli na Mpwapwa, ambapo wanafunzi 202,712 (wavulana 105,535 na wasichana 97,177) hunufaika na mradi. Tani 7,363 za vyakula zenyi thamani ya shilingi bilioni 5.5 zimetumika.
- Aidha, majiko 35 na matangi 6 ya maji yamejengwa katika shule za Makulo, Nyaha na Ilongo katika Halmashauri za Manyoni na Iramba;
- (i) kuratibu ukaguzi wa fedha za MMEM 2006/2007 na malipo ya posho za walimu wanafunzi ambapo Halmashauri 30 zilikaguliwa katika kipindi cha Desemba, 2007 na Machi, 2008;
- (j) kufanya tathimini ya MMEM II kama sehemu ya mapitio ya Sekta ya Elimu Septemba–Novemba 2007;

(k) kuratibu na kufuatilia utoaji wa elimu kwa watoto walioondolewa katika ajira mbaya katika Halmashauri za Kondoa, Iramba, Iringa, Arusha (M), Arumeru, Simanjiro, Urambo, Temeke, Ilala, Kinondoni, Mwanza (J), Lindi (V), na Kilwa kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani; na

(l) kuwaondoa katika ajira mbaya jumla ya watoto 1,494 (wasichana 530 na wavulana 964) na kuwaandikisha katika madarasa ya MEMKWA. Aidha, watoto 558 (wasichana 221 na wavulana 337) waliandikishwa madarasa ya elimu ya awali ikiwa ni hatua ya maandalizi ya kuwaepusha na ajira mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya mwaka 2008/2009, Wizara yangu itatekeleza mwaka wa pili wa awamu ya pili ya MMEM (2007-2011) kwa lengo la kuhakikisha kwamba azma ya serikali ya kutoa elimu ya awali na elimu ya msingi kwa wote inafikiwa. Katika kutekeleza azma hii, Wizara yangu itashirikiana na TAMISEMI na wadau mbali mbali kutekeleza yafuatayo: -

(a) kufuatilia uandikishaji wa wanafunzi 1,399,100 katika Elimu ya Awali na Elimu ya Msingi wenye miaka 5-6 na wanafunzi 1,232,570 wa Darasa la kwanza;

(b) kufuatilia matumizi ya Ruzuku ya Uendeshaji kwa ajili ya ununuzi wa vitabu na vifaa mbalimbali vya kujifunzia na kufundishia katika Halmashauri na Shule;

(c) kufuatilia matumizi ya Ruzuku ya Maendeleo katika kujenga na kupanua miundombinu katika shule za msingi inayojumuisha vyumba vya madarasa 5,732 vya Elimu ya awali, madarasa 10,753 ya Elimu ya msingi, matundu ya vyoo 17,864, nyumba za walimu 21,936, ununuzi wa madawati 131,200 na ukarabati. Aidha, ukarabati huu utahusisha “*Arusha School*” kwa awamu ya pili na shule za msingi za mazoezi 10;

(d) kuratibu na kufuatilia wanafunzi wa MEMKWA kundirika la kwanza (*peer group*) ili kuingizwa kwenye mfumo rasmi wa elimu ya msingi;

(e) kuratibu, kufuatilia na kutathmini ukaguzi, uhuishaji wa vituo vya walimu vilivyopo na kuhimiza Halmashauri kujenga vituo vipyta maeneo yasiyokuwa navyo;

(f) kuratibu utoaji wa mafunzo kazini kuititia vituo vya walimu kwa walimu 31,250 wakiwemo wa kutoka Halmashauri za Nanyumbu, Kondoa, Same, Meatu, Tunduru, Maswa, Masasi, Bariadi, Kishapu na Namtumbo zilizokuwa na matokeo yasiyordhisha katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2007. Mkazo utawekwa katika masomo ya Hisabati, Sayansi na Lughu;

(g) kuchapisha miongozo ya MMEM II na kuisambaza katika shule zote za msingi kuititia Halmashauri;

(h) kuratibu uandaaji na uendeshaji wa mitihani ya kitaifa ya Darasa IV na la VII na kufanya tathimini yake;

(i) kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Shule Zenye Mazingira Yanayomjali Mtoto katika Halmashauri za Hai, Magu, Bagamoyo, Mtwara (V) na Temeke kwa kushirikiana na UNICEF;

(j) kuendelea kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mradi wa Lishe Shuleni katika Halmashauri zinazotekeliza mradi huu;

(k) kushirikiana na *Bridgelt* kutoa vifaa vya TEHAMA kwenye shule 200 za msingi;

(l) kujenga uwezo wa watendaji na viongozi 540 wa ngazi mbalimbali ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi; na

(m) kuimarisha michezo shuleni kwa kujenga uwezo wa wavezeshaji ili kufundisha walimu wa michezo kwa kushirikiana na Right to Play na Serikali ya Ujerumani na kufuatilia utekelezaji wa mtaala wa michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Elimu ya Sekondari ni kiungo kati ya Elimu ya Msingi, Ualimu na Elimu ya Juu. Idara inajukumu la kusimamia uendeshaji na uratibu wa utoaji wa elimu bora nchini kuanzia Kidato 1-6, kutunga na kurekebisha sera, miongozo na viwango vya ubora wa elimu ya sekondari nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika elimu ya sekondari, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 ilielekeza serikali kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari kikamilifu, kuwa na angalau shule moja ya sekondari kwa kila Kata, kuimarisha ubora wa elimu ya sekondari, kuongeza viwango vya ufaulu katika Kidato 4 na 6, kujenga nyumba za walimu na kuongeza idadi ya wanafunzi wa Kidato 1-4 kufikia angalau 50% na wanafunzi wa Kidato 5-6 kufikia 25% ya watoto wa rika lengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika shule za Serikali na zisizo za serikali, wanafunzi wa elimu ya sekondari kidato 1-6 wameongezeka kutoka 524,325 mwaka 2005 (wasichana 244,571) kufikia 1,222,403 mwaka 2008 (wasichana 543,279) ambapo wanafunzi waliojiunga na kidato 1 wameongezeka kutoka 180,239 mwaka 2005 (wasichana 88,559) kufikia 438,901 mwaka 2008 (wasichana 186,785) na waliojiunga na kidato 5 wameongezeka kutoka 18,893 mwaka 2005 (wasichana 7,147) kufikia 37,816 mwaka 2008 (wasichana 15,867), walimu wameongezeka kutoka 18,754 mwaka 2005 kufikia 32,835 mwaka 2008, Aidha, idadi ya shule za sekondari zimeongezeka kutoka 1,745 mwaka 2005 kufikia 3,798 mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES). Katika kuimarisha elimu ya sekondari Serikali inatekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari - MMES (2004-2009) ili kwenda sanjari na kasi ya uandikishaji na ongezeko la ufaulu uliotokana na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi MMEM.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kwamba Serikali inafikia lengo la kuwa na angalau shule moja ya sekondari ya serikali kwa kila kata, jumla ya shule mpya

1,837 zilijengwa na kusajiliwa katika kipindi cha mwaka 2006 mpaka 2008 na kufanya jumla ya shule zote za serikali kuwa 3,039 ikilinganishwa na shule 1,202 zilizokuwepo Desemba 2005. Mafanikio haya makubwa yamepatikana kutokana na ushirikishwaji mkubwa wa wananchi, Halmashauri za Wilaya na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari MMES, (Angalia kielelezo Na. 1). Juhudi kubwa zilifanywa katika utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005. Kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa MMES, wizara yangu ipo katika hatua za mwisho za kuandaa Awamu ya Pili ya MMES ambao utazingatia ukamilishaji wa madarasa, nyumba za walimu, maabara ya sayansi na uanzishwaji wa TEHAMA kama chombo muhimu cha kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa malengo katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa elimu, ilitekeleza yafuatayo:-

- (a) Kugharamia elimu ya sekondari kwa wanafunzi 21,845 kutoka katika familia zenye kipato duni ambapo shilingi 3,242,141,000 zilitumika;
- (b) kukarabati shule za sekondari za Ufundı Moshi, Lugalo, Moshi, Mpwapwa, Korogwe, Iringa na Kazima zenye wanafunzi wenye ulemavu. Jumla ya shilingi 105,000,000 zilitumika;
- (c) kutoa ruzuku ya punguzo la ada ya shilingi 10,195,423,530 kwa ajili ya shule 1,699 za serikali za kutwa kwa wanafunzi 756,043;
- (d) kutoa ruzuku ya shilingi 9,153,759,200 kwa ajili ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi 822,440 wa shule za sekondari za serikali;
- (e) kutoa ruzuku ya shilingi 250, 000,000 kwa ajili ya kuchangia ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa shule 285 zisizo za serikali;
- (f) kujenga hosteli 12 kwa għarama ya shilingi 264,000,000 kwa ajili ya wasichana katika maeneo ya wafugaji na yaliyo nyuma kielimu;
- (g) kutoa ruzuku ya shilingi 5,674,000,000 kuchangia ujenzi wa madarasa 777 ya kidato 1–4 na vyoo 49 katika shule za serikali;
- (h) kugharamia ujenzi wa madarasa 88 ya kidato cha 5 na 6 kwa kiasi cha shilingi 616,000,000;
- (i) kugharamia ujenzi wa maabara 84, maktaba 27, mabweni 34 na majengo ya utawala 19 kwa kiasi cha shilingi 2,442,000,000;
- (j) kutoa ruzuku ya shilingi 13,509,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 1,501 za walimu;

(k) kuwapatia mafunzo ya kuwaongezaa uwezo wa kimenejimenti Wakuu wa shule 750, Waratibu wa elimu ya sekondari wa Wilaya 114, na Watendaji 11 wa Makao Makuu; na

(l) kugharamia mafunzo kwa Walimu 493 Chuo Kikuu Huria, 110 wa hisabati Chuo Kikuu cha Tumaini, 25 Stashahada ya Uzamili na 16 Shahada ya Uzamili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya mwaka 2008/2009, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itatekeleza yafuatayo:-

(a) kugharamia elimu ya sekondari wanafunzi 51,000 wanaotoka katika familia zenyenye kipato duni na yatima;

(b) kutoa mafunzo kazini kwa walimu 1,000 wa shule za sekondari wanaofundisha masomo ya Sayansi, Hisabati na Kiingereza;

(c) kugharamia mafunzo kwa walimu wa kifaransa kwa kushirikiana na serikali ya Ufaransa: Mafunzo tarajali katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Dar es Salaam na mafunzo kazini katika Chuo Kikuu Huria cha Dar es Salaam;

(d) kutoa ruzuku ya shilingi 2,000,000,000 kuchangia ujenzi wa madarasa 200 ya Kidato cha 5 na 6;

(e) kutoa ruzuku ya shilingi 9,100,000,000 kuchangia ujenzi wa nyumba 700 za Walimu;

(f) kujenga maabara 230 na vyumba vya maktaba 24 kwenye shule za kidato cha 5-6 kwa gharama ya shilingi 4,943,000,000;

(g) kutoa ruzuku ya punguzo la ada kiasi cha shilingi 1,603,142,000 kwa shule za kutwa;

(h) kutoa ruzuku ya shilingi 3,482,614,000 kwa ajili ya kununulia vifaa vya maabara, maktaba na vingine vya kufundishia na kujifunzia;

(i) kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari;

(j) kutoa fedha za kununua vifaa kwa wanafunzi wenye ulemavu katika shule 3 kwa gharama ya shilingi 30,000,000;

(k) kuimarisha michezo shuleni kwa kununua vifaa vyenye thamani ya shilingi 50,850,000 na kuwashirikisha wadau wengine wa michezo wakiwemo *Barrick Gold Mines Ltd* katika kuandaa mashindano ya michezo ya shule za sekondari kitaifa;

(l) kukamilisha zoezi la kuhamishia usimamizi na uendeshaji wa shule za sekondari za serikali kwenda ngazi ya Halmashauri; na

(m) kuendelea kugharamia walimu wa mwaka wa pili na wa tatu Shahada ya kwanza 500 Chuo Kikuu Huria, 71 Chuo Kikuu Tumaini; Shahada ya Uzamili 10 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na mafunzo ya Uongozi wa Menejimenti kwa Wakuu 60 wa Shule wapya katika chuo cha ADEM.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Elimu ya Ualimu, ina jukumu la kutoa na kusimamia mafunzo ya walimu tarajali na walimu kazini ngazi ya awali, msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 inaielekeza serikali kupanua mafunzo ya elimu ya ualimu ili kukidhi mahitaji makubwa ya walimu wa elimu ya awali, msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mafunzo ya ualimu Daraja A na stashahada hutolewa katika Vyuo vya Ualimu 33 vya Serikali na 34 visivyo vya serikali vyenye uwezo wa kuchukua jumla ya walimu wanafunzi 18,600 kwa mwaka. Katika kuongeza idadi ya walimu wa elimu maalumu, serikali itakipanua Chuo cha Ualimu Patandi. Mafunzo ngazi ya Shahada hutolewa katika vyuo vikuu vya serikali ambavyo ni Chuo Kikuu Cha Dar Es Salaam, Chuo Kikuu Dodoma, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar Es Salaam, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa na vyuo vikuu 10 visivyo vya serikali. Aidha, serikali inaendelea kuongeza nafasi za mafunzo ya ualimu katika ngazi ya shahada kwa kuhamasisha vyuo vikuu vingine kuanzisha masomo ya ualimu ambapo Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kitaanzisha shahada ya ualimu mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa malengo ya mwaka 2007/2008, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu ilitekeleza yafuatayo:-

(a) kutoa mafunzo ya Stashahada kwa wahitimu 6,287 na wanachuo 7,104 wa Daraja A;

(b) kutoa mafunzo kabilishi ya mbinu bainifu (*diagnostic*) kwa wakufunzi 105 na walimu wa shule za msingi 200, kwa ufadhili wa UNICEF na UNESCO;

(c) kutoa mafunzo kwa walimu 3,500 wa B na C wanaojiendezea kuingia Daraja A;

(d) kuunganisha mtandao wa TEHAMA kwenye Vyuo 32 vya Ualimu;

(e) kugharamia walimu wa leseni 850 wanaojiendezea Chuo Kikuu Huria mwaka wa pili;

(f) kugharamia mafunzo kwa wakufunzi 635 wanaojiendeleza katika Vyuo Vikuu wakiwemo Shahada ya Uzamivu 10, Shahada ya Uzamili 17, Shahada ya kwanza 328, na 280 mafunzo maalum ya *Teachers Educators Program*; na

(g) kutoa mafunzo ya VVU na UKIMWI kwa wakufunzi 105 kutoka vyuo vya ualimu 33.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya mwaka 2008/2009, katika mwaka 2008/2009 Wizara yangu itatekeleza yafuatayo:-

(a) kutoa mafunzo ya Stashahada kwa wanachuo 9,000 na wanachuo 9,000 kwa ngazi ya Cheti;

(b) kutoa mafunzo kabilishi (*orientation*) yanayohusu masuala mtambuka kwa wakufunzi 105 na walimu 200 wa shule za msingi;

(c) kutoa mafunzo kwa walimu 4,000 wa Daraja la B na C kufikia Daraja A kwa njia ya Masafa;

(d) kukamilisha miundo mbinu ya mtandao wa TEHAMA katika vyuo vya ualimu Shinyanga na Dakawa;

(e) kutoa mafunzo kwa wakufunzi 105 kuhusu mbinu za ufundishaji bainifu;

(f) kutoa mafunzo kabilishi kwa wadau 60 wa utekelezaji wa Mkakati wa Menejimenti na Maendeleo ya Walimu;

(g) kugharamia wakufunzi 635 waliopo katika Vyuo Vikuu;

(h) kuhamasisha wadau wa elimu kuongeza ujenzi wa Vyuo vya Ualimu vya sekta binafsi ikiwa ni pamoja na kufungua chuo cha Mufindi na kuendeleza ujenzi wa chuo cha Tunduru;

(i) kukarabati chuo cha ualimu Patandi na kutafuta fedha za kujenga vyuo vingine 2 vya elimu maalumu; na

(j) kufanya maandalizi ya kuanza kutumia TEHAMA katika kufundisha na kujifunza (*online teaching and learning*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi inabuni, inasimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 inaielekeza serikali kupanua mafunzo ya ufundi stadi kwa kushirikisha sekta binafsi na kuanzisha vyuo vya VETA angalau kimoja kwa kila Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuongeza nafasi na ubora wa mafunzo ya ufundi stadi mafunzo yamekuwa yakitolewa katika vyuo vya serikali ambavyo ni chuo

cha ufundi Arusha, vyuo vya VETA 21 na vyuo binafsi 900. Aidha, serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha vyuo vya ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa malengo ya mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008, Idara ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ilitekeleza yafuatayo:-

(a) kuandaa rasimu ya Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya mwaka 1996 yenye mtazamo mpana wa mstakabali wa utoaji na uendeshaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini;

(b) kudhamini mafunzo kwa wanafunzi 1,800 katika ngazi ya Ufundi Sanifu katika Vyuo na Taasisi za Ufundi zilizo chini ya Wizara;

(c) kugharamia mafunzo ya watumishi 2 katika mafunzo ya muda mrefu; na

(d) kutambua stadi zinazohitajika kutolewa katika vyuo vya ufundi stadi kwenye wilaya 28 katika mikoa 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya mwaka 2008/2009. Katika mwaka 2008/2009, Idara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi itatekeleza yafuatayo: -

(a) kukamilisha Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (*Technical and Vocational Education and Training Policy*);

(b) kudhamini wanafunzi 600 kupata mafunzo ngazi ya Ufundi Sanifu katika vyuo na taasisi za ufundi zilizo chini ya Wizara;

(c) kuhamasisha wanafunzi katika shule za sekondari ili wajiunge na vyuo na taasisi za ufundi nchini;

(d) kuimarisha na kuandaa mtaala wa vyuo vya ufundi stadi vya mikoa ili kuviwezesha kutoa mafunzo ya ufundi ngazi ya Stashahada;

(e) kufanya maandalizi ya ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi katika wilaya 25 ambazo hazina vyuo hivyo na kukarabati vyuo 3 vinavyoendeshwa na wilaya;

(f) kuratibu uchambuzi wa mahitaji ya stadi katika wilaya 20;

(g) kugharamia mafunzo ya muda mrefu kwa wahadhiri 6 na mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 32;

(h) kuandaa mpango wa uendelezaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ambao utalenga kuwa na chuo cha ufundi stadi katika kila Wilaya;

(i) kuratibu uwezeshaji wa vyuo vya wilaya kutoa mafunzo ya ufundi stadi ngazi ya I, II, III na kuandaa *Bridging Course* ya kuwezesha wahitimu wa ngazi ya III kujiunga na mafunzo ya ufundi sanifu katika vyuo vya mikoa; na

(j) kuratibu ujenzi wa vyuo vya Lindi, Pwani, Manyara na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Elimu ya Juu ina jukumu la kutunga, kusimamia na kutathimini Sera, Sheria, Taratibu na Miongozo ya utoaji wa Elimu ya Juu nchini kwa lengo la kusomesha wataalamu wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika elimu ya juu, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 inaielekeza serikali kuandaa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Juu kuwezesha 12.5% ya wanafunzi wanaomaliza Kidato 6 kujiunga na elimu ya juu, kuhamasisha wanafunzi wa kike wengi zaidi kuchukua masomo ya sayansi, kuongeza idadi ya wanafunzi wa elimu ya juu watakaofaidika na Mfuko wa Mikopo, kuimarisha Mfuko wa Elimu kwa kuwaelimisha na kuwashamasisha wananchi kuwekeza katika elimu na kuboresha mitaala ya elimu ya juu ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira na kujiajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, wanafunzi wa elimu ya juu wameongezeka kutoka 55,296 mwaka 2005/2006 (wasichana 17,885) kufikia 65,966 mwaka 2007/2008 (wasichana 24,236) katika vyuo vikuu vya Serikali na visivyo vya Serikali), wanachuo 55,584 wamepatiwa mkopo na Bodi ya mikopo ya Elimu ya Juu na taasisi 205 zimepatiwa mkopo na ruzuku ya shilingi bilioni 3.8 kutoka Mamlaka ya Elimu mwaka 2007/2008. Aidha, Serikali imeendeleza ujenzi na ukarabati wa Chuo Kikuu Dodoma kwa gharama ya shilingi bilioni 18 na inaendelea kukarabati vyuo vikuu vingine vya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa malengo ya mwaka 2007/2008, katika mwaka 2007/2008, Idara ya Elimu ya Juu ilitekeleza yafuatayo:-

(a) kukamilisha uhuishaji wa Sera ya Elimu ya Juu ya mwaka 1999 ambayo itajumuishwa katika Sera mama ya Elimu na Mafunzo;

(b) kuhuisha sheria ya vyuo vikuu Na 7 ya mwaka 2005;

(c) kuendeleza ujenzi na ukarabati wa Chuo Kikuu Dodoma kwa gharama ya shilingi bilioni 18;

(d) kudhamini wanafunzi 1,512 wa shahada ya kwanza ya udaktari kati ya hao 16 ni udaktari wa meno (DDS) katika Vyuo Vikuu Vitano vya Sayansi za Afya nchini;

(e) kudhamini wanafunzi 88 raia wa Uganda katika utaratibu wa kubadilishana wanafunzi wa Shahada ya Kwanza katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam,

Chuo Kikuu cha Ardhi, Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya Muhimbili na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo;

(f) kudhamini wanafunzi 4 wa Shahada ya Kwanza raia wa China katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili kutekeleza Mkataba wa Ushirikiano kati ya China na Tanzania ambapo Watanzania 51 walianza masomo nchini China;

(g) kudhamini mafunzo ya shahada za juu kwa wanataaluma 64 wa Shahada ya Uzamili na 16 Uzamivu katika Vyuo Vikuu vya Umma;

(h) kutoa elimu kwa watekelezaji na wasimamizi wa elimu ngazi ya Wilaya na Mikoa yote kuhusu dhana ya uchangiaji Elimu ya Juu; na

(i) kuratibu upelekaji wa wanafunzi 186 waliokwenda kusoma katika vyuo vikuu vya nchi marafiki: Algeria 36, China 51, Cuba 7, Czech 3, Poland 7, Urusi 81 na Uturuki 1.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya mwaka 2008/2009, katika mwaka 2008/2009 Idara ya Elimu ya Juu itatekeleza yafuatayo:-

(a) kudhamini wanafunzi 1,566 wa Shahada ya Kwanza ya Udaktari wa wanadamu (MD), wanafunzi 41 wa udaktari wa meno na wanafunzi 25 wa udaktari wa tiba ya mifugo katika vyuo vikuu nchini;

(b) kudhamini wanafunzi 90 raia wa Uganda katika utaratibu wa kubadilishana wanafunzi wa Shahada ya Kwanza katika vyuo vikuu vya Afrika Mashariki;

(c) kudhamini wanafunzi 5 raia wa China ikiwa ni kutekeleza Mkataba wa Ushirikiano kati ya Tanzania na China katika vyuo vikuu nchini;

(d) kuendelea kuelimisha Umma kuhusu dhana ya uchangiaji wa gharama za Elimu ya Juu na fursa za Elimu ya Juu ndani na nje ya nchi kupitia vyombo vya habari na maonyesho;

(e) kudhamini mafunzo ya shahada za juu kwa wanataaluma 80 katika Vyuo Vikuu vya Umma;

(f) kuendeleza ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kulingana na mpango wa maendeleo;

(g) kupata na kuratibu maoni ya wadau kuhusu Sera ya Elimu ya Juu inayohuishwa pamoja na marekebisho ya Sheria ya Vyuo Vikuu Namba 7 ya 2005;

(h) kuratibu nafasi 100 za wanafunzi watakosoma Urusi kwa utaratibu wa mkopo katika Chuo Kikuu cha Urafiki Lumumba nchini Urusi;

(i) kuratibu nafasi 120 zinazotolewa na nchi marafiki kama vile Algeria, Poland, China, Cuba, Urusi, Uingereza na New Zealand;

(j) kusimamia utekelezaji wa mradi wa *Science Technology Higher Education Project* unaodhaminiwa na Benki ya Dunia unaolenga kuimarisha na kuboresha mazingira ya ufundishaji wa sayansi na teknolojia katika Elimu ya Juu;

(k) kuratibu ukusanyaji wa madeni kwa wanafunzi wa taasisi za elimu ya juu waliokopa kuanzia mwaka 1994/95 ili wanafunzi wengine waweze kufaidika;

(l) kuratibu ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya taasisi na vyuo vikuu vya umma; na

(m) kusimamia utekelezaji wa mikataba ya kuendeleza, kuimarisha na kuboresha Elimu ya Juu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Ukaguzi wa Shule ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, kanuni na viwango vya elimu vilivyowekwa ili kuhakikisha vinazingatiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 inaielekeza serikali kuimarisha ukaguzi wa shule ili kuinua kiwango cha ubora wa elimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza maelekezo ya Ilani, kuanzia mwaka 2005 hadi 2008 Idara imeimarishwa kwa kuongeza wakaguzi 220 wa shule, kukanabati ofisi za ukaguzi wa shule za wilaya 50, kununua samani za ofisi za ukaguzi wa shule katika wilaya 30, kununua kompyuta kwa ajili ya ofisi za Kanda na Wilaya, kununua magari 42 ya ofisi za ukaguzi wa shule za Kanda na Wilaya na kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wakaguzi juu ya mitaala iliyoboreshwa. Aidha, kanda 3 mpya za ukaguzi wa shule Pwani, Nyanda za Juu Kusini na Ziwa Magharibi zitaanzishwa kuanzia Julai 2008;

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu mengine ya Idara ya Ukaguzi wa Shule ni kusimamia mtihani wa Kidato cha Pili ambao unalenga kutathmini utekelezaji wa mtaala ikiwa ni pamoja na kupima maarifa na ujuzi alioupata mwanafunzi katika miaka miwili ya elimu ya sekondari, kwa kupata alama zenye uwiano kitaifa. Alama hizi zinatumwa na Baraza la Mitihani la Tanzania kama sehemu ya maendeleo ya mwanafunzi (*continuous assessment*). Alama ya kufaulu ni wastani wa asilimia 30. Mtihani wa Kidato cha Pili utaendelea kuwepo. Hata hivyo, kuanzia sasa hakuna mwanafunzi atakayerudia endapo hatapata alama hizo. Shule zitatakiwa kuwapatia mafunzo rekebishi wanafunzi watakaoshindwa kufikia alama ya ufaulu. Aidha, mwanafunzi ambaye hatafanya mtihani wa kidato cha Pili hataruhusiwa kuendelea na Kidato cha Tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa malengo ya mwaka 2007/2008, katika mwaka 2007/2008 Idara ya ukaguzi wa shule ilitekeleza kazi zifuatazo:-

(a) kukagua asasi 18,240 sawa na asilimia 79 ya lengo la kukagua asasi 23,126 . Aidha, ukaguzi maalum kwa ajili ya usajili wa shule mpya ulifanyika;

(b) kukarabati ofisi za ukaguzi wa shule za wilaya 22, kununua samani za ofisi za ukaguzi wa shule katika wilaya 5, kununua magari 9 ya ofisi za ukaguzi wa shule wilayani;

(c) kuratibu mafunzo ya awali ya ukaguzi wa shule kwa wakaguzi wapya 53; na

(d) kuendesha Mtihani wa Taifa Kidato cha Pili mwaka 2007 katika vituo 2,360 vilivyojili watahiniwa 295,954. Watahiniwa 279,765 wakiwemo wasichana 133,620 sawa na asilimia 48 na wavulana 146,145 sawa na asilimia 52 walifanya mtihani huo. Watahiniwa 259,023 sawa na asilimia 92 walifaulu, wakiwemo wasichana 118,809 sawa na asilimia 46 na wavulana 140,214 sawa na asilimia 54.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya mwaka 2008/2009, katika mwaka 2008/2009, Idara ya Ukaguzi wa Shule itafanya kazi zifuatazo:-

(a) kukagua asasi 25,147 za elimu;

(b) kununua vifaa vya ofisi na samani kwa ajili ya wilaya 20 na magari 9 kwa ajili ya ofisi za wilaya;

(c) kukarabati ofisi 20 za wilaya;

(d) kutoa mafunzo ya awali ya ukaguzi wa shule kwa wakaguzi wapya 100;

(e) kuendesha Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Pili mwaka 2008;

(f) kuanzisha Kanda mpya 3 za Ukaguzi wa Shule ambazo ni: Kanda ya Mashariki itakayojumuisha Mkoa wa Dar es Salaam, Kanda ya Pwani itakayojumuisha Mikoa ya Pwani na Morogoro, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini itakayojumuisha Mikoa ya Iringa na Ruvuma; na

(f) kutoa Elimu ya UKIMWI, ushauri nasaha na unasihi na huduma kwa wafanyakazi wa Idara ya Ukaguzi wa Shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Afisa Elimu Kiongozi ni mhimili wa utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, utoaji wa Nyaraka na Miongozo mbalimbali kwa ajili ya kuboresha Elimu na Mafunzo ya Ufundu. Aidha, inaratibu Elimu ya Watu Wazima, Elimu kwa Redio, Usajili wa Shule, Elimu Maalumu na Mpango wa Elimu dhidi ya UKIMWI, Ushauri Nasaha na Elimu ya Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 inaielekeza serikali kufufua Mpango wa Awali wa Elimu ya Watu Wazima, kuboresha elimu ya watu wazima na kuimarisha Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA) na kuongeza uandikishaji wa watoto wenye mahitaji maalumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Wizara yangu kwa kushirikiana na serikali ya Cuba imefanya upembuzi bainifu wenye lengo la kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Kisomo kwa Njia ya Redio na Video. Serikali ipo katika hatua za mwisho za kukifanya Kitengo cha Elimu ya Watu Wazima kuwa Idara kamili mwaka 2008/2009. Aidha, kuanzia mwaka 2005 hadi sasa Kitengo cha Elimu Maalumu kimeimarishwa kwa kununua mtambo wa kuchapisha vitabu vya wasioona na kununua na kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia wanafunzi wenye mahitaji maalumu vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitengo cha Elimu ya Watu Wazima, katika mwaka 2007/2008 Kitengo cha Elimu ya Watu Wazima kilitekeleza yafuatayo:-

(a) kufanya upembuzi bainifu katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na Ruvuma, kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa mpango wa majaribio wa kisomo kwa njia ya redio na video;

(b) kuandaa Mpango Mkakati wa Elimu kuhusu Haki za Binadamu Kanda ya Ziwa;

(c) kukarabati Ofisi za kituo cha Uchapaji Makao Makuu kwa kiwango cha asilimia 90 na Kituo cha Kisomo Mwanza kwa asilimia 30; na

(d) kuratibu Mpango wa Matumizi ya Mbinu Bainifu katika kufundisha kisomo cha kuijendeleza ambapo umejumuisha wilaya 10 za Temeke, Mvomero, Morogoro (V), Iringa (V), Songea (V), Sumbawanga (V), Dodoma (M), Bagamoyo, Hai na Igunga. Aidha, mafunzo kwa watendaji 30 ngazi ya wilaya yamekamilika kwa asilimia 100. Kila wilaya inaendelea kutoa mafunzo haya kwa wawezeshaji wa vikundi vya Kisomo na ujasiriamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya mwaka 2008/2009, katika mwaka 2008/2009, kitengo kitatekeleza yafuatayo:-

(a) kutekeleza mpango wa majaribio wa kisomo kwa njia ya redio na video katika wilaya za Temeke, Ilala, Kinondoni, Ilemela, Dodoma (M) na Songea (M);

(b) kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mkakati wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi 2003/2004 – 2007/2008;

(c) kutekeleza Mpango Mkakati wa Elimu Kuhusu Haki za Binadamu katika Kanda ya Ziwa kwa kushirikiana na UNESCO;

(d) kuratibu mafunzo ya wawezeshaji wa MUKEJA katika Halmashauri 123 na MEMKWA katika Halmashauri 60;

(e) kuendelea kukarabati Kituo cha Uchapaji Makao Makuu na Kituo cha Kisomo Mwanza;

(f) kuratibu utoaji wa mafunzo ya ufundishaji bainifu kwa wawezeshaji na kufuutilia matumizi ya mbinu bainifu ya ufundishaji wa vikundi vyta kisomo katika wilaya 10 za majoribio ambazo ni Temeke (M), Mvomero, Morogoro (V), Dodoma (M) Igunga, Hai, Iringa (V) Sumbawanga (V), Songea (V) na Bagamoyo;

(g) kutekeleza Mkakati wa Mfumo wa Menejimenti wa Takwimu za Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi katika Halmashauri za Temeke, Ilala, Rombo, Mbulu, Kondoa, Shinyanga (M), Shinyanga (V), Kigoma (V), Makete, Mvomero, Sumbawanga na Mtwara Mikindani; na

(h) kuratibu uanzishwaji wa Idara ya Elimu ya Watu Wazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitengo cha Elimu Maalumu, utekelezaji wa malengo ya mwaka 2007/2008. Kitengo cha Elimu Maalumu kilitekeleza yafuatayo:-

(a) kuandaa Mpango Mkakati wa kupanua na kuendesha Elimu Maalumu na Elimu;

(b) kununua na kusambaza vifaa vyta kufundishia na kujifunzia katika shule 203 zinazotoa Elimu Maalumu kwa gharama ya shilingi 860,000,000;

(c) kuendesha mafunzo ya wawezeshaji 708 wa Elimu Jumuishi katika Halmashauri 32 kutoka katika mikoa ya Kigoma, Iringa, Lindi, Mtwara, Mara, Arusha, Shinyanga na Manyara;

(d) kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa walimu 200 wataalamu wa Elimu Maalumu kikanda: Wasioona na Wenye Uoni Hafifu 50, Wenye Ulemavu wa Akili na Wenye Otizim 50, Viziwi na Viziwi Wasioona 50 na Wenye Ulemavu wa Viungo 50; na

(e) kuratibu utengenezaji wa vitabu vyta elimu maalum kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya mwaka 2008/2009, katika mwaka 2008/2009, kitengo kitatekeleza yafuatayo:-

(a) kukamilisha uandaaji wa Mpango Mkakati wa kupanua na kuimarisha Elimu Maalumu na Elimu Jumuishi ikiwa ni pamoja na kuimarisha kitengo cha Elimu Maalum;

(b) kununua na kusambaza vifaa vya kufundishia, kujifunzia na visaidizi katika shule zinazotoa Elimu Maalumu: msingi 228, sekondari 24 na Chuo cha Ualimu cha Patandi;

(c) kuendesha mafunzo ya wawezeshaji 684 wa Elimu Jumuishi katika Halmashauri 31 ambazo hazikupatiwa Elimu hiyo katika mikoa ya Mbeya, Morogoro, Tanga, Tabora, Mtwara, Lindi, Singida, Mara na Dodoma; na

(d) kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa walimu 240 wataalamu wa Elimu Maalumu kikanda: Wasioona na Wenye Uoni Hafifu 60, Wenye ulemavu wa Akili na Wenye Otizim 60, Viziwi na Viziwi wasioona 60 na Wenye Ulemavu wa Viungo 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitengo cha Usajili wa Shule, utekelezaji wa malengo ya mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008, Kitengo cha Usajili wa Shule kilitekeleza yafuatayo:-

(a) kutoa vibali vya kuanzisha shule za Sekondari za Serikali 228 zilizojengwa kwa nguvu za wananchi;

(b) kusajili shule zisizo za serikali 140 (awali 9, awali na msingi 58, sekondari 67 na vyuo vya ualimu 7). Vyuo vya Ualimu vilivyofunguliwa ni Consolata - Iringa, Singida – Singida (M), Capital – Dodoma (M), Popatlal – Tanga(J), Sahare – Tanga (J), Tanga Elite – Tanga (J) na Ebonite – Dar es Salaam;

(c) kukusanya takwimu za walimu walio kazini kwa ajili ya kuwasajili kutoka Halmashauri 22;

(d) kushiriki katika Utafiti wa Kimataifa kuhusu Ubora wa Elimu ya Msingi katika nchi 15 za Kusini na Mashariki ya Afrika *SACMEQ Research Project III* na kutuma taarifa zilizohakikiwa Makao Makuu ya SACMEQ-Paris;

(e) kutoa vibali 126 vya kujenga shule na kuthibitisha wamiliki na mameneja wa shule 118; na

(f) kutoa leseni 337 za kufundisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya mwaka 2008/2009, katika mwaka 2008/2009, kitengo cha Usajili wa Shule kitatekeleza yafuatayo:-

(a) kusajili shule zisizo za Serikali 150 ikiwemo shule ya elimu maalumu ya Njombe Viziwi;

- (b) kuchambua maombi 250 ya vibali vya kujenga shule zisizo za serikali na kuthibitisha wenyewe shule na mameneja wa shule;
- (c) kuchambua maombi ya kuanzisha/kusajili shule za sekondari zitakazojengwa kwa nguvu za wananchi;
- (d) kuchambua maombi 500 ya leseni za kufundisha;
- (e) kukusanya na kuhakiki takwimu za walimu walio kazini kwa ajili ya kuwasajili katika mikoa 5, na kusajili walimu ambaa taarifa zao zimekamilika; na
- (f) kuchambua, kuandika taarifa na kusambaza matokeo ya utafiti wa Kimataifa kuhusu ubora wa Elimu katika Nchi 15 za Kusini na Mashariki ya Afrika ('SACMEQ Research Project III').

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitengo cha Elimu kwa Redio, utekelezaji wa malengo ya mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008, Kitengo cha Elimu kwa Redio kilitekeleza yafuatayo:-

- (a) kutayarisha na kurusha hewani vipindi 52 vya Boresha Elimu, 52 vya Ufundishaji kwa njia shirikishi na 480 vya English, Maarifa ya Jamii, Kiswahili na Sayansi kwa madarasa ya V, VI na VII pamoja na Historia, Jiografia na Uraia darasa la III, IV na V;
- (b) kutoa mafunzo kuhusu utumiaji wa Mwongozo wa Elimu ya Mazingira kwa Walimu 300 na Wakaguzi 50 wa kanda za Kusini, Kati na Mashariki;
- (c) kutoa Mafunzo ya Ushauri Nasaha kwa wawezeshaji 90 wa shule za Msingi na walimu wanaishi 45 wa shule za Sekondari na Vyuo Vya Ualimu Kanda ya Ziwa na Kanda ya Magharibi;
- (d) kukusanya na kuchambua taarifa za mwitikio wa afua (intervention) za Mpango Mkakati wa Elimu ya UKIMWI na kuendelea kuandaa Sera ya Elimu ya UKIMWI mahali pa kazi;
- (e) kutoa mafunzo ya ufuatiliaji wa Programu ya UKIMWI kwa maafisaelimu na maafisa mipango 80 wa Wilaya; na
- (f) kutoa mafunzo ya ufundishaji mada za UKIMWI kwa walimu 250 wa shule za Msingi na 300 wa shule za Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya mwaka 2008/2009, katika mwaka 2008/2009, kitengo cha Elimu kwa Redio kitatekeleza yafuatayo:-

- (a) kutayarisha na kutangaza vipindi 52 vya Boresha Elimu;

- (b) kuandaa na kutangaza vipindi 52 vya ufundishaji kuhusu mbinu shirikishi;
 - (c) kuandaa na kutangaza Vipindi 528 vya masomo ya English, Sayansi, Kiswahili Darasa la V, VI na VII na Historia, Jografia na Uraia Darasa la III, IV na V na Maarifa ya Jamii Darasa VI na VII;
 - (d) kuelimisha walimu 500 na wakaguzi wa shule 50 kuhusu elimu kwa maendeleo endelevu na utumiaji wa mwongozo wa elimu ya mazingira kwa shule za msingi;
 - (e) kuchapa na kusambaza nakala 50,000 za Mwongozo wa Elimu ya Mazingira kwa shule za msingi na somo la stadi za kazi kwa shule zilizoongezeka, vyuo vya ualimu, ofisi za elimu za Wilaya na ofisi za Ukaguzi wa shule za wilaya;
 - (f) kuchapa na kusambaza nakala 100,000 za vitini vya kufundishia mada ngumu za elimu ya mazingira kwa somo la stadi za kazi;
-
- (g) kuchapisha nakala 30,000 za Mwongozo wa Utoaji wa Elimu ya Ushauri Nasaha;
 - (h) kugharamia mafunzo ya ushauri nasaha kwa wawezeshaji 200 wa shule za msingi na walimu wapya 200 wa shule za sekondari;
 - (i) kuandaa mwongozo wa elimu rika kwa shule za sekondari Kidato cha 3 na 4;
 - (j) kuchapa na kusambaza nakala 60,000 za Mpango Mkakati wa Elimu ya UKIMWI 2008/2012;
 - (k) kuchapa nakala 20,000 za sera ya utoaji wa huduma na msaada kwa wafanyakazi wa wizara; na
-
- (l) kutoa mafunzo ya elimu rika na unasihi kwa walimu wanaofundisha masomo yanayobeba mada za UKIMWI katika shule za sekondari 300.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Sera na Mipango inashughulikia upangaji, utafiti, ufuatiliaji na kutathmini utekelezaji wa mipango ya elimu ili kufikia malengo ya kutoa elimu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa malengo ya mwaka 2007/2008. katika mwaka 2007/2008, Idara ya Sera na Mipango ilitekeleza yafuatayo:-

- (a) kukamilisha Mapitio ya andiko la MMES (2004-2009) linalozingatia upanuzi wa kidato cha 5 na 6, vyuo vya ualimu ili kukidhi mahitaji ya sasa yanayotokana na mafanikio ya upanuzi wa shule za sekondari hususani kidato cha 1-4;

- (b) kufanya ufuatiliaji na tathimini kuhusu matumizi ya fedha na utoaji huduma za elimu kwa shule za sekondari 48;
- (c) kutoa mafunzo ya kompyuta kwa Maafisa Elimu Mkao 21, Maafisa Elimu Taaluma Mkao 21, Maafisa Elimu Wilaya 126, Maafisa Elimu Vifaa na Takwimu 126 na Waratibu Elimu ya Sekondari wa Wilaya 104 Aidha, Wilaya 121 zimegawiwa kompyuta na Waratibu Elimu wa Sekondari wa Wilaya 107 wamegawiwa *Laptop*;
- (d) kuendelea kufanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995;
- (e) kutoa ithibati kwa machapisho 166 yaliyoombewa kutumika shulenii;
- (f) kuratibu ukarabati wa majengo ya *shule 43 na vyuo 11* vya ualimu, ofisi za Elimu ya Watu Wazima kanda ya Mashariki, kanda ya Kati na Kituo cha Kisomo Mwanza pamoja na kuanza ujenzi wa Chuo cha Ualimu Dakawa;
- (g) kufanya ukarabati wa majengo, kununua samani na kuboresha upatikanaji wa maji safi na uondoaji wa maji taka katika shule za sekondari 12; na
- (h) kukamilisha michoro ya ujenzi wa ofisi za Wizara na kupata kibali cha Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya mwaka 2008/2009, katika mwaka 2008/2009, Idara ya Sera na Mipango itatekeleza yafuatayo:-

- (a) kufanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, Sera ya Elimu ya Juu ya mwaka 1999 na Sera ya Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya mwaka 1996;
- (b) kufanya mapitio ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari na kukamilisha maandalizi ya awamu ya pili ya mpango huo;
- (c) kufuatilia utekelezaji wa mpango wa elimu ya sekondari katika shule 228;
- (d) kuanzisha mfumo wa uhifadhi wa takwimu na taarifa za elimu katika Halmashauri;
- (e) kuendesha mikutano 6 ya EMAC na kusambaza taarifa kwa wachapishaji na wagavi wa vifaa vya elimu;
- (f) kuandaa, kuchapa na kusambaza kwa wadau katalogi ya vitabu vya elimu vilivyopata ithibati;
- (g) kutathimini na kuratibu ukarabati wa vyuo vya ualimu, shule za sekondari na maktaba;

(h) kukamilisha mdahalo wa kitaifa kuhusu wanafunzi wanaopata mimba na kubaini sababu nyingine zinazosababisha mdondoko wa wanafunzi katika shule za msingi na sekondari;

(i) kuratibu utekelezaji wa Mpango wa TEHAMA katika shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu;

(j) kuangalia upya utaratibu wa kupeleka vitabu shulen;

(k) kufanya mapitio ya Matumizi ya Fedha za Umma na Mpango wa Kati wa Matumizi ya Fedha;

(l) kuanza ujenzi wa ofisi ya wizara Dodoma;

(m) kuandaa na kuratibu vipaumbele vya utafiti katika Sekta ya Elimu;

(n) kuandaa Andiko Mradi la kujenga maabara katika shule za sekondari litakalowasilishwa kwa wadau wa maendeleo;

(o) kuandaa mkakati wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Juu na Ufundji (MMEJU) unaokusudiwa kuboresha Elimu na miundombuni ya kusomea na kufundishia katika Vyuo Vikuu vya Umma; na

(p) kuangalia upya muundo wa Idara katika Wizara ili kuanzisha kitengo cha Utafiti na Takwimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitengo cha Mawasiliano na Habari, katika kuhakikisha kuwa wadau wa Elimu wanapata na kuelewa majukumu ya Wizara ipasavyo, Wizara yangu kwa kupitia vyombo vya habari itaendelea kutoa taarifa ya majukumu, mipango, na programu mbalimbali zinazotekelzeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa malengo ya mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008, Kitengo cha Mawasiliano na Habari kilitekeleza yafuatayo:-

(a) kuratibu utoaji wa habari za elimu katika vyombo vya habari ambapo maswali 82 yamejibiwa. Aidha, hoja 56 kutoka Tovuti ya Wananchi (www.wananchi.go.tz) zimetolewa maelezo;

(b) kuandaa, kuchapa na kusambaza kwa wadau nakala 165,000 za jarida la Ed-SDP; na

(c) kuandaa na kurusha hewani vipindi 36 na matangazo 12 ya redio na televisheni kuelezea Sera na Utekelezaji wa Programu za elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya mwaka 2008/2009, katika mwaka 2008/2009, Kitengo cha Mawasiliano na Habari kitatekeleza yafuatayo:-

- (a) kuratibu utoaji wa taarifa za elimu katika vyombo nya habari ili kufahamisha jamii na wadau wa maendeleo kuhusu maendeleo ya elimu na kuhamasisha kushiriki kuendeleza elimu;
- (b) kuandaa na kurusha hewani matangazo 20 na vipindi 60 nya televisheni na redio kueleza sera na mikakati ya utekelezaji wa mipango ya elimu; na
- (c) kuandaa, kuchapa na kusambaza kwa wadau nakala 165,000 za jarida la Ed-SDP.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Utawala na Utumishi ni kiungo katika kuwezesha idara nyingine kutekeleza majukumu yake. Inasimamia ajira, maslahi na maendeleo ya watumishi. Aidha, idara inasimamia sheria, kanuni, taratibu za utumishi na uratibu wa masuala ya Programu ya Kuboresha Utumishi wa Umma katika Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa malengo ya mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008, Idara ya Utawala na Utumishi ilitekeleza yafuatayo:-

- (a) kuajiri walimu 13,235 na watumishi wasio walimu 397;
- (b) kuidhinisha maombi ya ajira za walimu 645 raia wa kigeni kwa ajili ya shule zisizo za Serikali;
- (c) kuratibu upandishwaji vyeo watumishi 11,663 ambaao wamekaa katika madaraja waliyo nayo kwa muda mrefu;
- (d) kuratibu mafunzo na kutoa vibali nya kwenda mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi 1,559;
- (e) kugharamia mafunzo ya huduma kwa Mteja kwa watumishi 487 wa Makao Makuu ya Wizara;
- (f) kutoa mafunzo ya muda mfupi kuhusu sheria, kanuni, taratibu na maslahi ya watumishi kwa wakuu wa shule na wakuu wa vyuo, wakaguzi wa shule na Waratibu wa Elimu ya Sekondari;
- (g) kuanzisha ofisi ya kuratibu malalamiko ya wateja Makao Makuu ya Wizara;
- (h) kuanzisha ofisi na kuunda Kamati zitakazoshughulika na utoaji wa huduma kwa watumishi wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI na wenye UKIMWI; na
- (i) kufanya mapitio ya fomu za OPRAS ziweze kuendana na kazi ya ualimu na kuzifanya majaribio katika shule 30 za mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya mwaka 2008/2009, katika mwaka 2008/2009, Idara ya Utawala na Utumishi itatekeleza yafuatayo:-

- (a) kufanya mapitio ya Muundo wa Utumishi wa Kada zilizo chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii wakiwemo Walimu wa Shule za Msingi, Sekondari, Vyuo vya Ualimu na Wakutubi kwa lengo la kuhuisha sifa za kuajiriwa na kupanua upeo na wigo wa ngazi za mishahara na madaraja ili kuongeza ufanisi katika kazi. Aidha, Muundo unaohusu kada za Wahadhiri wa Vyuo Vikuu pia utafanyiwa mapitio;
- (b) kuajiri watumishi wapya 9,438 kati yao walimu 8,721 na wasio walimu 717 na kuidhinisha vibali vya ajira ya wataalamu wa kigeni 700;
- (c) kuthibitisha kazini watumishi 1,000 na kuratibu upandishwaji vyeo watumishi 5,000;
- (d) kuratibu Mpango wa Mafunzo wa Wizara katika muda mrefu na mfupi kwa watumishi;
- (e) kuandaa mfumo mpya wa utunzaji kumbukumbu za watumishi kwa kutumia teknolojia mpya kwa kutumia TEHAMA na kutengeneza *Data Base*;
- (f) kuandaa mikutano miwili ya Baraza la Wafanyakazi;
- (g) kufanya mapitio ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja;
- (h) kukamilisha mchakato wa ushirikishwaji wa Sekta Binafsi (PSP) katika utoaji wa huduma za usafi, Mapokezi na Ulinzi kwa baadhi ya shule za sekondari za serikali na vyuo vya ualimu vya Kanda ya Mashariki;
- (i) kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Tathimini ya Utendaji Kazi kwa njia ya Uwazi (OPRAS) kwa watumishi wa Wizara;
- (j) kukamilisha taratibu za kiutumishi za kuwahamishia watumishi wa shule za sekondari za serikali kwenda kwenye Halmashauri;
- (k) kubuni mfumo wa kupokea na kushughulikia malalamiko ya wateja; na
- (l) kuendelea kutoa huduma na elimu kwa watumishi wanaoishi na VVU na wanaouguia UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala, Taasisi na Mabaraza yaliyo chini ya Wizara yangu yanafanikisha utoaji wa elimu bora. Kila Taasisi na Baraza limetekeliza kazi zilizopangwa kwa kuzingatia malengo na mipango ya elimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, , Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (*CDK*) kina jukumu la kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika nyanja mbalimbali kwa lengo la kutimiza azma ya serikali ya kuinua

uchumi na kuleta maendeleo. Idadi ya wanachuo wanaosoma katika Chuo Kikuu cha Dar es Salam imeongezaka kutoka 15,081 (wasichana 5,146) mwaka 2005/2006 kufikia 21,156 (wasichana 7,572) mwaka 2007/2008.

Mheshimwa Naibu Spika, utekelezaji wa malengo ya mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilitekeleza kazi zifuatazo:-

(a) kudahili jumla ya wanafunzi 7,602, kati yao 6,005 ni wa Shahada ya kwanza ambao 3,927 ni wanaume na 2,078 ni wanawake. Wanafunzi wa shahada za uzamili walikuwa 1,597 kati yao 1,198 ni wanaume na 399 ni wanawake;

(b) kuimarisha skuli ya masomo ya uzamili kwa kuongeza watendaji na vifaa vya kufanya kazi;

(c) kujenga uwezo wa kutumia teknolojia ya mawasiliano kwa wanataluma 92 ili kuboresha ufundishaji;

(d) kuajiri wanataluma 130 kujaza nafasi za kazi zilizoachwa wazi na waliostaafu au walioondoka;

(e) kudhamini mafunzo ya uzamili kwa wanataluma 130 na waendeshaji 31;

(f) kuendeleza ushirikiano na serikali na mashirika mbalimbali katika kugharamia utafiti na mafunzo;

(g) kukamilisha kwa asilimia 80 ujenzi wa kumbi 2 zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kila moja;

(h) kuendeleza ujenzi wa makao makuu mapya ya Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS) sehemu ya Buyu, Zanzibar ulioanza Machi 2006;

(i) kukamilisha kwa asilimia 60 ujenzi wa jengo la Kitivo cha Biashara na Uongozi (FCM) na Kitengo cha Ujasiriamali (UDEC); na

(j) kukamilisha awamu ya pili ya mradi wa Mlimani City kwa kujenga ukumbi wa mikutano wenyewe uwezo wa kuchukua watu 2000 na nyumba 49 za kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya mwaka 2008/2009, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kitatekeleza yafuatayo:-

(a) kudahili wanafunzi 6,500 kati yao 4,000 ni wa Shahada ya Kwanza na 2,500 wa Shahada za Uzamili;

(b) kuendeleza ushirikiano na serikali na mashirika mbalimbali katika kugharamia utafiti na mafunzo na kusambaza matokeo ya utafiti;

- (c) kuboresha ufundishaji wa Kifaransa kwa kushirikiana na serikali ya Ufaransa;
- (d) kumalizia ujenzi wa kumbi 2 za mihadhara, kuendeleza ujenzi wa jengo la Kitivo cha Biashara na Uongozi (FCM), Kitengo cha Ujasiriamali (UDEC) na majengo ya IMS sehemu ya Buyu, Zanzibar;
- (e) kufuatilia utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi wa Mlimani City;
- (f) kukarabati majengo CKD-TTCL Kijitonyama, miundombinu na mfumo wa maji sehemu ya Mlimani;
- (g) kujenga madarasa mapya kupitia Mradi wa Benki ya Dunia;
- (h) kukamilisha makabidhiano ya majengo ya Chuo cha Bima Mikocheni kwa CKD; na
- (i) kujenga duka la walaji na hoteli ya kitalii yenyeye vyumba 100 katika mradi wa '*Mlimani City*'.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Sokoine. Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kinaendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa mafunzo ya Shahada za Kwanza na za Juu, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalam katika nyanja za Kilimo, Misitu, Mifugo, Mazingira, na fani nyingine za Sayansi na Teknolojia. Idadi ya wanachuo wanaosoma katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo imeongezaka kutoka 2,286 mwaka 2005/2006 kufikia 2,880 mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa malengo ya mwaka 2007/2008. Katika mwaka wa 2007/2008 Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimetekeleza yafuatayo:-

- (a) kudahili wanafunzi 759 wa Shahada za Kwanza na 669 wa Shahada za Uzamili;
- (b) kuendeleza miradi ya utafiti 127 katika fani zitolewazo chuoni katika mikoa ya Mbeya, Iringa, Dodoma, Morogoro, Pwani, Tanga, Kilimanjaro, Manyara na Kagera;
- (c) kutoa huduma na ushauri kwa wadau 8,500 katika fani za: tiba ya mifugo, upimaji udongo, kilimo mseto, hifadhi ya mazingira na vianzio vya maji, upimaji ubora wa vyakula vya mifugo, wanyama/viumbe waharibifu na athari zake kama vile magonjwa ya tauni na namna ya kukabiliana na balaa la panya; na
- (d) kuendelea kujenga mabweni mawili yenyeye uwezo wa kuchukua wanafunzi 660 kila moja na kukarabati mabweni na madarasa katika kampasi ya Solomon Mahlangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya mwaka 2008/2009, katika mwaka 2008/2009 Chuo kitatekeleza yafuatayo:-

- (a) kudahili wanafunzi 1,300 wa Shahada za Kwanza, 700 wa Shahada za Juu na kuanzisha Shahada mpya za kwanza ambazo ni: BSc. *Information and Technology*, BSc. *Tourism and Hospitality Management*, BSc. *Education*, na BSc. *Range Management*;
- (b) kuendeleza miradi 127 ya utafiti ikiwemo 23 inayofadhiliwa na Norway (PANTIL);
- (c) kutoa mafunzo na ushauri kwa wadau 10,800 kwa njia za semina, kozi fupi, warsha na ushauri vijijini;
- (d) kujenga kumbi 4 za miadhara zenyne uwezo wa kuchukua wanafunzi 250 kila moja, maabara 3 zenyne uwezo wa kuchukua wanafunzi 60 kila moja na kukamilisha ujenzi wa mabweni 2 ya wanafunzi yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,320;
- (e) kukarabati kumbi za miadhara na madarasa yaliyopo Solomon Mahlangu na Kampasi kuu; na
- (f) kukarabati nyumba 100 za wafanyakazi, mabweni 44 (Solomon Mahlangu Kampasi 30, Kampasi kuu 12, hosteli ya Kihonda 2) na kukamilisha ukarabati wa barabara za ndani zilizopo Kampasi Kuu zenyne kilometra 3.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Dodoma. Katika mwaka 2007/2008 Bunge lako tukufu liliarifiwa kuhusu kuanzishwa kwa Chuo Kikuu Dodoma. Napenda kuliarifu Bunge lako kwamba Chuo hiki kilifunguliwa tarehe 10 Septemba, 2007 kikiwa na Skuli 4 za Elimu, Sanaa na Lugha, Sayansi za Jamii na Sayansi za Kompyuta katika jengo la Chimwaga.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa malengo ya mwaka 2007/2008. Katika mwaka wa 2007/08, Chuo Kikuu cha Dodoma kimetekeleza yafuatayo:-

- (a) kudahili wanafunzi 1,116, katika ya hao 328 ni wanawake na 788 ni wanaume;
- (b) kuendesha programu 18, katika ya hizo, 17 ni Shahada za Kwanza na 1 ni Shahada ya Uzamili;
- (c) kuajiri wahadhiri 97 na wafanyakazi waendeshaji 105; na
- (d) kuanza ujenzi wa majengo ya skuli 3 za Sanaa na Sayansi za Jamii (*Humanities and Social Sciences*), Sayansi za Kompyuta (*Informatics and Virtual Education*) na Elimu (*Education*).

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya mwaka 2008/2009, katika mwaka 2008/2009 Chuo kitatekeleza yafuatayo:-

- (a) kudahili wanafunzi 5,000 wa shahada mbalimbali;
- (b) kuanzisha vyo na skuli zifuatazo: Chuo cha Elimu, Chuo cha Sanaa na Sayansi za Jamii, Chuo cha Sayansi za Kompyuta, Habari na Mawasiliano, Skuli ya Tiba, Skuli ya Uuguzi, na Skuli ya Sayansi za Viumbe Hai;
- (c) kuendesha programu 57 za mafunzo. Kati ya hizo, mpya ni 29 za Shahada ya Kwanza, 8 za Shahada ya Uzamili na 2 za Shahada ya Uzamivu;
- (d) kuajiri wanataluma 320 kati yao 70 kutoka nje ya nchi na wafanyakazi waendeshaji 260;
- (e) kuendeleza ujenzi na ukarabati wa jengo la utawala, ofisi na barabara mzingo; na
- (f) kununua samani za mabweni na majengo mengine yaliyokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Mzumbe. Chuo Kikuu Mzumbe kinajukumu la kupata, kukuza, kuhifadhi na kusambaza maarifa na stadi za menejimenti kwa njia ya mafunzo, utafiti na huduma za kiufundi na kitaalamu. Idadi ya wanachuo wanaosoma katika Chuo Kikuu Mzumbe imeongezaka kutoka 3,210 (wasichana 1,121) mwaka 2005/2006 kufikia 3,977 (wasichana 1,656) mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa malengo ya mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008, Chuo Kikuu Mzumbe kilitekeleza yafuatayo:-

- (a) kudahili wanafunzi 1,521 kati yao 1,015 ni wa shahada ya kwanza na 506 ni wa shahada ya uzamili;
- (b) kugharamia mafunzo ya wahadhiri 27 katika ngazi ya shahada ya uzamili na 7 katika ngazi ya shahada ya uzamivu;
- (c) kuendelea kujenga mabweni yenyewe uwezo wa kuhudumia wanafunzi 400 Kampasi ya Mzumbe;
- (d) kukamilisha ujenzi wa ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 300 kampasi ya Mbeya. Ukumbi mwingine wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 300 Kampasi ya Mzumbe unaendelea kujengwa;
- (e) kukamilisha miradi 10 ya utafiti wa Sayansi ya Jamii na kuanza miradi 14 mipyä ya utafiti;
- (f) kukamilisha ukarabati wa maktaba katika Kampasi ya Mzumbe; na

(g) kuchapisha vitabu 3 na kuendelea na uandishi wa vitini 6 vya kufundishia na majarida 35.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya mwaka 2008/2009, katika mwaka 2008/2009, Chuo Kikuu Mzumbe kitatekeleza yafuatayo:

(a) kudahili wanafunzi 1,727 kati yao 1,173 ni wa shahada ya kwanza na 554 ni wa shahada za uzamili;

(b) kugharamia mafunzo ya watumishi 15 katika ngazi ya shahada za uzamivu na 22 katika ngazi ya shahada za uzamili;

(c) kukamilisha ujenzi wa bweni la wasichana lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 400;

(d) kukamilisha ujenzi wa ukumbi wa miadhara wenyewe uwezo wa kuhudumia wanafunzi 300 Kampasi Kuu;

(e) kujenga ofisi za wahadhiri zenyewe uwezo wa kuhudumia wahadhiri 100 katika Kampasi Kuu;

(f) kujenga maktaba yenye uwezo wa kuhudumia wasomaji 400 kwa wakati mmoja kwenye Kampasi ya Mbeya;

(g) kununua viwanja 3 vilivyopo Upanga kwa ajili ya upanuzi wa Kampasi ya Dar es Salaam;

(h) kukamilisha miradi 20 ya utafiti katika maeneo ya Sayansi ya Jamii; na

(i) kuchapisha vitabu 6, makala za kufundishia 6 na makala nyingine 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kina jukumu la kufundisha kwa njia ya masafa na ana kwa ana, kutafiti, kutoa ushauri wa kitaalamu na kusambaza maarifa kupitia vituo vya chuo vilivyopo mikoani. Idadi ya wanachuo walioandikishwa katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania imeongezaka kutoka 3,085 (wasichana 742) mwaka 2005 kufikia 3,749 (wasichana 996) mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa malengo ya mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kilitekeleza yafuatayo:-

(b) kudahili wanafunzi 8,262 ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya wanafunzi wanawake kufikia asilimia 37 ya wanafunzi wote;

(c) kutoa mafunzo ya shahada ya kwanza kwa walimu wa shule za msingi na sekondari 1,500;

(d) kuanzisha kituo cha Teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT), kutoa mafunzo ya teknolojia ya mawasiliano kwa wafanyakazi 200, mafunzo ya *e-Learning* kwa wafanyakazi 80 na kuanzisha shahada ya BSc. (ICT);

(e) kupata majengo ya kudumu Dodoma, Singida, Ruvuma, Njombe, Mpanda na Mara. Aidha, Chuo kimepata viwanja kwa ajili ya kujenga katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Manyara na Kigoma;

(f) kuanzisha kitengo cha ushauri wa kitaalamu;

(g) kuanza maandalizi ya ujenzi wa jengo la mitihani na maabara katika eneo la Bungo – Kibaha; na

(h) kukamilisha mtandao wa mawasiliano ya intaneti kati ya Makao Makuu na vituo vya Ilala, Temeke, Kinondoni, Iringa, Mbeya, Mtwara na Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya mwaka 2008/2009, katika mwaka 2008/2009, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kitatekeleza yafuatayo:-

- (a) kuongeza udahili wa wanafunzi hadi kufikia 10,000;
- (b) kuanza ujenzi wa ukumbi wa mitihani katika eneo la Bungo – Kibaha;
- (c) kuendelea na ukarabati wa majengo katika vituo vyote vya mikoa;
- (d) kuweka huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika vituo vya mikoa 10;
- (e) kujenga vituo katika mikoa ya Mtwara na Manyara;
- (f) kukarabati vituo katika Wilaya za Mpanda na Njombe; na
- (g) kuandaa mipango ya ujenzi wa jengo la kitivo cha Biashara na Uongozi Makao Makuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi za Afya Muhimbili. Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi za Afya Muhimbili kina jukumu la kufundisha, kutafiti, tiba na kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika maeneo ya tiba na afya. Idadi ya wanachuo wanaosoma katika Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi za Afya Muhimbili kilikuwa na wanafunzi 2,056 (wasichana 630) mwaka 2005/2006 na wanafunzi 1,431 (wasichana 374) mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa malengo ya mwaka 2007/2008. Katika mwaka wa 2007/2008 Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi za Afya Muhimbili kilitekeleza yafuatayo:-

(a) kudahili wanafunzi 268 wa Shahada ya Kwanza sawa na asilimia 76.5 ya lengo na 99 wa Shahada ya Uzamili;

(b) kupata hati miliki ya kiwanja cha chuo eneo la Mloganzila na kusawazisha barabara kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara (TANROADS);

(c) kuajiri wahadhiri 11 ili kuongeza idadi ya wahadhiri kufikia 228;

(d) kununua vitanda, meza na magodoro kwa ajili ya mabweni ya Chole; na

(e) kuendelea kufanya tafiti zinazolenga kutatua matatizo yanayohusu UKIMWI (Chanjo), Kifua Kikuu, Malaria na magonjwa ya kina mama na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya mwaka 2008/2009, katika mwaka wa 2008/2009, Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi za Afya Muhimbili kitatekeleza yafuatayo:-

(a) Kudahili wanafunzi 350 wa fani mbalimbali za tiba na afya na kuweka samani na umeme katika majengo;

(b) kuwalipa fidia wananchi wa eneo la Mloganzila, kujenga barabara na kupeleka umeme na maji katika eneo hilo;

(c) kuajiri wahadhiri 30 katika idara mbalimbali za kitaaluma zilizopo Chuoni;

(d) kujenga kantini katika hosteli za Chole, kusafisha na kujenga ukuta kuzungukia eneo la hosteli; na

(e) kukamilisha tafiti zinazoendelea na kufanya tafiti za magonjwa mengine yanayoathiri jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Ardhi. Chuo Kikuu Ardhi kina jukumu la kufundisha, kutafiti, kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika maeneo ya ardhi na usanifu wa majengo. Idadi ya wanachuo wanaosoma katika Chuo Kikuu Ardhi imeongezaka kutoka 1,194 (wasichana 182) mwaka 2005/2006 kufikia 1,602 (wasichana 281) mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa malengo ya mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008 Chuo Kikuu Ardhi kilitekeleza yafuatayo:-

(a) kudahili wanafunzi 1,472 (26 stashahada, 1,321 shahada ya kwanza na 125 wa shahada za uzamili). Hili ni ongezeko la asilimia 7.8 ya wanafunzi 1,366 waliodahiliwa mwaka wa masomo 2006/2007;

- (b) kuunda vyombo vya utawala wa Chuo ambapo Baraza la Chuo, Seneti na kamati mbalimbali za kuendesha Chuo vimeanza kufanya kazi;
- (c) kupitia sera na mipango inayoongoza uendeshaji wa Chuo ambayo iliandaliwa chini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili iendane na hadhi ya Chuo Kikuu kinachojitegemea;
- (d) kuanzisha rasmi Skuli 6 zenyenye jumla ya programu 39 za mafunzo;
- (e) kuendelea kufanya utafiti katika fani mbalimbali za kitaaluma zitolewazo chuoni. Jumla ya miradi 78 ya utafiti iliendelezwa na Jarida la shughuli za utafiti liliingizwa kwenye Tovuti ya “*Africa Journal Online*”;
- (f) kutoa ushauri wa kitaalamu kwa taasisi 50 za umma na 66 za binafsi na kuendesha mafunzo ya elimu endelevu 12 katika nyanja za kupunguza maafa, GIS, kompyuta na mazingira;
- (g) kujenga mahusiano mema na vyuo vikuu na taasisi 30 za ndani na nje ya nchi katika nyanja za kitaaluma, tafiti na huduma kwa jamii;
- (h) kukuza matumizi ya Teknolojia ya Mawasiliano kwa kufanya tathmini ya majengo yasiyo na huduma ya intaneti;
- (i) kugharamia mafunzo kwa wanataaluma 26 wa Shahada za Uzamivu na wafanyakazi waendeshaji;
- (j) kundelea kujenga ofisi, madarasa, kukarabati na kuweka samani katika baadhi ya majengo ya chuo; na
- (k) kutoa ushauri nasaha na kulipia huduma za matibabu kwa wanafunzi na wafanyakazi kwenye Hospitali za Muhimbili, Lugalo, Mwananyamala na TMJ.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya mwaka 2008/2009, katika mwaka 2008/2009, Chuo Kikuu Ardhi kitatekeleza yafuatayo:-

- (a) kuongeza idadi ya wanafunzi wa shahada za kwanza kufikia 1,520, uzamili kufikia 152 na idadi ya wanawake kufikia asilimia 30 ya wanafunzi wote;
- (b) kukamilisha zoezi la kupitia upya sera na mipango inayoongoza uendeshaji wa chuo ili iendane na hadhi ya Chuo Kikuu kinachojitegemea na kuimarisha utendaji wa Skuli na Idara za mafunzo;
- (c) kuanzisha masomo ya jioni;
- (d) kuongeza idadi ya miradi ya utafiti ili ifikie 117;
- (e) kuendelea kuweka huduma ya Intaneti katika majengo yasiyo na huduma hii ili kukuza matumizi ya Teknolojia ya mawasiliano chuoni;

(f) kuanzisha kitengo maalumu cha kitaalamu cha 'Funding Promotion and Investment' kwa lengo la kuongeza idadi ya wanafunzi wasiotegemea mikopo ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu;

(g) kukamilisha ujenzi wa jengo la miadhara, madarasa, ofisi za walimu na kuendelea na ukarabati wa mabweni, ofisi, madarasa, nyumba za wafanyakazi, barabara na njia za watembea kwa miguu na miundo msingi ya usambazaji wa maji na umeme;

(h) kugharamia mafunzo ya wahadiri 40 katika shahada mbalimbali za uzamili na wafanyakazi waendeshaji 20 kwenye ngazi mbalimbali za masomo na ujuzi; na

(i) kuajiri watumishi 81 wa kada mbalimbali sambamba na upanuzi wa programu za mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam kina jukumu la kuandaa walimu na wataalam katika fani za Ualimu na Elimu ikiwa ni mkakati wa kupunguza uhaba wa walimu katika ngazi ya Shahada kutokana na ongezeko la wanafunzi kupitia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES). Idadi ya wanachuo wanaosoma katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam imeongezaka kutoka 527 (wasichana 196) mwaka 2005/2006 kufikia 3,326 (wasichana 1,246) mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa malengo ya mwaka 2007/2008. Katika Mwaka 2007/2008 Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, kilitekeleza yafuatayo:-

(a) kudahili wanafunzi wapya 137 wa masomo ya sayansi na 1,210 wa masomo ya Sanaa na Sayansi ya Jamii. Kwa sasa chuo kina jumla ya wanafunzi 3,310;

(b) kuajiri walimu 5 wa shahada ya Uzamivu, 17 Shahada ya Uzamili na 32 Shahada ya Kwanza na wafanyakazi waendeshaji 26;

(c) kuendeleza ujenzi wa madarasa, maabara, ofisi za walimu na upanuzi wa jengo la utawala. Ujenzi wa kumbi 3 za miadhara zenyewe uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,000 kwa wakati mmoja umekaribia kukamilika. Ujenzi wa madarasa mawili ya shule ya Mazoezi umekamilika. Awamu ya kwanza ya upanuzi wa jengo la utawala imekamilika na michoro ya awali ya ujenzi wa maabara imekamilika;

(d) kutoa mafunzo maalum kwa wadahiliwa 47 wanawake wa mwaka wa kwanza kwenye fani ya sayansi;

(e) kukamilisha awamu ya kwanza ya upanuzi wa maktaba na kununua vitabu 223 vya kufundishia;

(f) kuendelea kuimarisha miundombinu na matumizi ya TEHAMA; na

(g) kushirikiana na vyuo na taasisi za ndani na nje ya nchi katika utafiti na mafunzo, hasa kwa Shahada za Uzamili na Uzamivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya mwaka 2008/2009, katika mwaka 2008/2009, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam kitakeleza yafuatayo:-

(a) kudahili wanafunzi 1,500 kati yao 150 wa fani ya sayansi;

(b) kukamilisha ujenzi wa kumbi 3 za mihadhara;

(c) kununua vifaa vya maabara na vifaa vya kufundishia na kujifunza kwa ajili ya wanafunzi wenyewe ulemavu;

(d) kununua samani za maktaba na vitabu vya kufundishia/kujifunzia;

(e) kuimarisha miundombinu ya TEHAMA;

(f) kutoa mafunzo maalumu kwa wadahiliwa wanawake kwenye fani ya sayansi kwa lengo la kuongeza wahitimu wanawake kwenye fani hiyo;

(g) kushirikiana na vyuo na taasisi za ndani na nje ya nchi katika utafiti na mafunzo, hasa kwa shahada za uzamili na uzamivu; na

(h) kujenga kituo cha afya na kutoa elimu ya jinsia, UKIMWI na ushauri nasaha kwa Jumuia ya Chuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara Moshi cha Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara Moshi kina jukumu la kufundisha, kufanya utafiti na kutoa ushauri katika nyanja za ushirika, maendeleo ya jamii, biashara, oganaizesheni na ujasiriamali. Idadi ya wanachuo wanaosoma katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara Moshi imeongezaka kutoka 866 (wasichana 255) mwaka 2005/2006 kufikia 1,374 (wasichana 429) mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara Moshi kilitekeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi 662. Kati ya hao, 154 ni wanafunzi wa Stashahada, 185 ni wanafunzi wa Stashahada ya Uzamili na 323 ni wanafunzi wa Shahada ya Kwanza;
- (b) Kuongeza idadi ya wanafunzi wa kike kwa asilima 33;
- (c) Kuboresha miundombinu ya maktaba kwa kuimarisha mtandao wa TEHAMA katika maktaba;
- (d) Kugharamia mafunzo kwa wanataaluma 12 wa Shahada ya Uzamivu na 13 wa Shahada ya Uzamili;
- (e) Kuendelea kufanya utafiti na kuimarisha ushirikiano na vyuo vyta ndani na nje ya nchi;
- (f) kuimarisha vituo vyta Ushirika vyta mikoa na kufanya ukarabati katika vituo vyta Mwanza, Tanga na Shinyanga; na
- (g) kukarabati miundombinu ya maji safi chuoni na kubadilisha matumizi ya majengo yaliyopo ili yatumike kama kumbi za kufundishia, vyumba vyta semina na ofisi za wanataaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Mwaka 2008/2009. Katika mwaka 2008/2009 Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara Moshi kitatetkileza yafuatayo:-

- (a) Kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 662 mwaka 2007/2008 hadi kufikia wanafunzi 933 mwaka 2008/2009;
- (b) kugharamia mafunzo kwa wahadhiri 20 katika kiwango cha Shahada ya Uzamivu;
- (c) kufanya utafiti, kuchapisha makala na kusambaza matokeo kwa wadau;
- (d) kuimarisha matawi ya Ushirika ya Kanda katika mikoa ya Mtwara, Iringa, Mwanza na Tanga;
- (e) kushirikiana na vyuo vyta ndani na nje ya nchi katika kufanya utafiti ili kuboresha na kuongeza kiwango cha huduma za utafiti na ushauri;
- (f) kuendelea kuchukua hatua za makusudi kushughulikia mahitaji ya jamii katika masuala mtambuka, kama jinsia, UKIMWI, mazingira, wastaafu na wenye ulemavu;
- (g) kukamilisha utekelezaji wa masharti yaliyotolewa na Kamisheni ya Vyuo Vikuu ili kukiwezesha Chuo kupanda daraja na kuwa Chuo Kikuu kamili; na

(h) kuandaa Mpango Mkakati wa Chuo kwa mwaka 2009/2010 mpaka 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kilianzishwa kwa lengo la kukabiliana na tatizo la uhaba wa walimu kufuatia kupanuka kwa elimu ya msingi na Sekondari. Aidha, Chuo kinafanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa jamii, ili kuinua ubora wa maisha ya wananchi. Idadi ya wanachuo wanaosoma katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa imeongezaka kutoka 1,006 (wasichana 283) mwaka 2005/2006 kufikia 1,084 (wasichana 453) mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2007/2008. Katika mwaka wa 2007/08, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kilitekeleza yafuatayo:

- (a) kudahili wanafunzi 814 ambapo 741 ni wa Shahada ya kwanza na 73 ni wa Stashahada;
- (b) kuandaa michoro yakinifu ya ujenzi wa ukumbi wa miadhara;
- (c) kukamilisha ukarabati wa awali wa maktaba, kituo cha afya, ofisi za wahadhiri na waendeshaji, jengo la utawala, vyumba 10 vya maabara ya sayansi na mfumo wa maji ya mvua;
- (d) kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa uzio kwenye mipaka ya Chuo; na
- (e) kuajiri wahadhiri 38 na waendeshaji 51.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Mwaka 2008/2009. Katika mwaka 2008/2009, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kitatekeleza yafuatayo:-

- (a) kudahili wanafunzi wapya 650 wa shahada ya kwanza;
- (b) kukamilisha michoro, kuanza ujenzi wa ukumbi wa miadhara na kuanza maandalizi ya ujenzi wa mabweni;
- (c) kukarabati barabara za Chuo;
- (d) kuanza maandalizi ya ujenzi wa jengo la utawala;
- (e) kuanza awamu ya pili ya ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la Chuo;
- (f) kuendelea na upanuzi wa maktaba na kununua vifaa vya maabara;
- (g) kuajiri wahadhiri 42 na waendeshaji 12;

(h) kugharamia mafunzo kwa wahadhiri 20 kwenye masomo ya Uzamili na Uzamivu; na

(i) kuendelea kuwatumia wahadhiri wa muda kujaza pengo lililopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Taasisi ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma ina jukumu la kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika masuala ya habari, mawasiliano, mahusiano ya umma, matangazo pamoja na utangazaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008 Taasisi ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma ilitekeleza yafuatayo:-

(a) kudahili wanafunzi 84 wa shahada ya kwanza;

(b) kuanzisha kituo cha televisheni;

(c) kuandaa maandiko ya utafiti wa kitaaluma na kitaalam katika nyanja mbalimbali za Uandishi wa Habari, Mawasiliano ya Umma na Matangazo; na

(d) kufanya utafiti juu ya usikivu wa Redio Mlimani.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Mwaka 2008/2009. Katika mwaka 2008/2009, Taasisi ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma itatekeleza yafuatayo:-

(a) kudahili wanafunzi 120 wa ngazi ya Shahada, 20 Stashahada ya Juu na 20 wa ngazi ya Cheti;

(b) kuanzisha mafunzo ya jioni ili kukidhi mahitaji ya waandishi walioajiriwa ambao wanataka kujiendeleta;

(c) kuendelea kukarabati maabara ya picha na televisheni ili kukidhi mahitaji ya Taasisi;

(d) kugharamia mafunzo kwa wahadhiri 4 katika Shahada ya Uzamili na 4 wa Uzamivu;

(e) kuongeza madarasa ya kufundishia kwa lengo kuongeza idadi ya wanafunzi;

(f) kujenga uzio wa chuo ili kuimarisha usalama wa mali na vifaa vya chuo; na

(g) kurusha matangazo ya televisheni baada ya taratibu kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kimeanzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 6 ya Mwaka 2005 iliyoanza kutumika tarehe 01 Oktoba, 2005 kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 433 la tarehe 23 Desemba, 2005. Chuo kina jukumu la kuendesha mafunzo katika fani za Sayansi Jamii kwa kiwango cha Cheti, Stashahada na Shahada, kuendesha Mafunzo ya Uongozi, kufanya Utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa sekta ya umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008 Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kilitekeleza yafuatayo:-

(a) kudahili wanafunzi 654 kati yao 74 wa Cheti, 361 wa Stashahada na 219 wa Shahada ya Kwanza;

(b) kuajiri wanataaluma 20 na wafanyakazi waendeshaji 14;

(c) kugharamia mafunzo kwa wanataaluma 6 na wafanyakazi waendeshaji 6;

(d) kukarabati mabweni, kumbi za mihadhara na utamaduni; na

(e) kuandaa michoro ya ujenzi wa Tawi la Chuo eneo la Bububu – Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Mwaka 2008/2009. Katika mwaka 2008/2009 Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kitatekeleza yafuatayo:-

(a) kudahili wanafunzi 90 wa Cheti, 190 wa Stashahada na 326 wa Shahada ya Kwanza;

(b) kuajiri wanataaluma 15 na wafanyakazi waendeshaji 10;

(c) kuanza kuendesha programu ya Shahada ya Kwanza ya Jinsia na Maendeleo;

(d) kugharamia mafunzo kwa wanataaluma 10 na wafanyakazi waendeshaji 10;

(e) kuanza ujenzi wa Tawi la Chuo eneo la Bububu – Zanzibar; na

(f) kuanza ukarabati wa Hosteli ya Kisota - Kigamboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Ufundı Arusha. Chuo cha Ufundı Arusha kilianzishwa mwaka 1978 chini ya Ushirikiano wa Serikali ya Tanzania na Serikali ya Shirikisho la Ujerumani (FRG). Chuo kilianza kujitegemea kisheria kufuatia tangazo la Gazeti la Serikali Na 78 la tarehe 30/03/2007. Jukumu la chuo ni kutoa mafunzo ya

ufundi katika fani za Magari, Ujenzi, Mitambo, Umeme, Barabara, Elektroniki na Mawasiliano Anga kwa kiwango cha Cheti na Stashahada. Aidha, chuo hufanya utafiti na kutoa ushauri wa Kitaalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008, Chuo cha Ufundi Arusha kilitekeleza yafuatayo:-

- (a) kudahili wanafunzi 163 katika ngazi ya Stashahada;
- (b) kugharamia mafunzo ya muda mrefu kwa walimu 10; na
- (c) kuanza ujenzi wa hosteli ya wavulana yenyewe uwezo wa kulaza wanafunzi 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Mwaka 2008/2009. Katika mwaka 2008/2009, Chuo cha Ufundi Arusha kitatekeleza yafuatayo:-

- (a) kudahili wanafunzi 180 katika ngazi ya Stashahada;
- (b) kununua na kufunga mashine mpya kwa ajili ya kuimarisha ufundishaji;
- (c) kuendeleza ujenzi wa bweni la wanafunzi;
- (d) kukarabati mabweni na nyumba za wafanyakazi;
- (e) kuandaa mitaala mipyä na kuitia mitaala iliyopo ya Stashahada kwa lengo la kuiboresha;
- (f) kufanya matayarisho ya kutoa mafunzo katika fani ya maabara ngazi ya Stashahada;
- (g) kugharamia mafunzo ya muda mrefu kwa wanataluma 17; na
- (h) kuanzisha na kuendeleza uhusiano na vyuo vingine vyä kitaaluma ndani na nje ya nchi;

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Taifa ya *UNESCO*. Tume ya Taifa ya *UNESCO* ina jukumu la kulishirikisha Taifa katika utekelezaji na uratibu wa kazi za *UNESCO* katika Nyanja za Elimu, Sayansi, Sayansi ya Jamii, Utamaduni na Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2007/08. Katika mwaka 2007/2008, Tume ya Taifa ya *UNESCO* ilitekeleza yafuatayo:-

- (a) kuratibu ushiriki wa ujumbe wa Serikali uliohusisha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na viongozi wa ngazi za juu na wataalamu mbalimbali katika kazi za *UNESCO* kwenye Kikao cha 34 cha Mkutano Mkuu wa *UNESCO* kilichofanyika tarehe 16 Oktoba hadi 03 Novemba, 2007 mjini Paris, Ufaransa;

(b) kuandaa na kuwasilisha Bungeni rasimu ya Muswada wa sheria wa kuiwezesha Tume ya Taifa kuwa chombo cha Serikali kinachojitegemea. Muswada ulisomwa na kupitishwa katika kikao cha 11 cha Bunge;

(c) kuratibu utekelezaji wa Programu ya Kuhifadhi Historia ya Ukombozi Barani Afrika kwa kushirikiana na nchi za Afrika ya Kusini, Angola, Namibia, Msumbiji, Zambia, Zimbabwe na Tanzania;

(d) kuratibu mradi unaolenga kuimarisha ubora wa mafunzo ya ualimu katika nchi zilizo Kusini mwa Sahara kwa kushirikiana na Ofisi ya UNESCO Dar es Salaam na wadau wengine;

(e) kuratibu ukamilishaji wa mkataba wa uanzishwaji wa ‘UNESCO Chair’ katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ili kukiwezesha kupata msaada wa kuanzisha kituo cha kumbukumbu katika Eneo la Historia;

(f) kuratibu utekelezaji na kufanya tathmini ya miradi inayoendelea; na

(g) kuratibu kwa kushirikiana na Kamati ya Kitaifa ya Mwaka wa Kimataifa wa Sayari Dunia katika kuandaa Mkutano wa Uzinduzi wa Mwaka wa Kimataifa wa Sayari Dunia (*International Year of Planet Earth*) Barani Afrika uliofanyika Arusha, Mei 8 - 9, 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya mwaka 2008/2009. Katika mwaka 2008/2009, Tume ya Taifa ya UNESCO itatekeleza yafuatayo:-

(a) kutathimini miradi inayoendelea na itakayoidhinishwa na UNESCO nchini na kupeleka taarifa kwa wadau;

(b) kuratibu utekelezaji wa Programu ya Kuhifadhi Historia ya Ukombozi Barani Afrika;

(c) kuratibu utekelezaji wa maamuzi yaliyofikiwa wakati wa Mkutano Mkuu wa 34 wa UNESCO;

(d) kuratibu utekelezaji wa mkataba wa uanzishwaji wa ‘UNESCO Chair’ katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA);

(e) kuratibu utekelezaji wa Programu za Mwaka wa Kimataifa wa Sayari Dunia;

(f) kuratibu utekelezaji wa makubaliano (*Memorandum of Understanding*) kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na UNESCO yaliyowekwa saini tarehe 08/05/08, Ngurdoto, Arusha;

(g) kuratibu uanzishaji wa ‘UNESCO Chair’ katika Taasisi ya Sayansi za Bahari Zanzibar, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; na

(h) kuratibu uhuishaji wa mfumo wa Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi kwa kushirikiana na UNESCO na wadau wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania. Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania ina jukumu la kutoa ithibati, kuratibu uanzishwaji wa vyuo vikuu, kuhakiki ubora wa elimu na kuidhinisha programu zifundishwazo ili zikidhi mahitaji ya taifa na soko la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008 Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania ilitekeleza yafuatayo:-

(a) kutathmini ubora wa programu 93 za masomo kutoka vyuo vikuu 10 na vyuo vikuu vishiriki 8, kati ya hizo 38 ziliidhinishwa na 55 ziko katika hatua ya marekebisho;

(b) kuelimisha umma kupitia magazeti na televisheni kuhusu majukumu ya Tume hasa tahadhari zinazohusu vyuo visivyo tambilishiwa;

(c) kuchapisha vijitabu 4 na vipeperushi vya aina 4 vinavyoelimisha umma kuhusu majukumu na ufanisi wa Tume: Annual Report 2005/2006 na 2006/2007, Kuundwa kwa Tume, *Institutional profiles, Procedures for Recognition, Registration and Accreditation of Universities*, Taratibu za kutathmini Vyeti, *Facts and Figures 2006/2007* na *Guide to Higher Education 2006/2007*;

(d) kutathimini vyeti 327 kati ya hivyo vilivyothibitishwa uhalali na kufanyiwa ulinganisho ni 263, na vyeti 6 havikutambuliwa kutohana na kukosa uhalali wa mamlaka au vyuo vilivyo tunuku vyeti hivyo. Aidha, vyeti 58 viliwasilishwa NACTE ili wavitathimini;

(e) kukagua na kufanya tathimini ya vyuo 10, kati ya hivyo, vyuo 4 vipyo vilipatiwa Hati ya Usajili wa Muda. Vyuo hivyo ni Chuo Kikuu Dodoma, *St. John’s University*, Vyuo Vikuu Vishiriki vya Tumaini vya Sebastian Kolowa na Stephano Moshi. Chuo Kikuu cha Arusha kilipata hati ya usajili kamili. Aidha, vyuo 5 viliidhinishwa hati ambazo zitatolewa baada ya kutimiza masharti;

(f) kuratibu maonesho ya *Tatu ya vyuo vikuu yaliyoongozwa na kauli mbii* ‘Maisha Bora kupitia Sayansi na Teknolojia’ yaliyofanyika katika ukumbi wa Diamond Jubilee tarehe 17-19 Aprili 2008 ambapo taasisi 55 za Elimu ya Juu nchini na nchi za jirani zilishiriki;

(g) kukamilisha rasimu ya Mfumo wa Tuzo zitakazotambulika Kitaifa (*National Qualifications Framework*). Rasimu hiyo itajadiliwa kwenye warsha ya wadau wa ubora wa elimu na mafunzo nchini;

- (h) kuhuisha ithibati ya vyuo vikuu 7 vya umma na kutoa hati idhini; na
- (i) kuratibu udahili wa wanafunzi 24,488 na hivyo kufanya jumla ya wanafunzi katika vyuo vya Elimu ya Juu kufikia 62,335.
- Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Mwaka 2008/2009. Katika mwaka 2008/2009, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania itatekeleza yafuatayo:-
- (a) kukagua vyuo vikuu vipya 2 na kuhuisha ithibati ya vyuo vikuu 14 vya binafsi vitakavyopata hati idhini mwaka 2008/2009 kwa kushirikiana na wataalam kutoka nje ya Tanzania;
- (b) kutathimini vyeti 200 vya wahitim, wahadhiri na wafanyakazi wa vyuo vikuu na kuidhinisha mitaala ya programu 100 na nyaraka/miongozo 30 toka vyuo vikuu;
- (c) kutoa mafunzo ya mbinu za kutathimini ubora wa vyuo na mitaala kwa wakaguzi 40 na kuendesha mafunzo elekezi ya kuhamasisha wadau kuhusu ubora wa Elimu ya Juu;
- (d) kuratibu maonyesho ya 4 ya vyuo vikuu na kushiriki kwenye maonyesho yanayoratibiwa na '*The Inter University Council for East Africa*' kwa vyuo vya Afrika Mashariki yatakayofanyika Kampala, Uganda;
- (e) kuratibu na kutathimini mradi wa majaribio ya udhibiti ubora wa vyuo vikuu 7 vinavyotekeliza mradi chini IUCEA;
- (f) kuchapa ripoti za ukaguzi wa nje wa vyuo vikuu vya umma;
- (g) kutayarisha na kuchapa sera, kanuni na miongozo ya kuhakiki ubora wa elimu ya juu kulingana na sheria Na. 7 ya Vyuo Vikuu;
- (h) kuanzisha mfumo wa fomu moja ya kuratibu udahili katika vyuo vya elimu ya juu ili kurahisisha udahili, kupunguza udanganyifu na kurahisisha utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu;
- (i) kutayarisha michoro na mipango ya awali ya ujenzi wa jengo la ofisi katika kiwanja cha Uporoto/Ursino, Dar es Salaam; na
- (j) kukarabati ofisi za Tume zilizopo Posta House pamoja na kununua samani na vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Elimu Tanzania. Mamlaka ya Elimu Tanzania ina jukumu la kutafuta na kubaini vyanzo mbali mbali vya mapato kwa ajili ya kugharamia maendeleo ya sekta ya elimu nchini ikiwa ni pamoja na kuhamasisha wadau wa elimu kuchangia kwa hiari katika miradi anuwai ya elimu. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuhamasika kwa wadau wa elimu kuchangia fedha taslimu

na vifaa vya kufundishia, kujifunzia na ujenzi, kuwezesha taasisi za elimu kupanua miundombinu na kuongeza udahili wa wanafunzi, kuongeza wanafunzi wa kike katika masomo ya sayansi, kuboresha kiwango cha elimu pamoja na kuwafikia wanafunzi kwa njia ya masafa na kuwezesha vyuo vya ufundu kutimiza masharti ya usajili ili kupata ithibati.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008, Mamlaka ya Elimu Tanzania ilitekeleza yafuatayo:-

- (a) kutathmini utendaji wa Mamlaka ya Elimu Tanzania toka ilipoanzishwa mwaka 2002 na kusambaza kwa wadau matokeo ya tathimini hiyo;
- (b) kupendekeza marekebisho ya Sheria No. 8 ya 2001 iliyanzisha Mfuko wa Elimu Tanzania;
- (c) kuanzisha Mifuko ya Elimu 16 na kukamilisha taratibu za Mifuko ya Elimu ya Halmashauri za wilaya za Rufiji, Babati na Bagamoyo;
- (d) kufadhili maombi ya taasisi 205 ya jumla ya shilingi 3,822,385,800 kwa ajili ya kuboresha miundombinu, kununua vitabu, vifaa vya maabara na kugharamia mafunzo maalumu kwa wanafunzi wa kike wanaochukua masomo ya sayansi ili kuwawezesha kujiunga na elimu ya juu;
- (e) kufanya mikutano na wadau ikiwa ni pamoja na TASAF, NACTE na Bodi ya Mfuko wa Elimu ya Zanzibar. Aidha, Mamlaka imeingia makubaliano mapya na Mfuko wa Elimu ya Juu Zanzibar;
- (f) kutayarisha ramani ya jengo la ofisi za Mamlaka;
- (g) kugharamia mafunzo kwa wafanyakazi 19; na
- (h) Kuandaa, kuchapa na kusambaza taarifa ya mwaka ya 2006/2007, vipeperushi na kurusha vipindi vya radio na televisheni kwa lengo la kuelezea kazi na mafaniko ya Mamlaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Mwaka 2008/2009. katika mwaka 2008/2009, Mamlaka ya Elimu Tanzania itatekeleza yafuatayo:-

- (a) kukamilisha uandaaji wa rasimu ya marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Elimu Na. 8 ya mwaka 2001 iliyanzisha Mfuko wa Elimu na Mamlaka ya Elimu Tanzania;
- (b) kutafuta rasilimali kutoka kwenye vyanzo mbali mbali vya mapato ikiwa ni pamoja na wadau wa elimu walio ndani na nje ya nchi;
- (c) kuendelea kutoa ufadhilli wa miradi ya elimu inayolenga kuongeza ubora wa elimu na kuleta usawa katika upatikanaji wa elimu katika ngazi zote;

(d) kuendeleza ushirikiano na Halmashauri zilizopo chini ya Muungano wa Serikali za Mitaa (*ALAT*) na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (*TAMISEMI*) ikiwemo mifuko ya elimu ya wilaya ili kutekeleza miradi mbali mbali ya elimu;

(e) kuendelea kuelimisha na kuhamasisha umma kupitia majorida, vipindi vya redio, televisheni na tovuti ya Mamlaka ili kuhamasisha jamii kushiriki katika kuchangia miradi ya elimu;

(f) kuendelea kufanya tathmini ya miradi ya elimu iliyofadhiliwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania ili kubaini kama malengo tarajiwa yamefikiwa;

(g) kugharamia mafunzo kwa wafanyakazi 32 wa Mamlaka kwa lengo la kuboresha mazingira ya kufanya kazi ili kuleta tija na ufanisi zaidi; na

(h) kuanza ujenzi wa jengo la ofisi za Mamlaka ya Elimu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, iliundwa kwa Sheria Na.9 ya mwaka 2004, CAP 178 na kuzinduliwa mwezi Machi 2005 na kuanza kazi rasmi mwezi Julai, 2005 kwa lengo la kutoa mikopo na kukusanya madeni ya mikopo ya wanafunzi raia wa Tanzania wa taasisi za Elimu ya Juu wanaosoma ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ilitekeleza yafuatayo:-

(a) kutoa mikopo kwa wanafunzi 55,584 kwa kutumia mfumo wa kutambua uwezo wa kiuchumi wa waombaji ambapo waombaji wamekopeshwa kwa madaraja tofauti kulingana na uhitaji wao. Madaraja hayo ni A asilimia 100, B asilimia 80, C asilimia 60, D asilimia 40, E asilimia 20 na F asilimia 0. Mikopo hii imetolewa katika maeneo ya Ada ya masomo, chakula na malazi, vitabu na viandikwa, elimu kwa vitendo, mahitaji maalumu ya vitendo na utafiti;

(b) kuajiri watumishi 39 ili kuimarisha utendaji kazi;

(c) kuboresha taarifa za wanufaika wa mikopo toka mwaka 1994. Hadi sasa Bodi imewasiliana na waajiri 468 ambao wamewezesha wadaiwa 9,424 kati ya 113,240 kutambuliwa. Aidha kiasi kilichokusanywa hadi mwezi Mei, 2008 ni shilingi 716,617,882.83 sawa na asilimia 59.7 ya lengo la makusanyo kwa mwaka 2007/2008;

(d) kuendelea kutoa elimu kwa wadau wa mikopo, wanafunzi na umma kwa ujumla kuhusu dhana ya uchangiaji gharama za elimu ya juu, taratibu za uombaji wa mikopo, vigezo vya mikopo pamoja na taratibu za urejeshaji mikopo kupitia redio,

televisi, magazeti pamoja na kuzindua kampeni ya kitaifa ya urejeshaji mikopo iliyofanyika mwezi Agosti, 2007 katika viwanja vya Bunge mjini Dodoma;

(e) kutoa kipaumbele kwa wanafunzi wa masomo ya Sayansi, Ualimu, Kilimo, Uhndisi, Afya na Tiba ya mifugo waliopata udahili katika taasisi za Elimu ya Juu bila kujali kama wana daraja la kwanza au la pili;

(f) kugharamia mafunzo kwa watumishi 21 na kununua vitendea kazi mbalimbali vya ofisi; na

(g) kuweka mtandao wa *Internet (Local Area Network)* kwa lengo la kuboresha mfumo wa kushughulikia Mikopo (*Loan Management System*) kufanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya Mwaka 2008/2009. Katika mwaka 2008/2009, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu itatekeleza yafuatayo:-

(a) kuendelea kuahikiki taarifa zinazotolewa na waombaji mkopo kwa kutumia vyombo vya serikali katika ngazi zote;

(b) kutoa mikopo kwa wanafunzi 57,619 waliopo kwenye taasisi za Elimu ya Juu katika viwango kati ya asilimia 0 na 100 kulingana na uwezo wa kiuchumi wa kila mwombaji katika ada, mafunzo kwa vitendo na mahitaji maalum ya vitivo;

(c) kukusanya madeni ya shilingi bilioni 5.1 kutoka kwa waliokopa kuanzia mwaka 1994/1995 kwa kutumia wakala wa ukusanyaji madeni;

(d) kuendelea kuelimisha umma kuhusu dhana ya uchangiaji gharama za Elimu ya Juu, taratibu za utoaji na urejeshaji mikopo;

(e) kuendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji wa elimu wanaostahili katika maeneo yafuatayo: ada ya mafunzo, chakula na malazi, vitabu na viandikwa, mafunzo kwa vitendo, mahitaji maalumu ya vitivo, na Utafiti.

(f) kuongeza kiwango cha mikopo kwa ajili ya fedha za mafunzo kwa vitendo kutoka shilingi 6,000 hadi 10,000 kwa siku kwa mwanafunzi;

(g) kutoa mikopo kwa ajili ya mafunzo ya Shahada za Uzamili na Uzamivu ndani ya nchi kwa wahadhili wahitaji wanaofundisha kwenye Vyuo Vikuu vya Umma; na

(h) kufanya upembuzi yakinifu juu ya kuanzisha kwa awamu ofisi za kanda za Bodi ya Mikopo kwa lengo la kupeleka huduma zake karibu na walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufund. Baraza la Taifa la Elimu ya Ufund lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 9 ya mwaka 1997 ili kusimamia

na kuratibu mitaala, ubora wa mafunzo, mitihani, tuzo, usajili na ithibati za vyuo vya elimu ya ufundi nchini:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008 Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi lilitekeleza yafuatayo:-

- (a) kukagua vyuo 26 kati ya hivyo vyuo 10 vimepata usajili kamili, vyuo 11 usajili wa muda na vyuo 5 usajili wa awali;
- (b) kukagua vyuo 19 kwa ajili ya ithibati; kati ya hivyo, vyuo 9 vimepewa ithibati kamili, vyuo 6 ithibati ya muda na vyuo 3 vimeelekezwa kurekebisha mapungufu yaliyoonekana;
- (c) kuandaa na kuidhinisha mitaala kwa programu 25 za mafunzo;
- (d) kusimamia na kuwezesha vyuo 30 kuweka mfumo wa kudhibiti na kuhakiki ubora wa elimu na mafunzo ya ufundi;
- (e) kuratibu mitihani katika vyuo 20 ambavyo vinatumia mitaala ya '*National Technical Awards*' ambayo inazingatia umahiri wa wanafunzi. Aidha, Baraza limeratibu mitihani ya Stashahada ya Juu ya Uhndisi kwa kushirikiana na Baraza la Mitihani;
- (f) kuratibu udahili wa wanafunzi katika vyuo 15 vinavyotoa elimu ya juu ya ufundi; na
- (g) kuhakiki sifa za walimu katika vyuo 50 vya ufundi na kusajili walimu 484, kati yao walimu 328 wamepata usajili kamili na 156 usajili muda. Aidha, Baraza limeweka mfumo wa kumbukumbu wa taarifa mbalimbali za walimu kwa njia ya kompyuta (*database*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya Mwaka 2008/2009. Mwaka 2008/2009, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi litatekeleza yafuatayo:

- (a) kukagua na kutathimini vyuo vya ufundi 20 kwa ajili ya kutoa ithibati;
- (b) kuhakiki utekelezaji wa masharti ya ithibati katika vyuo vya ufundi 15 vyenye ithibati kamili;
- (c) kusajili vyuo 20 vyenye uwezo wa kuendesha mafunzo;
- (d) kuratibu na kuidhinisha mitaala yenyе kuzingatia mahitaji ya soko la ajira na umahiri wa mwanafunzi kwa programu 25 za mafunzo;
- (e) kuratibu mitihani ya ufundi katika vyuo 20 ambavyo vimeanza kutumia mitaala mipyä inayozingatia mahitaji ya soko la ajira na umahiri wa mwanafunzi;

- (f) kusajili walimu 500 wenyе sifa za kufundisha katika vyuo vya ufundi;
- (g) kusimamia na kuvizvezesha vyuo 30 vya ufundi kuweka mfumo wa kudhibiti na kuhakiki ubora wa mafunzo yatolewayo na vyuo hivyo;
- (h) kuratibu mafunzo yanayohusu ufundishaji katika mfumo wa *Competence Based Education and Training CBET* kwa walimu katika vyuo 15 vya ufundi;
- (i) kuratibu udahili wa wanafunzi katika vyuo 15 vinavyotoa elimu ya ufundi; na
- (j) kuimarisha ushirikiano na baadhi ya taasisi za ndani na nje ya nchi zilizo na majukumu yanayofanana na ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu. Katika kutekeleza azma ya serikali ya kuboresha uendeshaji wa Elimu nchini, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (*ADEM*) hutoa mafunzo kwa viongozi mbalimbali katika ngazi ya shule, vyuo na taasisi za elimu na kufanya utafiti, kutoa ushauri na huduma za kitaalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu ilitekeleza yafuatayo:-

- (a) kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uongozi wa Elimu kwa washiriki 272 ambapo wanachuo 148 walihitimu na 124 wanaendelea na mafunzo;
- (b) kutoa mafunzo ya uongozi kwa Maafisa Elimu Vifaa na Takwimu na Maafisa Elimu Taaluma 142 kati ya 180 kutoka mikoa ya Shinyanga, Tanga, Mtwara, Iringa na Mwanza;
- (c) kutoa mafunzo ya Ukaguzi kwa Wakaguzi wa Shule wapya 53 kutoka wilaya mbalimbali;
- (d) kutoa mafunzo ya awali ya Uongozi wa Elimu kwa Wakuu wa shule za sekondari wapya 550 kati ya walengwa 670;
- (e) kutoa mafunzo ya muda mfupi ya Uongozi wa Elimu kwa Wakuu 201 wa Shule za Sekondari;
- (f) kutoa mafunzo ya Uongozi wa Elimu kwa Waratibu Elimu Kata 802 kati ya 1,490 waliokusudiwa;
- (g) kutoa mafunzo ya Uongozi wa Elimu ngazi ya cheti kwa Walimu Wakuu wa shule za Msingi 81 kati ya 300;

(h) kutoa mafunzo ya Uongozi wa Elimu kwa Waratibu Elimu ya Sekondari 111;

(i) kutoa mafunzo kwa Watekelezaji na Wasimamizi 2,228 wa Mipango ya Maendeleo ya Elimu (MMEM na MMES) kutoka Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji pamoja na Mikoa; na

(j) kufanya tafiti 4 za uongozi na uboreshaji wa taasisi za elimu kwa ushirikiano na nchi za Malawi, Uganda na Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya Mwaka 2008/2009. Katika mwaka 2008/2009, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu utatekeleza kazi zifuatazo:-

(a) kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uongozi wa Elimu kwa washiriki 300 kutoka ngazi mbalimbali za Elimu;

(b) kutoa Mafunzo ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Maafisaelimu Taaluma na Maafisaelimu Vifaa na Takwimu 80 kwa kushirikiana na JICA;

(c) kutoa mafunzo ya Uongozi wa Elimu kwa Waratibu wa Elimu ya Sekondari wa Wilaya 124; Wakuu wa Vyuo vya VETA 150; Waratibu Elimu Kata 723; Wakuu wa Vyuo vya Ualimu na Wasaidizi wao 68; Wakaguzi wa shule wapya 100; Wakuu wa Shule 1,000 na Timu za Menejimenti za Shule za Sekondari kwa washiriki 1,800;

(d) kutoa mafunzo ya Cheti cha Uongozi kwa walimu wakuu wa shule za msingi 200 kuititia vyuo vya ualimu; na

(e) kugharamia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa Wafanyakazi 5 wa Wakala katika vyuo vya ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima. Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima hutoa mafunzo kwa wataalamu wa Elimu ya Watu Wazima na Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Cheti, Stashahada na Stashahada ya Juu na kufanya utafiti, kutoa ushauri na huduma za kitaalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ilitekeleza yafuatayo:-

(a) kutoa mafunzo kwa wanafunzi 757 wakiwemo wa Stashahada ya Juu 284, Stashahada 272 na Cheti cha Sheria 201;

(b) kutoa elimu ya sekondari kwa wanafunzi 9,492 kwa njia ya Ana kwa Ana na Elimu Masafa na kutathimini maendeleo ya utekelezaji wa programu ya Elimu Masafa katika mikoa 21;

(c) kurekebisha na kuandaa Mihutasari ya masomo ya *English / Communication Skills, Mathematics, Life Skills, Accountancy, Marketing, Entrepreneurship, Electrical Installation na Motor Vehicle Mechanics*;

(d) kutoa elimu ya UKIMWI kwa wafanyakazi 137 wa makao makuu ambapo 88 walipima na kupokea majibu;

(e) kuendesha mafunzo ya kujenga uwezo wa uratibu, usimamizi na menejimenti ya vituo vya MEMKWA na MUKEJA kwa Waratibu Elimu Kata na walimu wakuu wa shule za Msingi kwa walengwa 480 katika mikoa 8;

(f) kugharamia mafunzo ya watumishi katika Shahada ya Uzamivu 2, Shahada ya Uzamili 8, Stashahada ya Juu 1, Cheti 2 na Mafunzo ya kitaaluma ya muda mfupi 147;

(g) kununua majengo katika mikoa ya Ruvuma na Kilimanjaro, kwa ajili ya ofisi, kukarabati majengo WAMO- Morogoro na Mbeya na kujenga uzio katika kiwanja cha ofisi ya TEWW mkoa wa Rukwa;

(h) kufanya tathmini ya awali ya kufunga mtandao wa intaneti katika vituo vya Mwanza, Ruvuma, Arusha, Dodoma na Mbeya ili kuboresha mfumo wa kuhifadhi, kutunza na kutumia taarifa na takwimu za elimu; na

(i) kuajiri wafanyakazi wapya 47 na kununua magari 3 kwa vituo vya Mbeya, Tanga, na Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya Mwaka 2008/2009. Katika mwaka 2008/2009, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima itatekeleza yafuatayo:-

(a) kudahili wanafunzi wa Stashahada ya Juu 266, Stashahada 344, Cheti cha Elimu ya Watu Wazima na Maendeleo ya Jamii 30 na Cheti cha Sheria 260;

(b) kutoa Elimu Masafa na Ana kwa Ana kwa wanafunzi 31,520 kiwango cha elimu ya sekondari;

(c) kuandaa na kuchapa moduli za masomo ya Ufundis, Biashara, A-level na Utangulizi;

(d) kutoa elimu ya UKIMWI kwa wafanyakazi na wanafunzi wa TEWW;

(e) kuendesha mafunzo ya uratibu, usimamizi na menejimenti ya vituo vya MEMKWA na MUKEJA katika mikoa 21;

(f) kugharamia mafunzo kwa watumishi ngazi ya Shahada ya Uzamivu 3, Shahada ya Uzamili 12, Stashahada ya Juu 1, Cheti 2, elimu ya sekondari 20 na mafunzo ya muda mfupi 60;

- (g) kuajiri watumishi 39 wa kada mbalimbali na kununua magari 5;
- (h) kukarabati majengo ya Makao Makuu Dar es Salaam, Dodoma, Kilimanjaro na Ruvuma;
- (i) kufanya utafiti mdogo kuhusu Wanawake na Uongozi kwa ajili ya uandishi wa kitabu cha Sauti ya Wanawake Na.6;
- (j) kuandaa Mtaala wa Mpango wa Elimu ya Sekondari kwa Walioikosa (MESKWA) utakaofanyiwa majoribio katika wilaya 7 za Temeke, Hai, Siha, Bagamoyo, Makete, Mtwara (V) na Magu; na
- (k) kuandaa, kuchapa na kusambaza majorida ya *Studies in Adult Education (SAED)* Na. 65, *Journal of Adult Education in Tanzania (JAET)* Na. 17 na *Alumni Newsletter*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Elimu Tanzania. Taasisi ya Elimu Tanzania inajukumu la kubuni, kuandaa, kukuza na kuimarisha programu, mitaala na mihtasari ya elimu ya awali, msingi, sekondari, ualimu na elimu maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008, Taasisi ya Elimu Tanzania ilitekeleza yafuatayo:-

- (a) kurekebisha mtaala na kuandika mihtasari ya ualimu ngazi ya cheti ili iendane na mabadiliko ya mitaala;
- (b) kubuni na kuandaa mtaala wa mafunzo ya ualimu unaotumia teknolojia ya kisasa (*e-learning*);
- (c) kufanya utafiti kuhusu hali na matumizi ya maabara na ufundishaji wa masomo ya sayansi kwa vitendo katika shule za sekondari;
- (d) kufanya uchambuzi yakinifu wa ujenzi wa kituo cha kutolea mafunzo kwa walimu na wadau wa elimu katika kiwanja cha Mikocheni;
- (e) kutoa mafunzo ya wawezeshaji 100 wa kitaifa wakiwemo wakuu wa vyuo na wakufunzi wa vyuo vya ualimu vinavyotoa Stashahada;
- (f) kuanzisha mfumo wa kompyuta katika kitengo cha rasilimali watu na maktaba;
- (g) kutoa mafunzo kwa wafanyakazi 20 ili kuinua viwango vyao vya taaluma na kununua gari moja kwa lengo la kuboresha ufanisi; na
- (h) kununua vifaa vya elimu maalum kwa ajili ya kuwajengea uwezo walimu wawezeshaji wa kitaifa wa Elimu; na

(i) kutayarisha miongozo ya kufundishia elimu ya UKIMWI kwa shule za Sekondari na kufanya majoribio ya miongozo ya Elimu ya Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya Mwaka 2008/2009. Katika mwaka 2008/2009, Taasisi ya Elimu Tanzania itatekeleza yafuatayo:-

(a) kuandaa Mwongozo wa Taifa wa Mitaala na kufanya tathmini ya mitaala kwa kupata maoni kuititia mikutano 15 ya majopo ya masomo;

(b) kurekebisha mihtasari ya ualimu ngazi ya cheti ili iendane na mabadiliko ya mitaala, kufuatalia utekelezaji wa mitaala kwa shule za msingi na sekondari na kuboresha mitaala ya kidato 5-6;

(c) kuchapisha miongozo 17 ya walimu ya kufundishia na kujifunzia masomo ya kidato cha 1-4 na kuandaa miongozo ya kufundishia masomo ya kidato cha 5 na 6;

(d) kuandaa chati za masomo ya sayansi darasa la 5-7 kwa shule za msingi;

(e) kuandaa mtaala wa mafunzo ya ualimu unaotumia teknolojia ya kisasa (*e-learning*);

(f) kukamilisha mwongozo wa kuandaa mihtasari ya kufundishia elimu ya dini;

(g) kuandaa vivunge vya masomo ya Sayansi, Stadi za Kazi na Hisabati kwa Shule za Msingi;

(h) kurekebisha, kuchapa na kusambaza mtaala wa MEMKWA kwa kundi rika la pili;

(i) kugharamia mafunzo kwa wafanyakazi 45 ili kuinua viwango vyao vya taaluma;

(j) kujenga kituo cha kutolea mafunzo kwa walimu na kukarabati jengo la taaluma;

(k) kutathmini njia za kufundishia na kujifunzia zitumikazo katika shule na vyuo vya ualimu;

(l) kuendesha mafunzo kwa walimu wawezeshaji wa kitaifa 400 wa shule za msingi na sekondari kuhusu ufundishaji wa masomo mbalimbali;

(m) kuandaa mafunzo maalum ya kubuni, kukuza na kurekebisha mitaala na utekelezaji wake;

(n) kuendesha mkutano wa kimataifa wa ESACO; na

(o) kuendesha semina za kuwahisisha (*Sensitize*) wafanyakazi kuhusu VVU/UKIMWI na madhara yake ili kubaini waathirika na kutoa huduma zinazohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania. Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania inajukumu la Kutoa na kusambaza huduma za Maktaba kwa watu wote nchini, kuanzisha, kuendesha, kuongoza, kuboresha, kutunza na kuendeleza Maktaba za Umma kuanzia ngazi za Mikoa, Wilaya hadi Vijiji na kutoa mafunzo na kuendesha mitihani ya Taaluma ya Ukutubi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008 Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania imetekeleza kazi zifuatazo:-

- (a) kununua vitabu 35,850, magazeti na majarida 39,108;
 - (b) kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa madarasa, ofisi za utawala, bwalo, viwanja vya michezo, miundombinu ya maji na umeme katika Chuo cha Bagamoyo - *School of Library, Archives and Documentation Studies (SLADS)*;
 - (c) kuendelea na ujenzi wa madarasa 2 ya mafunzo ya cheti;
 - (d) kununua kompyuta na luninga Maktaba kuu;
 - (e) kusambaza vitabu 11,812 vya watoto;
 - (f) kutoa vipindi vya watoto na kazi za mikono katika vituo vyote
 - (g) kununua mashine 2 za kuandikia nukta nundu (Braille), vibao 4 na *styllus* 4;
 - (h) kuendesha Tamasha la vitabu katika vituo 19 vya huduma;
 - (i) kufanya mahema ya kusomea ya Jumuiya katika vituo 2 vya Hombolo na Dodoma;
 - (j) Vitabu 722 vilinunuliwa kwa ajili ya Tamasha na mahema na
 - (k) kuanza ukarabati wa jengo la maktaba ya Tanga.
- Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya Mwaka 2008/2009. Katika mwaka 2008/2009, Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania itatekeleza yafuatayo:-
- (a) kuimarisha na kuboresha huduma za Maktaba katika mikoa 19 ikiwa ni pamoja na kuongeza machapisho 50,000;

- (b) kuanzisha matumizi ya teknolojia ya kisasa ya utoaji habari kwa kufunga mtandao katika vituo vya Dar es Salaam, Dodoma na Morogoro;
- (c) kuendeleza ujenzi na kuimarisha Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka, Bagamoyo;
- (d) kutoa mafunzo ya cheti, stashahada na mafunzo mafupi kwa wafanyakazi wa Maktaba nchini;
- (e) kukarabati majengo ya maktaba katika mikoa ya Tanga, Morogoro na Mbeya na kuweka uzio kwenye kiwanja cha maktaba ya Dodoma;
- (f) kuhamasisha wananchi katika mikoa 21 ili wajenge utamaduni wa kusoma;
- (g) kuimarisha huduma za Maktaba za watoto katika mikoa ya Mtwara, Tabora na Ruvuma; na
- (h) kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya uanzishaji, upangaji na uendelezaji wa maktaba za shule, vyuo na taasisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Maendeleo Dakawa. Kituo cha Maendeleo Dakawa kilianzishwa mwaka 1982 na Chama cha *African National Congress* cha Afrika Kusini na kilikabidhiwa kwa Serikali ya Tanzania kama kumbukumbu ya Urafiki na Mshikamano kati ya ANC na watu wa Tanzania mwaka 1992 na kuendeshwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundsi ilikabidhiwa uendeshaji na Uendelezaji wa Kituo hiki kuanzia mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008 Kituo cha Maendeleo Dakawa kilitekeleza kazi zifuatazo:-

- (a) kuratibu makabidhiano ya kituo kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kwenda Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundsi;
- (b) kuratibu shughuli za asasi zilizomo ndani ya kituo;
- (c) kuandaa Mpango Mkakati wa Uendelezaji wa Kituo;
- (d) kukarabati visima vya maji, pampu za maji, matanki ya maji, bomba kuu na barabara ya kuingia kituoni; na
- (e) kusimamia ujenzi wa chuo cha ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya Mwaka 2008/2009. Katika mwaka 2008/2009, Kituo cha Maendeleo Dakawa kitatekeleza yafuatayo:-

- (a) kuratibu utekelezaji wa Mpango Mkakati wa kuendeleza kituo;
- (b) kuratibu uanzishaji na uendeshaji wa Chuo cha Walimu wa Stashahada wa mchepuo wa Sayansi; na
- (c) kuendelea na ukarabati wa miundombinu ya kituo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Mitihani la Tanzania. Baraza la Mitihani la Tanzania lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 21 ya mwaka 1973 na rekebisho lake Na. 4 la mwaka 1987 na Na. 2 la mwaka 1998. Baraza lina mamlaka ya kuendesha Mitihani ya Kumaliza Elimu ya Msingi, kuendesha na kutunuku vyeti vya Elimu ya Sekondari, Cheti na Stashahada ya Ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008, Baraza la Mitihani la Tanzania lilitakeleza yafuatayo:-

- (a) kuendesha Mitihani ya Kumaliza Elimu ya Msingi, Maarifa, Kidato cha 4, Kidato cha 6, Ualimu Daraja A, Stashahada ya Ualimu na Ufundu. Aidha, mitihani yote ya Kitaifa iliendeshwa kwa amani na utulivu bila kuwako uvujaji. Yalibainika matukio machache ya udanganyifu kwenye baadhi ya vituo na hatua zilichukuliwa kwa wahusika kwa mujibu wa sheria na kanuni za uendeshaji wa mitihani.
- (b) kusimamia mitihani ya nje ya nchi kwa niaba ya taasisi za Uingereza zifuatazo: Chuo Kikuu cha London, *Lincolnshire Institute of Purchasing and Supply, Chartered Institute of Marketing, The Royal Institute of Chartered Surveyors, The Institute of Chartered Secretaries and Administrators, Association of Chartered Certified Accountants, The Association of International Accountants, The Institute of Chartered Shipbrokers na London Association Board of Royal School of Music*;
- (c) kukamilisha upanuzi wa jengo la Kitengo cha Chapa na Uchapishaji na kununua mashine kwa ajili ya kuimarisha uchapaji wa mitihani ya taifa;
- (d) kuandaa fomati mpya ya Mitihani ya Kidato cha 4 kwa kuzingatia mabadiliko ya mtaala yaliyofanyika mwaka 2005;
- (e) kuandaa Mpango kamambe kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za Baraza la Mitihani la Tanzania - Zanzibar;
- (f) kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Usahihishaji Mitihani, “Mbezi Wani”; na;
- (g) kutoa mafunzo yenye lengo la kupunguza maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI na UKIMWI kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya Mwaka 2008/2009. Katika mwaka 2008/2009, Baraza la Mitihani la Tanzania litatekeleza yafuatayo:-

- (a) kufanya utafiti, tathimini na usanifu ili kuboresha uendeshaji wa mitihani ya Kitaifa;
 - (b) kuendesha Mitihani ya Kumaliza Elimu ya Msingi, Maarifa, Kidato cha 4, Kidato cha 6, Ualimu Daraja A, Stashahada ya Ualimu na Ufundu;
 - (c) kusimamia Mitihani inayotolewa na bodi za nchi za Nje inayofanywa na watahiniwa binafsi hapa nchini;
 - (d) kuandaa mfumo wa uchambuzi wa taarifa za Mitihani inayoendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania na kuweka mitambo maalumu (CCTV) ya uangalizi katika maeneo nyeti ya Baraza la Mitihani;
 - (e) kununua magari 5 kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usambazaji Mitihani na ufuatiliaji wa shughuli za Mitihani;
 - (f) kukamilisha ukarabati wa majengo ya ofisi za Baraza la Mitihani na michoro ya ujenzi wa ofisi za Baraza Zanzibar;
-
- (g) kuanza ujenzi wa jengo la ofisi makao makuu kwa lengo la kuongeza nafasi ya kufanya kazi kutokana na ongezeko la watahiniwa na vituo vya mitihani;
 - (h) kukamilisha ujenzi wa kituo cha kusahihishia mitihani cha Mbezi Wani;
 - (i) kununua vitendea kazi vya kisasa kwa lengo la kuongeza ufanisi katika uendeshaji mitihani; na
-
- (j) kutoa mafunzo yenyenye lengo la kupunguza maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI pamoja na kubaini na kuwahudumia wafanyakazi wenyewe maambukizi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi. Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi (VETA) imeanzishwa chini ya Sheria ya Bunge Na 1 ya mwaka 1994 kwa lengo la kuratibu, kudhibiti, kugharimia, kutoa na kukuza elimu na mafunzo ya ufundu stadi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Malengo ya mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi imetekeliza yafuatayo:-

- (a) kukamilisha Andiko la Mradi wa Ujenzi wa Vyuo vya ufundu stadi vya Wilaya na kuandaa Programu ya Utekelezaji;
- (b) kutathmini ajira kwa wahitimu wa mafunzo ya ufundu stadi ili kupima ubora wa mafunzo yanayotolewa;

(c) kufunga vifaa vipya vya kufundishia kwa ajili ya vyuo vya VETA vya Kagera, Mara, Songea, Mikumi, Oljoro na Dakawa. Aidha, kuendelea kujenga na kukarabati vyuo vya Shinyanga, Mpanda, Tabora, Arusha, Singida na Ulyankulu;

(d) kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa vyuo vipya vya Lindi, Pwani, Manyara, na Dar es Salaam;

(e) kutoa ruzuku ya shilingi 465,137,450 kwa vyuo na asasi zisizo za Serikali ili viongeze ubora na nafasi za mafunzo ya ufundi stadi na kujenga uwezo wa walimu;

(f) kutoa mafunzo ya taaluma za ufundi kwa walimu 66 na mafunzo ya ualimu kwa walimu 197 kwa lengo la kuboresha mafunzo yatolewayo katika vyuo vya ufundi stadi. Aidha, walimu 23 walipatiwa mafunzo ya ujasiriamali na kuimarishe mitaala;

(g) kukamilisha utaratibu wa kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa waajiri wanaolipa '*Skills and Development Levy*';

(h) kuandaa kwa kushirikiana na NACTE utaratibu utakaowezesha wahitimu wa mafunzo ya Ufund Stadi kuendelea na elimu na mafunzo ya juu ya ufundi;

(i) Kutoa mafunzo ya ufundi stadi ya muda mrefu na mfupi katika vyuo vya VETA kwa vijana 24,055 kati yao wasichana ni asilimia 35. Aidha, vijana 168 wenye ulemavu wamepatiwa mafunzo ya ufundi katika stadi mbali mbali;

(j) kuratibu mafunzo ya ufundi stadi kwa vijana 96,589 (asilimia 47 ni wasichana) katika vyuo vya ufundi stadi visiviyomilikiwa na VETA;

(k) kuendelea kuboresha mitaala ya fani za magari na ujenzi; na

(l) kuendesha mitihani ya Ufund Stadi na Biashara kwa washiriki 25,336 (475 walitoka Zanzibar) ambapo asilimia 74 walifaalu. Aidha, washiriki 9,430 (79 walitoka Zanzibar) walifanya mitihani katika utaratibu mpya (*Competence Based Assessment*) ambapo asilimia 85 walifaalu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya Mwaka 2008/2009. Katika mwaka 2008/2009, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufund Stadi itatekeleza yafuatayo:-

(a) kuongeza fani na nafasi za mafunzo ya ufundi stadi kwa kuzingatia mahitaji ya Taifa pamoja na kuongeza uwiano wa kijinsia;

(b) kuendelea kutoa madaraka zaidi ya upangaji na utoaji wa mafunzo ya ufundisti stadi katika ngazi ya Kanda na Vyuo ili kuongeza ufanisi na kuyafanya mafunzo yanayotolewa yalingane na mahitaji halisi ya kanda husika;

(c) kuboresha karakana za mafunzo kwa vitendo na kuongeza vifaa vya kufundishia na kujifunzia ili mafunzo yatolewayo yaendane na mabadiliko ya teknolojia;

(d) kuendeleza, kukuza na kurekebisha mitaala ya masomo ya ufundisti stadi kulingana na mahitaji ya soko la ajira;

(e) kukamilisha ukarabati wa vyuo vya Shinyanga, Mpanda, Tabora na Ulyankulu pamoja na ujenzi wa vyuo vipyta vya Arusha na Singida;

(f) kuanza ujenzi wa vyuo vya Lindi, Pwani, Manyara na Dar es Salaam;

(g) kutoa ruzuku kwa vyuo vya ufundisti stadi vya asasi zisizo za serikali ili kuongeza idadi ya wanachuo na kuboresha mafunzo;

(h) kuongeza nafasi na kutoa mafunzo ya ualimu wa ufundisti stadi kulingana na mahitaji;

(i) kuwezesha vyuo vya ufundisti stadi kutoa mafunzo ya ngazi I, II, III na kuandaa *Bridging Course* kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundisti kwa lengo la kuwezesha wahitimu wa ngazi ya III kuendelea na mafunzo ya ngazi ya IV ambayo yatatolewa katika Vyuo vya Ufundisti Stadi vya Mikoa;

(j) kutekeleza utaratibu wa kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa waajiri wanaolipa *Skills and Development Levy*; na

(k) kuhuishaa Corporate Plan ya VETA ili kuendana na malengo mapya ikiwa ni pamoja na kuwezesha vyuo vya ufundisti stadi kutoa mafunzo ya ngazi ya I, II na III ili wahitimu wa ngazi ya III waweze kuendelea na mafunzo ya ngazi ya IV katika Vyuo vya Ufundisti Stadi vya Mikoa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Changamoto. katika kutekeleza malengo, mipango na programu mbalimbali za elimu zilizopangwa, Wizara yangu kwa mwaka 2008/2009 itaendelea kukabiliana na changamoto zifuatazo:-

(a) mahitaji makubwa ya madarasa, nyumba za walimu, hosteli, mabweni, maktaba, karakana, kumbi za miadhara na majengo ya utawala katika shule, vyuo vya ualimu na vyuo vikuu;

(b) upungufu wa maabara, wataalamu wa maabara (*laboratory technicians*) na walimu wa TEHAMA katika shule za sekondari, vyuo vya ualimu na vyuo vikuu;

- (c) uchache wa walimu na wahadhiri katika shule za msingi, sekondari, vyuo vya ualimu na vyuo vikuu;
- (d) uchakavu wa miundombinu katika vyuo vya ualimu na vyuo vikuu;
- (e) shule nyingi kuwa katika mazingira magumu na kufanya watumishi kutopenda kufanya kazi katika maeneo hayo;
- (f) kushuka kwa nidhamu ya wanafunzi katika shule na vyuo;
- (g) uelewa mdogo wa lugha ya Kiingereza, Hisabati na Masomo ya Sayansi katika shule za Msingi na Sekondari.
- (h) mdondoko wa wanafunzi katika shule za msingi na sekondari;
- (i) uhaba wa vitendea kazi kwa wakaguzi wa shule;
- (j) uwiano mdogo kati ya bajeti inayotengwa ikilinganishwa na mahitaji halisi ya Wizara;
- (k) idadi ndogo ya wanafunzi wenye sifa ya kujiunga na vyuo hasa katika fani za sayansi;
- (l) uchache wa vyuo vya elimu ya juu na shule za serikali zinazotoa elimu ya sekondari kidato 5 na 6;
- (m) ongezeko la watu wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu;
- (n) kutokuwepo kwa mfumo endelevu unaokidhi mahitaji ya kielimu kwa wenye ulemavu; na
- (o) UKIMWI kuendelea kuathiri nguvu kazi na ubora wa utoaji wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maamuzi muhimu. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itatekeleza yafuatayo:-

- (a) kuendelea kufanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, Sera ya Elimu ya Juu ya mwaka 1999 na Sera ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis ya mwaka 1996;
- (b) kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa, ujenzi na ukarabati wa miundombinu, madarasa, nyumba za walimu, maabara, karakana, maktaba, kumbi za mihadhara, hosteli, mabweni na majengo ya utawala katika shule, vyuo na vyuo vikuu;

(c) kuongeza nafasi za mafunzo na kutoa kipaumbele katika kuajiri walimu, wahadhiri na wataalamu wa maabara (*laboratory technicians*) katika shule, vyuo na vyuo vikuu;

(d) kufanya maandalizi ya kuanza kutumia TEHAMA katika kufundisha na kujifunza (*online teaching and e-learning*) ili kukabilia na tatizo la upungufu wa walimu, kumudu kwa kiwango cha chini cha masomo ya masomo ya Kiingereza, Hisabati na Sayansi;

(e) kushawishi wadau mbalimbali wa elimu ikiwa ni pamoja na ‘*Development Partners*’ katika kuchangia maendeleo ya elimu ya msingi, sekondari, sekondari, ufundi na elimu ya juu;

(f) kuimarisha utoaji wa elimu ya sayansi na kushawishi wanafunzi wengi kuchukua masomo ya sayansi katika ngazi ya Sekondari na Vyuo Vikuu;

(g) kuandaa utaratibu wa kujenga shule 2 za sekondari kidato cha 5 na 6 kila wilaya chini ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES);

(h) kuanza kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Watu Wazima;

(i) kukamilisha Mpango Mkakati wa Maendeleo ya elimu Maalumu na Elimu Jumuishi kwa lengo la kuanzisha mfumo madhubuti wa utoaji wa elimu kwa wenyе mahitaji maalumu wakiwemo wenyе ulemavu;

(j) kupitia upya mtaala wa elimu ya msingi na sekondari ili kuimarisha ujenzi wa ujuzi kwa kutila mkazo masomo ya Sayansi Lughu na Hisabati na kutoa kipaumbele kwa waombaji wa mafunzo wa ualimu waliofaulu vizuri katika masomo ya Sayansi English na Hisabati; na

(k) kuendelea na utaratibu wa kutoa huduma na faraja kwa watumishi wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI na wenyе UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani na pongezi. Natoa shukrani za pekee kwa wananchi, viongozi na Wahisani mbalimbali kwa kuchangia utekelezaji wa Mipango ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Wahisani hao ni Serikali ya Sweden, Uingereza, Ufaransa, Ireland, Japan, Norway, Finland, Canada, Uhlanzi, Ujeruman, China, Cuba, Jamhuri ya Watu wa Korea, Ubelgiji na Umoja wa Nchi za Ulaya (EU). Aidha, mashirika yaliyochangia ni pamoja na Benki ya Dunia (WB), WFP, UNICEF, UNESCO, ILO, UNFPA, UNDP, Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), NORAD, GTZ, DFID, Sida, CIDA, JICA, USAID, JOVC, VSO, CELTEL, CBP, OPEC, DANIDA, Barclays Bank, NMB, CRDB, NBC, *Peace Corps*, *Book Aid International*, *Aga Khan Education Foundation*, *Plan International*, *Sight Servers International*, UNAIDS, *World Vision*, *Irish Aid*, *Care International*, *Oxfam*, *Children International*, *International Reading Association* na mashirika mengineyo.(Makofî)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na misaada hiyo, utekelezaji wa Mipango ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu kwa mwaka 2007/2008 haungefanikiwa na kukamilika katika kiwango nilichoelezea bila jitihada, ushirikiano na uongozi wa pamoja katika Wizara. Natoa shukrani zangu za dhati kwa Wakurugenzi wa Idara zote, Viongozi wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu katika ngazi mbalimbali, walimu, wahadhiri na wafanyakazi wote wa Wizara kwa ushirikiano walionipa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu na katika maandalizi ya Bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu pia kwa Wenyeviti, Wakurugenzi Watendaji, Makatibu Watendaji na Wajumbe wa Mabaraza na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara yangu na Wafanyakazi wote katika ngazi mbalimbali kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuimarisha na kuendeleza Elimu na Mafunzo ya Ufundu. Aidha, natoa shukurani na pongezi kwa; Mwenyekiti na Wajumbe wa Baraza la Ushauri la Elimu la Taifa (*National Education Advisory Council*), Uongozi wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Chama cha Mameneja na Wamiliki wa Shule na Vyuo Visivyo vyta Serikali (TAMONGSCO), Umoja wa Wakuu wa Shule za Sekondari Tanzania (TAHOSA), Chama cha Wachapaji na Asasi za Kiraia (*Civil Society*) kwa ushirikiano wao mzuri na Wizara katika kutatua matatizo mbalimbali. Napenda kuwashukuru viongozi wa matawi ya TUGHE na CWT Makao Makuu ya Wizara kwa ushirikiano na ushauri wao katika kushughulikia masuala ya wafanyakazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Makadirio ya Bajeti ya Wizara Mwaka 2008/2009. Baada ya kueleza yote hayo, ninaomba sasa Bunge lako lijadili hoja yangu pamoja na kuzingatia Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii na kuitisha makadirio ya matumizi ya shilingi 527,475,961,300 ili kuwezesha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu kutekeleza mipango ya mwaka 2008/2009. Kati ya fedha hizo:

- (a) Shilingi 397,889,941,300 zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu; na
- (b) Shilingi 129,586,020,000 zinaombwa kwa ajili ya Mipango ya Maendeleo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu na Taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafika.

(*Hoja Ilitolewa Iamuliwe*)

MHE. OMAR S. KWAANGW' – MWENYEKITU WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii ili

niweze kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii kuhusu utekelezaji wa malengo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa fedha 2007/2008 na malengo ya mwaka wa fedha wa 2008/2009 kwa mujibu wa Kanuni ya 115 (2007), ikisomwa na kifungu cha 9(1) cha Nyongeza ya Nne ya Kanuni za Bunge Toleo la 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilipata muda wa kutosha kufikiria na kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa malengo ya Wizara ya Elimu na mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa fedha wa 2007/2008 na pia kupitia malengo na maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009 na kutoa maoni na mapendekezo katika maeneo yafuatayo:-

Majukumu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi;
Taarifa ya Utelelezaji wa Maagizo ya Kamati kipindi cha 2007/2008;

Makadirio ya Mapato na Matumizi na Mpango wa Maendeleo wa Wizara kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Wizara. Baada ya mabadiliko ya hivi karibuni ya Muundo wa Serikali, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iliongezewa jukumu la kusimamia Elimu ya Juu na hivyo kuwa na majukumu yafuatayo:-

(a) Kutunga na kusimamia utekelezaji wa Sera, kuratibu, kufuatilia na kutathimini mipango ya elimu katika ngazi zifuatazo:-

Elimu ya Awali, Elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari, Elimu itolewayo kwa watu wenyewe mahitaji maalum, Elimu ya Watu wazima nje ya mfumo rasmi, Elimu ya Ualimu Daraja ‘A’ na Stashahada, Elimu ya Mafunzo ya Ufundi; na Elimu ya Juu.

(b) Kundaa na kusimamia Mitaala ya Shule, Vyuo vya Ualimu na Ufundi;

(c) Kuhakiki na kupima ubora wa Elimu katika ngazi zote;

(d) Kutunga na kuendesha Mitihani ya kitaifa ya darasa la Nne, Saba, kidato cha Pili, Nne na Sita, na mitihani ya Elimu ya Ualimu;

(e) Kutoa mwongozo wa uendeshaji na kusimamia shughuli za Taasisi na Bodi, Asasi, Tume, Mabaraza na Vyuo vilivyo chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya awali na msingi. Katika Elimu ya awali Serikali iliweka malengo ya kuhakikisha kuwa kila Shule ya Msingi nchini ina darasa la

Elimu ya Awali na kuhamasisha sekta binafsi kwa ajili ya kuandaa watoto kuanza Elimu ya Msingi. Tatizo la msingi ni madarasa haya ya Elimu ya Awali kutokuwa na Walimu wa kufundisha ipasavyo. Tunashauri kuwa Wizara iondoe matatizo yanayoikabili Elimu ya Awali.

Matatizo ya Elimu ya Msingi

(i) Utoro wa Wanafunzi

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio ya kutekeleza MMEM kwa kujenga madarasa, kuandikisha wanafunzi wengi darasa la kwanza na kuwepo Kanuni na Waraka wa Elimu Na. 25 ya uandikishaji na mahudhurio shulenya lazima ya mwaka 2002 '*The Primary School Compulsory Enrolment and Attendance Rules*,' kumekuwepo vitendo vya utoro wa wanafunzi katika Shule za Msingi kwa sababu mbali mbali ikiwa ni pamoja na ukosefu wa mahitaji ya shule, vifo, mimba, maradhi, wazazi walezi kuugua, na utoro mwingine ambao unaonyeshwa kwenye Jedwali ni kwamba asilimia 77 ya mdondoko ni Utoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili limekuwa kubwa kiasi cha kukatisha tamaa na kufikia kuleta dhana kuwa hatupo makini katika kusimamia masuala ya msingi, Kwa mfano mwaka 2002 wanafunzi waliokatishwa masomo walikuwa 36,680 ikilinganishwa na wanafinzi 48,221 mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuchukua hatua madhubuti na kali dhidi ya Wazazi, wananchi na wanafunzi wanaoendekeza tabia hii ambayo inazidisha ongezeko la wajinga katika jamii. Ni muhimu Serikali ifahamu ni nani anazembea katika eneo hili wakati utawala wa Serikali unaanzia katika ngazi za Vitongoji, Mitaa na Serikali za Vijiji.

(ii) Umuhimu wa Masomo ya lugha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ni muhimu kufahamu kuwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza ni ufunguo kwa masomo mengine. Kiswahili ni lugha ya Taifa, lugha ya kufundishia shule za Msingi na lugha ya mawasiliano kwa watu wengi nchini. Aidha Kiingereza ni muhimu sana katika utoaji wa Elimu katika masomo yote ya Sekondari ukiacha lugha ya Kiswahili. Kiingereza pia ni lugha inayotumika sana kuwasiliana kimataifa. Hivyo ni muhimu shule zikafundisha lugha hizi kwa ustadi na kuwajengea wanafunzi uwezo wa kutosha.

(iii) Mtihani wa Darasa la Nne - (STD IV).

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya Mtihani wa Taifa wa Darasa la Nne ni kupima mafanikio na maendeleo ya mwanafunzi ili kuona iwapo malengo yaliyokusudiwa katika ufundishaji na kujifunza yamefanikiwa, pia kubaini kasoro zilizoko na kufanya marekebisho na kuboresha njia na mbinu ya ufundishaji na kuwasaidia watoto wenye matatizo maalum katika kujifunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Serikali itoe ufanuzi kwa wananchi juu ya dhana ambayo si sahihi kuwa Serikali imefuta mtihani wa darasa la nne;

(b) Serikali iboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia ili wanafunzi waweze kufaulu masomo yote na kuhakikisha kuwa watakaoshindwa wapatiwe mafunzo rekebishi (*Remedial teaching*);

(c). Walimu watakaotumia muda wao katika kuwasaidia wanafunzi wenye matatizo wapewe motisha iliyo wazi na kuwa na bajeti maalum ili kuondoa matatizo hayo; na

(iii) Fedha za kuendeshea Shule - *Capitation Grant*.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zinazotengwa kwa ajili ya kuendesha Shule '*Capitation grant*' zinatakiwa zifkishwe kwenye akaunti za Shule kwa wakati na kwa usahihi. Ni vema Serikali itimiza ahadi yake ya kutoa dola 10 za Marekani ambayo kwa sasa ni karibu na Shilingi 12,000/= kwa kila mwanafunzi kwa mwaka. Katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Serikali imekiri kupeleka wastani wa Shilingi 6,000/= tu kwa kila mwanafunzi. Upungufu huu unaziweka shule kwenye matatizo ya uendeshaji na pia unaweza kushusha ari ya Walimu na watoa huduma kwa ujumla na hatimaye kushuka kwa taaluma. Serikali ileze mkakati wa kutoa dola 10 kwa mwaka 2008/2009 kama ilivyokubaliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu ya Sekondari. Katika mwaka 2007/2008 Serikali ngazi zote iliweka msukumo wa pekee katika kujenga Shule za Sekondari katika ngazi ya Kata ikiwa ni juhudini za kupokea mafanikio ya utekelezaji wa Mpango wa MMES ambayo ni pamoja na idadi kubwa ya Wanafunzi kufaulu mtihani wa darasa la Saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtihani wa Kidato cha pili. Imejitokeza dhana ambayo pia sio sahihi kuwa Serikali imefuta rasmi Mtihani wa Kidato cha Pili. Kamati inatoa maoni kuwa Mtihani wa Kidato cha Pili unapima maarifa na ujuzi aliopata mwanafunzi kutokana na masomo alijojifunza katika kidato cha Kwanza na cha Pili. Mtihani huu pia unalenga kutoa alama zenye uwiano wa Kitaifa kwa ajili ya kupima maendeleo ya Wanafunzi ambayo hutumiwa na Baraza la Mitihani la Taifa kama sehemu ya maendeleo ya mwanafunzi kitaaluma. Hivyo, Kamati inashauri ifuatavyo:-

(i) Serikali itoe maelezo sahihi juu ya dhana iliyoenea kuwa Mtihani huu umefutwa.

(ii) Tunaishauri Serikali kwa nguvu zote kuwa utaratibu wa mtihani huu uimarishwe zaidi kwa kuhakikisha kuwa shule zinakuwa na vitabu vya kutosha, vifaa vya

maabara na walimu wenyе sifa na kuhakikisha kuwa masomo yote yanafundishwa na syllabus kukamilishwa vizuri.

(iii) Matokeo ya Mtihani wa kidato cha pili yaendelee kutambuliwa na kupewa uzito na Baraza la Mitihani la Taifa katika rekodi zake za upimaji endelevu (*continuous assessment*).

(iv) Ili kutoa uzito unaostahili, ni lazima Wizara iwe na bajeti maalum kwa mtihani kama huu kama inavyofanya kwa Mtihani wa Kidato cha Nne na cha Sita.

(v) Wanafunzi watakaoshindwa mtihani wa kidato cha pili wawekwe kwenye utaratibu wa kuwapatia mafunzo rekebishi (*remedial teaching*) ambayo ni muhimu ifanyiwe ukaguzi. Pia walimu watakaofanya kazi hii walipwe na utaratibu uwekwe wazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna mjadala unaoendelea mionganoni mwa jamii kuhusu maana ya elimu bora ni nini, na kwa kuwa katika jamii kuna mitazamo tofauti kuwa:-

Wapo wanaoangalia ubora wa elimu kwa kulinganisha na vitendea kazi, rasilimali watu na vitu kama madarasa, maktaba, maabara, idadi ya Walimu, Nyumba za Walimu na vitabu.

Wengine wanaangalia ubora katika kufaulu mitihani ya darasa la Saba, Kidato cha Nne na cha Sita.

Wengine wanaangalia ubora wa elimu kutokana na ubora wa Walimu.

Wapo pia wanaoangalia ubora wa elimu kuititia wahitimu wanaopata kazi na kuishi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu bora inahitaji jitihada na michango ya kila mtu kuanzia wanafunzi, wazazi, Kamati za Shule, Walimu, jamii, wataalam, uongozi wa elimu katika ngazi zote za Serikali na Asasi za kiraia. Wote tunawajibika katika kujenga na kuendeleza elimu bora inayozingatia uwezo wa wanafunzi kumudu maisha yao ya baadaye kuititia stadi za maendeleo binafsi, stadi za utambuzi na maadili. Pia wote tunawajibika kuimarisha mafunzo ya kitaalam kwa Walimu tarajali na walio kazini na kujenga mfumo bora wa tathmini ya nini hasa kinatendeka darasani kati ya mwalimu na mwanafunzi kuhusu upatikanaji wa elimu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mabadiliko yanayoendelea katika Sekta ya Elimu, Kamati inashauri kuwa wakati sasa umefika wa kuiangalia Sera ya Elimu ya Taifa ili mawazo ya wadau wa elimu katika mabadiliko yapate nafasi katika harakati za kutoa elimu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matayarisho ya Elimu ya Sekondari Kidato cha V na VII. Kamati inashauri Serikali kuwa, kwa kuwa kumekuwapo na mafanikio katika ujenzi wa Shule za Sekondari za Kata zinazoendelea kufunguliwa, na kwa kuwa kiwango cha kufaulu katika Shule za Sekondari kimekuwa kinaongezeka kila mwaka, ni vema Serikali na jamii kwa ujumla ikaandaa na kutekeleza mkakati wa jinsi ya kuweka miundombinu ya Kidato cha tano na cha Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati. Kamati inaipongeza Serikali kwa mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa malengo katika Elimu ya Msingi na Sekondari kama yaliyoelezwa katika Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu ukrasa wa 57, 58, na 59. Aidha kutokana na mafaniko haya Kamati ilishauri Serikali na jamii nzima kujipanga upya katika kuendeleza, kufanikisha na kulinda mafanikio haya katika maeneo yafuatayo:-

Kujenga majengo yote muhimu ya Madarasa, Ofisi za Walimu, Vyoo na msisitizo wa pekee ukiwa katika kujenga nyumba za Walimu mashulenii.

Kuajiri na kusambaza Walimu wenyе sifa za kufundisha Elimu ya Sekondari wa kutosheleza nchini kote.

Kuimarisha miundombinu ya Shule za Sekondari kwa kununua vitabu vya kutosheleza mahitaji ya wanafunzi kwa mujibu wa Mitaala inayofundishwa, kuimarisha maktaba za Shule, kununua vifaa vya Maabara vya kutosheleza kufundishia na kufanya majoribio kwa vitendo – ‘practicals’. Ushauri huu unatokana na ukweli kwamba Kamati ilishuhudia vyumba vilivyojengwa kwa ajili ya maabara vikiwa vinatumika kama madarasa ya kawaida katika ziara zake Mikoani. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu bora kwa kiasi kikubwa inatokana na mafunzo ya Ualimu na hasa tukizingatia kuwa Walimu ni chimbuko la Uzalendo wa Kitaifa na Utaifa. Walimu ni wazalishaji wa nguvu kazi ya Taifa katika nyanja zote za kiuchumi na za kijamii, hivyo ili kuboresha taaluma ya Ualimu na kuweza kukabiliana na changamoto za kupata Walimu wenyе sifa na taaluma nzuri tunaishauri Serikali kufanya yafuatayo:

(i) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iandae mpango maalum wa mafunzo kazini *In-service Training na Up-grading Courses* ya Walimu wa ngazi mbali mbali. Mfano: Walimu ngazi ya Daraja la IIIA, asilimia 50 yao wakipewa mafunzo ya Ualimu ngazi ya Diploma, Serikali itakuwa imetatua sehemu kubwa ya upungufu wa Walimu wenyе sifa za kutosha kwenye ngazi ya Shule za Msingi na Sekondari ya kawaida (*O level*);

(ii) Vivyo hivyo ukitoa nafasi za kutosha kwa Walimu wenyе Diploma kuchukua mafunzo ya Shahada kwenye Vyuo Vikuu utapata Walimu wa kutosha wa Sekondari ya kawaida na ya juu (*A-level*); na

(iii) Kufungua Vyuo zaidi vya Walimu Daraja la III A na Diploma ya Ualimu na kuimarisha Vyuo vilivyopo sasa ili viweze kuchukua wanachuo wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi ndizo njia muafaka ya kuondokana na mipango ya muda mfupi ya (*Crash programmes*) ambayo huzalisha watu wasio na taaluma ya kutosha ya Ualimu na zaidi imeongeza tatizo la kuwa na watu ambao hawakusomea ualimu kuacha kazi bila utaratibu na hivyo kuleta matatizo zaidi pamoja na Serikali kutumia gharama kuwaajiri kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ina maoni kuwa lengo la Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu kudhamini Walimu 1500 kwenye Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (*OUT*) pamoja na wale wanaosomea Shahada za Ualimu kwenye Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki bado ni ndogo. Hivyo Kamati inashauri Serikali kutenga fedha za kutosha kudhamini wanafunzi wengi zaidi wa Shahada za Ualimu na Elimu ili kupata Walimu wa kutosha kukidhi mahitaji ya shule nyingi zilizojengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu Maalum: Chuo cha Ualimu Patandi, ni Chuo cha Ualumu pekee kinachotoa Elimu Maalum Tanzania Bara. Kutokana na umuhimu wa elimu maalum katika jamii yetu, tunashauri kuwa wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu itoe kipaumbele kwa Chuo hiki cha Patandi kwa kukamilisha yafuatayo:-

(i) Kuanzisha programu ya Elimu kwa Masafa ambayo itafundisha Walimu wengi zaidi wa kufundisha Elimu Maalum;

(ii) Kununua vifaa vya kutosha vya kujifunzia na kufundishia Elimu Maalum kama *Braillers, Braillon papers, Audiometers na Assessment kits* na kadhalika;

(iii) Kukamilisha ujenzi wa jengo la *Assesment* ambalo limechukua muda mrefu bila kukamilika;

(iv) Kuongeza majengo ya madarasa, mabweni, maktaba na nyumba za Wakufunzi; na

(v) Kuanzisha kozi za Otizimu, Uziwi, Upofu, Uoni hafifu na ulemavu wa viungo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chombo cha Ajira ya Walimu. Kamati imeendelea kutafakari matatizo mbalimbali ya Walimu na kubaini kuwa mojawapo ya mambo yanayochangia matatizo yao ni ajira yao kuwa chini ya mamlaka tofauti ambazo huleta ukiritimba badala ya ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa ajira ya Walimu wa Shule za Awali na Msingi ipo chini ya Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Walimu wa Sekondari, Vyuo vya Ualimu, Ukaguzi, Shule za za Mazoezi ipo chini ya Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, na ajira ya Walimu wa Vyuo vya Maendeleo

ya Jamii ipo chini ya Katibu Mkuu Wizara wa Wanawake, Jinsia na Watoto. Vile vile kuhusu kupandishwa vyeo na nidhamu Walimu wapo chini Tume ya Huduma za Walimu (*TSD*) ambayo ipo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ili kuleta ufanisi na mtiririko mzuri katika utumishi wa Walimu kwa kuzingatia kuwa Walimu idadi yao ni zaidi ya asilimia ya 50 ya watumishi wote wa Serikali, Kamati inashauri Serikali ione umuhimu wa ajira ya Walimu kuwa chini ya Idara au chombo kimoja cha ajira. Aidha kutokana na mfumo wenye dosari wa ajira yao matokeo yake ni kuendelea kuwepo matatizo ya stahiki zao hasa kucheleweshwa kupandishwa madaraja na vyeo, malimbikizo ya Mishahara, posho za Uhamisho, Nauli ya likizo, n.k. Kwa mfano; madai ya malimbikizo ya walimu kutoka Mikoa yote kwa shule za msingi yamefikia bilioni 12.2, na sekondari, vyuo na ukaguzi, bilioni 4.2. Kufikia Desemba 2007 kwa mujibu wa taarifa ya Chama cha Walimu Tanzania, pamoja na Serikali kulipa bilioni 7 na milioni 800 kwa upande wa walimu wa vyuo na sekondari. Aidha motisha kwa ajira ya Ualimu na kufanya kazi ya Ualimu yenye ujira mzuri na kutambua wale watakofanya kazi katika mazingira magumu ndiyo njia muafaka ya kuifanya kazi ya Ualimu kuwa na mvuto kwa wale watakaopenda kusomea kozi ya Ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa wakati umeanza kupita kwa Serikali kutekeleza mapendekezo ya Ripoti ya Utafiti ya muda mrefu iliyolenga kuwaondolea Walimu urasimu na usumbuwa wa matatizo yanayotokana na mfumo wenye urasimu na matatizo. Tunawashukuru Walimu kwa kuendelea kuonyesha uvumilivu wa hali ya juu. Hivyo tunaomba Serikali imalize kero hii na tusilazimike tena kurudia ushauri ambao kimsingi umeishakubaliwa na Bunge kupitia Taarifa ya Kamati Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu ya Ufundis- Veta, kumekuwepo na ahadi ya Serikali tangu mwaka 2005/2006 kuhusu ujenzi wa Vyuo vya *VETA* katika Mikoa ya Lindi, Pwani na Manyara, lakini hakuna taarifa ya hatua iliyofikiwa katika mradi huu mkubwa unaofadhiliwa na Serikali kwa ushirikiano na Jamhuri ya Watu wa Korea Kusini. Tunaomba Wizara itoe taarifa ya hatua iliyofikiwa kwa kila Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika Kamati pia inashauri Serikali kuwa utaratibu wa kuwa na vyuo vya *VETA* kwa kila wilaya ukamilishwe kutokana na kuwa na wingi wa vijana wanaomaliza elimu ya Msingi chini ya MMEM na hawapati nafasi ya Elimu ya Sekondari, na wale wanaomaliza Elimu ya Sekondari ambao hawapati nafasi ya kuendelea katika fani nyingine wajijunge na Elimu ya Ufundis chini ya *VETA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kamati inashauri kuwa ili kuleta maendeleo na mafanikio ya haraka katika kupanua Elimu ya Ufundis Stadi, Serikali kupitia Baraza la Ufundis iandae mpango maalum utakaowezesha wahitimu wa Vyuo vya *VETA* kujiendeleza kitaaluma na kufikia ngazi za juu za ufundis hadi kuwa na Shahada ya Uhandisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Mitihani la Taifa: Baraza la Mitihani ni chombo nyeti na ni jicho la Taifa kinachoipatia nchi uhalali wa viwango vya elimu wanayopata watu wake. Kamati inashauri Serikali kuendelea kutenga fedha za kutosha kuboresha vitendea kazi vya Baraza hasa maandalizi ya uchapaji wa Mitihani na Vyeti na kuboresha na kuimarishe mfumo wake wa kompyuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliwhi kutembelea ujenzi wa Kituo cha kusahihisha mitihani cha Mbezi ambacho kilikuwa katika hatua za mwisho za ujenzi. Pamoja ma mafanikio ya ujenzi wa kituo hicho, Baraza lilikuwa linadaiwa kiasi cha Shilingi bilioni 13.2 na wakandarasi ambao walifikia hatua ya kutaka kulifikisha Baraza kwenye vyombo vya Sheria. Tunaipongeza Serikali kwa kutenga fedha katika mwaka huu wa fedha wa 2008/2009 za kulipia gharama za wakandarasi na kuondoa aibu ya Baraza kufikishwa mahakamani na Wakandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu ya Juu: Ingawaje nchi yetu ina idadi kubwa ya watu wapatao zaidi ya milioni 36, ina wanafunzi wachache zaidi katika vyuo vya Elimu ya Juu vya Umma na binafsi ikilinganishwa na nchi zote jirani zikiwemo Kenya, Uganda, Botswana, Lesotho, Afrika ya Kusini, na nchi za SADC kama inavyoonekana kwamba kwa mwaka 2006 takwimu zetu zinaonyesha kwamba tulikuwa kwenye asilimia 0.27 wakati Afrika Kusini asilimia 9.11, Kenya 1.47, Uganda 1.23, Lesotho 0.98, Malawi 0.42, Msumbiji 0.33.

Mheshimiwa Naibu Spika, Takwimu hizi za mwaka 2006 zinaonyesha asilimia ya ushiriki wa wanafunzi wetu katika vyuo vya Elimu ya Juu. Tunaomba Wizara ya Elimu na Mafunzi ya Ufundji itoe takwimu za mwaka 2008/2009, kuona kama kuna mabadiliko kwa sababu maendelo ya nchi yanategemea sana ushiriki wa wanafunzi na jinsi wanavyohitimu Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Dodoma. Kamati inapongeza Serikali kwa kujenga baadhi ya miundombinu ya Chuo Kikuu cha Dodoma kwa mafanikio na hivyo kuweza kudahili Wanafunzi wa mwaka wa kwanza 5,000 mwezi Augost/Septemba 2008 katika Kampasi tatu kama ilivyoonyeshwa kwenye taarifa hii:-

- (i) *College of Education* - kudahili Wanafunzi 2000.
- (ii) *College of Humanities and Social Sciences* – kudahili Wanafunzi 2500.
- (iii) *College of Informatics and Virtue Education* – kudahili Wanafunzi 500.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi ni hatua nzuri katika kuelekea kutekeleza lengo la Chuo Kikuu cha Dodoma kuwa na wanafunzi 40,000 ujenzi utakapokamilika. Kamati inahimiza Serikali iendelee kujenga Kampasi zingine ili kufikia lengo linalotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika Chuo Kikuu Cha Dar Es Salaam – CDK: Historia ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam na mchango wake ni muhimu sana katika nchi yetu. Kwa kumbukumbu, Chuo Kikuu cha Dar es salaam kilianzishwa mwaka 1961 kikiwa

ni kampasi ya Chuo cha London. Mwaka 1963 Chuo kilibadilishwa kuwa Chuo Kishiriki cha Jumuiya ya Afrika Mashariki na baadaye mwaka 1970 kilipanda hadhi yake na kuwa Chuo Kikuu cha Taifa kikiitwa Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika muda wote huo Chuo hiki kimezalisha wataalam mbalimbali, kimefanya tafiti mbali mbali na pia kimetoa ushauri wa kitaalam katika nyanja mbalimbali. Chuo Kikuu cha Dar es salaam kimeendelea kulinda hadhi ya nchi kwa kutambuliwa na Taasisi ya *Webometrics Ranking of Universitie* kuwa kati ya Vyuo Vikuu 7,670 duniani. CDK kilichukua nafasi ya 13 kwa ubora katika Vyuo vya Afrika mwaka 2006/2007. Pia Chuo kilitambuliwa kwa kujenga na kupanua mifumo ya Mawasiliano ya Habari *IT*, kwa kiwango cha kuvipiku Vyuo vyote vya Afrika Kaskazini ya Mto Limpopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali halisi ya Chuo hiki kwa sasa inahitaji uwekezaji mkubwa sana kwa sababu katika kipindi kirefu Serikali hajitatua matatizo yafuatayo ambayo yanahitaji fedha za kutosha:-

Makazi ya wanafunzi Sehemu ya Mlimani yamechakaa sana na ni HATARI kuendelea kuweka wanafunzi. Pamoja na idadi ya wanafunzi kuongezaka hadi 20,000 hivi sasa, makazi ya Wanafunzi yaliyopo ni asilimia 40 tu na hivyo kujitokeza matatizo yafuatayo:-

- (i) Ukosefu wa makazi ya kutosha kwa wanafunzi.
- (ii) Kujazana kwa Wanafunzi katika makazi yao
- (iii) Uhaba wa maji

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondokana na matatizo ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Serikali inahitaji raslimali za kuwezesha kufanya ukarabati mkubwa na ujenzi wa miundombinu ya Chuo. Makisio ya gharama za kutekeleza mradi huo ni kama ifuatavyo:- Mtandao wa maji, Makisio ya gharama Tshs. 4.8 bilioni, Vyumba vya Madarasa na Semina Tshs. 6.4 bilioni, Ofisi za Wafanyakazi Tshs. 3.6 bilioni, Ukarabati Nyumba za Wafanyakazi Tshs. 5.7 bilioni, Ujenzi wa nyumba mpya Tshs. 13.5 bilioni, Taasisi ya sayansi za Bahari Tshs. 6.2 bilioni, Ukarabati wa makazi Tshs. 7.5 bilioni, Ujenzi wa jengo la makazi ya Wanafunzi Tshs. 36.1 bilioni, Ukumbi wa wanafunzi waishio nje ya Chuo Tshs. 16.5 bilioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, zinahitajika Bilioni 100.3 ili kufanya ukarabati katika miradi ya mtandao wa maji, vyumba vya madarasa na semina, ofisi za wafanyakazi, ukarabati wa nyumba za wafanyakazi, ujenzi wa nyumba mpya, taasisi za sayansi ya bahari, ukarabati wa makazi, ujenzi wa jengo la makazi ya wanafunzi na ukumbi wa wanafunzi waishio nje ya chuo. Jumla ni bilioni 100.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2008/2009, Serikali imetenga karibu Tshs. 2.4 bilioni kwa ajili ya ukarabati wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Ni wazi kuwa fedha hizi ni tone tu katika bilioni 100.3 zinazohitajika katika kurekebisha miundombinu ya CDK.

Kamati inashauri kuwa ili kupunguza matatizo ya CDK likiwepo tatizo la migomo ya mara kwa mara, ukarabati mkubwa na Ujenzi wa makazi mapya ya Wanafunzi hauna budi kufanyika kwa haraka iwezekanavyo. Ni lazima Serikali yenye we iweke mkakati wa pamoja na wafadhili wakubwa, nje ya utaratibu wa kawaida wa bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Mwaka 2008/2009, Bodi ya Mikopo imetengewa kiaso cha shillingi 117 bilioni kwa ajili ya mikopo kwa wanafunzi. Kiasi hiki ni sawa na kiasi kilichotolewa mwaka 2007/2008. Athari zinazotokana na kutengewa kiasi hiki ni pamoja na kupunguza idadi ya wanafunzi wenye udahili ambao wangepatiwa mikopo kwa mwaka huo kutoka 60,000 ambao wanahitaji jumla ya shs. 138 bilioni hadi kufikia 49,738 sawa na punguzo la asilimia 18.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itafute upungufu wa bilioni 21 katika mafungu yake kwa kupunguza matumizi ili fedha hizi zipatikane na wanafunzi 60,000 wakopeshwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kutoa kipaumbele kwa wanafunzi kujifunza masomo ya Sayansi, tiba ya binadamu na mifugo, kilimo, uhandisi na teknolojia ili taifa liweze kupata wataalam kwa ajili ya kuweka misingi ya maendeleo ya Taifa badala ya kuendelea na utaratibu wa sasa wa mikopo. Masomo ya teknolojia ambayo ndiyo muhimu kwa nchi hii wanakopeshwa 2% tu, masomo ya kilimo 4%, masomo ya afya 5%, masomo ya uhandisi 6% na masomo ya sayansi yenye we 7% na masomo ya biashara 8%, masomo ya ualimu 28% na masomo ya sanaa 40%.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inaonyesha kuwa idadi kubwa ya wanafunzi walio katika taasisi za Elimu ya juu wanatosomea masomo ya Sanaa (40%) ikilinganishwa na wanafinzi wanaosomea shahada nyingine. Aidha idadi ya wanafunzi wanaosomea Shahada ya Ualimu imeongezeka kutokana na kipaumbele kilichowekwa, pamoja na ongezeko la idadi ya taasisi zinazotoa Shahada hizo katika vyuo vya umma na vile vya binafsi. Hata hivyo programu nyingine zilizo za kipaumbele na hasa za sayansi na kilimo bado ziko nyuma ya kozi ambazo siyo za kipaumbele kwa Taifa. Hivyo tunashauri Serikali kuona umuhimu wa kuboresha mvuto wa masomo ya Sayansi ili Taifa lipate wataalam wa fani hizo. Vivyo hivyo Mikopo inayotolewa itoe kipaumbele kwa wanafunzi wanaosomea masomo ya Sayansi na pia serikali ichukue hatua zaidi za kuwavutia wanafunzi kusomea masomo ya Sayansi kwa kutoa ufadhili (*Grants*) badala ya Mikopo katika programu za Sayansi ili kuwavutia waombaji wengi kusoma fani hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamisheni ya Vyuo Vikuu – TCU: Kamisheni hii ni chombo muhimu kilichoanzishwa kwa ajili ya kusimamia na kudhibiti viwango vya ubora wa Vyuo vya Elimu ya Juu katika taasisi ya Umma na Mashirika ya watu binafsi. Kamisheni hii ni jicho la Serikali lenye wajibu wa kuhakiki mitaala, vifaa vya

kufundishia na mazingira ya elimu inakotolewa katika Vyuo vya Elimu ya Juu vya Umma na binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamisheni hii mpaka sasa haina jengo la Ofisi na kiasi kilichotengwa kwa ajili ya ujenzi ni kidogo sana ni Tshs. 385,000,000/=. Tunashauri Serikali kutenga fedha za kutosha ili *TCU* ipate ofisi ya kudumu na itekeleze jukumu lake kwa ufanisi badala ya kuendelea kupanga ofisi kwa kodi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Elimu Tanzania (*TEA*). Mamlaka ya Elimu Tanzania imekuwa ikihamasisha wadau mbali mbali kuchangia mfuko huu maalum wa kuendeleza elimu na pia kwa kutoa Mikopo kwa ajili ya kuendeleza miundo mbinu ya Shule, Vyuo na Taasisi mbalimbali za elimu. Kamati imekuwa hairidhishwi na utaratibu wa Serikali kupunguza kiwango cha fedha kinachotengwa katika Bajeti kwa ajili ya Mfuko huo kila mwaka. Pamoja na Sheria iliyoanzisha mfuko kutamka wazi kuwa Serikali itachangia kiasi kisichopungua asilimia mbili ya pato la Taifa baada ya kutoa gharama za madeni ya Taifa; asilimia ya bajeti inayotengwa kila mwaka. Mchango wa Serikali kuititia bajeti umeendelea kushuka kutoka asilimia 0.45 mwaka 2002/2002 na sasa tumefikia asilimia 0.11 mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hali ya kusikitisha sana na kwa vigezo vyovyyote, Serikali haioneshi hata kidogo katika kutekeleza ushauri uliotolewa kwa mara ya nne sasa. Sasa tunaliachia Bunge kujadili kwa undani na kuielekeza Serikali. Vinginevyo azma ya Serikali kuimarisha elimu kuititia Mamlaka ya Elimu Tanzania haioneshi mafanikio yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ufinyu wa Bajeti. Ufinyu wa bajeti kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu umeleta tatizo kubwa la uhaba wa chakula katika shule za Sekondari kutokana na kasma ya chakula kutengewa fedha kidogo ikilinganishwa na mahitaji halisi ya chakula. Ufinyu huu umesababisha Wazabuni kutolipwa madai yao kwa wakati hali inayowafanya kutoendelea kutoa huduma ya chakula kikamilifu. Deni la Wazabuni lilifikia Shs.10.1 bilioni pamoja na kuwa baada ya uhakiki wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu - *CAG* kundi la kwanza bila shaka wameanza kulipwa jumla ya shilingi 6.3 bilioni. Gharama halisi kwa mwaka 2007/2008 bilioni 11.2 ndizo zilizotakiwa, Serikali ilitoa fedha bilioni 7 ambayo kuna upungufu wa bilioni 5 ambayo ni 30%. Lakini mbaya zaidi, mwaka 2008/2009 gharama halisi ya chakula shulenii ni shilingi bilioni 29, lakini Serikali imetenga bilioni 7 tu. Kwa hiyo, kuna tatizo la bilioni 22. Tunaishauri Serikali kuangalia upya mafungu ya ndani ya Wizara hii ili kuongeza fungu la chakula kufikia bilioni 29 katika kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza malengo ya elimu, hata hivyo tunaipongeza Serikali kwa maamuzi yake katika mambo mawili:- kwanza, kwa kuipa

Sekta ya Elimu kupaumblele namba moja kwenye bajeti ya Serikali ya 2008/2009 kwa kuitengea asilimia 19.8 kutoka asilimia 18 (2007/2008) ambayo ni kubwa kuliko Sekta nyingine. Pili; tunaipongeza Serikali kwa kutoa kipaumbele namba moja kwa Sekta ya Elimu kwa kutenga ajira mpya kwa Sekta ya Elimu ambayo imetengewa nafasi 17,037 ambazo ni sawa na asilimia 49 ya ajira mpya Serikalini. Kamati inashauri Serikali kuweka msukumo zaidi katika kukabiliana na tatizo la upungufu wa Walimu katika shule zote. Aidha, Kamati imebaini kuwa mgawanyo wa hizo asilimia 19.8 za Bajeti ya Serikali ya 2008/2009 katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii, elimu ya msingi imepewa 67.4%, sekondari 9.2%, vyo vya walimu 1.7%, Ukaguzi 0.4%, elimu ya juu imepewa 21.3% tu. Kwa mujibu wa hali hii ni wazi kuwa Serikali inatoa kipaumbele kwenye elimu ya awali na msingi kwa 67.4%. Kutokana na mgawanyo huo ni wazi kuwa Kurugenzi ya Elimu ya Juu haikupewa fedha za kutosha (21.3%) kuimarisha Elimu ya Juu ambayo ni muhimu katika maendeleo ya Taifa. Tunashauri Serikali iangalie tatizo hili katika Muundo mpya wa Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shukrani: Naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Spika, kwa jinsi anavyoendesha Vikao vya Bunge kwa umahiri na busara kubwa. Aidha nakupongeza wewe na Wenyeviti wanaosaidia kukalia kitin na kuongoza Vikao vya Bajeti. Bila kusahau Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge ambao ndio msingi wa mafanikio ya Bunge katika shughuli zake za kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati ninamshukuru Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, (Mb), Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii akisaidiwa na Manaibu wake Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, (Mb), na Mheshimiwa Gaudensia M Kabaka, (Mb), pamoja na watendaji wa wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu Profesa Hamis Dihenga kwa jinsi walivyoshirikiana na Kamati kutoa majibu ya hoja za Wabunge kuhusu utekelezaji wa Wizara kwa mwaka 2007/2008, na Bajeti ya mwaka wa fedha 2008/2009

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwisho ninamshukuru Kaimu Katibu wa Bunge Ndg. Dk. Thomas D Kashililah na Ofisi yake kwa kutuhudumia vema kipindi chote Kamati ilipokuwa kazini. Nawapongeza Makatibu wa Kamati hii Ndg. Hosiana John, Ndg. Helen Mbeba na Theonest Ruhilabake kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi Taarifa hii kutoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 113(5) ya Kanuni za Bunge (2007), naomba niwatambue wajumbe wa Kamati kwa majina:- Mheshimiwa Omari S.Kwaangw', Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr.. Haji Mwita Haji, M/Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, Mheshimiwa Prof. Feetham F. Banyakwa, Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Hemed M. Hemed, Mheshimiwa Janeth B. Kahama, Mheshimiwa Dr. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Omari A. Mzee, Mheshimiwa Usi Amme Pandu, Mheshimiwa Faustine K. Rwilomba,

Mheshimiwa Dr. Luka Jelas Siyame, Mheshimiwa Ali Haroon Suleiman, Mheshimiwa Fatma Abdulla Tamim.

Mwisho kabisa, naomba nitumie vile vile nafasi hii kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Babati Mjini kwa uvumilivu wao na kwa kuendelea kuniunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. SUSAN A. LYIMO – MSEMAJI WA UPINZANI – WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa fedha 2008/2009 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(7) toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kuwa kwa takribani miaka miwili iliyopita, nilikuwa Waziri Kivuli wa Elimu ya Juu Sayansi na Teknnolojia. Lakini, kufuatia mabadiliko ya Baraza la Mawaziri yaliyofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kujiuzulu kwa Waziri Mkuu, Kiongozi wa Upinzani Bungeni naye ilimbidi kupanga upya timu yake na akaniteua kuwa Waziri Kivuli wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kama Msemaji Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufund,i naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed (Mb) na Naibu wake Dr. Willibrod Peter Slaa (Mb), kwa kunateua kushika nafasi hii. Vile vile napenda kuwashukuru kwa kunipatia msaidizi mahiri, Mheshimiwa Nuru Bafadhili (Mb) kama Naibu Waziri wangu. Naomba nimhakikishie Kiongozi wa Upinzani Bungeni na Watanzania wote wazalendo, kuwa nitafanya kazi hii kwa kushirikiana na Naibu wangu kwa uwezo wetu wote kwa lengo la kusaidia maendeleo ya Taifa letu la Tanzania. Hotuba hii imefika hapa kwa msaada wake mkubwa sana. Nawashukuru pia Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani walio katika Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii wakiwemo Mheshimiwa Meryce Mussa Emmanuel, Mheshimiwa Hemed Hemed, Mheshimiwa. Ali Mzee na Mheshimiwa Dr. Tarab. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru Kambi ya Upinzani, kambi makini kabisa chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, pamoja na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, kwa uongozi wao madhubuti unoijenga kambi hii na kuifanya kuwa kambi imara na isiyotetereka na hivyo kuweza kufanya kazi yake ya kuikosoa Serikali bila woga wowote. Ninamhakikishia Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni na Watanzania wote wazalendo kuwa nitafanya kazi hii, kwa

kushirikiana na Naibu wangu kwa uwezo wetu wote kwa lengo la kusaidia maendeleo ya Taifa letu zuri la Tanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa udhati kabisa, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Chama changu cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kwa kuendelea kunipa ushirikiano ndani na nje ya Bunge. Nami naendelea kuwaahidi kuitunza imani ya Chama changu na kuendelea kuitangaza kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu ya Msingi. Elimu ya msingi ni msingi kwa taifa lolote na ndiyo maana inaitwa msingi. Maendeleo yote ya elimu huanzia hapo na msingi wa elimu ukijengwa vizuri, bila shaka ngazi zote za elimu za juu zitaendelea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na umuhimu huo, Serikali kwa kushirikiana na nguvu za wananchi, pia imefanikiwa kuongeza idadi ya shule za msingi, ambazo zimeongezeka kutoka 14,700 mwaka wa 2006 hadi 15,624 mwaka 2007. Hili ni suala la kujipongeza na kupongezana lakini tunashauriwa kutodanganyika na taswira ya takwimu tu. Tujiulize je, hivi kweli elimu inayotelewa inawiana na nguvu inayowekezwa na wananchi? Kwa sababu wananchi wanajitahidi kwa upande wao na Waingereza wanasesma “*they have played their part*” lakini, je, Serikali inafanya nini? *Has it play its part?* Je, Walimu wako wapi? Vitendea kazi viro? *Teaching materials* zipo za kutosha? Hili ni suala ambalo Wizara ya Elimu inatakiwa kulispatia majibu ambayo yanarandana na uzito wa jambo hili na sio vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunafahamu kuwa ubora wa elimu haupimwi kwa uwingi wa shule wala idadi ya wanafunzi, la hasha! Ingawaje mjadala wa Kitaifa kuhusu uboreshaji wa elimu umejikita na kuelekezwa zaidi katika wingi wa vitendea kazi, hii inashangaza ingawaje sote tunatambua kuwa *quality is different from quantity* yaani ubora ni tofauti na uwingi. Kambi ya Upinzani, inasikitika sana kuona ubora wa elimu katika shule zetu za msingi kutetereka. Tafiti nyingi zilizofanywa na taasisi tofauti zinadhahirisha hilo, lakini utafiti wa kisayansi uliofanywa na taasisi ya Hakielimu ndio haswa ulioweza kuweka bayana, ni kwa kiasi gani elimu ya msingi imeshuka ubora. Kwa mujibu wa utafiti huo, ubora wa elimu kwa shule za msingi umeshuka. Hii inatisha na kukatisha tamaa. Kwa sababu kama hatujengi msingi mzuri maana yake tunajenga Taifa la wasomi wasio na uwezo kushindana katika ulimwengu huu wa utandawazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ngazi ya msingi, suala ambalo limefanikiwa kwa kiwango kikubwa, Tanzania imefanya vizuri sana na naona fahari kwamba mtandao wa shule za msingi unaofuata mtaala mmoja hata kama ni mzuri au mbovu kwa maarifa ya kusoma na pia kutahiniwa darasa la IV na la VII. Umbali toka shule hadi nyumbani, umepungua sana tangu 1978 na 2001, msukumo wa *UPE*, kwamba sasa wastani mtoto anatembea kilomita 1 - 4. Kuondolewa kwa ada na michango mbalimbali kumeongeza

sana watoto kwenda shule kwa wingi, tatizo kubwa ni ukosefu wa Walimu, vifaa vya kufundishia na miundombinu ya staha. Shule nyingi ziko katika hali mbaya, shule nyingi hazina madarasa ya kutosha hivyo mlundikano wa zaidi ya watoto 100 kwa darasa ilhali linatakiwa kuwa na wanafunzi 45, watoto kukaa kwenye sakafu, mawe, magazeti na chini ya miti. Bado wanashirikiana vitabu katika uwiano wa 1:6, Mwalimu mmoja akifundisha darasa zaidi ya mmoja kwa wakati. Huu ugawaji usio sawa wa rasilimali unapelekeea matokeo mabaya katika usomaji. Hii pia itapelekeea kutokuwa na usawa kati ya jamii. Ufutaji wa ada umepelekeea gharama nyingine kuanzishwa kama uchangiaji madawati na madarasa ambavyo pia inapelekeea tofauti ya ubora wa elimu kwani jamii zinatofautiana sana kimapato. Hii ni lazima ibadilishwe kwani ni wazi kwamba kila mfumo wa elimu unategemea uwezo wa kifedha toka kwa jamii na familia ni wazi haitakuwa na usawa (*inherently inequitable*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hilo, Kambi ya Upinzani, inaitaka Wizara husika kutoa majibu katika masuala yafuatayo:-

- (i) Je, nini hasa kiini cha poromoko hili katika elimu?
- (ii) Je, Serikali inafanya nini ili kuweza kukabili tatizo hili ambalo limeikumba sekta ambayo inajenga Taifa la kesho?

Mheshimiwa Naibu Spika Mtaala wa Shule ya Msingi. Mtaala ni msingi wa elimu ya mahali popote kwani bila mtaala wanafunzi wasingegekuwa na cha kusoma. Kwani mtaala ndio unaozaa masomo. Katika dunia ya sasa ya habari na mlipuko wa maarifa, nchi nyingi zinafikiria ni mambo gani yawe-*covered* ili kutosheleza mahitaji muhimu ya wanaomaliza elimu ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtaala wa elimu ya msingi Tanzania umeparaganyika ukiwa na maeneo mengi mno (*content areas*). Wanafunzi wanachukua hadi masomo 11 na hawa ni wanafunzi wa darsa la kwanza, tumesahau zile KKK ambazo ni K3 yaani Kusoma, Kuandika na Kuhesabu! Sasa hivi wanafunzi wanasoma masomo 11 ikiwamo Kiswahili, *English*, Hisabati, Sayansi, Stadi za Kazi, Haiba na Michezo, Maarifa ya Jamii, Teknohana, Dini, *French*, *Civics* na kadhalika. Hili ni tatizo kubwa hasa katika mazingira ya kutokuwa na Walimu wa kutosha. Labda hii ndio sababu wanafunzi hawafanyi vizuri katika yale masomo muhimu ya lengo la elimu kwa wote, yaani Kusoma na Kuhesabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhara ya mgawanyiko huu katika hatua za awali ni kutokuwa na umakini na uelewa mzuri wa masomo. Mjadala kuhusu kuunganisha masomo ya msingi yalifikiwa mwaka 1990's. Ni wazi kuwa pamoja na kuongeza masomo haya, hakuna bajeti ya kufundisha na kujifunza kwa mfano fedha za kusomeshea Walimu wa masomo haya mapya na vitabu. Matokeo yake vile vitabu vichakavu na uwiano wa Mwalimu na vitabu imekuwa mbaya na bajeti ni finyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema hapo awali, kuwa elimu ni chachu ya maendelo kwa Taifa lolote lenye dhamira ya kufikia kilele cha ustawi wa jamii katika nyanja zote za kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa. Lakini ili kufikia lengo hili, elimu inastahiki kutunzwa kwa sera endelevu na thabiti. Elimu ndio inayowawezesha ugunduzi wa kisayansi tena ni chimbuko la ustaarabu kote duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika suala la mitaala, itakuwa si busara Kambi ya Upinzani kutokugusia suala zima la shule zinazofundisha kwa kutumia lugha ya Kiingereza maarufu kwa jina *English Academy*. Hivi hii sera inayoruhusu shule hizi imeanza lini? Ni kifungu gani cha sheria ambacho kinaruhusu hili? Kambi ya Upinzani inapenda kujua kama sheria hii inaruhusu kuanzisha shule hii zinazotumia lugha ya Kiingereza pekee au pia lugha nyingine pia zinaruhusiwa, kama vile kuanzisha *French Academy, Italian Academy* au hata *Chaga Academy!* (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa chakula mashuleni. Ukosefu wa chakula mashuleni, ni tatizo kubwa nchini na linaleta adha kubwa kwa wanafunzi wetu. Kuwepo kwa chakula cha kutosha katika shule zetu, itahakikisha kuwa watoto wetu wanapata elimu inayotakiwa bila kuwa na fikra kuhusu chakula. Hii inatokana na ukweli kwamba watoto wanahitaji chakula kwa kiasi kikubwa kutokana na sababu nyingi zikiwemo za kibaiolojia ambazo zinahusiana na makuzi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili sio dogo na wala halihitaji kufanyiwa mzaha. Kwa sababu inasikitisha kuona kuwa shule nyingine hufikia hata hatua ya kufungwa kwa sababu ya ukosefu wa chakula. Kwa mfano, shule za sekondari za Manispaa za Tabora, zilizofungwa kwa sababu hiyo na Shule ya Kazima, Milambo, Shule ya Wasichana Tabora na Shule ya Wavulana Tabora, Kilosa pamoja na na Shule ya Sekondari ya Wavulana Bwiru. Mkoaa wa Mbeya na Rukwa nayo imeathirika sana. Inatia fedheha kuona kuwa sababu ya msingi ambayo ilipelekea shule hizi ni Serikali kushidwa kuwalipa wazabuni ambao wanasantaza chakula mashuleni kwa wakati. Hali hii inahitaji maelezo ya kina kunusuru elimu ya watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti tofauti zinaonesha ya kuwa ukosefu wa chakula mashuleni, husababisha wanafunzi wengi hasa katika shule za kawaida kuwa na uelewa mdogo darasani kutokana kutokuwa na lishe bora inayomwezesha kutulia darasani hadi mwisho wa masomo. Njaa imekuwa ni tishio kubwa mashuleni kwani ndio kimeonekana chanzo cha kushusha taaluma. Watoto wengi wamekuwa hawahudhurii madarasani kwa kushindwa kupata mlo utakaomwezesha awepo shule hadi mwisho wa vipindi hivyo na kuamua kushinda nyumbani au kutoroka shulenii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 30 Juni mwaka huu, Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliyahimiza wananchi wachangie wenyewe chakula hicho cha wanafunzi mashuleni. Hivi Mtanzania anasaadiwa nini na Serikali yake kama kila kitu ajitahidi mwenyewe? Hivi kwa nini Serikali inahamishia majukumu yake kwa wananchi walio wanyonge na wasio na uwezo? Mwanachi achangie ujenzi wa shule, anunue mavazi ya shule, alipie mwenge, wanunue karatasi za mitihani, vitabu, madaftari, walipie majengo, hivi faida ya kuwa na Serikali inayojali wananchi wake uko wapi? Hii kweli inamsaidia mwananchi au inamzidishia matatizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa chakula kwa maendeleo ya afya na taaluma watoto wetu, Kambi ya Upinzani, inahitaji ufanuzi unaojitosheleza ni kwa nini Wizara husika haikuwalipa wazabuni kwa wakati na hivyo kusababisha wanafunzi kurudishwa nyumbani bila ya kuzingatia watoto hao wako masomoni na mwisho wa siku wanapewa mitihani ya pamoja bila kujali usumbufu waliopata wakiwa shulen? Pamoja na hilo, Kambi ya Upinzani, inaitaka Wizara kueleza ni mkakati gani ambao wamepanga ili kuhakikisha kuwa tatizo hilo halitajirudia tena katika mwaka huu wa fedha 2008/2009. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tathmini ya Michango ya Wananchi. Katika nchi yetu, wananchi wanatimia idadi ya milioni 34,569,232 kwa kutumia takwimu za sensa ya mwaka wa 2002. Kati ya hao wananchi ambao wana umri wa kati ya miaka 20 hadi 60 ni 13,657,215. Lakini kwa kuzingatia hilo, tuchukue kata ndogo ya Mwampembele, Wilayani Nkansi, Mkoani Rukwa, yenyeye jumla ya watu 10,064 tuseme kati yao wenye uwezo wa kuchangia kuwa ni 8500 na kama kila mmoja atachangia shillingi 10,000, hii inamaanisha kuwa katika kata hiyo wananchi wameweza kuchangia shillingi 85,000,000. Hapo bado hatujaongeza mkono wa Serikali wala wa wafadhili katika ujenzi huo huo wa shule. Hivi nani mwenye mamlaka ya kuhakikisha kuwa hizi pesa za wananchi zinatumika kama ilivyopangwa? Pia ni nani mwenye jukumu la kuhakiki pesa hizo? Isije ikawa kuwa sisi tunahangaika na mafisadi wakubwa ilhali vifisadi vidogo vidogo vinaendelea kuzaliwa katika kata zetu! Je, vita hii itapungua? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutofanya tathmini ya pesa za wananchi, madhara yake hayaishii tu kwa wananchi bali hii inadhihirisha pia kwamba Serikali haitajua hata thamani ya rasilimali zake wenyewe. Hii ni hatari, kwani watu wachache wasio na mapenzi na maendeleo ya Watanzania wote kwa ujumla na waliojawa na tamaa watajichukulia nafasi hiyo na hivyo kujilimbikizia mali. Hii itazalisha ufisadi usioepukika kwa sababu, Serikali haitaweza kumkamata mtu huyu kwa sababu hajui hata wananchi walichangia kiasi gani. Kwa kuzingatia hilo, Kambi ya Upinzani, inahitaji ufanuzi wa kutosha ni kwa nini hakuna tathmini ya nguvu za wananchi katika ujenzi wa shule na hivyo kuweza kuwashakikishia wananchi juu ya matumizi ya fedha zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Vitabu vya Kiada Shulen. Wizara ya Elimu mwaka 1992 ilitoa tamko kwamba Serikali itajitoa katika kuchapisha vitabu. Pia mwaka 2004 Kamati ya Kuthibitisha Vifaa vya Elimu, iliundwa ili kuwezesha uwepo wa vitabu vya aina mbalimbali lengo likiwa ni wachapishaji waweze kuwa na ushindani wa kuchapisha na kusambaza vitabu mashulen ili mradi wapate vibali kutoka *EMAC* (*Educational Materials Approval Committee*), wanaoangalia ubora wa vifaa husika kwa ajili ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2005, Wizara ikapeleka madaraka ya kununua vitabu mashulen. Tunaamini kuwa utaratibu wa kupeleka madaraka ya kununua vitabu mashulen, ni mzuri na ni njia mojawapo ya kuboresha ubora wa elimu na kuboresha usomaji. Ni masikitiko makubwa kuona Wizara ikilipia gharama za uchapishaji wa vitabu na kuvipeleka mashulen. Hii ni kinyume na sera ya mwaka 1992. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kutoa maelezo ya kina juu ya utaratibu huu amba ni kinyume na sera hii. Kuna maswali ya kujuliza ni kwa nini Taasisi ya Elimu inachapisha vitabu vya shule za msingi na kwa nini Wizara imekuwa ikivinunua vitabu hivyo haswa ikizingatiwa kuwapo kwa ushindani wa kibiashara?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ubora wa vitabu hivi unatia shaka sana kwani inaonekana kama havijaidhinishwa na wala kuhakikiwa na *EMAC*, kitu ambacho ni kuwa vitabu vyote vya kiada vinapaswa kupita na ama kupitishwa (*certified*) na *EMAC*. Cha ajabu zaidi hapa ni kuwa Taasisi ya Elimu ni mjumbe wa *EMAC* kwa ajili ya kutathimini wachapishaji vitabu, wana wajibu wa kukuza na kuandika mitaala na kutoa mafunzo kwa Walimu. Ni kwa vipi tena wawe wachapishaji wa vitabu kwa mtaala huo huo huku wakishindana na wachapishaji wengine? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inajuliza na kuiuliza Serikali ni kwa nini Wizara na Taasisi wanataka kurudisha uchapishaji na urudufu (*printing*) wa vitabu kwa Taasisi ya Elimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inahoji pia ni kwa nini hakuna program za kujisomea Tanzania? Ukweli ni kwamba hakuna usomaji na haswa shule za msingi na pia hakuna msingi wa kujijengea tabia ya kusoma katika jamii kwani msingi huu ulipaswa kujengwa kuanzia mashulen na cha ajabu zaidi ni kuwa hakuna maandalizi yoyote ambayo yamefanywa ili kuweza kulijengea Taifa letu tabia hii kwani kila ukiuliza utaambiwa kuwa bajeti ni finyu na hairuhusu kununua vitabu na vifaa vingine muhimu kwa ajili ya kukuza tabia hii ya jamii kupenda kujisomea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kupongeza utaratibu mzuri wa shule kujinunulia vitabu, bado kunahitajika usimamizi mzuri zaidi kutoka Wizarani na kwenye Halimashauri husika kwani zimeshindwa kuthibiti utaratibu wa shule kujinunulia vifaa vya elimu, utaratibu uliopo sasa hauko wazi sana, matumizi mabovu ya fedha kama vile kupeleka sehemu nyingine fedha zilizokusudiwa kununulia vitabu na pia hakuna ufuatiliaji madhubuti ili kuhakikisha kuwa fedha zinatumika kwa ajili ya kazi ambazo zilikuwa zimekusudiwa na haswa kununulia vitabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania inatumia karibia dola 20 milioni kwa mwaka kwa ajili ya ununuvi wa vitabu, ambapo kati ya fedha hizo 95% ni kwa program za elimu zinazogharimiwa na Serikali au shule. Hivyo kwa mwaka kama Serikali inatumia \$20 milioni katika vitabu ukilinganisha na dola 700 milioni katika simu na dola 200 milioni

katika vinywaji (vileo). Ni lazima sisi kama viongozi tuone umuhimu wa elimu na kuipa elimu kipaumbele. Sasa hivi kila kukicha ni kuwa Bar mpya zinafunguliwa na wengine wamefikia hatua ya kuwa na *mini bars* majumbani mwao, sijui kwa hali hii watoto watapenda vipi kusoma, ni lazima pawepo na motisha kwenye ujenzi wa maktaba na vituo vya elimu utolewe ili watu wetu waweze kujenga utamaduni wa kujisomea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu ya Walimu. Moja kati ya wadau muhimu katika elimu ni Walimu wenyewe. Uwekezaji katika Walimu ni jambo muhimu sana. Tanzania tunamshukuru Mungu, vyuo vinavyofundisha fani hii ya Ualimu katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, umeongezeka kutoka 53 hadi 55 sawa na ongezeko la asilimia 3.6. Hili linaonyesha dhahiri kuwa sasa Watanzania tunatambua umuhimu wa kuwekeza katika elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini linalotupa shaka Kambi ya Upinzani, ni idadi ya wanafunzi katika vyuo hivyo. Kwa mfano, idadi ya wanafunzi katika vyuo vya ualimu vya Serikali ilipungua kutoka 26,681 mwaka 2006 hadi 18,754 mwaka 2007. Wakati idadi ya wanafunzi wa Ualimu kiwango cha Diploma ilipungua kutoka 7,411 mwaka 2006 hadi 5,959. Idadi ya wanafunzi wa Ualimu Daraja A ilipungua kutoka 11,609 mwaka 2006 hadi 3,238 mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa ya Serikali ya hali ya uchumi katika mwaka huo wa 2007/2008, sababu iliyotolewa na juu ya upungufu huo, ni kuongezeka kwa wigo wa masomo katika vyuo vikuu vya ndani. Kambi ya Upinzani, inaona kuwa hoja hiyo ni dhaifu na haiwezi kukidhi katika kujibu hoja hii, kwa sababu zifuatazo:-

- (i) Vyuo vya Ualimu vinawezaje kuongezeka lakini vikaweza kuchukua kiwango kidogo cha wanafunzi kuliko kile cha mwaka jana?
- (ii) Wigo wa elimu ulipanuka tofauti na mwaka jana?
- (iii) Je, ni nini hasa kilichopelekea kupungua kwa wanafunzi katika fani hii?
- (iv) Baada ya kulitambua hilo je, Serikali ilichukua hatua gani katika kutatua tatizo hilo hasa ukizingatia kuwa nchi inakabiliwa na tatizo la upungufu wa Walimu? Kwa mfano, Wilaya ya Sengerema pekee yake ina upungufu wa walimu zaidi ya 1,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubora wa elimu ni muhimu na unatokana na ubora wa ufundishaji. Kwa sasa shule za misingi zinafundishwa na Walimu wa *Grade A* (70%) wengi wao hawajaweza ku-*internalize* na kufundisha mitaala vizuri kwani hata wao walikuwa na ufaulu mdogo kwa *Form IV*. Bado wapo Walimu wahitimu wa darasa la saba ambao ni Walimu wa *Grade B/C* 26.9% wakati wa Diploma ni 2.8 % na wenye Digrii ni 0.2% tu. Hii ni hatari kwa ubora wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi kama USA shule za msingi hufundishwa na wenye Digrii wakiamini kuwa huwezi kuacha kizazi cha vijana katika hali duni ya kiakili. Ni wakati muafaka sasa Tanzania kufuta kabisa *Grade B/C* ya Ualimu na pia wabadili *Grade A* kwenda kwenye Diploma ili tuboreshe elimu yetu ya msingi. Ninaamini katika dunia ya sasa ambapo wimbo unaoimbwa ni anga sio tena mwisho wa akili inayojengwa na uelewa thabiti na kuongozwa na wataalam waliobobe, mwanzo wa akili za vijana zinahitajika kilicho bora zaidi na sio walioshidwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, panapokuwa na janga kubwa, ni lazima tupime na kulitatua kwa makini. Ni lazima tuwe na uwezo wa kuhakiki yale yote yanayotokea darasani. Watanzania tuna mtazamo hasi kwamba darasa ni mwalimu pekee. Ni mara chache sana Walimu Wakuu wa masomo kuingia darasani na wakaguzi ni mara chache na pengine kutoenda kabisa huku tukijua ufundishaji ni mbovu sana. Mbaya zaidi muda wanaotumia watoto shulenii unatosha, lakini muda unaotumiwa kwa kufundishwa ni mdogo sana zaidi ya majaribio ya mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa wanafunzi katika taaluma ya ualimu inafedhehesha nguvu za wananchi katika ujenzi wa shule, hivyo basi, Kambi ya Upinzani inataarifu Wizara husika kuchukua hatua za haraka katika kutatua tatizo hili ili kuweza kukidhi mahitaji ya walimu katika shule zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chama cha Walimu Tanzania (*CWT*) ni ukweli usiopingika kuwa walimu ndio watekelezaji wakuu na muhimu katika utoaji wa elimu bora na sio bora elimu. Kama walimu hawakuandaliwa vizuri kimaisha, katika mazingira yao ya kazi na pia mahali wanapoishi, hata kama Serikali itajenga madarasa na mashule mengi kwa kutumia almasi na dhahabu, bado elimu itakayotolewa haitakidhi viwango vya kimataifa katika ulimwengu huu wa utandawazi.

Kwa kuzingatia hilo, leo Kambi ya upinzani inataka matatizo ya walimu yatatuliwe haraka, kwa sababu taaluma ya ualimu inadharaulika na kuendelea kutovitia vijana wetu. Sikatai kuwa hii inawezekana kuchangiwa na sababu nyingine, lakini kero za kudumu ndani ya Wizara hii ambazo zinaendelea kurudisha maendeleo ya walimu nyuma, ni moja ya sababu ya msingi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sijui sababu ya msingi ni nini hasa, lakini kila mwaka tunaongelea suala la kupunguza madeni ya walimu kwa Wizara husika, lakini ulimbikizaji wa madeni unendelea.

Pamoja na kuwa Serikali iliahidi kutolimbikiza madeni baada ya Tume ya Waziri Mkuu ya 2004, lakini nasikitika kusema kuwa ndani ya mwaka huu pekee madeni yaliyokusanya ndani ya Mikoa mitano tu, Wilaya 30 tayari Serikali inadaiwa wastani wa Shillingi bilioni 6.3. Hii itakwisha lini? Hivi Serikali ya awamu ya nne ina mpango gani na walimu wa nchi hii ambao ni muhimu sana kwa maendeleo ya jamii zetu? Au inasubiriwa karibu na uchaguzi ndio walipwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, kero za walimu sio tu katika upande wa malimbikizo, bali moja katika matatizo sugu ambayo huwapata walimu ni katika suala la kupandishwa madaraja. Kumekuwa na kero ya walimu wenyewe uzoefu tofauti kulimbikizwa katika cheo kimoja, lakini pamoja na Serikali kuchukua hatua mwaka 2006, baada ya Mheshimiwa Rais kuagiza, hii ni sawa na mtu aliyechochea moto badala ya kumwagia maji ili chakula kisiendelee kuungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inakatisha tamaa na inasababisha walimu waendelee kuwa wanyonge kama vile raia wasio na haki na taaluma ya kujivunia. Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri mhusika atueleze hasa, sababu za msingi hasa ni zipi zinazosababisha kero hii iendelee kukomaa? Je, Wizara inasubiri nini ili iweze kuchukua hatua?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaungana na walimu wote Tanzania na inapenda kuwatanabahisha kuwa iko nao siku zote, kwa kutumia nafasi yake itaendelea kuikumbusha Serikali juu ya matatizo yanayowakuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalamu wa elimu kwa muda mrefu wamekuwa na njia mbalimbali za kupima juhudzi za nchi katika nyanja ya elimu. Kwa vyovvye vile, kiwango cha ushiriki (*participation rate*) ndicho kipimo kitumikacho.

Kwa mfano, uandikishaji wa udahili wa watoto unaonyesha Tanzania kufanya vizuri sana katika elimu ya msingi, lakini kwingine haiendi vizuri kwani *pyramid* inakuwa nyembamba sana kadiri unavyoolekea juu.

Kwa mfano, elimu ya msingi 97.3%, sekondari 11% na elimu ya juu ni 2.2% tu. Ukiilinganisha na majirani zetu Kenya ni 23% elimu ya sekondari na elimu ya juu ni 3%, Uganda ni 12% elimu ya sekondari na elimu ya juu ni 3%. *UNDP Human Report (2007)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida viwango vya ushiriki vinatokana na kiasi cha rasilimali kilichowekwa kwenye elimu na hivyo kila mara lazima tarakimu mbili ziwe sambamba nazo, ni *GDP* (utajiri wa nchi na asilimia ya bajeti ya Serikali).

mHESHIMIWA sPIKA, Ni ukweli kuwa bajeti ya elimu Tanzania bado sio ya kuridhisha sana pamoja na kupewa kipaumbele ukilinganisha na jirani zetu. Kwa uchumi mdogo na idadi kubwa ya watu, rasilimali bado ni ndogo kwa kazi tulionayo mbeleni.

Ulinganishi wa fedha kwa ajili ya sekta ya elimu 2006/2007

Nchi	GDP%	% Bajeti ya mwaka
Tanzania	4.5	18.10

Kenya	6.4	29.0
Uganda	4.2	26.0
Malawi	5.3	25.0

Source: World Bank (2007) BEST (2007)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania lazima ifikirie mara mbili kuhusu rasilimali inayoelekezwa kwa sekta ya elimu, kama kweli tunataka malengo ya MKUKUTA na Dira ya Maendeleo ya 2025 yafikiwe. Kama kawaida, suala muhimu ni uwezo dhidi ya utayari wa kugharamia huduma za elimu. Hali inayojionyesha katika jedwali, upanuzi wa mfumo wa kupata viwango shirikishi vya asilimia 100 kwa elimu ya msingi, 50% ya sekondari *O-level* na 25% *A-level* na 12.5. Elimu ya juu, itapima kwa uzito wa hali ya juu tayari (uhiari) wa Serikali kugharamia badala ya uwezo kugharamia elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, ni ushauri wa Kambi ya Upinzani kwa Serikali kujitahidi na kuwa na utayari wa kugharamia elimu kwani elimu ndio chimbuko la maendeleo na ni haki ya msingi ya binadamu kama ilivyo kwenye 1948 *United Nation Declaration*. Ni lazima kuwa na uwiano katika mfumo mzima wa elimu. Sasa hivi kuna msukumo wa kijamii kuliko wa kiuchumi katika elimu ya sekondari na ile ya juu na kidogo sana katika elimu ya ufundi na ile isiyo ya vyuo vya elimu ya juu, yaani *non-tertiary* kama inavyojionyesha katika jedwali lifuatalo:-

Uandikishaji kwa jinsia, Aina na ngazi: 2007

NGAZI	ME	KE	Total	%
Awali	387,868	407,143	795,001	7%
Msingi	4,215,171	4,107,754	8,316,925	81%
O Level	511,416	455,671	967,087	9%
A Level	31,780	21,643	53,423	1%
Vyuo Vikuu-Umma	27,937	13,341	41,278	0.4%
Vyuo Chini ya				
Wizara Nyingine	9,645	7,227	16,872	0.2%
Vyuo Vya Ualimu-Dip	10,036	8,718	18,754	0.2%
Ufundu	2,777	767	3,544	0.05%
Vyuo Vikuu Binafsi	6,713	4,033	10,752	0.01%
Jumla	10,223,606	100%		

Chanzo: BEST (2007)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa katika elimu ya sekondari. Tukiwa na *Gross Enrollment Ratio* ya 5% (2004) na sasa kufikia 11% kwa nchi ya watu takribani milioni 40, ni vigumu kusema kwa uhakika kama tunaendelea vizuri.

Jedwali la 4: Viwango vya Ushiriki kwa Shule za Sekondari

Nchi	Viwango%
Tanzania	5
Kenya	23
Uganda	12

Liberia	23
Lesotho	20
Namibia	34

Mheshimiwa Naibu Spika, Ongezeko la 50% kwa wanaofaulu kuingia sekondari za serikali na wale wanaokwenda shule binafsi kutapelekea kuona mabadiliko makubwa. Pamoja na kwamba malipo yake ni kidogo, mfano *USD 20 kwa day Schools* na karibia *USD100 kwa boarding schools*, bado wazazi wengi zaidi 50% wanaishi chini ya mstari wa umasikini na wenye familia kubwa watashindwa kulipia watoto hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule nzuri za Serikali zimetawanyika nchi nzima kwamba mtoto anaweza kusafiri kilometra 1,000 na zaidi kwenda shule, mfano Sumbawanga kwenda Ilboru na kadhalika. Hii inapelekea wengine washidwe kusafiri kutohakika na nauli.

Ujenzi wa shule za kata ni mzuri, lakini zile jamii maskini zimeshidwa kutumia mwanya huu. Lakini inaonekana pamoja na wazo la kujenga shule hizi zitapelekea kutokuwa na usawa ambavyo inaweza ikaleta mashaka katika jamii ya kutokuwa na amani ama upatanifu hapa baadaye, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kutenga kiasi kidogo cha rasilimali kila mwaka kwa nia ya jamii ambazo hazina uwezo wa kujijengea shule.

Aidha, tunashauri kuwa ule mwongozo wa kukataa katika maeneo yanayozunguka shule, kusiwe na milango ya biashara ufutwe ili kuwawezesha Halmashauri kushirikiana na sekta binafsi katika kuziboresha shule na kuzifanya zijitegemee, ili mradi maadili yalindwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu bora hujenga uchumi bora. Lakini ubora wa elimu umeangalia jambo moja la msingi nalo ni maarifa yatolewayo kuanzia kukumbuka (*memorization*) hadi kuainisha kufikiri na kutatua tatizo kwa kuweza kutathmini, kupanga, kusaini na kutumia kanuni kutatua matatizo ya maisha na maendeleo kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushahidi unaonyesha kwamba ubora wa elimu katika masomo yafundishwayo inatoa mchango mkubwa kwa jamii na pia kwa mtu binafsi . Kwa hiyo, thamani ya fedha (*value for money*) na kwa mantiki hiyo shule nzuri zinakuwa na mdondoko mdogo na pia wakariri wachache na hivyo zinachangia mafanikio ya kitaaluma na uzalishaji uchumi bora wa baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunajua umuhimu wa masomo ya sayansi katika dunia ya leo. Hali ya Sayansi katika nchi yetu ni tishio na hatua zisipochukuliwa tutakuwa na madaktari na maprofesa wa tunguri. Hakuna maabara katika shule nyingi na zilizopo hazitumiki kwa kukosa vifaa na mbaya zaidi ni kwenye shule za jumuiya.

Ukweli ni kwamba uanzishwaji wa shule za jumuiya na sasa Kata italeta mifumo miwili (mlinganisho) *parallel* moja wa matajiri na mwingine wa maskini. Bila kukusudia

tunaua elimu kwa watoto masikini na wakulima kwa kuwa wataendelea kuwa kwenye mzunguko wa umasikini, usio na matumaini badala ya kuwa katika mzunguko ulio uadilifu bora na wa matumaini. Hii ni taaluma dhalimu (*apartheid*) ambavyo ni lazima iepukwe kwa garama yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya kujifunza na kufundisha sayansi na hisabati; kwa kawaida kunakuwa na mitihani ya darasa la 4, 7, Kidato cha II, na IV na matokeo huwa yanakuwa kwenye daraja la “A, B, C, D, E”. Daraja D na E ni kufeli. Mtihani wa msingi (7) mwaka 2000 ulitoa viwango vya kufeli kwa 78% yaani kwa wale waliopata chini ya alama 60% kati ya 150. Katika shule za sekondari ukichukua alama A, B, C kama kufaulu kidato cha nne, viwango vya kufeli katika masomo ya Sayansi inatisha. Kwa hiyo, ni vyema kukawa na mkakati wa makusudi kukazania masomo ya sayansi kwa kuwa sasa imefika pabaya au hatari vyovytote vile, Maarifa ya namba hasa katika hisabati na fizikia zimekuwa hatarini hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imeamua kwa makusudi kuweka mkazo kwa masomo ya Sayansi na teknolojia kwa kuwa uchumi wetu unasukumwa na teknolojia na ufahamu (*knowledge based*). Uwepo wa msukumo kidunia na kiutandawazi, huu ni mwelekeo chanya na unawakilisha mawazo mazuri ambayo yataletea:-

- (a) Kufundisha wanafunzi vizuri msingi wa sayansi;
- (b) Kufundisha hisabati na teknolojia (*basic*) vizuri kwa wanafunzi;
- (c) Kufundisha lugha ya Kiingereza vizuri kwa wote kwani duniani lugha hii inatumika; na
- (d) Kuhakikisha tunatoa upendeleo kwa kuwaingiza shulenii wale wanaopenda hisabati, sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonyesha kuwa bado vyuo vya elimu ya juu vina wanafunzi wachache katika fani ya sayansi. Hili limepelekea kuwa na madaktari wachache sana na manesi wachache. Kambi ya Upinzani inashauri Serikali iwekeze kwenye sayansi sasa kwa kutoa ufadhili (*Grant*) kwa wanafunzi wanaofanya vizuri kwenye masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna tishio kubwa, kwani wanafunzi waliochukua masomo kama kemia, fizikia, teknolojia, hisabati wameonyesha uwezo mkubwa wa kuchukua uhasibu, utawala, sheria, biashara na uchumi na hivyo kupata ajira haraka pindi wamalizapo. Hivyo, mahitaji ya wanafunzi wa sayansi bado inaendelea kupanda kwa kasi na hivyo ni vigumu kwenda na kasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa kama Tanzania inataka kufikia lengo la dira ya 2025 na MKUKUTA, basi ni lazima hali hii ibadilishwe mara moja kwa kuwa na Kamati ya Bunge itakayoanzisha mchakato wa mabadiliko. Changamoto sio ufundi au sayansi inayohitaji suluhisho, bali maendeleo ya jamii katika kununua sura na hali (*profile*) ya sayansi na teknolojia ndani ya jamii na uchumi kwa ujumla, Kamati hii iwe shirikishi na wajumbe mbalimbali kwa kila sekta kama sekta ya watu binafsi, viwanda, wanataluma na kadhalika. Tunaamini kuwa tatizo la kijamii lazima lipatiwe utatuzi wa kijamii na huu utakuwa ni mkakati wa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mashaka kwamba elimu ya juu inachangia sana uzalishaji kwa Taifa katika nyanja zote za maisha ambazo baadaye inabainisha kiwango cha ubora wa viwango vya maisha, kwani siku zote pato huboreshw na uzalishaji. Uwezo wa nchi yoyote kushindana kiuchumi katika ukanda na kimataifa utategemea sana katika elimu ya juu. Uchumi wote duniani unaongezeka kwa kutegemea teknolojia na maarifa ya hali ya juu ambapo bila elimu ya juu nani atashindana? Taasisi za teknolojia (utafiti na Mafunzo) vinatoa msaada mkubwa kwa teknolojia na maarifa yanayoendesha ukuaji wa uchumi na hivyo kupunguza umasikini na sio wa darasa la saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya juu ni muhimu sana, kwani mbali na kutoa wafanyakazi kwa sekta mbalimbali nchini na nje, pia inajenga uwezo wa kushiriki katika dimbwi linalokuwa la dunia ya maarifa na kuweza kupokea na kutumia maarifa hayo hapa nchini. Ni dhahiri kuwa elimu ya juu inaweza kuletelea ubunifu, uvumbuzi na kugundua mbinu ambazo zitasaidia maendeleo katika nyanja zote za maisha. Katika nchi maskini kama yetu, elimu ni sharti ileté mabadiliko ya kudumu. Kama tunataka kukuza uchumi wetu wote, hilo halitawezekana kama hatutajenga uwezo katika mfumo wa elimu ya juu. Hivyo ni muhimu sana kutegemeana na kuimarisha mahusiano kati ya elimu katika ngazi zote za uchumi kwa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ngazi za elimu ya juu, zinaonyesha ufinyu mkubwa kufikia, yaani kwa idadi yake na umbali wa kuvifikasi (*physical access*). Uwezo wa kuchukuwa wanafunzi wengi pia ni mdogo kwa mfano vyuo vyote vya umma havijafikia wanafunzi 50,000. Ukijumlisha idadi ya wanafunzi wote katika vyuo vya ufundi, Mbeya, Karume, Arusha na Dar es Salaam hata hawafiki 3500. Vyuo vingine 18 vinavyotoa Diploma kwenye Wizara mbalimbali vinachukua wanafunzi 16,873 tu. Wanafunzi wengi wanaomaliza kidato cha Nne hawapati nafasi katika *A-level* na zaidi ya 50% wanaomaliza kidato cha sita hawafaulu kujiunga na Elimu ya Juu, hivyo viwango vya ushiriki (*participation votes*) vimeendelea kuwa chini sana kama jedwali No. 5 linavyoonyesha:-

NA.	NCHI	V/U	NA	NCHI	V/U
1	Tanzania	2.2	15	Sri Lanka	5
2	Brazil	18	16	Mauritius	21
3	Botswana	4	17	Australia	65
4	Ivory Coast	7	18	Korea kusini	82
5	Misri	38	19	Ufaransa	54
6	Ghana	5	20	Uingereza	59
7	Namibia	7	21	Canada	59
8	Senegal	5	22	Amerika	81
9	Africa Kusini	15	23	Uganda	3
10	India	11	24	Kenya	3
11	Malaysia	27	25	Nigeria	10
12	Thailand	37	26	Rwanda	3
13	Jamaica	17	27	Ethiopia	3
14	Singapore	45			

Chanzo: UNESCO (2006), World Bank (2007)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa uwezo, elimu ya juu bado inawezekana kwa wengi hasa baada ya Serikali kutoa mikopo ya ada, malazi, chakula na vitabu. Lakini bado vyuo vikuu nyeti viko mashariki mwa nchi hivyo baadhi ya wanafunzi kutoka Kaskazini, Magharibi na Kusini yawapasa kusafiri umbali mrefu sana kilometra 1000 hivyo kupelekea masuala ya usawa katika kupata elimu hiyo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu, akili za kawaida na tafiti zilizofanywa katika jamii mbalimbali zinaonyesha kwamba umuhimu wa elimu ya juu katika nyanja zote za uchumi na maendeleo ya watu kwani inasaidia (*promote*).

- (1) Kukua kwa uchumi, inaboresha mapato na kipato, inaongeza uzalishaji, ujasiriamali, inaongeza pia kukua kwa jamii, ushiriki katika siasa na utawala wa kidemkrasia, kuondoa umasikini na uboreshaji wa umri wa kuishi na ubora wake.
- (2) Uongofu kwa viongozi, elimu inawapa ujasiri kuongoza kwa uadilifu, Maarifa na Maarifa ya teknologia na pia kutengeneza kada za walimu bingwa katika ngazi zote za elimu nchini

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo makubwa manne yanayohitajika katika mfumo wa elimu yaani kupata elimu hiyo kwa watoto wengi bila kujali rangi, dini, jinsia na utaifa, umuhimu wake kwa mahitaji ya watoto, familia na mahitaji ya uchumi; ubora wake kwa maana ya kupata Maarifa na mtazamo. Mfumo wetu wa elimu unahitaji uwazi/unyofu na uainisho wa uhakiki (*intrinsical analysis*) ili kuwa na elimu bora na si bora elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya kuwakopesha wanafunzi asilimia 20, 40, 60 na wao kuchangia gharama za mafunzo yao kwa asilimia tofauti itaendelea kuwa chanzo cha migomo isiyokwisha katika vyuo vyetu vikuu. Serikali intaka kufanya elimu ya juu kuwa matakwa ya mtu binafsi badala ya mahitaji ya kijamii. Wakati mashirika haya dunia ya fedha yakitushauri sisi kuacha kuwekeza katika elimu ya juu, Serikali za huko kwao zimejiwekea utaratibu wa kuhakikisha kuwa hakuna mtu anayeshindwa kusoma Chuo Kikuu kwa sababu ya kukosa pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tamko la kuchangia asilimia 40 na zaidi ni gumu sana na litarudisha nyuma juhudini hizi za Serikali za kuongeza namba ya wanafunzi katika elimu ya juu na kuongeza namba ya Watanzania wenye elimu ya juu. Watanzania wengi hawaelewi maana ya asilimia 40 ya gharama za elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama kubwa kabisa ni ada ambayo hutofautiana kufuatana na aina ya shahada na hata chuo. Kwa mujibu wa mwongozo huu, ada ya chini kabisa ni ile inayotozwa katika vitivo vya elimu, sanaa na sayansi ya jamii na uhandisi ambayo ni Sh. 600,000/= kwa mwaka. Gharama nyingine na bila kujumlisha gharama ya malazi kwa mwanafunzi anayesoma shahada ya kwanza zilizotajwa hapo juu, ni Sh.1,564,500/. Asilimia arobaini ya hii ni Sh. 625,800/. Kwa hiyo, gharama ya chini kabisa ambayo Serikali intaka mzazi wa mwanafunzi anayesoma Chuo Kikuu achangie

ni Sh. 625,800/= kwa mwaka. Kwa kuthibitisha hilo, hata baada ya mgomo wa Vyuo vya *UDSM* na *SUA* pamoja na Vyuo Vikuu Shiriki ni asilimia 41.8% ndio waliyoweza kulipa na 58.2% walishindwa kulipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaritibu wenyewe unaonekana hauna uwiano. Kwa mfano, mwanafunzi wa Chuo cha Ardhi analipa Sh. 720,490/= kati ya Sh. 1,754,150/= wakati *group D* analipa Sh. 561,600/= kati ya Sh. 936,000/=

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii inagusa pia gharama za mafunzo kwa vitendo. Asilimia 40 inapunguza gharama za mafunzo kutoka Sh. 6,000/= ambazo ukitoa asilimia 80 inabaki Sh. 1,200/= kwa siku. Kwa hali ya uchumi ilivyo sasa, kweli wanafunzi hawa watamudu kufanya mafunzo kwa vitendo katika sehemu walizopangiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa ripoti ya Serikali ya hali ya umasikini na maendeleo ya watu ya mwaka 2005, kipato cha wastani kwa Mtanzania ni Sh. 9,900/= katika siku 28 (mwezi) kiwango ambacho inasemekana kimekua kwa asilimia chache sana mwaka jana. Kwa kiwango hiki na kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya kupima umasikini, asilimia 57.5 ya Watanzania ni maskini wa kutupa. Hii inamaanisha kwamba, pato la wastani la Mtanzania kwa mwaka ni Sh. 546,956.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tujiulize, Serikali inaposema wazazi walipie asilimia 40 ya gharama za kusoma Chuo Kikuu (zaidi ya Sh. 625,800) inawalenga Watanzania gani? Kwa takwimu hizi, zaidi ya asilimia 50 ya Watanzania hata kama wangeamua kuacha kula, kutibiwa ambako wanachangia pia gharama na kuvala kwa mwaka mmoja, wasingewenza kumudu hata asilimia 10 ya gharama za kumsomesha mtoto wao mmoja katika vyuo vyetu vikuu vya umma? Kwa misingi hii, hata vyuo vikifunguliwa vipyta watasoma akina nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya upinzani inasisitiza kuwa, Watanzania kwa hali ya umasikini tuliyonayo, wazazi wengi wa Kitanzania hawawezi kumudu gharama za watoto wao kusoma Chuo Kikuu. Serikali ina uwezo wa kulipia gharama za elimu ya juu kuititia Bodi ya Mikopo bila kutetereka na kuwapatia wanafunzi mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, Kambi ya Upinzani inaendelea kuhoji yafuatayo kuhusiana na mikopo. Hadi kufikia June, 2008 ni kiasi gani cha fedha ambazo zilitolewa kama mkopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu nchini na kwa wastani wa shilingi ngapi kwa kila mwanafunzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, jinsi mikopo inavyotolewa inapendelea vyuo vya binafsi. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja wa Chuo Kikuu cha Umma analipa ada kama Sh. 600,000/= na Chuo cha binafsi mwanafunzi mmoja analipa kama Sh. 2,500,000. Hivyo kwa mwanafunzi mmoja, chuo cha binafsi kitapata Sh. 1,900,000 zaidi ya kile cha umma. Matokeo yake vyuo vya umma ambavyo ndiyo kimbilio la wanyonge na ambavyo ndiyo vinatoa elimu kwa idadi kubwa zaidi ya wanafunzi, vinakosa pesa za

kuboresha miundombinu ya utoaji elimu na vinashindwa kuwapa wanafunzi hawa elimu iliyo bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vyuo vya elimu ya juu binafsi, tunaendelea kushauri Serikali yetu kufanya yafuatayo, kuvifua tilia kwa karibu vyuo hivi ili kuhakikisha vinaweka mbele umuhimu wa kukidhi viwango kuliko manufaa ya kibashara. Serikali ihakikishe kuwa vyuo hivi vinatambua umuhimu wa kusaidia utoaji wa elimu hiyo kwa Watanzania wote bila ya kuangalia tofauti za kimapato, kiitikadi, kidini na hata kijinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ihakikishe kuwa wenyeji wa maeneo ambayo vyuo vikuu hivi vinapatikana, hasa katika ile Mikoa ambayo wenyeji wake wapo nyuma kielimu kama ilivyo kwa Mkoa wa Morogoro, wanafaidika na kuwepo kwa vyuo katika maeneo yao. Serikali ihakikishe inalipitia upya suala la kulipia wanafunzi wa vyuo binafsi kupitia Bodi ya Mikopo ama ruzuku mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya upinzani inaipongeza Serikali kwa kuongeza kiasi cha posho za wanafunzi kutoka Sh. 3,500/= hadi Sh. 5,000/=. Bado kiasi hiki hakitoshi. Kambi ya Upinzani pia inapendekeza kuongezwa kwa posho ya mafunzo kwa vitendo na visifanyiwe *mean testing*, kuongezwa kwa viwango vya malipo wanayopewa wanafunzi kwa mahitaji yanayohusiana na masomo ya wanafunzi kama vile *stationaries, study tours*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzishwa kwa vyuo vikuu vipyta na kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga katika vyuo vyetu ni lazima kuendane na juhudhi kubwa za kuboresha mazingira ya kazi ya wahadhiri na wasomi watarajiwu. Vyuo vyetu vikuu hivi sasa na vile vya kihistoria kama Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na vile vilivyo zaliwa upya kama Chuo Kikuu cha Mzumbe, kwa miongo kadhaa sasa vimekumbwa na tatizo la kubwa la upungufu mahitaji muhimu. Mapungufu hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) Upungufu, ufinyu na uduni wa vyumba vya miadhara. Vyuo vyetu vimekuwa vikikumbwa na tatizo hili kwa miaka kadhaa sasa.

(b) Ukosefu wa maabara za utafiti na mawasiliano ya kompyuta. Hali hii imepelekea wasomi wetu kuacha tabia za utafiti wa kisayansi na kulazimisha hata wanafunzi wetu kufanya mitihani inayopaswa kufanyiwa utafiti wa kimaabara kwa kutumia kifaa kimoja kwa watu zaidi ya kumi. Wengine kutumia njia ya nadharia tu kukamilisha tafiti zao.

(c) Ukosefu wa wahadhiri wa kutosha na walio na sifa za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuona umuhimu wa wahadhiri wetu na kuwaongeza mishahara yao kwa asilimia mia. Hii sio tu itawafanya vijana wengi wafanye vizuri ili wabaki vyuoni kama wahadhiri, bali pia itawafanya wahadhiri wengi kutokukimbilia nje ya nchi, hivyo kujenga ile dhana ya uzalendo, tofauti na ilivyokuwa huko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hayo Serikali haikupandisha mishahara ya wafanyakazi katika Taasisi hizi, wasio wahadhiri (*non teaching staff*) ambao uzoefu unaonyesha kuwa wanafanya kazi zinazofanana na kuwiana, pia makundi haya yanategemeana kiutendaji. Aidha, sababu nyine ambazo zinawafanya wastahili pia kuongezewa mishahara ni kama vile, ongezeko la idadi ya wanafunzi, kupanda kwa gharama za maisha, kuhama kwa wanataaluma na kushindwa kuajiri wanataaluma wa ngazi za juu kutokana na mishahara kuwa midogo. Kazi za watumishi hawa zinachangia sana katika ufundishaji na utafiti. Utekelezaji wa uboreshaji wa mishahara hiyo iliamuliwa ufanyike katika awamu mbili. Aidha, kutotekelezwa kwa maamuzi wa upande wa waendeshaji kutaathiri ubora, viwango na thamani ya elimu inayotolewa katika vyuo vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuwaengua wafanyakazi waendeshaji katika utekelezaji wa maamuzi ya Kamati kumeleta matatizo mengi, kama kuwepo kwa tofauti kubwa kati ya mfanyakazi mwanataaluma na mfanyakazi mwendeshaji. Tofauti hizi zimetokana na kutekelezwa kwa maamuzi ya Kamati kwa upande mmoja wanataaluma na kuacha kundi lingine la wafanyakazi waendeshaji wakati maamuzi ya Kamati yalizingatia kulinda uwiano uliokuwepo kabla ya utekelezaji huu wa kibaguzi. Kambi ya Upinzani inasilitiza kuwepo kwa uwiano na kuboresha mahusiano haya ya kipekee. Jitihada za kuboresha mazingira ya kazi kwa wakati wote zililenga kuwakwamua waliomo katika mazingira ya kazi kwa kuzingatia uhalali na uwiano lingenifu mionganoni mwa watumishi wote. Tunaitaka Serikali itoe tamko ni lini wafanyakazi hawa watatekelezewa maamuzi ya Kamati ya Rais ya Oktoba, 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba katika kikao cha bajeti cha mwaka juzi na jana katika Bunge hili Tukufu, Mheshimiwa Waziri akijibu hoja hii, alisema, suala hili linafanyiwa kazi. Kambi ya Upinzani inataka kujua ni kwa kiasi gani suala hili limetekelizwa katika bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo lisilopingika kwamba elimu katika ngazi ya juu ni gharama kubwa na sio jambo la kubishana ya kwamba elimu ya juu inahitaji kupanuliwa. Hili ni jambo muhimu na la haraka ambalo ni kipaumbele. Ni dhahiri kabisa pia kwamba uchumi wetu unaweza kulipia gharama zitakiwazo kwa elimu hiyo. Kusema tu hakuna fedha, hilo sio jibu la kweli. Ukweli ni kwamba, fedha zipo, suala hapa ni namna gani tunagawa fedha kwa ajili ya matumizi mbalimbali na kama kweli tunajali maendeleo ya wananchi wetu na ya nchi yetu. Jambo hasa ni katika namna tunavyochagua vipaumbele na kwa hiyo, ni lazima kujua kwamba ipo haja ya kuacha mengine kwa ajili hiyo. Kwa hiyo, kama tunajali na tunaamua kuwa elimu ni kipaumbele, basi bajeti itatengwa kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana atoe tamko kuwa madai ya nyongeza ya mishahara kwa wafanyakazi waendeshaji ni halali na ni lini watalipwa? Kwa pamoja, tuamue kweli na tuone nini kinaweza kufanyika katika kurekebisha hali hiyo na kupata ufumbuzi wa kudumu na endelevu?

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya Wizara kwa ujumla, sote tunafahamu ya kuwa wananchi wetu wanaishi katika mazingira magumu na yenye umasikini mkubwa. Kwa kuzingatia hilo, bajeti yetu ya Serikali imekuwa ikitafuta kila namna ili tu kuhakikisha kuwa tunamsaidia Mtanzania huyu kuondokana na umasikini uliokithiri. Tunapokuwa tunapanga kiasi gani cha pesa kiende wapi, pia huangalia kiasi gani cha pesa kilitumika vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuikumbusha tuu Serikali, naomba kuwataarifu kuwa katika bajeti ya mwaka 2007/2008 kama yalivyochambuliwa katika kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa, Jedwali Na.26, elimu imetumia shilingi bilioni 552.7 sawa na asilimia 51 tu ya fedha zilizotengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama pesa iliyotengwa mwaka jana sekta hii ilishidwa kumaliza: Je, leo bajeti yetu inaipangia tena sekta hii kiasi cha shilingi trillioni 1.43 sawa na mara mbili na uchee ya zile za mwaka jana, hivi katika hali ya kawaida tu sekta hii itaweza kutumia pesa hizi? Kwa nini sekta hii ilimbikiziwe pesa nyingi ilhali tunafahamu kuwa haitaweza kuzitumia? Kwanini basi hata kama kunahitajika ongezeko kubwa, kwa nini basi katika mwaka wa fedha wa mwaka jana ilishidwa kutumia karibu ya asilimia 50 iliyopewa? Kwani kunaongezeko gani la mahitaji ambalo mwaka wa 2007/2008 halikuwapo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, Kambi ya Upinzani inapenda kuikumbusha Serikali iliyoko madarakani maneno aliyosema Baba wa Taifa mwaka wa 1967: “Elimu itolewayo katika shule zetu za misingi inapaswa kuwa elimu iliyokamilika.”

Mheshimiwa Naibu Spika, inatia simanzi kubwa kuona hata maneno haya ya baba yetu yanashidwa kuenziwa. Ni wazi kuwa Marehemu hafurahii huko aliko, kwani aliacha msingi mzuri lakini leo hata kama mtoto wako anakwenda shule, lakini mzazi hana imani na elimu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu basi Serikali ifanye yafuatayo ili kurekebisha hali hii: Kubadili mfumo wa elimu toka 7:4:2:3 kwenda 10:4:3, mfumo huu haujagawanyika sana, lakini ni *comprehensive and less selective*. Lakini kubwa zaidi utakwenda sambamba na mabadiliko ya kikanda *regions* na kimataifa, mfano, Kenya ni 8:4:4, Uganda 12:2:3, Zanzibar 10:2:2:3 na nchi nyingi zilizoendelea ni 12:4. Nchi nyingine zinaendelea kwenye *Universal tertiary Education*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kila sababu na haja ya kuwa na maboresho kwenye mfumo wetu wa elimu. Nguvu ya ufundishaji kuanzia waliomaliza Darasa la Saba, Kidato cha Nne na Sita na wenye elimu ya shahada wachache ni lazima usukwe upya ili uwe uwiano wa 85% ya Diploma na 15 ya shahada ya kwanza katika elimu ya sekondari idadi iwe *reversed* ili waalimu wengi wawe na shahada na haswa waalimu wa sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hilo, Kambi ya Upinzani inawahakikishia wananchi wote kuwa haitathubutu kukaa kimya. Pale mambo yanapokuwa yanakwenda vinginevyo na matarajio yao, tunaahidi kuendelea kushirikiana nao siku zote na kwa upande wa Serikali, ni matarajio ya Kambi kuwa Wizara husika itatoa majibu yanayoshabihiana na maswali yaliyotolewa na Kambi hii na si vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza kwa makini na naomba kuwasilisha. Ahsanteni Sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana waliota hotuba za uongozi. Wachangiaji wetu wako 42, ambao hawajachangia hata mara moja walioomba ni watatu, waliochangia mara moja walioomba ni 28, waliochangia zaidi ya mara mbili walioomba ni 11, jumla yake ni 42. Wizara hii ni ya siku mbili. Kwa asubuhi hii tutaweza kuwa na wale wasiochangia hata mara moja watatu, tukirudi jioni watakuwa 11, kwa siku ya leo jumla watachangia 14, kesho tukijitahidi sana, tuanje kuchangia saa 4.15 tutakuwa na wachangiaji 11 tu katika kipindi cha asubuhi, jioni inabidi tuwaacie Mawaziri. Kwa hiyo, watu 25 katika 42 wanaweza kupata nafasi.

Waheshimiwa Wabunge, nitamwita Mheshimiwa Felix Kijiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Dokta Ali Tarab Ali na Mheshimiwa A-Shymaa John Kwegyir. Hawa ndiyo watakaochangia asubuhi hii.

MHE. FELIX N. KIJIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu kwako kwa kunipatia nafasi hii. Labda niungane na wenzangu waliochangia, nikisema tu kwamba sina tatizo kuhusu kuiunga mkono kwa asilimia mia moja hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kufanya hivyo, ningependa nichangie katika vipengere vichache vifuatavyo:- Sisi kama Wabunge ndiyo tuna Walimu huko, tuko nao kila siku. Matatizo ya Walimu tunayajua. Nakumbuka niliwahi kuhudhuria hafla ya kumuaga Mwalimu kijijini, alikuwa anastaafu. Lakini nikasikitika sana, kwa sababu unapokwenda kwenye hafla ya kumuaga mtu ambaye amemaliza utumishi Serikalini kwa muda wa miaka aliyofanya kazi, inafurahisha kuona kwamba ametendewa haki au amepewa kitu ambacho kitamsaidia kuishi maisha yaliyo bora katika muda wake ambao ameubakiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokwenda pale, nilishangaa kwamba Mwalimu amefanya kazi nzuri, tena Mwalimu Mkuu wa Sekondari amesomesha watoto wamekwenda mpaka Chuo Kikuu, lakini siku ya mwisho Mwalimu kwa kazi nzuri amekabidhiwa jembe, upanga na shoka. Sasa huyu si atakufa baada ya siku moja?

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ndiyo anakwenda kuanza wakati amefanya kazi kwa uvumilivu na utiifu kadri sheria za nchi zinavyokwenda. Kwa hiyo, mimi kwanza kabisa ningependa kusema kwamba ni vizuri sasa Serikali kujipanga

iboreshe maisha ya Walimu. Walimu wanafanya kazi kubwa sana, wanaishi maisha duni na mishahara yao haitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu ndiyo wanakaa vijijini. Ukienda kijiji ambacho hakifiliki utakuta kuna shule na Serikali kwa kweli imejikita katika kuboresha sekta hii ya elimu kwamba kila kijiji kiwe na shule na Waheshimiwa Wabunge tunasimamia zoezi hili. Lakini unapokwenda kule unamkuta Mwalimu, ukimwuliza umetoka wapi? Anakwambia nimetoka Mtwara na yupo wapi? Yupo kijiji cha kule Kibondo ambacho hata mimi Mbunge wa Kibondo sijawahi kukanyaga. Ni kumwonea! Kwa hiyo, nilikuwa nasema kwa nia njema kabisa, Serikali ijipange vizuri na kujipanga vizuri ni Wizara ambayo kwenye makadirio ya Wizara kama hii itaandaa vizuri kabisa mahitaji ya Walimu na hasa kuboresha kipato chao kimaisha kwani mshahara hautoshi .

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mshahara hautoshi, usitegemee mtu ambaye anapata mshahara ambao hauridhishi atafanya kazi nzuri ya kutoa matunda ambayo yatakuwa ni changamoto kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nije kwenye kipengele cha utendaji. Sina hakika Wizara imejikita vipi na ushirikiano gani katika utendaji kwa kushirikiana na Chama cha Walimu kwa sababu chama hiki mimi nimekuwa nakisikia toka nikiwa shule ya msingi. Chama cha Walimu ndiyo kinajua matatizo ya Walimu wote. Siyo chama cha Walimu wawili ama wa Shule moja, ni Chama cha Walimu kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Wizara ya Elimu inaweza ikafanya kazi kwa kukaa kikao kimoja na Chama cha Walimu nina hakika kwamba Wizara ingeweza kufanya kazi bila matatizo kwa sababu matatizo yote yanajekuwa yanajulikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema sina hakika wanakwendaje kwa sababu ukibahatika ukakutana na Mjumbe wa Chama cha Walimu atakwambia kwamba Chama hakina ushirikiano wa karibu na Wizara. Mimi nilikuwa naomba Wizara ifanye kazi sambamba na yale mambo ambayo Chama cha Walimu kinaona kwamba kwakweli Wizara haitekelezi, hilo ni jambo la pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ni madeni ya Wizara ya Elimu. Sasa yanatisha! Sasa hivi baada ya malipo ambayo Serikali imefanya ambayo ni makubwa sana kwa mfano imelipa Shilingi bilioni 7.1 kwa shule za msingi na baadaye imelipa shilingi milioni 700 kwa shule za sekondari pamoja na vyuo. Lakini bado mpaka sasa Serikali inadaiwa Sh. 12,266,216,697.99. Hizi fedha nadhani ni fedha ambazo kama kweli tungekuwa tunafuata utaratibu kwamba kila deni linapokuja linalipwa, basi bajeti ya Wizara hii isingekuwa na matatizo, lakini sasa tunaanza kuzungumzia madeni kwa sababu ni deni kubwa sana na hali ya nchi ndivyo ilivyo.

Sasa hili deni litakwenda namna gani? Tunapitisha deni lilipwe ili wanafunzi waendelee kupata huduma kwenye vyuo na kwenye mashule, kwa sababu tatizo kubwa ni kwamba utakuta deni kubwa linakuja, ni kwa ajili ya marekebisho ya vyeo vya walimu

vinapofanyika kwa sababu walimu wanatakiwa walipwe *immediately* lakini hilo halifanyiki. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni posho za Walimu. Hata pale inapothibitishwa kwamba inahitaji walipwe, lakini utakuta inachukua muda mrefu Mwalimu kupata malipo yake. Ndiyo malalamiko ya Walimu huko vijijini. Lakini lingine ni wazabuni wanaosaidia kutoa huduma kwenye shule hasa hizi za *boarding*. Mtu anatoa huduma kwa miezi mitano halipwi kitu mpaka anakausha mtaji wake, ukienda kudai unaondoka bila kulipwa: Je, utaendelea kutoa huduma hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake ni wanafunzi kutokupata chakula ambacho kinafaa kwa afya zao wakiwa kule mashulenii au vyuoni. Hili ningeomba lichukuliwe hatua madhubuti na Serikali iingilie kati kuhakikisha hayo madeni yanayokabili Wizara ya Elimu yanalipwa katika muda unaotakiwa. Lakini pia liende sambamba na haya marekebisho ya malipo kwa Walimu wanapopandishwa vyeo, kubadilishwa ngazi, yalipwe kwa muda unaotakiwa na hii inakwenda pamoja na mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku ya Mshahara unakuta Walimu wanajipanga, utafikiria wanakwenda kujiandikisha kupiga kura, lakini kwa sababu wana njaa kule wanapoishi wote wanahama kutoka kijijini wanakuja Mjini kwa ajili ya kufuata mshahara. Mshahara unaotakiwa upatikane kuanzia tarehe 22 mpaka 25, lakini mshahara wa Mwalimu unapatikana mpaka tarehe 10 ya mwezi unaofuata. Hii kwa kweli siyo haki wanavyotendewa. Walimu tunawategemea, ndiyo wanaotusomeshea watoto wetu, lakini kama hali zao ni duni namna hiyo, kwa kweli itashindikana kujulikana kama wataweza kutoa huduma zinazotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni nyumba wanazoishi Walimu hazitoshi. Tulikuwa na matatizo, walimu wanapangiwa kwenda kufundisha, mwali mu anatoka Mkoa mmoja anakwenda Mkoa mwengine, huko unakuta hakuna nyumba na akikuta hakuna nyumba anakimbia anaondoka tunaanza kuwatafuta. Sasa utapangiwa kufanya kazi bila aliyekuajiri kukuambia utakwenda kuishi namna gani? Utakwenda kuishi chini ya mti? Ama masharti ni kwamba unapopangiwa kazi ujenge nyumba kwanza uishi humo ndani ndiyo uendelee na kazi au vinginevyo ukute nyumba imejengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nadhani suala la nyumba za Walimu kwa kweli lingefanyiwa harambee kama Serikali ambavyo imefanya harambee katika ujenzi wa shule za msingi na shule za sekondari ambazo tunaendelea nazo kwa ngazi za Kata na sasa nadhani tutakwenda kwenye ngazi za vijiji. Tukifanya hivi, hatutakuwa na lile suala la Walimu kutoroka. Mtu anapangiwa shule anatoka Tarime anakwenda Kigoma, anakimbia. Hili ningeomba sana lizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ambalo ningependa kulizungumza, nimelishuhudia mwenywewe. Ni muda mrefu unaochukuliwa kwa hii mikopo ya wanafunzi. Mwanafunzi anayestahili kupata huo mkopo, basi apate bila kuhangaika, lakini mwanafunzi anatembea mpaka wewe mzazi inakuwa ni kero kwako kumtafutia

nauli kwa ajili ya kwenda kuomba mkopo ni kama anabembeleza. Kama ana haki na taratibu zipo, kwa nini hiyo haki isipatikane na taratibu zipo na kwa nini hiyo haki isipatikane katika muda unaotakiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nalo ningependa kusema kweli Wizara isimamie hilo kwa kile chombo kinachohusika kwa utoaji wa mikopo ili kutoa usumbufu ambao unawapata wanafunzi kwa ajili ya kupata mikopo ya kwenda kuendelea na masomo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshuhudia shule nydingi sana za Sekondari na Vyuo unakuta hawana usafiri na hawa ndiyo wanakaa vijijini huko. Hakuna zahanati wala kituo cha afya, leo usiku mwanafunzi ataugua, akishaugua sijui itakuwa ni jukumu la Mwalimu la kumbemba mgongoni kumpeleka hospitali ambayo ipo kilomita ishirini! Mimi nilikuwa nadhani kwa makusudi mazima hii bajeti ya Mheshimiwa Waziri aliyoitoa ingekuwa imejikita katika hilo, nimejaribu kuangalia kwenye bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Mheshimiwa Waziri angekuwa ameungana na wataalamu wake kupanga vyuo na shule za sekondari wawe na magari ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina hakika na maeneo mengine ambayo yana barabara nzuri, lakini kwangu mimi Mbunge wa Kigoma, Wilaya ya Kibondo na Wilaya za Kigoma kwa ujumla ninavyozielewa ni kwamba barabara ni mbovu na shule za sekondari ziko ndani sana. Hakuna usafiri, kwa hiyo, wanafunzi wanapouqua kutoka huko kuwafikisha hospitali ni matatizo makubwa sana. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani suala la usafiri lingefikiriwa sana ili kurahisisha kwa wale ambao wanapata matatizo ya dharura.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Diallo naomba ukae hapo ulipofikia.

MHE. FELIX N. KIJKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nadhani kwamba mbali na hilo kuna upungufu mkubwa sana wa walimu kwenye shule zetu, hili halina ubishi. Lakini kama tungkuwa tunatumia vyuo tulivyonavyo vyote vinafanya kazi, nina hakika hilo tatizo hata kama lingekuwa lipo, tusingekuwa na matatizo ya kiasi hicho. Kwa mfano, kuna vyuo vilivyofungwa kwa mfano chuo cha Ndwiika ambacho kipo Mtwara kimefungwa na kilikuwa kinachukua wanafunzi wanaokwenda kujifunza ualimu; kuna chuo cha Urambo Tabora, hiki chuo kilikuwa kinatoa mafunzo kwa wanafunzi waliokuwa wanakwenda kuchukua mafunzo ya Ualimu. Hivi vyuo nadhani wakati umefika sasa kwamba mbali na hivi vilivyofungwa, tungeomba vifunguliwe pia tuwe na TCC za kutosha, hata walimu hawa tulionao ambao tayari wanafanya kazi siku za nyuma kulikuwa na utaratibu ambao sasa hivi haupo. Ni utaratibu wa Walimu kwenda kwenye kozi za mara kwa mara, kwani sasa hivi Mwalimu kwenda kwenye kozi ni kitendawili? Inamchukua muda mrefu kwenda huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja kama nilivyosema, lakini kwa sababu ya muda nimekatizwa mambo mengi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kijiko, hata hivyo umesema mengi. Sasa namwita Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali.

MHE. DR. ALI TARAB ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Labda niseme kwa sisi ambao tunaishi karibu na bahari tunasafiri sana kwenye bahari, nafikiri ukiwa katika jahazi ukaona ubao chini unapitisha maji, hiyo ni alama ya hatari. Ukiona hivyo ni bora kuwasiliana na Mabaharia na ukawasiliana pia na Nahodha ili kuweza kufanya hali yoyote kunusuru hali ile, vinginevyo kutakuwa na janga kubwa ambalo litawakumba wasafiri wote. Kwa sababu hiyo, ndiyo maana narejea kusema maneno ambayo nyuma nimeshayasema, lakini nitayaeleza kwa upana zaidi leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimebahatika kuwa Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii ya Bunge na kwa nafasi yangu pamoja na wenzangu, moja kati ya kazi za Kamati yangu ni kutembelea hospitali nchi nzima. Hivi leo nenda kokote katika hospitali zetu, mnajua ninachokisema. Tafadhali tembelea katika hospitali yoyote katika nchi hii, nenda Mbeya, Babati, Kigoma, Dar es Salaam, Songea, kokote utakakokwenda kuna upungufu mkubwa wa wafanyakazi katika Sekta ya Afya. Nasema hivyo kwa sababu Sekta ya Afya hasa Madaktari wanasmeshwa na Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ripoti ya Wizara ya Afya ya 2006, imethibitisha kwamba Sekta ya Afya kuna upungufu mkubwa sana wa wafanyakazi kwenye Sekta ya Afya ni asilimia 32 tu. Kwa hiyo, zaidi ya hapo, hao ambao wanahitajika hawapo katika kazi. Katika hao, waliopo wengi wao wameshapindukia miaka 40. Kwa hiyo, wanaelekeaa kustaafu. Ndiyo pale nikasema kwamba ukiwa msafiri ukiona jahazi linatoboka, uongee na mabaharia ili jambo hilo liweze kufanyiwa ukarabati haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naongelea leo Madaktari, kwa sababu kama nilivyosema, Madaktari wanasmeshwa na Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa mujibu wa takwimu za *WHO* za mwaka 2004, zinasema Tanzania ina Madaktari 2.3 kwa watu laki moja. Hilo ni Shirika la Afya Duniani (*WHO*) linashauri kwamba nchi zetu hizi za ulimwengu wa tatu ziwe na angalau Madaktari 10 kwa watu laki moja, lakini sisi tunao madaktari 2.3 kwa watu laki moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiachilia mbali visiwa vingi vya *Polynesia* hivi visiwa vidogo vidogo (*island state*), *Polynesia na Pacific*, Tanzania ni nchi ya tatu kutoka mwisho kwa idadi ya Madaktari kwa uwiano wa watu nchini, tukiwa mbele juu ya Rwanda na Malawi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie hizi nchi za jirani, tusiende huko mbali, Lesotho ina Madaktari 5.4 kwa watu laki moja; Zimbambwe ina madaktari 5.7 kwa watu laki moja; Zambia ina madaktari 6.9 kwa watu laki moja; Madagascar ina madaktari 8.7 kwa watu laki moja; Kenya jirani zetu hapa ina madaktari 13.2 kwa watu laki moja; Swaziland ina madaktari 17.6 kwa watu laki moja; Congo Brazzaville ina madaktari 25.1 kwa watu laki moja; Namibia ina madaktari 29.5 kwa watu laki moja; Botswana ina madaktari 28.8 kwa watu laki moja. Sisi tuna Madaktari 2.3 kwa watu laki moja. Msiba! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie nchi za jirani zetu ambazo zimetuzunguka ambazo miaka yote zimekuwa katika migogoro au zina vita vya wenyewe kwa wenyewe au zimekuwa zikitawaliwa na Serikali za mabavu. *Mozambique* imekuwa na vita miaka mingi ina madaktari 2.4 kwa watu 100,000 zaidi ya sisi; *Ethiopia* ina madaktari 2.9 kwa watu 100,000; *Eritrea* madaktari watatu kwa watu 100,000; Somalia ambao wanapigana mpaka hivi leo wana madaktari wanne kwa watu 100,000; Uganda inapigana na *LRA* Kaskazini ina madaktari 4.7 kwa watu 100,000. Burundi jirani zetu hapo ina madaktari 5.2 kwa watu 100,000; *DRC Congo* wana madaktari 6.9 kwa watu 100,000; *Comoro* juzi tumepeleka majeshi yetu, wao wana madaktari 7.4 kwa watu 100,000. Angola wana madaktari 7.7 kwa watu 100,000; hali iko hivyo. Sisi ambao tumekuwa katika amani na utulivu miaka yote, miaka 40 na ushee tuna madaktari 2.3 kwa watu 100,000. Aibu aibu, msiba! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kuna haja ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii, Wizara ya Afya na chuo pekee cha umma ambacho kinafundisha madaktari nchini hapa Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya Muhimbili (*MUHAS*) wakae pamoja waunde mkakati kama ule ulioundwa wa *MMES* au kwenye afya *MAM* unaokuja huo ili kunusuru hali hii. Jahazi linazama hili! *We are just ringing warning bells.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie sasa hivi ingawa tuna upungufu mkubwa huo wa Madaktari hebu tuangalie hali ilivyo katika vyuo vyetu. Chuo chetu pekee hicho cha kufundisha madaktari hapa nchini, *MUHAS* kimekuwa na ongezeko la wanafunzi ambao wanaomba kudahiliwa katika chuo hicho. Mwaka 2000/2001 kulikuwa na wanafunzi walioomba ambao walikuwa na sifa wamefaulu, walikuwa na sifa za kuingia *MUHAS*.

(*Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika*)

MHE. ALI TARAB ALI: Mbona haraka hivyo!

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2000/2001 kulikuwa na wanafunzi 459. Mwaka 2006/2007 kulikuwa na wanafunzi 1215. Tuangalie kwa miaka mitano tu kuanzia mwaka 2002/2003 mpaka 2003/2006 wanafunzi ambao walikuwa na sifa wangeweza kudahiliwa, lakini hawakudahiliwa ni wangapi. Mwaka 2002/2003 kulikuwa na wanafunzi 552, walioomba walikuwa na sifa za kuingia, lakini waliochukuliwa ni asilimia 57.6, basi. Mwaka uliofuatia 2003/2004 waliomba wanafunzi 834 walikuwa na sifa wote hawa za kuanza chuoni hapo, walichukuliwa asilimia 44.6, inapungua ile *percentage* ya wanafunzi wanaodahiliwa.

Mwaka 2004/2005 wanafunzi 754 waliomba, waliochukuliwa ni 45.8. Mwaka 2005/2006 waliomba wanafunzi 1,154 asilimia 30.5 walichukuliwa, zaidi ya 70% wakaondoka. Mwaka 2006/2007 wameomba wanafunzi 1,215 waliochukuliwa ni asilimia 25.9, asilimia 74.1 hawakuchukuliwa, *percentage* inapungua kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, chuo hiki kina nafasi kubwa, mwaka wa tatu huu kimepata eneo kubwa, eneo la Mloganzila, kina ekari 3,800, kwa kweli ilikuwa ni wakati wa kuweza kuwekeza kule. Tuwapatie miundombinu wapate walimu, tuongeze udahili wa wanafunzi wa kusoma *medicine* lakini hakuna kilichofanyika mpaka hivi leo. Mpaka hivi ninavyozungumza, hakuna kilichofanyika.

Chuo hiki cha *MUHAS* ni chuo cha nane kwa idadi ya mafungu ya bajeti ya fedha zilizopewa juu yake, hatuna shida yoyote ile. Juu ya matatizo yote hayo, *MUHAS* ni chuo cha nane vilivyopelekwa kwa ajili ya fedha iliyopata katika bajeti hii. Mimi sisemi kwamba hawa wengine wasipate, wapate walichowekewa, lakini maadam tuna shida, tuna tatizo, tutazame tujaribu kuwa-*finance* hawa jamaa wa *MUHAS*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitamalizia kwa kusema maneno ambayo yamechapishwa katika Gazeti la *Lancet*, ni *Journal* la Kisayansi la kiulimwengu ambalo linasifika. Linasema, naomba ninukuu: “*Africa carries 25% of world disease burden, yet has only 3% of the world health workers and 1% of the world economic resources to meet that challenge.*” Kazi hiyo! Tafsiri yangu ambayo sio ya kiutalaam inasema, Afrika inayo asilimia 25 ya magonjwa ulimwenguni, lakini inayo asilimia tatu tu ya wafanyakazi katika sekta ya afya ulimwenguni na asilimia moja ya rasilimali ya kiuchumi kupambana na changamoto hiyo. Kwa hiyo, tusitarajie miujuza kutarajia kuwa labda tutapata madaktari kutoka sehemu nyingine na kadhalika. Mzigo huu ni wetu sisi, tuubebe wenyewe. *Otherwise we are going to the rocks.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongee kuhusu Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Serikali yetu imeanzisha mpango huu wa *MMEM* na *MMES* na tumeona idadi kubwa ya wanafunzi kuingia katika shule za msingi na hivi sasa shule za sekondari zinajaa hata kusababisha kujenga shule nyingine kwenye Kata huko. Kwa hiyo, katika miaka miwili, mitatu ijayo kutakuwa na wahitimmo wengi wa kutoka sekondari: Je, tumejiandaa vipi kuwachukua hawa katika vyuo vikuu? (*Makofi*)

MHE. AL-SYMAA J. KWEGYIR: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na afya ili niweze kusimama hapa nilipo pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote mliokuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, natoa salaam zangu za rambirambi kwa maafa yote pamoja na mauaji yanayoendelea kutokea ya Maalbino wanaoendelea kuuawa mpaka hivi sasa. Hivi juzi tu mtoto wa miezi saba ameuawa. Kwa kweli nawapa pole hiso familia kwa matukio haya ni mazito, kwa kweli nawapa pole sana. (*Makofi*)

Pia, natoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kunitfea kuwa Mbunge. Namshukuru sana. Pia namshukuru Mheshimiwa Spika, wewe Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wote mliokuwemo humu ndani kwa kunipa ushirikiano mkubwa tangu siku niliyoteuliwa mpaka hivi leo mmekuwa karibu na mimi. Mmenisaidia sana, nawashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Kamati ya *Scout*. Hii Kamati ilikwenda Mwanza kufutilia mauaji. Natoa shukrani zangu za pekee kwao kwa moyo wao kwenda kule Mwanza kufutilia haya mauaji. Nafikiri ripoti imeshafika kwenu, tunasubiri matokeo. (*Makofi*)

Halafu natoa pungezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri Mkuu, nampongeza sana na ninamu-*admire* sana ile siku ya Alhamisi anavyojibu maswali kwa umahiri mkubwa. Nampongeza sana Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda. Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, sasa naanza kuchangia Wizara ya Elimu. Nawapongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Maafisa wote wa Wizara ya Elimu. Nawapongeza kwa utendaji wao na *speech* yao ilikuwa nzuri sana aliyoitoa Mheshimiwa Waziri. Nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi mchango wangu katika Wizara hii, naomba Wizara ya Elimu ni Wizara ambayo itasaidia kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na hii imani potofu iliyoenea sasa hivi. Wizara ya Elimu ndiyo pekee ambayo itatusaidia sisi maalbino kuepukana na haya mauaji yanayoendelea, wao wakitoa elimu kwa jamii. Jamii itakuwa kidogo na uelewa kuhusu hawa Maalbino ni akina nani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nieleze kidogo kwamba Albino ni nani, kabla sijaendelea na huu mchango wangu kwenye Wizara ya Elimu. *Albino*, uzuri ni kwamba mimi mwenyewe niko hapa, ni mfano mzuri. *Albino* ni binadamu kama binadamu mwingine, tatizo la Albino anazaliwa anakosa *melanin*. Kuna *condition* ambayo anaikosa, inaitwa *melanin*. Hii *melanin* ni rangi ambayo inakosekana kwenye ngozi, kwenye macho na kwenye nywele. Inasababisha Albino awe na *challenges* kubwa. Adui mkubwa wa Albino ni juu! Jua linamuathiri sana Albino anapotembea kwenye juu. Pia macho, anatakiwa apate miwani.

Mfano mnioniona hapa nilipo mnapata mfano, nina miwani, nimeva nguo za mikono mirefu. Natakiwa kuva nguo za *cotton*, mikono mirefu kufunika ili juu lisinipige. Pamoja na kwamba unavaa nguo za *cotton*, kuna *lotion*, ambazo zinatakiwa kwa huyo Albino. Hizi *lotion* ni *very expensive!* Kama utaniruhusu nionyeshe mfano wa hizo *lotion* ninazo hapa.

NAIBU SPIKA: Unaruhusiwa.

MHE. AL-SYMAA J. KWEGYIR: Mheshimiwa Naibu Spika, hizi *lotion* ni *very expensive*, zinaghari Sh. 40,000/= kwa chupa. Albino gani atawezu kununua *lotion* hii? Hakuna! Maalbino ni maskini, wamekosa elimu! Elimu hawana! Tatizo la hizi *lotions*, zinazwa bei kubwa, hakuna *Albino* yejote anamudu *lotion* hii kwa shilingi 40,000. Kwa hiyo, tatizo kubwa ni ngozi. Albino wasiokuwa na uwezo anaweza akapaka mafuta ya nazi, anaweza akapaka mafuta ya nyonyo lakini ni lazima avae nguo ya mikono mirefu afunike ule mwili. Mnioniona mimi uvaaji wangu! Najifunika sehemu zote, nabakiza uso tu na viganja vya mikono kwa ajili ya kumwogopa adui juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, juu ni adui mkubwa wa *Albino*. Sasa *Albino* huyu huyu ana maadui wengine kisaikolojia. Kisosholojia ni jamii inayomzunguka wanavyo-*react* juu yake. Kisaikolojia ni jamii inamtenga, akikaa anatengwatengwa, anaonekana kama siyo binadamu. Lakini namshukuru mwenyezi Mungu Wabunge wamenipokea vizuri sana wameni-*regard* ile hali ya kutengwatengwa ndio maana inamfanya *Albino* anakuwa kama kachanganyikiwa kisaikolojia, matokeo yake akionekana anaonekana ni mtu asiyekuwa na akili timamu. Ni binadamu, wana akili, wako wenyе *masters*, wako *graduates* kibao *Albino*, hapa wapo waliosoma. Tuna akili kama binadamu wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naingia kwenye elimu. Upande wa elimu, kikubwa ni wazazi na walimu. Nawaomba wazazi wasiwafiche watoto Maalbino ndani. Wanawaficha ndani kwa kuogopa. Kuna *challenge* nyingine imeingia ya mauaji, wazazi wanawaficha watoto ndani. Wanaogopa kuwapeleka shulen, wakiwapeleka shulen anaweza akampeleka, akichelewa kwenda kumchukua keshanyakuliwa, amekwenda kuuawa.

Kuna mfano Mbeya, mtoto wa *form two* amekwenda shule vizuri, anarudi, njiani akanyakuliwa akaenda kuuawa, maskini ya Mungu wakakuta madaftari yametupwa. Sasa hebu niambieni, kweli tutasoma? Hatuwezi kusoma! Wizara ya Elimu naomba itusaidie, wazazi wasiwafiche watoto, wapelekeni shulen. Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Manaibu Waziri wanansikia, wasaidieni hawa watoto *Albino* wasome wapate elimu ya awali.

Nimesoma katika hiki kitabu cha *best*, kuna kitabu kimeandikwa *Best Education Statistics in Tanzania*, nimeangalia Mikoa iliyoorodheshwa kuwa na watoto *Albino*, wameorodheshwa watoto wa shule ya awali. Nimeona Mkoa wa Kigoma shule ya awali mtoto mmoja mwanafunzi. Haiwezekani kama Mkoa wa Kigoma watoto *Albino* hakuna. Wapo. Lakini wazazi wanaogopa kuwapeleka shulen.

Mbali ya kuogopa, pengine uwezo hawana pia. Nimeona Mkoa wa Kagera mtoto mmoja, Manyara mtoto mmoja, Tabora mtoto mmoja, Arusha watoto saba, Rukwa watoto nne, Shinyanga watoto watano, Shinyanga huko ndiko kunatisha Mheshimiwa Charles Mlingwa, wanauawa kama nini! Mwanza, Mara, ohoo wanauawa kweli kweli! Kwenye Mikoa ambayo nimeona kidogo ipo katikati ni Morogoro wanafunzi 13, Singida watoto 15, Pwani watoto nane, Mbeya nimeona *at least* kuna hao ambao kidogo wapo juu, Mkoa wa Tanga ninaotoka mimi hapa kuna usalama mkubwa, watoto 22; Ruvuma watoto 24, Mwanza watoto 20, hawa watoto 20 wa Mwanza wamechukuliwa kwenye ile shule ya Misungwi.

Wilaya ya Misungwi kuna shule ya msingi inaitwa Mitindo, hapo ndipo kuna watoto wa *Albino* wapo pale. Lakini Mwanza watoto hao wanauawa kama nini! Wakitoka wakipita wanakamatwa wamechinjwa, wanachukua mikono, wanachukua miguu wanakwenda kufanya habari zao wanazozijua wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanalamika kuhusu simba, sasa simba watu wameingia. Hao ni simba watu wananyofoa watoto miguu na mikono wanakwenda kufanya mambo wanayoyajua wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Shule ya Mitindo ipo Wilayani Misungwi. Shule hiyo imepeleka maombi yao ya fedha kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, wameomba shilingi milioni 240 kwa ajili ya kukarabati ile shule. Shule ile ina watoto wasioona na watoto *Albino* wapo pale kwenye ile shule na watoto wengine. Ile shule ina watoto mchanganyiko. Maana yake mtoto *Albino* anatakiwa apelekwe kwenye shule ili achanganyike na watoto wengine, asiwekwe peke yake, peke yake anajiona kama vile anakuwa *isolated*, anaonekana kama anabaguliwa baguliwa. Lakini mtoto *Albino* apelekwe kwenye shule, achanganywe na watoto wengine hivyo ndivyo inatakiwa. Lakini akitengwa tengwa anajiona kama vile amebaguliwa baguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii Shule ya Mitindo iliyopo Misungwi wamechanganywa na watoto wengine. Pia watoto hawa Maalbino kama hiyo shule ya Mitindo ni ya bweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, hao watoto maalbino wapelekwe shule za bweni ndipo kutakuwa na usalama. Kwa sababu wakiwa mabweni kule kidogo usalama utakuwepo, lakini hii nenda rudi wanakamatwa njiani wanauawa. Kwa hiyo, nafikiri hilo wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha hoja yake atakumbuka hilo. Namwomba sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kidogo nigosie *VETA*. *VETA* ni Chuo kwa ajili ya mafunzo. Kwenye Ilani aya 106 (b) inazungumzia wale mavu inasema: “Kuwaendeleza na kuwaimarisha utoaji wa mafunzo ya ufundu kwa watu wenye ulemavu na kuwapatia vitendea kazi na fursa ya mikopo ili waweze kujajiri na kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapa kwenye mafunzo ya ufundu mimi sidhani nimekwishapita kwenye Vyuo vya *VETA* sijaona *Albino*. Vijana *Albino* wamejaa wengi mno, hawana shughuli ya kufanya, lakini wakipelekwe *VETA* wanaweza kwa sababu wako kivulini, wataweza kupata ufundi wao na wataweza kuishi na hawatakuwa tegemezi kwa kutegemea tegemea, wataweza kujimudu wenyeewe, kwa sababu watakuwa wamepata ufundi na watakuwa wamepewa mikopo kama ilivyolezwa kwenye Ilani ya CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, naiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu kwa ajili ya jamii. Nimeona kwenye *TV*, kwenye *Radio* na hasa kwenye *TV* kuna matangazo yanatoka yanaelezea habari ya wale mavu na kwenye *Radio* wanaelezea juu yaa wale mavu wapatiwe elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri kwenye hivyo vipeperushi, kwenye magazeti na kwenye *TV* na maalbino nao waingizwe watolewe kama mfano, ili kusudi jamii ielewé. Jamii ikishaelewa, itasaidia kupunguza haya mauaji. Tunauawa sana, nikijichanganya na mimi mwenyeewe, maana sijui lini nitapona. Pengine pale *VETA* naweza kuja kuvamiwa siku moja, sijui.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nashukuru kuna ulinzi na Waheshimiwa Wabunge ninaokaa nao pale wana- *take care of me*, mume wangu akiwa hayupo wananiangalia kwa macho mawili. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wana *take care* sana, ninawashukuru sana. Mheshimiwa Wilson Masilingi niko naye pale, ananilinda sana na Mheshimiwa Charles Mlingwa hapa nataka nimbaje wakati ye ye Msukuma ataniua tu huyu, ninamwogopa! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wanapokwenda kwenye Majimbo yao, chonde chonde nawaombeni wakiwa na Mikutano yao ya hadhara wawataje na hao Maalbino wawahushe kwenye hotuba zao wapate ajira, wapate elimu ili watu waondoe imani potofu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaombeni Waheshimiwa Wabunge wazungumzie hii hali ya imani potofu, wananchi waelewe. Mnajua tatizo ni elimu. Mnajua unaweza ukamsingizia mtu kitu kumbe hana elimu, hajui! Lakini utakapomuelimisha, atakuwa anaelewa na anajua. *Albino* ni binadamu. Mimi nimefundishwa na Mama Margaret Sitta amenifunisha katika shule ya sekondari, Mheshimiwa Vita Kawawa, nimesoma naye, ananijua vizuri na ananielewa mimi shulenii nilikuwa na-*participate* vipi. Yaani hakuna tatizo kwa kweli, ni uelewa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninamwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anatembelea mashule na Waheshimiwa Manaibu Mawaziri wakifanya ziara kwenye mashule naomba na mimi waniingize kwenye hiyo *delegation* na mimi nikatoa maneno mawili, matatu pale kwenye yale mashule nipate kuwaelewesha kuhusu *Albino* ni nani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka hapo naona kidogo nimeeleweka. Ninaunga mkono hoja hii mia kwa mia. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, nakushukuru sana. Kwa hiyo, tunashukuru hata sisi kuelimishwa kuhusu *Albino* ni mtu wa namna gani na vitu gani vinaweza kumlinda *Albino* kwa afya yake. Hii kampeni dhidi ya hao wenzetu ambao wanawaua watu, nadhani Waheshimiwa Wabunge, watafanya vizuri tu watakapokuwa katika maeneo yao ya kazi. Kwa sababu Tanzania hii tumeanza kusikia miaka ya karibuni watoto wa namna hiyo wanaondolewa duniani bila hatia yoyote. Bahati mbaya hao wenyewe mkiwaangalia ni maskini hao, wanaoua wanatafuta utajiri ndiyo kwanza wanakuwa maskini hata kuliko walivyokuwa mwanzo, maana ni laana tu. Kwa hiyo, tunakuahidi kwamba hili suala tutalishughulikia kwa pamoja.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika, amekwenda kuhudhuria Kikao cha *Commonwealth Parliamentary Association Africa Region*. Hivi Vikao vyataga Commonwealth tuna *Branch* kila nchi. Halafu kuna Commonwealth East Africa, kuna Commonwealth Speakers Conferences. Sasa hii ni Commonwealth Conference ya Region

Africa na inatangulia Mikutano Mikuu ya Kiulimwengu ambayo itafanyika *Kualalumper* mwezi Agosti, 2008. Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika, kwa sababu sisi mwaka kesho kutakuwa wenyeji wa Mkutano Mkuu wa *Commonwealth* kwa hiyo, wanaendelea kujenga *solidarity* ya kujenga uhusiano mpaka 2009 ambapo sisi tutakuwa wenyeji, basi tutakuwa tumekwishakuwa tunawasiliana na wenzetu wengine. Kwa hiyo, hatakuwepo hapa mpaka wiki ijayo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, napenda kusitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(*Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

Mwenyekiti (Mhe. Zubeir Ali Maulid) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Sasa napenda nimwite Mheshimiwa Meryce Mussa Emmanuel, atafuatiwa na Mheshimiwa Felista Aloyce Bura na Mheshimiwa Charles Keenja ajiandae.

MHE. JACKSON M. MAKWETTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Naam! Mwongozo!

MHE. JACKSON M. MAKWETTA: Mwenyekiti, katika matangazo ambayo yemewekwa kwenye maeneo muhimu ya matangazo, Mheshimiwa Makwetta ndiye msemaji anayeanza mazungumzo kwa jioni hii. Ningependa kupata maelezo.

MWENYEKITI: Ahsante, ni sahihi. Imechelewa kuletwa hii karatasi kwangu. Sasa basi ninamwita Mheshimiwa Jackson Makwetta, atafuatiwa na Mheshimiwa Manju Salum Msambya na Mheshimiwa Juma Killimbah ajiandae. (*Makofit*)

MHE. JACKSON M. MAKWETTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa kwanza kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuwa msemaji wa kwanza kwa jioni hii. Nakuomba radhi labda kwa yale niliyotaka kuingilia kati kumbe ratiba ilikuwa ni hiyo hiyo. Pili, nimesimama hapa kuunga mkono hoja ya Wizara hii na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri wake, Katibu Mkuu, Watumishi wa Wizara na Mashirika yaliyo chini ya Wizara yake pamoja na Walimu wote popote pale walipo katika nchi hii. Natambua kazi ya ualimu na nikikumbuka ukubwa na unyeti wa kazi ya ualimu machozi hunilengalenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu tunawatumia kwa kuhesabu kura, sensa, kampeni mbalimbali, mapokezi lakini tunapokuja kwenye mambo ya kimsingi ya kuzungumzia maslahi yao tunasitasita. Wako wengi kwa sababu ya uwingi na umuhimu

wa kazi yao. Kwa hiyo, kama sisi tunapuuzia umuhimu wa walimu tunajipuuzia wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kwa kutumia nafasi hii niipongeze Wizara hii kwa kazi kubwa na nzuri iliyofanywa ya kupanua elimu ya sekondari na vyuo vikuu katika nchi hii. Kazi kubwa iliyobaki sasa ni kuboresha na kuweka misingi imara kutokana na mambo tuliojifunza katika zoezi hili. Maneno hayatoshi kuelezea shukrani zetu na pongezi zetu kwa kazi hii nzuri ambayo wameifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ushauri au wa Bodi ya Ushauri ya Wizara hii. Kwa hiyo, baadhi ya mambo nitayastahi kwa sababu ya nafasi hiyo. Lakini tusiache watu wafe ndipo tuanze kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Bodi ni kwamba tuwe tunakutana mara kwa mara hasa kwa wakati huu ambapo mabadiliko ni mengi, kusudi tuweze tukasaidia Wizara. Ubora wa Taifa lolote lile duniani hutegemea ubora wa elimu inayotolewa kwa watu wake. Kwa hiyo, kama elimu ni mbaya, sio bora, basi watu wake wataathirika na ubaya huo. Kama Watanzania tunataka kuwa na Taifa bora au kama Watanzania tunataka kuua ubora wa Taifa, basi tuue misingi ya utoaji wa elimu bora. Kwa bahati mbaya matokeo ya kitendo kama cha kuua elimu ni ya pole pole sana. Makosa tunayoyafanya leo yatakuja kupatikana baada ya miaka 20 au 40. Kwa hiyo, naomba tuangalie hilo kwa sababu inawezekana tusilione kwa haraka kwa sababu ya sababu hizo ambazo nitazielezea baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tukikiuka misingi, misingi itatukiuka. Kwa hiyo, Waltanzania tutasimama au kuanguka katika miguu yetu wenyewe. Kila tunalolifanya leo linajenga au kubomoa misingi ya kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yamesemwa kuhusu elimu na yatasemwa. Lakini labda niwaachie wenzangu baadhi ya hayo ambayo ni muhimu kwa Wizara hii. Lakini ningependa nimpongeze Ndugu Kwaangw, kwa mchango wake wa leo kuhusiana na suala hili. Nampongeza sana. *We owe him a great deal.* (*Makofi*)

Baada ya hapo ningependa kwa haraka haraka nitoe mchango wangu kwa mambo muhimu, ninayoyaona ni muhimu kwangu. Moja, nasikia kuna mwelekeo wa kupeleka elimu au shule au usimamizi wa elimu TAMISEMI.

Naomba tuwe waangalifu, TAMISEMI ina kazi nyingi na inatosha, sahani imejaa. Nashauri kwamba mambo ambayo yanahusu Wizara ya kitaaluma yazingatiwe na Wizara hizo. Vinginevyo tutazua matatizo mapya na kuvuruga elimu. Uzoefu wa miaka mingi wa Wizara hii ni hazina kubwa kwa nchi yetu. (*Makofi*)

Ni rahisi kusikia mambo mazuri na kudhani kwamba yatakwenda kama tunavyotaka. Lakini siyo katika elimu. Naomba Wizara hii isimamie elimu kutoka elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vikuu. Kama ni lazima tufanye mabadiliko, basi tuondoe elimu ya juu na tukabaki kama tulivyokuwa mara ya kwanza. Kwa sasa hivi

naona kwamba huu mzigo kwa kurudisha elimu ya juu kuwa chini ya Wizara moja na Wizara hii iliyokuwa ya elimu ya kwanza.

Kwa kweli hapa ni vizuri tuwe waangalifu, kuna ugonjwa unaitwa *eleventhiasis*. Huu ni ugonjwa wa matende ambao mguu unakuwa mkubwa kuliko sehemu ile nyingine ya mguu. Sasa katika Wizara hii elimu ya msingi, elimu ya sekondari, elimu ya ufundi, walimu halafu na vyuo vikuu kwa kweli ni mzigo mkubwa.

Nashauri tusifanye makosa. Tutakuja kujuta baadaye. Mambo ya taaluma yasimamiwe na Wizara zinazohusika na taaluma. TAMISEMI inahusu vijiji, utawala Mikoani, Wilayani. Kuna matatizo mengi tu. Hata elimu ya msingi bado kuna matatizo. Sasa sijui nani anajibu maswali hapa Bungeni! Nadhani mnajjua wenyewe. (*Makofi*)

Mimi nilikuwa nashauri kwamba kwa sababu ya matatizo haya ambayo yameongezeka kwa mfano sasa hivi Wilaya moja inaweza kuwa na shule za sekondari karibu 40 na Mkoa ukawa na shule zaidi ya 200, haiwezekani shule za sekondari zisimamiwe na Mkurugenzi Mkuu kutoka Wizara ya Elimu Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua inayofanywa ni kusema kwamba *REO* asimamie elimu ndani ya Mkoa. *REO* kazi yake ni kusimamia elimu ya msingi. Lakini bila kuathiri sheria tumempelekea majukumu haya mapya kibinadamu, binadamu anachagua kile anachoona chepesi na kinachopendwa na watu. Naamini kwamba kama *REO* atapendelea elimu ya sekondari itasababisha aue elimu ya msingi.

Mimi nashauri kwamba katika hili tutazame upya tena muundo wa Wizara ya Elimu. Tutazame upya, lakini Wizara ya Elimu isimamie elimu kutoka ngazi za juu mpaka elimu ya awali ili iweze kuratibu na kujua mikakati ya kuboresha elimu kwamba inahusu kila ngazi, ya awali, msingi, sekondari mpaka vyuo vikuu. Lakini tukianza kuachaniana hapa, hasa kwa wakati huu mambo bado ni mabichi, tutaleta athari kubwa sana kwa nchi yetu. Huu ndiyo ushauri wangu na kwamba kwa msingi huu twende hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli tunafanya mabadiliko, lakini kasi hii huenda inaweza ikazua matatizo. Tusibadili magurudumu ya gari wakati bado gari linatembea. Wakati mwengine lazima usimamishe kwanza, tuanze kutoa magurudumu, lakini kama unabdalisha magurudumu huku gari linatembea, kwa kweli inawezekana ukasababisha madhara makubwa zaidi.

Napendekeza muundo ufuatao kwa maana ya kuboresha elimu katika nchi yetu. Kamishna wa Elimu katika Makao Makuu ya Wizara a-delegate madaraka mikoani, ndani ya mkoa kuwe na *REO* au Mkurugenzi wa Elimu ambaye atakuwa na uwezo mkubwa kwa maana ya kutoa maamuzi, siyo mshauri. Maana siku hizi ni mshauri, aweze kutoa maamuzi fulani ya kimsingi kuhusu elimu. Awe na wataalam wengi pale maana mme-prone hana watu, amebaki ye ye na watu wawili watatu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu pale awe na Idara kama tatu muhimu, Idara ya Msingi, kwa elimu ya msingi, Idara ya Sekondari, kwa elimu ya Sekondari na Idara ya Walimu kwa Shughuli za Walimu na mengineyo, ili Wizara kutoka Makao Makuu iwe inaratibu tu, kwa sababu kwa sasa hivi ni kazi kubwa sana. Kule hana wataalam, hana watumishi, hana madaraka yuko kwenye sekeretarieti ya Kimko ambayo kazi yake tena ni ushauri tu.

Sasa kama wanashauri kwa nchi kubwa kama hii kila jambo lipelekwe Dar es Salaam ndiyo mkaamue, ye ye apendekeze tu. Halafu hana cheo. Kuna siri katika cheo! Awajibike, sasa atakaa kwenye sekretarieti ya Mko halafu ndiyo ashauri. Kwa nini asiende Wilayani kama *REO*. Anakwenda kama mwizi tu kwa sasa hivi? Nashauri tutazame upya *REO* cheo chake kirudi au tumpe cheo kingine kipy, Mkurugenzi wa Elimu awe chini ya Kamishna na huyu *REO* asimamie mpaka *DEO* Wilayani. Kunyofoa utapoteza muungano wa Wizara kwa nchi nzima, halafu wale watakuwa hawana mahali, watakuwa wanaelea tu hewani.

Kwa sasa hivi wazo kwamba Wilaya zichukue majukumu, haya majukumu ambayo mmewapa mbona wanashindwa? Kodi mmesema tena irudie *TRA* kwa sababu wana matatizo. Hawana wataalam na wala hawakuandaliwa kwa jambo kama hili. Sasa jambo nyeti kama elimu nalo unataka kusukuma kama kilimo au kama jambo jepesi jepesi tu.

Mheshimiwa Spika, hili linahitaji Wizara na wataalam wake mabingwa kusimamia utaratibu wote kutoka juu mpaka chini na kuunganisha. Vinginevyo mtaanza kuleta tofauti kati ya Mko na Mko, Wilaya na Wilaya kwa sababu itategemea na Mkurugenzi anavyoona. Kama Mkurugenzi *back ground* yake ni Bwana Nyuki atawapendelea wafugaji wa nyuki, kama ni Bwana Mifugo atakwenda kwenye ng'ombe. Misitu ni misitu.

Jamani tusicheze na mambo muhimu kama haya na *treat them superficially* kama vile sawa sawa na mambo ya kupanda mti. Hili ni nyeti na tuna mambo mengi ambayo tumejifunza mahali pengine. Ningeshauri kwamba tujiepush. Baada ya kusema hayo, kwa haraka haraka niseme kwamba suala la shule za Kata halihitaji mjadala.

Tumejifunza nini kwa muda huu tangu tuanzishe? Kata ni nini? Tuwe na Kata za elimu na Kata za Utawala. Vinginevyo, tutakuwa tunamega kila wakati shule kwa sababu tu ya Mbunge amemua kuwe na Kata tano, basi kila shule tena, kila Kata inakuwa na shule ya sekondari, wakati kuna shule moja tu. Shule moja ingefaa na kwa mtindo huu hatuwezi *ku-maximize* matumizi ya wataalam na *resources* kwa sababu kama shule moja mnasema iwe na mikondo angalau minne na Kata nyingine hata miaka 10 hazitakuwa na uwezo wa kutoa mikondo minne. Hivi mnasema kitu gani? Tusiingize siasa katika mambo ya kimsingi! ukikiuka misingi, misingi itatukiuka! (*Makofi*)

Pili, shule za *Form Five* na *Six* zijengwe na Wizara. Zisimamiwe na Wizara, *tusi-obligate from our responsibility*, sasa hivi nina mashaka zitakuwa ngapi, mwaka

kesho maana hujui. Zinaota kama uyoga tu. Tatu, shule chache katika Wilaya zijengewe maabara kamili. Maabara ni majengo yanayohitaji uangalifu wa hali juu na vifaa vya hali ya juu na maabara moja iliyo kamili sio chini ya shilingi milioni 400. Sasa Wilaya zitawezaje kujenga maabara kwenye shule zake? Haiwezekani! Tuwe *honest!* Kwa hiyo, kama tunataka kuwa na maabara katika kila shule ya sekondari maabara kamili, tunajidanganya hapa. Mimi napendekeza kwamba tuwe na maabara

MWENYEKITI: Ni kengele ya pili Mheshimiwa Makwetta.

MHE. JACKSON M. MAKWETTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Ahsante sana Mheshimiwa Makwetta. Sasa namwita Mheshimiwa Manju Salum Msambya, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Killimbah na Mheshimiwa Dr. Binilith Satano Mahenge ajiandaye.

MHE. MANJU S.O. MSAMBYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kabla sijaendelea, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu pamoja na Timu yote ya Wataalam walioko Wizarani. (*Makofi*)

Baada ya kutoa pongezi hizo, naomba niseme, akishaanza kuchangia Mwalimu Mkuu kabla yako, ambaye ni Mheshimiwa Makwetta, Mtaalam wa elimu unapata matatizo kidogo. Lakini hata hivyo, kwa sababu ye ye kazungumzia hasa masuala ya muundo na namna ya kuendesha Wizara na elimu kwa ujumla. Mimi nitakwenda kwenye maeneo mahususi. La kwanza nitaelekea kwenye suala la uhaba wa walimu tangu shule za msingi mpaka sekondari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nilieleze, nilimsikiliza Mheshimiwa Waziri asubuhi wakati anatoa hotuba yake nzuri. Alieleza katika baadhi ya aya za hotuba yake kwamba Serikali inafanya maandalizi ya kuwa na angalau shule mbili za sekondari ya juu kwenye kila Wilaya, lakini vile vile akaeleza kwamba upo mkakati wa kujitahidi kupata wanafunzi wengi wa kusoma masomo ya sayansi. Tunahitaji wanasayansi wengi, tunahitaji shule za kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa hivi zipo shule za msingi na sekondari, kilio kikubwa sana ni uhaba wa walimu. Niende mahususi kwenye eneo ambalo mimi nawakilisha. Unakuta shule ya msingi yenye mikondo minane, shule ya sekondari yenye mikondo minne. Hii ya msingi ina walimu wanne, shule ya sekondari na tayari wanafunzi wako kidato cha tatu ina walimu watatu.

Sasa tunafikiria kuwa na shule ya sekondari ya kidato cha tano na cha sita. Tunafikiria tuwe na wanafunzi wengi wa kuchukua masomo ya sayansi. Hivi tunafikiria tu, kwa sababu tunataka idadi au tunataka kitu kilicho bora? Tusiende bora elimu. Ila twende kwenye elimu bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri Wizara ijikite kwenye mkakati kama ambavyo imekwishaanza wa kupata walimu wa kutosheleza kwenye ngazi zote, Elimu ya Msingi ipate walimu wa kutosha kwa nchi nzima. Elimu ya Sekondari ipate walimu wa kutosha kwa nchi nzima na tuna maeneo ya kuiga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mfano wa nchi mbili. Moja ni Uturuki na nyingine ni ya Uyahudi. Wakati Mataifa haya yanaanza, yalikuwa na uhaba wa wanataluma hawa. Lakini walifanya mikakati ya makusudi kuona lazima kwanza ili waweze kujitosheleza katika fani nyingine kwanza wawekeze zaidi kwenye elimu. Kwa kweli waliwekeza hasa! Sisi tunajua kile ambacho Mataifa haya yanafanya. Nikitoa mfano wa Uturuki, wameanza (hata nitumie neno la Kiingereza) *ku-export* elimu na sisi hapa Tanzania tunayo matunda na ile kazi yao ya *ku-export* elimu. Tunayo shule ya Sekondari ya Feza pale Tegeta. Sasa tusikurupuke tu kutaka tupate wanasayansi wengi ambaio itakuwa ni bora wanasayansi ila siyo wanasayansi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya juhudu kubwa sana ya kujenga shule nyingi za msingi na kama alivyosema Mheshimiwa Makwetta, tunazo shule nyingi sana za Kata ambazo zimejengwa na zinaendelea kujengwa. Kwa hiyo, ni vizuri shule hizi kusiwe tu kuna majengo yamesimama kwenye Kata hizi, ila yawe majengo ambayo vile vile yana watu wenye kuweza kufanya kazi pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Wizara ifanye kazi kubwa sana ya kupata walimu na lipo jambo la kusikitisha. Mwaka 1995 Wizara ilipokea dozi ya kutoka Benki ya Dunia, wakaambiwa kwamba wamefundisha walimu wengi sana. Kwa hiyo, wakaambiwa wafunge baadhi ya Vyuo vya Ualimu, kimoja cha Mtwara na kingine cha Tabora Urambo vilifungwa. Leo tunaanza kuona athari za maelekezo tuliyopewa. Wanaotoa maelekezo hayo wamejitosheleza kielimu. Sasa wanatuambia sisi tuondoe. Sasa tunaona taabu tunayoipata sasa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nitakalozungumzia ni suala la mgao wa pesa za ujenzi wa majengo haya ya shule, tangu msingi mpaka sekondari. Watu wote wanafikiri Tanzania ni Dar es Salaam au Mkuranga. Samahani kwa Wabunge wanaotoka maeneo hayo. Zinatolewa pesa za kujenga madarasa, thamani ya mfuko wa *cement* Kigoma leo ni Sh. 22,000/=. Dar es Salaam inawezekana pengine ni Sh. 7,000/=. Mtaniambia ninyi? Haya 12,000 kwa 22,000 maana yake ni shilingi 10,000 tofauti. Lakini hapo ndiyo umekwenda Kigoma Mjini.

Ukienda kwenye Jimbo langu, Kata ya mwisho mfuko wa *cement* ni Sh. 27,000/= na ninaamini katika nchi hii maeneo mengi yapo hivyo. Lakini Wizara inapotoa pesa, inatoa kama vile shule zote zinajengwa Dar es Salaam. Sasa kuna haja ya kutazama namna ya kugawa pesa hizi ili ziweze kukidhi, tujenge madarasa bora, sio bora madarasa. Tujenge nyumba bora za walimu, sio bora nyumba za walimu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la nyumba hizo hizo za walimu. Mimi nilipata bahati nikawa Mkuu wa Wilaya na kwenye Wilaya moja sitaki kuitaja, siku moja nilikwenda kuhutubia kuhamasisha kujenga nyumba za walimu. Nilizungumza mwaka

jana, nitalizungumza tena na nikipata nafasi tena nitalizungumza. Kwenye mkutano wa hadhara naambiwa mwalimu yeye nani? Mimi nikamtaja Rais wa wakati huo; nikasema huyo yeye nani? Maana sisi tunajipanga mstari kumpigia Rais kura, tayari keshajua atakwenda kukaa wapi, ana nyumba Magogoni ipo tayari pale. Lakini mtu anauliza, Mwalimu yeye nani? Kwa uelewa wangu, mimi najua Mwalimu anazo nyumba tatu. Anazo Ofisi tatu.

Ofisi ya kwanza ni darasa, Ofisi ya pili bahati mbaya mimi sijapata jina lake la Kiswahili, watanisaidia Wataalam. Lakini inaitwa *Staff Room* (Ofisi ya Mwalimu) na ofisi ya tatu, ni nyumba ya mwalimu. Akishamaliza kazi zake kule kwenye zile Ofisi mbili anahamishia nyumbani kwake.

Kwa hiyo, mwalimu huyu anatakiwa apate nyumba bora. Sasa ukitoa pesa hizi ni sawa sawa na kujenga nyumba Dar es Salaam, huyu mwalimu hawesi kupata Ofisi ya tatu bora. Ni kweli kwamba ipo nguvu ya wananchi inatakiwa iwepo pale. Lakini Serikali haiwezi kujivua jukumu lake ya kusimamia ili mwalimu apate Ofisi bora ya tatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri amezungumzia kwenye hotuba yake kuhusu vyuo vya VETA. Nilizungumza mahususi kuhusu chuo cha VETA Kigoma. Nikasema ingekuwa ni vizuri mitaala itolewe kutokana na mazingira maalum ya mahali pale chuo kilipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti sisi kule ni wavuvi, basi tungeiomba Wizara iweke mitaala itakayowafaidisha watu katika maeneo yale ili wasije kwamba wamepata taaluma, anakuwa ni fundi mchundo, lakini anakwenda kuwa manamba sehemu nyingine kama tulivyokuwa zamani. Lakini huyu akipata taaluma ya mambo ya ujengaji na uundaji wa mitumbwi ya uvuvi, atakuwa na uhakika kwamba kiwanda ni Ziwa Tanganyika. Kwa hiyo, ni vizuri Wizara ikaangalia mitaala kwenye Chuo cha VETA Kigoma ili iweze kuendana na mahitaji ya kwetu pale Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la lugha. Mimi nimekuwa nakerwa sana na hili nimekuwa nalizungumza sana. Wizara ya Elimu nadhani kuna watu hawataki kukipa Kiswahili nafasi inayostahili.

Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake ya maombi ya makadirio hapa alisifia sana umuhimu wa Kiswahili na akaeleza vile vile kwamba kwenye vikao tofauti vya kimataifa na vya kikanda, Kiswahili kinatumika. Lakini kwa bahati mbaya, mtu wa kwanza kutumia Kiswahili kwenye vikao hivyo wala hakuwa kiongozi kutoka Tanzania. Alikuwa Rais wa Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wenye ambao ndiyo tunatakiwa tuwe walimu mahiri wa lugha ya Kiswahili, Kiswahili kinaanza kutangazwa na wenzetu nje ya nchi kuliko sisi wenye. Sisi ukitulinganisha na wengine wote wanaotuzunguka sisi ndiyo tunaozungumza Kiswahili fasaha kuliko wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti sasa mimi najiuliza hivi kuna tatizo gani la kufundisha Kiswahili kuanzia darasa la kwanza mpaka Chuo Kikuu? Ukilitamka hili watu wanapata ubaridi. Wengine wanatuambia kwamba unajua tunatakiwa tuje Kiingereza ili tuwasiliane na wengine!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza, hawa Wakorea ambao wameharibu mitambo yao ya *Nuclear* kule, ile mitambo walijenga kwa kujifunza kemia kwa kutumia lugha gani? Walijifunza kemia kwa Kikorea. Warusi wanajifunza kwa Kirusi, Wachina kwa Kichina. Sisi kwa nini hatuwezi kuanza na utaratibu wa makusudi. Leo hii tukaanza kufundisha vijana wetu tangu darasa la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, alipokuwa anawatambulisha wataalam kutoka Vyuo Vikuu hapa nimesikia maprofesa wengi tu leo asubuhi. Naamini maprofesa hao wakikaa na maprofesa wa Idara ya Kiswahili kwenye Vyuo vikuu tulivyonavyo watakuja na misamiati ambayo itasaidia kufundisha mashuleni tangu darasa la kwanza mpaka chuo kikuu. Hivi Wizara inaona ubaridi gani wa kukuza hiki Kiswahili mpaka kwenye ufundishwaji na kwenye ngazi ya mwisho kabisa ya ufundishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nashukuru mkakati wa Serikali wa kuanzisha Chuo Kikuu cha Dodoma. Ukumbi ule ulikuwa unatumika kwa mikutano ambayo pamoja na kwamba ilikuwa na faida lakini ilikuwa haina tija kama ile ambayo inatolewa na taaluma zitakazotoka pale. Lakini imeanza kuwepo minong'ono Chuo Kikuu cha Dodoma. Mimi nafikiri Wizara ifuatilie hii. Hatutaki tupate watu waliopitia Chuo Kikuu cha Dodoma.

Tunataka tupate watu waliopitia Chuo Kikuu cha Dodoma na wakahitim kwa kuwa kweli wanastahili kuhitim. Chuo Kikuu cha Dodoma kumeanza kuwa kuna upendeleo wa ukabila katika kutoa taaluma hasa usahihishaji wa masomo. Ndiyo!

Sasa ni vizuri Wizara ikalifuatilia hili. Hiki ni chuo kipy. Chuo kipy kama hiki kinatakiwa kiende kwenye muala mzuri. Siyo kianze na picha chafu. Hii ndiyo sura tunasema watu wahamie Dodoma! Tunahamia Dodoma na mambo mazuri yatakayokuwa Dodoma na mambo mazuri ni pamoja na chuo. Baada ya kueleza hayo, Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKIT: Ahsante Mheshimiwa Msambya. Sasa namwita Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge na Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili ajiandae.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nipate nafasi ya kuweza kuchangia katika Bajeti ya Wizara hii, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina haja ya kuwapa shukrani, nimeshawaandikia huko. Shukrani nimeziweka katika maandishi. Nitakwenda moja kwa moja katika

kuchangia. Hapa ninavyo vitabu vitatu mfululizo vinavyohusiana na Wizara hii, cha kwanza ninacho cha mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti hii katika vitabu vyote hivi, bahati nzuri Wizara hii imekuwa na maneno matamu sana tunapoanza mwanzoni na imekuwa ikiyaita marejeo, imekuwa kama ni *mission statement*. Lakini haya maneno ni maneno ambayo yalitamkwa na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitasoma haya marejeo jinsi yalivyo halafu mtasoma na baadaye mtakuja kuelewa nina maana gani katika mazungumzo. Marejeo katika kitabu cha mwaka 2006/2007, anasema; “Elimu itakuwa ajenda muhimu ya Serikali ya Awamu ya Nne ambayo itaboresha taaluma ili kuongeza viwango vya ufaulu. Kuongeza ajira ya walimu wa elimu ya msingi na sekondari, kuimarisha taasisi za kudhibiti ubora wa elimu inayotolewa, kuhakikisha kuwa mafunzo ya ufundi stadi yanaendelezwa na kuimarishwa kama mkakati wa kupambana na tatizo la ajira. Kuboresha maslahi ya walimu katika shule na vyuo nchini.” Hiki ni kitabu cha Bajeti cha mwaka 2006/2007. Wameyanukuu maneno ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikaja cha mwaka 2007/2008, wamechukua maneno ya Rais; “Nawahakikishieni kuwa mnayo Serikali inayosikia, inayosikiliza, inayojali na iliyotolewa, kuhakikisha kuwa mafunzo ya ufundi stadi yanaendelezwa na kuimarishwa kama mkakati wa kupambana na tatizo la ajira. Kuboresha maslahi ya walimu pamoja na mazingira ya kufanya kazi.”

Mheshimiwa Spika, maneno yanafanana fanana na yale yaliyopita na hiki ambacho tunaendelea nacho marejeo yake yanasema; “Serikali ya awamu ya nne imeweka kipaumbele kikubwa katika elimu, hivyo Serikali itafanya kila iwezekananvyo ili kuhakikisha elimu bora inatolewa kwa wote. Kwa kutambua hili sasa masuala yote yanayohusu elimu kuanzia ya awali hadi elimu ya juu yatashughulikiwa na Wizara moja, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya ambayo yametolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni maneno thabiti ambayo yalikuwa yanaelekezwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa utekelezaji na si vinginevyo. Wizara ya Elimu, Waziri mwenye dhamana alikuwa anaelezwa ili kwamba atekeleze yale ambayo yamekusudiwa na Serikali ya awamu ya nne.

Sasa mimi naweza kusema tumekuwa na *priority* kwamba katika kipindi hiki mfululizo, fedha nyingi tumeelekeza Wizara ya Elimu na fedha nyingi zimekwenda Wizara ya Elimu ili kuboresha haya ambayo yamesemwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini hebu tuangalie na tulinganishe kati ya ile thamani ya fedha iliyotolewa na ubora wa hii elimu ambayo sasa tunazungumza, tulinganishe iko vipi? Na ni lazima twende hivyo kwa kujipima. Mimi ninaamini kabisa Waziri, Mheshimiwa Profesa Juamnne Maghembe, anafahamu hilo, yeye ni mwalimu na anajua, hata walimu wana utaratibu, wanafanya tathmini wanapofundisha wanafunzi. Kwa hiyo,

hatuwezi pesa ikawa imepitishwa, tunapitisha pesa nyingi na tunaamini tunasema *priority* yetu ni elimu lakini utekelezaji wake ukaonekana bado hauridhishi machoni mwa watu bado tutakuwa tunaharibu kauli za Rais, hilo jambo sio jambo ambalo litakuwa sawa sawa kabisa. (*Makofi*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba tulilalamika mara ya kwanza tukasema fedha za sekondari kupelekwa kwa wakuu wa shule moja kwa moja ni makosa. Kwanza ilipokuwa zikipelekwa hizi fedha za sekondari moja kwa moja, mkuu wa shule ilikuwa ni siri yake na *REO*. Walikuwa wanaweza wakafanya mambo na wakapelekwa wakafanya taratibu wao wenyewe wanavyoja na hata kamati za shule zisijue kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunafanya hivyo na tukapiga kelele sasa hela zikawa zinapitishwa Halmashauri. Sawa tunakubali hela zinapita Halmashauri, lakini mimi nasema Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu kuacha jukumu moja kwa moja la sekondari na shule za msingi liachwe moja kwa moja kwenye Halmashauri ni kosa sana. Halmashauri ina kazi nyingi, suala la sekondari lingebaki moja kwa moja Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu. Hivi kuna ugumu gani Mheshimiwa Waziri? Pesa mnapopeleka mnafanya *tracking*, ni *tracking* ya aina gani mnafanya? Mna uhakika gani? Kwa sababu *project* ni ninyi wenyewe ndio mnaziandaa, mnaandaa miradi, *proposal* mmetengeneza, mnawapelekea watu lakini utekelezaji unapotekelezwa hiyo *proposal*, nani anayekwenda kukagua kwamba huu ndio ubora amba tulikuwa tunauhitaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona hapa suala la *value for money* halipo, kwa hiyo, tunachotaka kusema Mheshimiwa Waziri, kwamba ni lazima tuangalie hatuwezi kusema kwamba kila jambo sasa tunawaachia Halmashauri, Halmashauri wana mambo mengi sana. Halmashauri wanafanya shughuli nyingi sana, shule za msingi zenyewe zimewaelemea. Sasa mimi nilikuwa naona kwamba bado upo umuhimu na bado ipo wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wako wote kwamba lazima sasa mtoke ili muwe mnahakikisha hizi fedha tunazozipitisha nyingi zinazokwenda huko mnazisimamiae. (*Makofi*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa kabisa kwamba tunapoweza kuelimisha jamii kwa kiwango kikubwa tutakuwa tunaweza kufikia hata yale malengo ya MKUKUTA. Kwa sababu mtu ukimuelimisha elimu, anaweza kupambana na rushwa, atapambana na maradhi, atapambana na umaskini, kwa sababu ya ile elimu. Sasa ninachotaka kusema ni kwamba lazima Wizara ihakikishe ubora wa suala la elimu na elimu inayotolewa na hasa hii elimu ya sekondari, kwa sababu elimu ya sekondari ndiyo inayoanza kumuandaa mtu kwenda katika maisha mapya. Kwa sababu ukitoka elimu ya sekondari hapo atakwenda na mwisho wake atafika katika vyuo na baadaye anarejea katika maisha ya kawaida kufanya kazi. Nilikuwa nataka niseme hilo na nilisisitize kwamba bado narudia naomba Wizara isiwe mbali na wananchi. (*Makofi*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, na lingine wamezungumza wazungumzaji waliopita, tunakuwa na miradi ya ujenzi wa hizi shule lakini tunajenga hapo hapo tunajenga nyumba za walimu. Tunapojenga nyumba za walimu, tumeeleza viwango hafifu ambavyo

vinatumika kwa ujenzi wa majengo ya nyumba za walimu, lakini kwa sababu jukumu la kumuajiri mwalimu ni la Wizara, mimi nilikuwa naomba Wizara inapomuajiri mwalimu ihakikishe yule mwalimu anapokwenda kule basi ihakikishe na kwamba atafikia mahala gani. Wewe huwezi kupewa ajira, hata ye ye Mheshimiwa Waziri, wakati anateuliwa kuwa Waziri, aliandaliwa nyumba nzuri na akaandalila akaambiwa hapa ndio utaishi ili utekeleze majukumu ya Wizara. Sasa na walimu ni lazima tuwaandalie mazingira, tuwaachie wananchi wafanye kazi moja ya kujenga hayo maboma kwa ajili ya madarasa. (*Makofii*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana mmeweza kutenganisha zile kofia kama Rais alivyosema kuwa na Maafisa Elimu, wawili. Yule Afisa Elimu wa Shule za Msingi na Afisa Elimu wa Shule za Sekondari, lakini nilichokuwa naomba kadri tunavyoshuka chini ndio majukumu yanavyoongezeka.

Mimi naomba Wizara, iangalie eneo la kata kuwe na mtu mmoja anayeitwa *MEK* ambaye ndiye anashughulikia elimu ya msingi na anashughulikia elimu ya sekondari pia, nalo ni mzigo kulinganisha na Kata zetu tulizonazo. Mfano mzuri unaweza ukaangalia mimi nina Kata moja inaitwa kata ya Ndago, ina vijiji karibu vitano na ukubwa wake ni kubwa sana au Kata ya Shelui. Sasa unaweza ukakuta huyu *MEK* anashindwa kuweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa hiyo, nilikuwa nataka niangalie nione na hilo uwezo wake uweze kuufanya *u-turn up* katika eneo hilo ili kuweza kuboresha hiyo Idara ya Elimu katika ngazi ya Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti zote zilizopita zimezungumzia namna walimu walioajiriwa, walimu wa sekondari na katika kuzungumzia tangu mwaka 2006 ilikuwa ni katika kuboresha namna ya kupata walimu kwa wingi. Na ilieleza katika Bajeti ya mwaka 2006, walieleza wakasema kwamba ili kuweza kurahisisha kupata walimu wa kutosha Wizara pia itakaribisha wale walimu ambao waliokuwa wamestaafu na hawa walimu wakiwa na sifa na afya njema basi waombe ili warejee kufanya kazi kwa mkataba. Najua hili nikisema Mheshimiwa Waziri, unaweza ukasema liko Utumishi au liko Wizara ya Fedha, lakini wenye shida ni Wizara ya Elimu, sisi tunashida na hao walimu. Usipofuatilia hilo wewe mwenye Wizara, bado tunaweza tukaendelea mafanikio yakawa madogo.

Mimi nina mfano mmoja mzuri mwaka 2006, walimu wanne amba walikuwa wastaaafu wamewasilisha maombi. Yuko Mwalimu Godfrey Pyuza, yuko mwalimu Nesphoro Mathayo, yuko mwalimu Shani na yuko mwalimu Kassim Maksoud, wamewasilisha maombi mpaka leo hawajajibiwa, kweli tunadhamira ya kuweza kuendana na hii *statement* ambayo imezungumzwa katika vitabu vyenu vya mwanzo kauli ya Rais? Iramba tuna matatizo makubwa ya walimu, tuna upungufu mkubwa wa walimu sasa hata ile kuomba tunasema kwamba hawa waweze kuwezesha ili sasa waingie waweze kufanya kazi ya kufundisha kwa mkataba lakini imeshindikana. Kwa hiyo, naliomba sana hilo lipewa kipaumbele. Naomba na najua mwakani tutakuwa na shule mbili za *High School*, tutakuwa na shule ya Lulumba halafu tutakuwa na Iguguno Sekondari, zote hizi zitakuwa ni shule za *High School*, tunaomba tutakapoanza vitu vyote

vinavyohitajika katika *high school* tuvipate. Tuvipate kwa lengo la kuhakikisha kwamba tunapata elimu bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa haraka haraka niliwahi kuongea Bajeti ya mwaka 2006 hapa kuhusiana na shule ya sekondari ya Kizaga juu ya mwalimu aliyekula pesa za mradi pale na hili Mheshimiwa Waziri, nitaomba majibu makini sana ili kuhakikisha, kwa sababu lile jengo toka lilipoachwa liko vile vile na fedha ilishaliwa na kesi ile haipo na yule mwalimu tunajua ameshahamishwa amepelekwa shule nyingine.

Sasa nitaomba katika majibu yako unipe jibu la kutosheleza kuhusiana na hilo vinginevyo kwa ukweli itakuwa ni vigumu sana kukuunga mkono. Bweni lilijengwa lakini limeshindwa kumaliziwa kutokana na zile fedha ambazo yule mtu aliondoka nazo lakini mnaendelea na ajira yake bado anaendelea mpaka sasa, kwa hiyo, nitaomba majibu ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie majengo ya Kampuni ya *CHICO* yaliyoachwa pale na wajenzi wa barabara ambayo sasa tumekabidhiwa *WDC* ya Ulemo. Naomba kwamba yale majengo sisi tumeomba *VETA*, japo hatumo katika mpango huu wa Wilaya 25 nina hakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. DR. BINILITH S. MAHENG: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na ningependa kutamka moja kwa moja kwamba naunga hoja hii mkono na nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Naibu Mawaziri wote wawili wote wawili na watendaji wa Wizara yote kwa kuleta hotuba nzuri ambayo kimsingi imechambua hoja baada ya hoja na kuainisha nini tunatakufanya. Nataka nianze kuchangia kwa kuchambua Tume ya Vyuo Vikuu, *TCU*, Baraza la Ufundi, *NACTE* na *VETA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Vyuo Vikuu kazi yake kubwa ni kutoa ithibati kwa vyuo vinavyoanzishwa. Lakini vile vile Tume hii kazi yake ni kuangalia, kuandaa mazingira ya vile vyuo ambavyo vinataka kusajiliwa kuona kama vinafaa ili viweze kusajiliwa baada ya kutimiza masharti yanayostahili. Na jukumu lingine ambalo ni muhimu sana ni kuhakiki ubora wa elimu inayotolewa na vyuo hivyo ambavyo vinakuwa vimeshapewa ithibati na Tume hii ya Vyuo Vikuu. Vile vile ukingalia Baraza la Ufundi la Taifa, (*National Council for Technical Education – NACTE*), wao pia kazi yao kubwa ni kusajili vyuo ambavyo ni *non-universities*. Lakini vile vile ni kutoa ithibati kwa vile ambavyo vinakuwa vimetimiza yale masharti baada ya kusajiliwa. Na jukumu lingine muhimu la tatu ni kufuatilia au kuhakiki ubora wa ile elimu inayotolewa pamoja na kuruhusu kuandikisha programu nyingine mpya ikiwa vile vile ni kusimamia taratibu zote za mitihani. Lakini ukienda upande wa *Vocation Education and Training Authority (VETA)*, wao kwanza wanajukumu la kusimamia vile vyuo vyote ambavyo vinatoa mafunzo ya *VETA*. Lakini vile vile wao wenywewe wanafanya *role* ya *training*, kama unavyofahamu tuna vyuo karibu 21 nadhani katika kila mkoa ambavyo vinasimamiwa na *VETA*. Kwa hiyo, upande mmoja wana kazi ya kufundisha vyuo vya wao wenywewe lakini

upande mwingine wana kazi ya kusimamia na kuhakiki ubora unaotolewa na vile vyuo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa kuna *conflict of interest*, haiwezekani ukatoa mafunzo mwenyewe halafu ukajihakiki mwenyewe kwamba ubora unaoutoa ni huu na hasa ukizingatia kwamba sekta hii ya *VETA* bado kuna vyuo vingine ambavyo ni vya watu binafsi ambavyo vinategemea *VETA* huyu huyu aweze kuhakiki ubora wa vyuo hivyo, kwa hiyo, hakuwezi kuwa na usawa katika mchezo huu wa elimu bora kwa vijana wetu.

Kwa hiyo, nilikuwa namuomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anatoa ufanuzi wa hoja yake akubali mapendekezo yangu kwamba ni muafaka sasa kitengo cha kuhakiki ubora wa mafunzo yanayotolewa na *VETA* kihamie katika Baraza la Ufundis yaani *National Council for Technical Education Authority (NACTE)*, wao wabaki na *role* ya kufundisha tu au la sivyo basi waondoe hiyo ya kufundisha, ambayo nadhani haitawezekana kwa sababu hiyo ndio tunayoitegemea sana kwa ajili ya kufundisha vijana wetu wa Tanzania. Kwa hiyo, hiyo ni hoja yangu ya kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili ukiangalia kwenye kitabu cha hotuba cha Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 68 kifungu cha 105, anaelezea Tume ya Vyuo Vikuu kupewa jukumu la kuandaa mpango maalum unaoitwa *National Qualification Framework (NQF)*. Mpango huu ni muhimu sana na nadhani kimsingi nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwamba amefikia kuwa na mpango huu ambao unaainisha sehemu mbalimbali za mafunzo yanayotolewa na nchi yetu. Lakini mpango huu unatakiwa uainishe katika *system* nzima uonyeshe *relevance* ya zile *qualifications* ambazo zinatolewa *versus* suala la ujenzi wa uchumi wa nchi yetu, lakini vile vile mfumo huu uonyeshe *credibility* kwa maana kwamba ile *recognitions* ya hizo *qualifications* Kitaifa na Kimataifa. (*Makofi*)

Lakini vile vile huu mfumo lazima uonyeshe *flexibility* ya hizi *qualifications* na *programs* katika vyuo mbalimbali. Mfumo huu vile vile lazima uonyeshe *vertical progression* kwa namna gani kijana anayesoma katika vyuo vya *VETA* anaweza aka-*progress* mpaka akawa pengine ni *Engineer* au *craftsman* anaweza akawa *chief craftsman* au mtu ambaye ametoka kwenye elimu ya ufundi akaona ni namna gani anaweza akaenda sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hilo ni wazi kwamba hili ni jukumu kubwa sana, kwa hiyo, najiuliza labda Waziri atanieleza ni kwa nini waipe *TCU* kuandaa *National Qualification Framework* wakati ni jukumu ambalo ni la wadau wengi. Kwa nini hawakuwapa *National Council for Technical Education Authority (NACTE)* nasema hivi kwa sababu elimu ya ufundi imekuwa ikikandamizwa sana na hii imejionesha hata katika *enrolment* za vyuo vya ufundi kama *Arusha Technical College, DIT, Mbeya* na vyuo vingine. Leo kwenye hotuba hapa imeonesha kwamba Arusha wana-enrol mwaka huu wanafunzi 163, chuo hiki kimeanzishwa mwaka 1978, kweli tutasema tunatilia maanani suala la ufundi? Kwa hiyo, ndio maana nadhani kwamba ipo haja ya ushirikishwaji wa sekta hii ya ufundi katika kuandaa hiyo *National Qualification*

Framework ili iweze kuonyesha namna hawa watu wanavyoweza ku-progress na namna wanavyoweza kuchangia katika suala zima la uchumi.

Kwa hiyo, ninachomuomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anajumuisha, kwanza atueleze ni kwa nini wamepewa *TCU* hili jukumu, lakini pili akubaliane na mimi kwamba basi hatu kama wamepewa *TCU* tuone hiyo *composition* ya timu ambayo itaandaa hiyo *NQF*. Tuone kama ina wataalamu wa aina mbalimbali na hasa ukizingatia taasisi za ufundi na wataalamu wengine wa kiufundi ili iwe na mwelekeo mzuri ambaio sio wa kuuwa taaluma hii ya ufundi. Wote mmeona vyuo vya ufundi vimechukua muda mrefu sana kukua lakini tunasema kwamba tunapotaka kwenda kwenye *semi industry* tutaendaje kama hatuna watu ambaio wamepitia mafunzo ya ufundi. (*Makofi*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, linalofuata ni suala zima la Vyuo vya Ufundi vya *VETA* kujengwa katika Wilaya, Ilani ya Chama cha Mapinduzi inasema wazi kabisa kwamba tumedhamiria kujenga chuo kimoja katika kila wilaya. Na ninaipongeza Wizara hii kwa mkakati wake kwamba mwaka huu tayari imeshatoa dhamira yake kwamba iko tayari kuanza kujenga Vyuo 25 kama inavyooneshwa kwenye kitabu hiki ukurasa wa 103, lakini nilitaka kujifunza Mheshimiwa Waziri, mwaka jana ndani ya Bunge lako hili Tukufu tulitoa mapendekezo kwamba viko vyuo vilivyoko chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ambavyo kama vingehamishiwa *VETA* vingeharakisha kutekeleza hili wazo la kuwa na chuo cha *VETA* katika kila Wilaya, limefikia wapi? Kwa nini limeachwa? Nadhani hii ingeweza kuchangia haraka zaidi ili Serikali ingeweza ku-concentrate kwenye zile Wilaya ambazo hazina vyuo hivyo kuanzisha vyuo vingine vipyta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi nimeshangazwa sana kwenye jedwali lile la 103 kwamba katika vile vyuo wamevigawa kwa kanda sasa najiuliza, unakuta kanda moja imepeleka vyuo viwili katika mkoa mmoja, au vyuo vitatu katika mkoa mmoja. Angalia kwa mfano Kanda ya Kusini, vyuo vimekwenda Mbeya, Iringa hakuna chuo hata kimoja. Sasa najiuliza tumekuwa tukipiga kelele tunasema kwamba Wilaya ya Makete ina matatizo ya UKIMWI, Wilaya ya Makete ina watoto wengi yatima, tutawasaidiae hawa watu kama hatuwezi kuwapelekea shughuli za maendeleo kama haya kufungua Vyuo vya Ufundi vya *VETA* ambavyo vitachukua wanafunzi wa kuwasomesha ili waweze kupata *skills* na hivyo kuwa *busy* katika shughuli za uzalishaji. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nilikuwa namuomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuja atoe ufanuzi walifikiaje uamuzi wa mgawo wa hivyo vyuo lakini ningependa sana aje na jibu kabisa kwamba kwa kweli ameelewa kwamba matatizo ya Makete yanahitaji kuwasaidia katika elimu na sio vinginevyo ili kuweza kuondokana na matatizo haya yaliyotukumba kule Makete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu nyingine ni kuhusu ufundi stadi. Nataka nichukue nafasi hii vile kumpongeza Mheshimiwa Waziri, mimi nimepitia mkondo wa ufundi, tumekuwa tukipiga kelele sana wakati nikiwa chuoni huko kuona namna ya vijana wanavyoweza kutoka katika mfumo wa *VETA* na baadaye kuingia vyuo vya ufundi au kwenda vyuo vingine. Kwenye hotuba yake ameeleza umuhimu wa *NACTE* kikutana

na VETA ili waweze kuandaa utaratibu kuwa na *bridging course* au aina fulani ya muundo kutoka kwenye *level III* kwenda kwenye *level IV*, hiyo ni hatua nzuri. (*Makofî*)

Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza kwa wenzetu wa VETA kwamba hii ni nafasi nzuri ya kuona ni namna gani wanaweza waka-*include* kwenye hizo *modules* zao kama za kiingereza, hisabati na sayansi ili waweze angalau kufikia vile vigezo vitakavyohitajika kuingia katika hiyo *level IV* kwa sababu bila hivyo tunaweza tukashusha thamani ya elimu. Lakini vile vile kufanya vile kutasaidia vijana wengi kwenda kwenye mfumo huu wa VETA kwa sababu walikuwa wanaona kwamba hauna *vertical progression*, kweli ilikuwa inaonekana kama ni *dumping place* na wazazi wengi walikuwa hawawapeleki watoto wao kule. Kwa hiyo kwa kweli hili ni zuri na tungedhani kwamba lifanyiwe kazi haraka ili watoto wanaoamua kwenda VETA wajue wanaweza wakaingia na mfumo wa kwenda juu au wakenda *horizontally*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya mwisho ni sekondari za Kata. Kwanza naungana na wenzangu kwamba upo umuhimu mkubwa wa kuboresha maslahi ya walimu. Mimi nadhani hapa lazima tuwe na hoja ya msingi, hatuwezi tukayapeleka maslahi ya walimu tukalinganisha na maslahi ya wafanyakazi wengine. Nchi za wenzetu huko nje waliweza mpaka kutunga sheria ambayo ilikuwa inaongelea maslahi ya walimu tu, na walifikia mahala wakahakikisha kwamba kwenye sheria ile inaelezea mwalimu analipiwa nyumba, analipiwa umeme na hata kwenye usafiri wa umma anasafiri bure.

Sasa nilikuwa nadhani hii ni hoja ya msingi ambayo Serikali ichukulie kwa juhudhi zake zote ili kuweka mazingira mazuri kwa walimu wanaofundisha, kwa sababu kwa namna hii mimi kule Makete, sitapata walimu kwa sababu mazingira ni magumu, mishahara ni midogo na nyumba ndio hivyo tena kwa hiyo, nilikuwa nadhani ni vizuri kuwe na hilo. Lakini nilidhani vile vile niseme kwamba kutokana na tatizo hili la walimu labda Wizara wakati inaandaa hii mikakati mingine ya muda mrefu iunde kikundi cha wataalamu wanaojua sana masomo ya sayansi kama hesabu, fizikia, kemia na masomo mengine, hawa waipitie ile *syllabus* waandae vile vipindi kwa kutumia *video* na *CD/DVD* ili vite vitu viweze kusambazwa kwenye shule kwa sababu uzoefu unaonyesha kwamba ziko shule zina walimu wote lakini bado kufeli kuko pale pale. Kwa hiyo, vile vile ni vizuri kama wanafunzi wanaweza wakapata vite kama vile ambavyo vina *content* nzuri wanaweza wakajisomea na huenda wakafaulu vizuri zaidi. Kwa hiyo, hayo ni mapendekezo yangu, lakini naomba nirudie tena kumuomba Mheshimiwa Waziri, afafanue vizuri kuhusu hoja ya *NQF* kupewa watu wa *TCU*, kwa misingi ipi? Na kama imeshirikisha vipi hasa vyuo vya ufundi ambavyo vimeonekana vikiwa nyuma kwa Bajeti wakati wote na hata kwa *enrollement*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofî*).

MHE. NURU A. BAFADHIL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipatia nafasi hii kuweza kuchangia. Na mimi pia naungana na wenzangu katika kuiomba Wizara iwaangalie sana walimu katika kuboresha maslahi yao, kwa sababu leo hii tuna maprofesa, wahandisi, madaktari na kadhalika na kadhalika, lakini yote hii ni

kazi ya walimu, kazi ya walimu ndiyo iliyofanyika mpaka tukaweza kupata watu namna hii. Kwa hiyo, walimu tuwaboreshee maslahi yao ili waweze kufanya kazi, kutokana na maslahi duni ya walimu ndio maana inapelekea walimu kufanya vitu ambavyo ni vya ajabu ajabu, hususan katika shule nyingi za msingi. Utakuta mwalimu kabla hajaanza somo ataanza kuuza biashara kwanza ili aweze kupata pesa apeleke kidogo nyumbani watoto wapikiwe chakula wakati yeYe akiwa yuko kazini na hii pia inasababisha utoro kwa baadhi ya wanafunzi. Wanafunzi wanakopeshwa vitu, wengine wazazi wao hawana uwezo wa kulipa pesa, kwa hiyo, haendi shule kutokana na kuwa akifika kule mwalimu atamda pesa zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia kuhusu michango. Tunashukuru Serikali imeanzisha shule nyingi za Kata na wanafunzi wengi wamefaulu kuingia katika zile shule. Lakini kuna tatizo linalojitokeza katika hizo shule, michango imekuwa ni mingi sana. Serikali ilituonea huruma sisi wazazi ikaona kwamba ada ya shilingi 40,000/= mzazi hataimudu, ikaiteremsha kutoka shilingi 40,000/= mpaka shilingi 20,000=/. Lakini cha kushangaza sasa hivi mwanafunzi anaanza kidato cha kwanza anatakiwa achangie takribani shilingi 120,000/= mpaka 150,000/= mpaka 200,000/= shule nyingine. Anatakiwa achangie vitu kadhaa ambavyo vingine havina umuhimu, anatakiwa aende na kwanja, jembe na ndoo, mpaka sare za shule pia anatakiwa akazinunue pale pale shulenii, hata kama baba yake ana duka labda au mama/baba yake ni fundi chereheni lakini hatakiwi ashonewe nyumbani lazima akashonewe vitu vile pale shulenii. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kwa njia hii inapelekea watoto wengi wazazi wao wanashindwa kuwapeleka shule kutokana na kuchangia fedha hizo. Mimi ninayo mifano hai ambayo watoto sasa hivi hawaendi shule kutokana na wazazi wanashindwa kulipia ada au hiyo michango ambayo ni mingi sana ambayo mzazi hawezi kuilipia. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, atueleze je, huu uchangiaji wa hizo pesa nyingi labda ni *circular imetolewa* au ni walimu shulenii wamekutana wenye tu wakaamua mtiririko huo ufanyike? Maana yake kila shule mwanafunzi anayokwenda ni kuchangia, kila shule anayokwenda mwanafunzi ni kuchangia. Ni vitu vya kuchekesha kwa mfano mtu anaanza kidato cha kwanza, wanafunzi 80 ambaa ni labda kidato cha kwanza A na B, wanatakiwa wapeleke ndoo ina maana ni ndoo 80 sijui walimu wanaenda kufanya biashara za ndoo? Au sijui wanaenda kufanya nini na ndoo hizo. (*Makofi/Kicheko*)

Kwa hiyo, tuangalie hii itadhoofisha hali na zaidi inadhoofisha kwa wasichana wetu tunaowalenga kupata elimu halafu baadaye tuje kwenye hilo zoezi la 50/50, kwa hali hii 50/50 haitafikia kwenye lengo lake kwa sababu watoto wa kike wanakatishwa tamaa na wazazi wao na hasa wazazi wetu wengi wa Pwani wanawaambia aah, mimi nauza maandazi mbona naishi? Kakae na wewe unisaidie kuuza maandazi kama mwalimu anataka michango kiasi hicho. (*Makofi*).

Kingine napenda kuzungumzia kuhusu ubora wa madarasa, kwa kweli ubora wa madarasa hauridhishi, wazazi wanachangia pesa zao, Serikali nayo inaongeza pesa zake lakini utakuta darasa halifai kabisa. Mwaka jana tulipokuwa na ziara na aliyekuwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa, tulitembelea Kata moja ya Tongoni hata darasa halijahamiwa tayari darasa limepata ufa kuanzia juu ya ukuta mpaka kwenye sakafu ni

ufa mtupu. Yaani ile Kamati ya Ujenzi haifikirii pia au haina hata imani na zile pesa zinazochangiswa. (*Makofi*)

Mimi nilisoma shule moja ya msingi ilikuwa inaitwa *Tanga Girls School* hiyo shule toka imejengwa mpaka leo sidhani kama ina ufa. Kuna shule za sekondari kwa mfano Mkwakwani ambayo zamani ilikuwa inaitwa *Karimjee Primary School* ambayo sasa hivi ni *Mkwakwani Secondary School*, kulikuwa na *Karimjee Secondary School* ambayo sasa hivi inaitwa *Usagara Secondary School*, au kuna *Old Tanga Secondary School* ambayo ilijengwa toka mwaka 1905 lakini zile shule ziko katika ubora mzuri, hawa wenzetu walipojenga walijenga kwamba angalau kuchukue hata miaka 30 au 40 au 50 shule iwe haijafanyiwa *repair*. Lakini shule ikijengwa leo, kesho inatakiwa ifanyiwe *repair*, ikinyesha mvua nyingi pia upepo kidogo ukija shule yote inaezuliwa bati. Kwa hiyo, tuangalie jamani tuzifikirie hizi hela zinazochangishwa na ndiyo maana wazazi wengi wanakataa kuchangia hizi pesa kutokana na kwamba wanaona pesa zinakwenda kusikostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine napenda kuchangia kuhusu walimu ambao ni walimu wanaofundisha watoto wenye matatizo maalumu kwa mfano kuna watoto ambao hawaoni, kuna watoto walemovu wa viungo, wengine hawasikii na wenye mtindio wa ubongo. Walimu wale pia nao wafikiriwe, wanafanyakazi katika mazingira magumu, utakuta mwalimu yupo na wale watoto yaani yale matendo wanayofanya watoto yanafanana na mwalimu yule yule inabidi awaigize vile wanavyotaka ili wale watoto wawe wapo shulenii wanasoma, lakini bado wanaishi katika mazingira magumu na wanafanya kazi katika mazingira magumu na wakati mwengine yabidi mwalimu amsindikize mtoto mpaka nyumbani kwao...

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mwongozo wa Spika.

MHE. ZUBEIR ALI MAULID – MWENYEKITI: Mwongozo!

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 136 ukurasa wa 84. Kifungu hicho kwa sababu mzungumzaji anayezungumza sasa hivi amazungumza mambo ya maana na kifungu hicho kinazungumzia ruhusa kwa wageni kuingia Bungeni. Sasa kwa sababu ruhusa hii huwa tunatoa sisi kupitia utaratibu wetu maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale juu kuna watu viziwi yaani walemovu hawasikii lakini kulikuwa na mtu pale mkalimani anafanya tafrisi ya haya yanayozungumzwa sasa hivi na Mheshimiwa ili wale wenzetu wafuatilie haya mazungumzo yanayofanywa hivi sasa. Lakini kwa bahati mbaya askari wa Bunge hili wamekwenda kumuondo yule anayefanya tafsiri na alikuwa hasemi anafanya kwa mikono. Sasa tunawanyima haki wananchi wale. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba mwongozo wako ili yule mtu arudi ili wenzetu hawa wapate haki ya kusikia haya yanayozungumzwa humu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako. (*Makofi*)

MHE. ZUBEIR ALI MAULID – MWENYEKITI: Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, ahsante sana.

Kwa kuwa hili ni Bunge la wananchi wote sasa mimi natoa agizo kwa Makatibu Mezani ili waweze kulisimamia hilo na kuhakikisha kwamba wote waliomo humu wanafaidika na hiki kinachoendelea hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Nuru Bafadhili unaweza ukaendelea!

MHE. NURU A. BAFADHIL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante itabidi na dakika zangu zilizoliwa niongezwe. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. ZUBEIR ALI MAULID – MWENYEKITI: Tutazingatia kidogo.

MHE. NURU A. BAFADHIL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sasa walimu hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu. Mfano siku moja mimi nilisafiri kwenda Handeni, nilipokuwa njiani narudi nikakutana na mwalimu mmoja amekwenda kuwachukua watoto ambao wanasoma katika shule ya msingi Pongwe ya watoto wasioona. Yule mwalimu ilibidi amepewa nauli tu ya kwenda kule Handeni nikapakia naye pamoja mpaka tukafika Mkata pale wakati anasubiri gari ya kumchukua na wale wanafunzi ambao walikuwa ni wawili na mizigo yao kuelekea Pongwe, kila basi lililokuwa linapita kwa kweli lilikuwa limejaa baadaye lilipita lori ambalo lilikuwa limebeba mahindi, kutohana na kwamba mwalimu yule alikuwa amechoka akaomba hivyo hivyo apate msaada na ilikuwa ni kama saa kumi na mbili kasoro robo jioni, ikabidi apakiwe na wale wanafunzi ambao maskini hawaoni. Wale wanafunzi wakapakiwa nyuma kule kwenye magunia nikamwambia lakini mwalimu si afadhali ungepaki tu hapa akasema kwa kweli pesa nilizonazo hapa hazitanitosheleza hata kulala katika nyumba ya kulala wageni kwa hiyo, itabidi mimi kila itakavyokuwa niende Tanga kwa ajili ya kufika Pongwe, kwa hiyo akapakia nao.

Kwa kweli nilisikitika sana kitu kama hicho kwa mfano itatokea ajali wale vijana ambao hawaoni maskini ya Mungu watajisaidia vipi? Kwa hiyo, naiomba Wizara, walimu wanaoshughulika na watoto wale wenye matatizo maalum wawe angalau wakati wanapowerudisha watoto wale majumbani kwao kuwe na gari maalum itakayowawezesha kuwafikisha mpaka nyumbani kwa sababu walimu wanapata adha sana kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu nikizungumzia kuhusu walimu, kuna walimu mbao wamejiendeleza mpaka wamefikia ngazi ya *Diploma* baada ya kufikia *Diploma* kuna hizi shule zetu za Kata zilizoanzishwa kwa hiyo walimu wanatolewa katika zile shule za msingi wanapelekwa katika shule za Kata. Lakini tatizo linakuwa kwamba wanapopelekwa kutoka kwenye shule ya msingi na kupelekwa kwenye shule zile za sekondnari za Kata hakuna mabadiliko yoyote kwa sababu kule ina maana kwamba anakwenda kuingia kwenye ajira nyingine kwa sababu anatoka kwenye shule ya msingi anakwenda kuingia kwenye shule ya sekondari. Anatakiwa pia anapoondoka pale

anakwenda kwenye shule nyingine ahamishwe lakini utaratibu huo hakuna, hakuna utaratibu wowote unaomfanya mwalimu ahamishwe, halipwi marupurupu yoyote, hakuna taratibu zozote za mabadiliko ya ajira kwa hiyo, mwalimu anakuwa anafanya kazi katika mazingira ambayo kwa kweli hayastahili. Kwa hiyo, naiomba Wizara nayo ilifikirie hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ninachotaka kuelezea kwa masikitiko sana kwa kweli kuna wazazi wengine wanakuwa hawana huo uwezo wa kusomesha watoto wao lakini na Halmashauri zetu nazo pia vile vile zinakuwa zinaandaa utaratibu wa kufanya vikao vya kuweza kusaidia watoto wale ili waweze kusoma bure. Sasa kuna baadhi ya watendaji kwa kweli wanaskitisha sana wanaingia itikadi za kisiasa ndani ya maendeleo ya wananchi kwa sababu unaposomesha mtoto usiangalie anatoka katika chama gani, wewe muangalia asome kwa sababu pengine atakuja kukufaa wewe ambaye uko kwenye hicho chama kingine. Lakini leo mtoto anakwenda pale shulenii anakwenda pale ofisini kuombewa na mzazi wake anaambiwa kuwa wewe chama chako ni chama fulani kwa hiyo, hatuwezi kukusaidia, nendeni mnaye Mbunge wenu huko akawasaidie. Sasa tutawasadidua wangapi sisi na sisi tunajua Tanzania yote ni moja. Kwa hiyo, nadhani hawa watendaji wanaskia na jambo kama hili naomba wasilirudie tena. (*Makofi*)

Pia napenda kuwapongeza wananchi wangu wa Tanga wa Kata ya Chongoleani kwa kweli wamefanya mambo mazuri sana, Kata ya Chongoleani wameweza kujenga shule mbili za sekondari lakini ninachoomba shule ya Chongoleani, shule moja iko Chongoleani na shule moja iko Ndaoya, basi angalau hiyo shule moja ya Chongoleani isiwe ni *O-Level* na hiyo na hiyo ya Ndaoya iandaliwe kwa ajili ya *A-Level*. (*Makofi*)

Kwa hiyo, wananchi wenzangu wa Tanga tuhakikishe tunaanza Msaragambo kusaidiana kuweza kujenga nyumba kwa ajili ya walimu na tuweze kujenga maabara, tuweze kujenga hata *hostel* ili watoto wetu waweze kupata sehemu ya kuweza kusoma kwa sababu huu utitiri wa sekondari zilizozuka tutakuja kukwama katika kupata shule nyingi za *A-Level*. Kwa hiyo, watu wa Tanga nadhani mnanisikia na kwamba tushughulike na tusaidiane na mimi nitaungana na ninyi pamoja ili tuweze kupata angalau shule ya *A-Level* na watoto wetu watakomaliza Kidato cha Nne waweze kuingia katika shule hiyo ambayo imeshaandaliwa iko huko Kata ya Chongoleani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa mimi naomba wazazi wetu ni wazuri wana miyo ya kujitolea na wanachanga pesa zao lakini tatizo linakuja kwamba mzazi anapohoji matumizi ya pesa zilizochangwa kwa ajili ya kujenga shule, mzazi huyo anafunguliwa mashitaka na anapelekwa Mahakamani na hili hapa kwa mzazi mmoja mwanakijiji wa kijiji cha Kilulu, Kata ya Muheza amehoji tu kwamba kwa nini pesa hizi zimetumiwa vibaya, hivi sasa kwa habari zisizo na uhakika ameshafunguliwa kesi Mahakamani. Je, hivi jamani sisi tunawatakia mema hawa wazazi? Tunaendeleza Taifa au tunabomoa taifa? (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi ninachoomba Serikali ihakikishe hasa hizo fedha za vijiji vyetu itikadi za kisiasa zitupwe mbali sisi tunachotafuta tunatafuta maendeleo, siasa zitakuja sasa hivi hatupu katika siasa tunafuta maendeleo, mwaka 2010 tutakuja kupambana

kwenye vilinge ili tuhubiri hayo tunayoyataka lakini kwa sasa hivi tunachotaka ni maendeleo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi naomba Serikali hasa Serikali zetu za vijiji hasa Serikali zetu za mitaa zihakikishe kwamba zinatoa maelekezo kuhusu matumizi ya pesa zao walizochanga. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. ZUBEIR ALI MAULID - MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Nuru Bafadhil, huo ushahidi ulionao nadhani ungempelekea Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri ili waweze kukusaidia. (*Makofi*)

Sasa ninamuita Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, atafuatiwa na Mheshimiwa Bernadetha Mushashu na Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, ajiandae.

MHE. MWADINI ABBAS JECHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na uzima siku ya leo kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kadhalika nichukue nafasi hii kukupongeza wewe kwa kunipa nafasi hii na ningependa pia nichukue nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Waheshimwa Naibu Mawaziri, watendaji wa Wizara kwa hotuba yao nzuri ambayo wameileta hapa Bungeni leo na ambayo Wabunge wako wanajitahidi kuichangia na kuiboresha hotuba hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mnyimi wa fadhila kama sikuwapongeza walimu. Walimu wa Tanzania kwa kweli wanastahili pongezi kubwa sana, ni watu wanaojituma, watu wengine wanasema ualimu ni wito kwa sababu hata uchawi ni wito vile vile. Lakini ualimu ni kazi ya kujituma, ni kazi inayohitaji maarifa, ni kazi ambayo inahitaji uvumilivu mkubwa sana. (*Makofi/Kicheko*)

Sasa mimi leo nataka kuzungumza habari ya walimu tu, na kwa kuanzia mchango wangu ningependa kuzungumzia suala ambalo linaboresha labda maslahi ya walimu, kaka yangu na shemeji yangu mpendwa Mheshimiwa Manju Msambya, amezungumzia suala la nyumba, hilo silirudii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna malalamiko ambayo walimu wetu hapa Tanzania wanalamika kwa siku nyingi, mionganii mwa malalamiko hayo yalikuwa ni madeni wanayodai na ni malimbikizo makubwa. Sisi Watanzania tunahitaji elimu bora lakini ni dhahiri ya kwamba elimu bora ina vitu vyake, ina vikorombwezo vyake ili uipate hiyo elimu bora. Elimu bora si madarasa tu wala elimu bora si mazingira mazuri tu, wala elimu bora si maneno mengi tu lakini elimu bora pia ni kumuandaa mwalimu bora kufundisha wanafunzi wakafaulu vizuri. (*Makofi*)

Sasa mwalimu anapofundishwa na akajituma kufundisha kwa mintarafu ya kupata wanafunzi walioboreka kielimu hapana shaka mwalimu huyu kwanza huwa hana muda mwingine wowote wa kufanya kazi ya kujiogezea kipato, kipato chake chote

kinategemea kazi yake ya ualimu, kwa maana hiyo walimu ni watu wa kuengwaengwa, ni watu wa kutunzwa, ni watu wa kuheshimiwa na ni watu wa kupewa lile ambalo wanastahili kupewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa walimu wana madai ya siku nyingi na Serikali hivi karibuni ilifanyia uhakiki wa madeni ambayo walimu wanadai na wamejaribu baadhi yake kulipa madeni hayo. Lakini bado kuna madeni makubwa ambayo walimu wanadai mathalani katika mikoa yote ambayo ina shule za msingi madeni ya walimu ni takriban shilingi bilioni 12.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye elimu ya sekondari labda na ukaguzi ni karibu shilingi bilioni 4.2 sasa huo ni mzigo mkubwa sana kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii. Serikali kwa busara zake kama katika mashirika ya umma linapokuwa shirika limezidiwa na madeni Serikali hubeba mzigo na mzigo huo hulipwa na Hazina ili kuweka mizania sawa. Naishauri Serikali ichukue juhudii kubwa na kwa azma ile ile ya kuhuisha Wizara ya Elimu basi mzigo huo wa madeni ya walimu ambao wanadai kwa muda mrefu yabebwe na Hazina na siyo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tulikuwa tunasikia kuna kashfa hii ya watumishi hewa, kwa kweli Serikali imefanya utafiti na ni kweli imegundulika kwamba kuna watumishi hewa si walimu tu lakini ni pia ni katika baadhi ya Wizara nyingine. Lakini katika hatua ambazo zimechukuliwa kutatua tatizo hili limewakumba baadhi ya walimu ambao wako kazini wanaendelea na kazi lakini kadhalika imewakumba baadhi ya walimu ambao wako likizo. Sasa ni dhahiri ya kwamba hawa walikuwa ni kenge katika msafara wa mamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wajibu sasa hivi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii ikishirikiana na Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma kuhakikisha kwamba wanafanya uhakiki wa nguvu wa uhakika kuona ya kwamba wale walimu ambao wamekumbwa na msafara huu wa mamba kuingizwa katika kadhaa hii ya kuondolewa katika *payroll*, hali ya kuwa wako likizo au wako masomoni au bado wako shulenii wanafundisha basi Wizara iwarejeshe na iwarejeshee pesa zao ili wawze kujikimu kwa sababu kuwatoa katika *payroll* walimu kama hawa kwanza ni kuwavunja moyo lakini kadhalika ni kuwatia katika maisha magumu ambayo kwa kweli ni kuwafanya hiyo kazi yenye wekuichukia na kuwafanya hata wengine amba wako nyuma yao kuja kuichukia ikawa bado hatuna walimu wazuri nchi hii kila mtu akawa anaikimbia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika hivi karibuni tumekuwa tunashuhudia tabia moja ambayo si nzuri, tabia moja mbaya sana ya kushambulia walimu shulenii. Tabia hii imeanza kujengeka mionganii mwa jamii. Sisi wakati tukiwa wadogo miaka hiyo walikuwa walimu tunawaheshimu kama lulu ndani ya chaza. Wazee wetu walikuwa ukikosea ndani ya nyumba anakwambia nitakushitaki kwa mwalimu wako. Walimu walikuwa na heshima kubwa wanaenziwa ipasavyo na walikuwa mbele ya jamii basi ilikuwa ni kioo kizuri cha mtu kujitazamia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kumezuka tabia kupiga walimu eti kwa sababu ya kumtia adabu tu mwanafunzi ambaye ametovuka adabu ndani ya darasa au vinginevyo. Sasa nadhani tumefika mahali ambapo Serikali ni lazima ichukue hatua madhubuti, vinginevyo kuwafanya walimu ni *punching bags*, hii itakuwa hatufanyi haki kwa walimu, walimu wanajituma, wanapoteza muda wao mwingi na shukrani yao siyo kuwapiga lakini shukrani ni kuwaenzi na kuwatimizia haja zao waweze kuipenda kazi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza masikitiko yangu kwa walimu, sasa nageuza upande wa pili wa shilingi. Hivi karibuni tumekuwa tunasikia wanafunzi wanapata mimba na hali hii inatisha na hata Waziri Mkuu wakati anazungumza katika hotuba yake aliitaja sana hii kudhia ya kutia mimba na kwa bahati mbaya mionganoni mwa wanaotia mimba wanafunzi ni walimu wao. Sasa sijui wanapata raha gani kwa watoto wadogo kama wale, ni aibu kwa kweli ni aibu. (*Makofi/Kicheko*)

Mimi naona niwashauri walimu, kama Mwalimu mate yake hayawezi, ahaa! Unajua vitabu vya dini vinazungumza mambo mengi na vinatusaidia sana Mwenyezi anasema hivi; “*Fankihuu maa twaba lakum, mathna, wathulatha wa rubaa*” kwa tafsiri ni kuwa mkitaka kuoa basi oeni wake wazuri kuanzia wawili au watatu mpaka wanne, sasa iweje yakhe ukachukue tumba la ua uliharibu yakhe, kwa raha ipi unayoipata wewe? Huu si ni uhasidi tu bwana! (*Makofi/Kicheko*)

Sasa mimi nadhani Serikali hapa kwa hili isilifumbie macho na mimi ndiyo maana wakati mwingine huwa najaribu kukubaliana na Mheshimiwa Ali Bin Salim, Mbunge wa Ziwanı kwamba kwa kweli watu wanaotia mimba wanafunzi wahasiwe, maana yake tukiendelea hivi hawa wengine wanataka *fifty fifty* na wengine wanataka *seventy five* na kadhalika, mtaifikasi wapi katika hali kama hii? Hamuwezi! Kwa sababu leo watatoka watoto wasiopungua sijui wangapi wametiwa mimba katika mwaka mmoja, kwa kweli hili ni tatizo na kama hatukilivalia njuga hili tatizo tutakuja kuishia huko shulenı kuna wanaume watupu na athari yake mnaijua wakibaki wanaume watupu katika shule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia nataka nizungumzie suala dogo la Bodi ya Mikopo. Mimi nasema nichukue nafasi hii kwanza kuwashukuru sana Bodi hii kwa kazi kubwa wanayoifanya na kwa kweli madhumuni hasa ya Bodi hii ni kukuza hii elimu ya juu kwa Watanzania. Lakini kumekuwa na manung’unico mengi kidogo na hapa ni lazima Serikali ichukue juhudhi ya kuyaangalia kwa undani zaidi manung’unico haya ili kuboresha hili suala la kutoa mikopo kwa wanafunzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na manung’uko kwamba mwanafunzi anaweza ku-*apply* mkopo kwanza wanao-*apply* mkopo wanaweza kuomba mia, lakini majibu yake wakaja wachache mno wanaopata mkopo ule haidhuru pesa inayotolewa ni ndogo sana. Lakini utaratibu wa kutoa mikopo hivi sasa utakuta unaelekeea zaidi kuwasaidia wale ambao wana uwezo zaidi kwa maana gani? Kama unasema unampa mkopo mtu mwenye *division one* au *two* ni mtu ambaye ameandaliwa vizuri kutoka *primary* kwenda *secondary* na kwenda *high school* na hawa si wengine isipokuwa ni watoto wenye kipato cha juu. Sasa wale maskini kama wengine ambao katika matokeo ya

shuleni hawafikii hizo *division one* au *two* nidhahiri kwamba mkopo huu wanaukosa na ndiyo maana nikasema utoaji wa mikopo hii unahitaji kuangaliwa vizuri zaidi ili kuona kwamba watoto wa kimaskini nao wanafaidika na mkopo huu. (*Makofi*)

Lakini sasa nasema hivi, kwamba unaweza ukapata mkopo huu muhula wa mwanzo wa masomo lakini katika muhula wa pili pesa isiingie. Sasa hili ni tatizo kwa wanafunzi, unamkatisha mkopo, unampa hali ngumu katika kusoma.

Lakini lingine ni kwamba kutokana na ile wanayoita *mean test* wanawafanya wanafunzi kupata hii mikopo situmii neno ubaguzi lakini nitumie neno la kwamba hakuna usawa mzuri katika kugawa hii mikopo kwa maana ya kwamba utakuta mwingine kwa sababu ya hii *test* yao anakwenda mwanafunzi *field* wanapewa shilingi 6,000/= wengine 1,000/= kwa siku. Sasa hali kama hii nadhani inahitaji kuangaliwa vizuri zaidi kuona kwamba wanafunzi wanapokwenda mafunzo ya vitendo basi wanafanya kazi zao vizuri ili kujielimisha vizuri na kuweza kufaulu masomo yao vizuri. (*Makofi*)

Sasa wanafunzi ambao wanasoma *Law* hawa ndiyo *akhasi* kidogo hawa mara nyingi kozi zao ni miaka minne na kwa mujibu wa utaratibu uliopo ni kwamba wanasoma miaka mitatu lakini baadaye mwaka wa mwisho wanatakiwa waende katika *Law Schools*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. ZUBEIR ALI MAULID - MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha na sasa ninamwita Mheshimiwa Bernadetha K. Mushashu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mushashu samahani kabla hujaanza labda nitoe maelekezo kidogo, uliombwa mwongozo hapa kuhusiana na yule ambaye anatoa tafsiri kwa njia za ishara kilichofanyika ni kwamba alikuwa anaegemea hii *hand rail*, kwa hiyo, kwa kuhofiya kwamba asije akaangukia huku ndani askari ndiyo walikwenda kumtahadharisha lakini sasa ye ye alifahamu kwamba asifanye ile shughuli. Kwa hiyo, nafikiri kapewa maelekezo na yupo hivi sasa hivi anaendelea. (*Makofi*)

MHE. BERNADETA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia kwenye hoja hii. (*Makofi*)

Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri wote wawili, Katibu Mkuu, Afisa Elimu Kiongozi, Wakurugenzi pamoja na watendaji wote ambao wameandaa hotuba hii kwani hotuba yenyewe ni nzuri na imeandaliwa kitaalamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili naipongeza Serikali kwa mafanikio makubwa sana ambayo yamepatikana katika muda mfupi. Wote tumeshuhudia ongezeko la madarasa,

ongezeko la wanafunzi *katika O-Level na A-Level* na pia katika vyuo vikuu na hasa hasa katika shule za sekondari. Mpaka sasa hivi tunajivunia tumefika zaidi ya shule ya 3,798.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hizi zinaitwa majina mbalimbali wengine wanaziita *yeboyebo* na kadhalika majina ya kejeli lakini kwangu mimi naona kwamba hizi shule ni mkombozi kwa wanafunzi walio wengi ambao wangeishia darasa la saba wakaishia kwenye vijiwe na wakawenza kuwa vibaka.

Lakini rai yangu kwa Wizara ya Elimu basi sasa muendelee kuboresha hizi shule kusudi ziwe shule kweli na ziweze kufikia hali ya kutoa elimu bora kama ilivyokusudiwa. Pamoja na mafanikio haya sekta ya elimu ina matatizo mengi sana na matatizo haya tusipoyashughulikia sasa athari zake haziwezi kuonekana sasa zitakuja kuonekana hapo baadaye tutakapojikuta kwamba tumekosa hata wataalamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nilikuwa na mambo mengi ya kuchangia lakini kwa kutambua kwamba muda hautoshi nitachangia kiasi na mengine nitachangia kwa maandishi.

Naanza kwanza kwa *ku-declare interest* kwamba mimi ni mdau wa sekta ya elimu kwa zaidi ya miaka 31 sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na tatizo la kwanza, mitihani ya darasa la nne na mitihani ya kidato cha pili. Wote tunafahamu kwamba mitihani inapima uwezo wa mwanafunzi je, huyu mwanafunzi ameiva? Je, huyu mwanafunzi yuko tayari kuweza kupanda kwenye darasa lingine? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitihani hii iliwekwa kwa sababu tulifikia mahali mtoto anamaliza darasa la saba hajui kusoma wala kuandika. Mitihani hii iliwekwa kwa sababu *division zero* katika kidato cha nne zilikuwa nyingi sana na baada ya kuweka hiyo mitihani wanafunzi waliokuwa hawapendi kusoma wale wavivu walianza kusoma kwa sababu waliogopa kukariri madarasa. Walimu waliongeza bidii katika kufundisha kwa sababu hawakutaka watoto wao washindwe. Leo hii mnataka kuondoa huo mtihani eti usiwe wa kukaririsha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuhakikishia wanafunzi hawatasoma. Kwa nini asome? Atakayepata mia sawa anapanda darasa, atakayepata wastani wa maks 13 sawa, atakayepata sifuri yenye masikio, sawa anapanda darasa, kwa nini asome? (*Makofi/Kicheko*)

Sasa mimi kwa kweli nashangaa kidogo Wizara ya Elimu mnataka kutupeleka wapi, mimi nafikiri mnachotaka kufanya sasa hivi ni kuwafurahisha wafadhili kwamba watoto walioingia darasa la kwanza ndiyo hao hao waliomaliza darasa la saba, na wale watoto walioanza kidato cha kwanza ndiyo hao hao waliomaliza kidato cha sita, hii haitufikishi mahali popote hili Taifa tunataka kulipeleka wapi? Kwa hiyo, mimi napendekeza kama mitihani ya darasa la nne na mitihani ya kidato cha pili iendelee

kuwafanya wale ambao hawatashinda waendelee kukariri mpaka hapo watakapokuwa wameiva na kushinda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia kuhusu kuondoa shule za bweni za *O-Level*, wakati Waziri anajibu swali langu nilouliza hapa Bungeni alisema shule za kidato cha kwanza mpaka cha nne za bweni zitabadilishwa ziwe kidato cha tano na cha sita za bweni. Lakini tutambue kwamba watoto wanakua, wanapofikia kwenye miaka kumi na tatu mpaka kumi na nane, hapo ndipo watoto wanafikia *adolescence stage* watoto hao wanabalehe, wanakuwa na matatizo mengi vichwani, wanakuwa watukutu, si wasikivu, wanakuwa na misongo ya mawazo, wanakuwa na mihemko mbalimbali, hupenda kujihusisha na makundi mbalimbali hata kuingia kwenye mambo ya mapenzi na ulevi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ndicho kipindi ambacho wanafunzi wanahitaji malezi ya karibu zaidi na hiki ndicho kipindi ambacho watoto wanakuwa kidato cha kwanza hadi cha nne. Kuwaweka bweni kunawalinda hawa watoto waepukane na hivyo vishawishi, wanapata ushauri nasaha kutoka kwa walimu kwa sababu wanakaa nao, inawakinga watoto wa kike wasipate mimba, vilevile inawalinda hawa watoto wa kike ambao wanashawishiwa na baba watu wazima kwa kutumia fedha na zawadi mbalimbali wakafanya nao ngono, wakaambukizwa UKIMWI na wakawapa mimba. Leo hii mnataka kuziondoa hizo shule, mtakuwa mmemnyima huyu mtoto wa kike matunzo na malezi bora katika hiki kipindi ambacho ni nyeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nitoe angalizo, mwaka 2001 wanafunzi wasichana 2666 walifukuzwa shule kwa sababu ya mimba. Mwaka 2002, wanafunzi 2380 nao walifukuzwa. Hivyo hivyo mpaka mwaka 2005 wamefukuzwa wanafunzi 2590 kwa sababu ya mamba, yaani kuanzia mwaka 2001 mpaka 2005, wamefukuzwa wanafunzi wasichana 12,413.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uhakika kufikia mwaka huu watakuwa wamesha-*double*, namba imeshakuwa zaidi ya hapo. Sasa zitakapoondolewa hizi shule za bweni za kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha nne nina uhakika mimba hizi zitaongezeka. Kwa hiyo, ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba, naomba iendelee kujenga *high schools*, hizi zilizopo za bweni iziache hivi hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nilikuwa napendekeza, nimemshukuru sana Mheshimiwa Waziri amesema kwamba wataleta mchakato wa kuliangalia hili suala la mimba za utotoni, wanazopata watoto wakiwa shulen, je, tuendelee kuwafukuza, tumeshafukuza sasa hivi nafikiri itakua imeshafika elfu ishirini na nne. Ukimfukuza mwanafunzi ina maana kwamba na yule mtoto aliyezaliwa hawezi kupata matunzo bora. Nafikiri sasa wakati umefika Serikali ifikirie ni namna gani wanaweza kulijadili, walilet tulijadili tuone tutafanya nini kwa sababu nafikiri hii adhabu ya kumfukuza msichana shule bado haijaleta matunda tarajiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie kuhusu madeni shulen. Jamani, Wizara ya Elimu inaongoza kwa madeni sugu yasiyolipwa kwa wakati. Najua Waziri wa

Elimu ni mgeni, Naibu Waziri nao pia, madeni mengi wameyakuta na sina uhakika hata wakati wanakabidhiwa mliambiwa kwamba mnarithi madeni kiasi gani. Nazungumza kwa uhakika kwa sababu nimetokea huko huko. Kwa hiyo, nayaelewa lakini ngoja niwaambie madeni waliyokuwa nayo. Wana madeni mengi kama vile madeni ya walimu, matengenezo, vifaa vya kufundishia, watoto yatima na wale watoto wanaoishi katika mazingira magumu ambayo waliahidi kuwalipia lakini bado hawajawalipia, madeni ya ruzuku kwa shule za kutwa kwa kufidia karo zilizopunguzwa, ya umeme, maji, simu na ya wazabuni wa chakula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba Wizara inieleze kwa nini sasa hivi mpango ni kwamba *bill* ya maji inapopelekwa shulenii mkuu wa shule aigonge muhuri aileté tena Wizarani mpaka Wizara ipate fedha ndiyo iandike cheki. Katika mlolongo huu unakuta shule zimeshakatiwa maji na umeme. Kengele? Mungu wangu!!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madeni ya chakula, Bajeti ya elimu imeongezwa, naomba kuelezwaa kwa nini wazabuni hawalipwi kwa wakati? Wanadai hadi fedha za miaka miwili na zaidi. Nasikia sasa hivi wanahakiki madeni, mwaka jana mwishoni walituma wahasibu wakaenda kwenye Kanda, mwezi wa nne na wa tano Wakuu wa Shule zote za Tanzania za Serikali wamekuja hapa Dodoma wameleta madeni na viambatanisho. Mwezi wa sita maboharia wote wamekwenda Dar es Salaam kupeleka madeni na *ledger*, wakati huo shule zimefungwa kwa sababu watoto wamekosa chakula. Jamani hii ni aibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara wana *Internal Auditors*, kwa nini wanasubiri madeni yana-*accumulate* kiasi yanakuwa hivyo? Waziri wa Elimu ametangaza kwamba sasa analipa lakini kabla ya hapo akumbuke kwamba mtoto anatengewa shilingi mia nane sitini na saba na senti arobaini na mbili, kiwango ambacho kiliwekwa mwaka 2005. Hivi nikimpa Mheshimiwa Waziri shilingi mia nane anaweza kunywa uji asubuhi, chakula cha mchana na cha jioni, inawezekana? Haiwezekani. Wafungwa nasikia wanapewa zaidi ya shilingi elfu mbili, kwa hiyo, tunamthamini mfungwa kuliko mwanafunzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2005 walipoweka kiwango hiki unga wa dona ulikuwa shilingi mia tatu hamsini lakini sasa hivi ni shilingi mia saba, maharage yalikuwa shilingi mia tano sasa hivi ni shilingi elfu moja na mia tano na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nipate ufanuzi kwa nini Serikali inapeleka fedha kidogo wakati idadi ya wanafunzi wanajua, walimu wakuu wa shule wanajaza *TSS 1 -10* kila mwezi wa tatu wa kila mwaka, kwa nini idadi ya wanafunzi isijulikane? Jamani hivi kwa nini wanafunzi wale vibaya kuliko wafungwa!! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu Mheshimiwa Waziri afanye *surprise check-up* aone chakula wanachokula wanafunzi. Juzi ametangaza kwamba, wamelipa amewafanya wazabuni wamekasirika, Wakuu wa Shule wamebebwa mabango wanafikiri fedha zipo, nimechukua lile tangazo, nimekuta wamelipa vyuo ishirini tu na shule za sekondari hamsini na tano tu. Katika Mkoa wa Kagera ni Chuo kimoja cha Ualimu ndicho kimelipwa, shule za sekondari zote hakuna. Mwanza ni vyuo viwili tu vimelipwa, Lindi

ni shule moja tu ya sekondari na kadhalika. Sasa napenda nielezwe ni lini madeni ya wazabuni yatakuwa yamelipwa yote? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nilikuwa nataka kuzungumzia madeni ya walimu. Madeni ya walimu yanazidi kuongezeka mwaka hadi mwaka, walimu wanafanya kazi katika mazingira magumu, hata ile haki yao ya msingi hawapewi, unakuta walimu wanalipwa pale wanapokuwa wametishia kugoma au kabla ya kila mwaka wa uchaguzi basi ndio unakuta Serikali inaunda Tume. Hiyo Tume ianze kuchunguza madeni ya walimu. Nauliza kulikoni mbona Wizara nyingine watumishi wake wanalipwa *on time*, kuna tatizo gani katika Wizara ya Elimu? Naomba nielezwe ni lini madeni yote ya walimu yaliyopo yatakuwa yamelipwa na kuna mikakati gani ya kuhakikisha kwamba madeni haya hayaendelei kuongezeka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wana matatizo makubwa sana, unakuta katika shule moja kuna watoto zaidi ya elfu moja lakini walimu wa hisabati wawili, mwalimu mmoja ana vipindi zaidi ya themanini. Lakini pamoja na matatizo hayo hata haki yake ya msingi ananyimwa. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza kwamba hayo madeni yalipwe na vile vile nilikuwa nauliza, Wizara ina mpango wa kuwakopesha walimu vyombo vyaa usafiri kama magari na pikipiki angalau kuwapunguzia adha ya usafiri? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie masomo ya sayansi.

(*Hapa kengele ya pili ililia*)

WABUNGE FULANI: Kengele ya pili hiyo.

MHE. BERNADETA K. MUSHASHU: Aaaah, Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja *on condition* kwamba hayo maswali yangu niliyouliza kwa kuchangia kwa maneno na nitakayouliza kwa maandishi yajibiwe. (*Makofi*)

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa uzima kwa siku hii ya leo unaonifanya niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Kwanza kabisa, napenda kusema kwamba ualimu ni kazi ngumu sana na asilimia sabini na tano kama si themanini ndani ya Bunge hili Tukufu walikuwa walimu. Kwa hiyo, tunaelewa wazi kabisa kwamba kazi ya ualimu ni kazi ngumu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya ualimu ni kazi ya lawama, wanafunzi wanapofanya vibaya hulaumiwa mwalimu kwamba hakuwafundisha hata kama alifanya kazi kwa jitihada zake. Lakini mwalimu huyu anapewa darasa lenye wanafunzi zaidi ya mia na hamsini, mwalimu huyu ukimkuta anafundisha ni kama anahutubia mkutano wa hadhara. Sasa ndani ya mkutano wa hadhara kuna anayeelewa na asiyelewa nini umekiongea, ndivyo ilivyo katika shule zetu sasa hivi, kuanzia shule za msingi. Wengine

wanakuwa wamekaa juu ya madawati na wengine wamekaa chini kwenye mawe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunajiuliza au najiuliza, mwalimu huyu ambaye anafanya kazi ngumu na muda wake wote anautumia kufanya kazi ya kufundisha akirudi nyumbani aandae masomo kwa ajili ya kwenda kufundisha kesho, akifika shuleni watoto ni zaidi ya mia na hamsini, hivi kweli huyu mwalimu anaweza kusahihisha madaftari ya wanafunzi wote na akayasahihisha kwa usahihi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kitu gani kifanyike ili madarasa yaweze kuongezeka, walimu waweze kuboreka na wanafunzi waweze kufundishwa na kuelewa ni kitu gani wanafundishwa. Lakini bila kuwajali walimu hakuna elimu itakayoboreka kwa sababu mwalimu atafanya kazi yake kwa kulipua kwa sababu kwanza akiangalia mshahara wake ni mdogo, akirudi akiangalia malimbikizo yake yote hajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, sasa hivi nimepata takwimu kama ni sahihi za malimbikizo ambayo kwa Mkoa wa Mwanza tunadai shilingi bilioni moja, milioni mia moja kumi na tatu na ushehe huko. Hayo ni malimbikizo mapya si ya zamani. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri wakati anajumuisha anieleze kama haya malimbikizo ni kweli na kama ni kweli je, yatalipwa kwenye Bajeti hii ambayo tunaijadili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi hapo hapo kwa walimu, nafikiri elimu bila ukaguzi wa shule kweli inakuwa duni. Kipindi tunasoma tulikuwa tunaona wakaguzi wakija mara mara shulen, lakini sasa hivi shule inaweza kumaliza muda mrefu wakaguzi hawajafika kukagua shule ile wala kutembelea shule ile. Tunasubiri wakaguzi kutoka katika Kanda, ni lini wataizungukia Kanda na shule sasa hivi zimeongezeka ili waweze kukagua shule hizi na kuzimalizia ukaguzi. Wakaguzi wenyewe pia wamesahaulika kama walimu wao. Wakaguzi wana malimbikizo mengi ya madai yao, wakaguzi hawa hawa hawana vitendea kazi vya kutosha, hawana kipaumbele katika Bajeti, hivi kweli elimu bila ukaguzi tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundiboreshe kitengo cha wakaguzi waweze kuzikagua shule, waweze kupitia walimu na kuona ugumu wa walimu jinsi gani wanavyofundisha katika shule hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuzungumzia suala la kero za walimu wakati wanakwenda likizo. Naweza kutoa mfano mmoja, mwalimu kutoka Mwanza kwenda Nzega anapewa fedha ya likizo shilingi elfu kumi na mbili ambayo haiwezi kukidhi mahitaji yake ya nauli. Pamoja na kupewa fedha kwa mwalimu huyo aliyeleta taarifa hizo, aliambiwa ili kupewa fedha hizo mpaka apeleke vyeti vya watoto kwanza, ndiyo apewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaiomba Serikali iwajali walimu ili kuweza kuboresha elimu maana yake pasipo na walimu bora hakuna elimu bora. Vinginevyo, tutakaa hapa tutasema madarasa mengi, sekondari za Kata lakini ni ushahidi dhahiri kwamba sekondari za Kata hazina walimu. Sekondari moja inakuwa na walimu

wawili au watatu, kwa hali hii tunasema kwamba tumeongeza vyumba vya madarasa na hatukuweza kuboresha elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naiomba Wizara ikae chini, ifikirie ni jinsi gani itaweza kuboresha na kuboresha walimu ni kuwaongezea maslahi yao na kuwalipa malimbikizo yao kwa wakati muafaka, nafikiri wanaweza kuwa na ari ya kufanya kazi na wakaweba kutufundishia watoto wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetembelea Kata moja ya Kigela, shule ya Kigela, Wilayani Musoma, nikaambiwa hii shule ni mpya. Shule hii mpya ndani haina sakafu yaani sakafu imewekwa lakini wanafunzi wamesoma kwa miezi miwili tu imebomoka, yule mwalimu amekaa kwenye dawati nusu dawati, watoto wote wamekaa chini kwenye mawe, malalamiko ya wazazi ni kwamba wanachanga pesa za maendeleo ya kujenga shule lakini shule hizo hazijengwi na wala hazijulikani fedha hizo zinakwenda wapi. Nafikiri katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nilichangia hoja hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upande wa mapato na matumizi, mapato na matumizi yamekuwa magumu sana, wananchi wanaochanga fedha zao wanapoomba wasomewe unakuwa ni mzunguko. Shule hiyo ikibomoka lakini bado wananchi wanatakiwa wachangie mara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi, naiomba Serikali, watoe maelekezo ni jinsi gani katika Halmashauri moja watu wawe na uwiano wa kuchangia ili kuondoa utata kwa wananchi kwa sababu katika Halmashauri moja unakuta Kata moja, shule nyingine inachangisha shilingi elfu kumi kwa jengo na unaambiwa ulipie taratibu kwa muda hata wa miezi mitatu au sita. Kata hiyo hiyo unakwenda shule nyingine unaambiwa uchangie shilingi elfu ishirini na uzilipe zote kwa pamoja. Tunaomba tofauti hii iondoke, wananchi wajue wanachangia shilingi ngapi ili waweze kuondoa mtafaruku uliopo sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuchangia kuhusu Kata ya Igogo, nilitembelea Kata hiyo, nikakutana na masuala mengi suala moja likiwa ni walimu kung'ang'aniza wanafunzi kununua uniforms shulen. Silaumu sana hili huenda katika kukosa kwao mishahara au kucheleweshewa mishahara yao wanatafuta njia ya kujikimu. Lakini kama wanaweza kuwahishiwa madai yao na malimbikizo yao nafikiri matatizo haya madogo madogo kwamba walimu wanataka *uniforms* zinunuliwe shulen wakati shule ni ya kutwa, walimu wanaagiza ndoo wakati shule ni ya kutwa, yanaweza kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa nichangie kuhusu eneo moja ambalo lina shule za Kasoka na Mandunga. Shule hizi nimezitembelea ni katika Kata ya Igoma, nimekuta tangu zimeanza kujengwa mpaka leo pamoja na fedha za *MMEM* na *MMES* kwenda na michango ya wananchi lakini shule hizi haziendi ziko pale pale, watoto wanakaa chini, watoto wa sekondari wanakaa chini na majengo hayajaisha. Kwa hiyo, tunasema shule zimekwisha, lakini hakuna utaratibu wa zile shule kuwa zimekwisha, ni kwamba tunawahisha ili tuonekane tuna shule nyingi, lakini elimu inayopatikana katika

shule ile inakuwa si nzuri, shule hiyo haiwezi kutoa elimu na mtoto akawa ameelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kwenye Bima ya Afya ya walimu. Walimu wanakatwa Bima ya Afya, wanapokatwa Bima ya Afya na si walimu peke yao hata wafanyakazi wengine, anapokwenda hospitali pamoja na kukatwa Bima ya Afya atapewa kadi, akishapewa kadi anakwenda kwa Daktari, akishamwona Daktari dawa anatakiwa aende kununua.

Sasa naomba kuiuliza Wizara hasa kwa upande wa walimu wanaokatwa Bima ya Afya ni kwamba mwalimu anakatwa Bima ya Afya kwa kupata kadi tu au anakatwa ili apate huduma ikiwa ni pamoja na dawa? Kama anakwenda kununua dawa mtaani wakati amekatwa Bima ya Afya anarejeshewaje hizo fedha zake? Hili suala liwekwe wazi kwa sababu walimu wengi wanauliza kuhusu hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuongelea michango ambayo wazazi wengi wanailalamikia. Wanachangia majengo lakini bado pia wanatakiwa kuchangia na wafanyakazi kama vile mlinzi wa shule. Kwa hiyo, wazazi walio wengi wanauliza swalii kwamba Serikali iwaeleze wanachangia maendeleo ya majengo ya shule au wanachangia na mishahara ya wafanyakazi wa shule amba ni walinzi na wale wanaosafisha bustani. Hili pia naomba wakati Mheshimiwa Waziri anajumuisha aweze kunieleza ni kipi wachangie wananchi katika maendeleo ya shule zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufikia hapo napenda kushukuru na pia kuwashukuru Wabunge wote kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

MHE. ZUBEIR ALI MAULID – MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga.

Waheshimiwa Wabunge, nilitangaza kwamba baada ya Mheshimiwa Kimwanga atakuwa ni Mheshimiwa Profesa Feetham Banyikwa na nikasema atafuatiwa na Mheshimiwa Estherina Kilasi. Lakini kwa vile Mheshimiwa Estherina Kilasi ametoa jina lake na walikuwa wameshakubaliana na Mheshimiwa Felister Bura kwa hiyo, nafasi hiyo itachukuliwa na Mheshimiwa Felister Bura na baada ya hapo atafuatia Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia. (*Makofi*)

MHE. PROFESA FEETHAM F. BANYIKWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniruhusu nami niweze kuchangia hoja ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii. Kwanza kabisa nitoe pongezi kwa Waziri kwa kutoa hoja nzuri, yenye matumaini. Vile vile nitoe pongezi kwa Naibu Mawaziri na watumishi wote Wakuu wa Wizara hii kwa kumsaidia Waziri kutengeneza hoja ambayo ndiyo tunaijadili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema naunga mkono hoja. Naunga mkono hoja kwa sababu hoja ni nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naanza kuchangia kuhusu elimu ya awali. Kwa sasa hivi elimu ya awali inafundishwa katika shule za msingi. Kwa hiyo, vijana ambao ni wa umri wa miaka mitano mpaka sita wanachanganyika na vijana wenyе umri wa miaka saba mpaka kumi na tano. Kwa mawazo yangu naona hii si sawa. Walimu na wanafunzi wa shule za awali inabidi watenganishwe na walimu na wanafunzi wa shule za msingi kwa sababu mahitaji ya watoto wadogo ni tofauti kidogo na watu wakubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hayo, napendekeza kwamba mikakati itengenezwe au mipango iwezekane ili watoto hawa wa *groups* hizi mbili watenganishwe. Kama inawezekana *nursery schools* zijengwe karibu na shule za msingi lakini madarasa yawe tofauti kwa sababu inavyoonekana sasa hivi watoto wadogo hawapati nafasi ya kusoma katika hizo shule za msingi. Hiyo ni muhimu sana ama sivyo msingi wa vijana wanaoanza shule wenyе umri wa miaka mitano mpaka sita watakuwa *disadvantaged* kwa sababu kuna upendeleo wa wale watoto walioko kwenye shule ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niongelee shule za msingi. Kwa sasa hivi shule za msingi ni madarasa saba, wote tunajua, *primary education programme is a seven years programme*. Kwa sasa hivi inaonekana *it is a four years programme and then a three years programme for a total of seven*. Huo ulikuwa ni mpangilio wa kikoloni, *it is colonial*, tumeurithi na hauna *application* kwa wakati huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ukoloni *programme* ilikuwa shule ya msingi ni miaka minne, baada ya miaka minne unafanya mtihani, huo mtihani inabidi ushinde ili uende *middle school* kwa wakati huo na huo mtihani ulikuwa *a disaster* ndugu zangu, tuelewane, watu wanaupenda sijui wanaupenda nini, huu mtihani ulikuwa ni kuwazua vijana wasiende darasa la tano. Wakati huo darasa la tano ilikuwa ni nafasi finyu, kwa hiyo, ilikuwa kumaliza darasa la nne kwenda darasa la tano ni lazima ushinde mtihani wa darasa la nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi madarasa yamejaa, mtihani wa nini? Inaongeza kudondoka, kudondoka kwa sasa hivi ni asilimia arobaini. Watoto wanaoingia darasa la kwanza mpaka kufikia darasa la saba, wamedondoka kwa *forty percent*, hatuwezi kustahimili mdondoko wa namna hiyo. Katika suala zima la *education for all we are being disadvantaged* kwa mfumo wa ukoloni ambao inabidi tuondokane nao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba mtihani huo uondoke, wanafunzi wafanye mtihani wa mwisho wa mwaka darasa la kwanza, la pili, la tatu na kuendelea tutajua wale ambao hawana uwezo na wale ambao hawana uwezo. Suala la kwamba mtihani utatueleza maendeleo ya mtoto sikubaliani nalo kwa sababu maendeleo

unayapima kwa *continuous assessment* siyo unamvizia mtoto baada ya miaka minne unampa mtihani akifeli basi hajui, kwani ulikuwa hujui kwamba hajui tangu darasa la kwanza, la pili na la tatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachopendekeza kwa Waziri wa Elimu ni *ku-rethink of the whole programme ya primary education, it is a seven years programme, it should be made to be a seven years programme*, hii ya kuivunja darasa la nne kwa kuweka mtihani, wengine wanadondoka, unaingia na wachache darasa la tano, darasa la sita, darasa la saba unawapa mtihani tena, naona mfumo huo ni wa kikoloni na tuachane nao, tuwe na *seven years programme* ambayo inabidi tukazane nayo kwa kuboresha mazingira ya kufundishia, mishahara ya walimu lakini siyo kutunga mitihani eti ujue kwa nini watoto wanafeli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani na mfumo huo. Hiyo *education system tunaiita elitist education system, education for the few which will not help us*. Tumekuwa nayo mbona hatujaendelea, tunawasomesha wachache, tunawapa kila kitu lakini haijatusaidia, naona tuondokane na mfumo huo twende mbele badala ya kupiga *mark time*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende katika elimu ya sekondari, *form one to form four*. Naelewa kabisa kwa nini kuna mtihani wa *form four*, hilo halina mjadala lakini mtihani kazi yake ni kupima au kuchuja wale wanaoweza au kuchuja wale wanaoweza kufaulu ili waweze kwenda *form five* na uelewa, je, mtihani wa *form two* una faida gani, *what is it for?* Ni mtihani ulikuwa unaitwa *standard ten territorial examination* ya kikoloni kuwazuia waafrika wasifike *form four*, leo watu wanatetea hapa kwamba wawe na mtihani wa *form two* kuwazuia vijana wasifike *form four*, tunataka *universal secondary education* baada ya kupata *universal primary education*, sasa tunajiwekea *hand break form two* ili watoto wasifike *form four, what type of a driver?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa hivi tuondoe mtihani wa *form two*, tufanye *continous assessment* ya *form one*, mwisho wa mwaka watunge mtihani, *form two* mwisho wa mwaka watunge mtihani, *form three* vile vile *and then* kuwe na *final examination* ya *form four*, hiyo nitialewa ama sivyo tunajizua kwenda mbele sisi wenyewe, programu ibadilishwe, mtihani wa *form two* uondoke, ubaki mtihani wa mwisho wa mwaka tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu ya juu. Elimu ya juu *form five* na *six*, bado nasema kwamba hii ni mipangilio ya kikoloni, wenzetu walioendelea *secondary education program is a six years programme*, tujielekeze huko katika kuhakikisha kwamba kila sekondari ambayo ina *form one* basi iwe na uwezo wa *progression* mpaka *form six, that should be the vision of our education development in this country*. Tusijiwekee vizingiti vyta mtihani wa *form four* mahali ambapo utakuwa hauhitajiki, kwa mfano, kama tukiwa na *high schools* kwa kila sekondari, mtihani wa *form four* utakuwa na faida gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utawapima *form one, form two, form four, form five*, basi tuwe na mtihani wa mwisho tu, kazi ya mtihani ni kuchuja ili uwe na *criteria* ya kujua anayefaa kuendelea na ambaye hafai. (*Makofî*)

Madarasa ya *form five* na *form six* kwa wenzetu walikuwa wanaita *junior colleges* ni *preparation* kwa wale watakaokwenda kujiunga na Chuo Kikuu. Kama tunaweza kuwapa elimu wote mpaka *form six*, hatuhitaji tena mtihani wa *form four*, tutawapima tujue nani ana uwezo wa kuingia *first year*, ambaye anaweza kufaidika na *University Education*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ninachopenda kukizungumzia ni *University Education* iwe *four year programme, mandatory* na *as much as possible* tujielekeze katika kutafuta uwezekano wa kupanua Vyuo Vikuu. Katika *table* ambayo imesomwa na Mheshimiwa Omar Kwaangw', ukichukua *participation for University, age cohort in Africa* wanaoingia katika Vyuo Vikuu *South Africa* wana asilimia tisa, Kenya wana asilimia 1. 47, Uganda wanatushinda wana asilimia 1.23, Tanzania tuna asilimia 0.27; tupo *one third of Kenya*. Tunaingia kwenye ushindani *East African Community*. *For every graduate in Tanzania? Kenya wana-graduate* wanne mpaka sita; sasa tukiwa tuna *compete* katika ajira sisi tutakuwa wapi? Watakuwa wanachukua kazi zote hapa na sisi tutakuwa wafagiaji; haikubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuongeze *funding* kwa *University* na tupanue Vyuo Vikuu ili watu wengi zaidi waweze kuingia katika Vyuo Vikuu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, lazima niruke nizungumzie Ngara. Ngara tumejenga Shule za Sekondari. Shule za msingi zipo lakini hazina walimu, tunaomba walimu. Shule za Sekondari za Kata zimejengwa; sawa tunaomba walimu na *laboratories*. Vilevile ziboreshwé kwani mazingira ni mabaya sana. Nimetembelea Shule za Sekondari nyinyi wote wanalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ninachowea kukizungumzia ni Elimu ya Ufundî. Ngara hatuna Chuo cha Ufundî, tunaomba Chuo cha Remela kibadilishwe kiwe Chuo cha Ufundî chini ya VETA. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Ngara hatuna sekondari za kidato cha tano na sita. Tunaomba angalau kila Tarafa ipate sekondari moja ya kidato cha tano na sita. Kwa sababu hakuna nchi iliyoendelea kwa *ku-concentrate on training primary school teachers* au *primary school level graduate*. Tukijienendeza katika *Universal Primary Education* hatutaenda mbele ni lazima tuwe na watu wanaoingia katika Vyuo Vikuu na watu

wanaojiunga na Vyuo Vikuu unaweza kuwapata tu pale utakapokuwa na *High Schools* za kutosha. *After all*, huko tunakoenda ni ulimwengu wa Sayansi na Teknolojia. Kwa hiyo, tujielekeze katika kutatua hayo matatizo.

Mwisho kabisa, nizungumzie Uratibu wa Elimu ya Sekondari Ngara. Kuna Mratibu wa Elimu ya Sekondari Wilayani pale, hakubaliki katika Halmashauri. Kwenye Mkutano wa Kamati ya Fedha na Mipango hashiriki. Sasa ujenzi wa Shule za Sekondari katika Wilaya ya Ngara unajengwa chini ya Mfuko wa *TASAF*. Fedha hizo zipo kwenye Halmashauri, yaani kwa *DED*. Huyo Mratibu haendi kwenye mikutano hiyo; anaratibu vipi Elimu ya Sekondari? Kuna tatizo hapo au ahamie kwa *DED* ili awe *integrated* na ye ye awe kama Diwani, atetee matatizo ya Elimu ya Sekondari na apewe vitendea kazi; hana gari, hana ofisi, hana msaidizi, hana *secretary* na hana chochote. Sasa mtu huyo mnampa uratibu anaratibu vipi? Naomba tumwezeshe ili aweze kufanya kazi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsanteni. (*Makofi*)

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni ya leo. Pia ninamshukuru sana dada yangu, Mheshimiwa Estherina Kilasi, kwa kukubali kunipa nafasi ambayo angeitumia ye ye kuchangia ili nami nichangie katika Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundsi, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe na Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Gaudentia Kabaka na Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya katika Wizara hii, yenye kazi nyingi na Wizara ambayo ina mambo mengi hasa katika maisha ya elimu kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundsi, kwa nia yake ya dhati kabisa, kuamua kujenga Jengo la Wizara yake katika Mkoa wa Dodoma. Hii inaonyesha jinsi anavyothamini Makao Makuu ya Nchi na ninaamini kabisa kwamba, Jengo lile atakalolijenga Dodoma litakuwa zuri kuliko la Dar es Salaam. Ninawaomba Mawaziri waliobaki au Wizara zilizobaki, wachukue mfano wa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundsi, kujenga ofisi zao za kazi katika Mkoa wetu wa Dodoma, kwa sababu ndiyo Makao Makuu ya Nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali, kwa juhudi kubwa inayofanya katika kujenga na kuimarisha Chuo chetu Kikuu cha Dodoma. Chuo hiki ni kikubwa kama alivyosema Mheshimiwa Rais kwamba ni kikubwa katika Afrika na ni kikubwa katika nchi yetu. Ninaamini kabisa kwamba, Serikali itachukua juhudi za dhati kabisa kuhakikisha kwamba, inaweka miundombinu muhimu katika Chuo hicho kwa haraka iwezekanavyo na vifaa vinavyohitajika kabla wanachuo hawajaanza masomo kwa mwaka unaokuja. Naamini mwaka huu wa fedha, watatahiniwa wanafunzi wengi na kuna mahitaji mengi katika Chuo hicho. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali itimize mahitaji muhimu ya miundombinu kuhakikisha kwamba, Chuo chetu kinakidhi mahitaji kwa wanafunzi ambao wataanza masomo mwezi Septemba, 2008. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge walio-*support* kwamba, mtihani wa darasa la nne na mtihani wa kidato cha pili uendelee na wanafunzi ambao hawatafaulu warudie. Nam-*support* sana mdau mkubwa, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, kwa aliyoazungumza. Anajua kwamba, shule zetu zina upungufu wa walimu, watoto wengine wanakaa chini na vitendea kazi havitoshi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama mtoto huyo hakufaulu mtihani wa darasa la nne unataka aendelee, hatutaki watoto ambao mwisho wa siku wamalize darasa la saba wakiwa hawajui kusoma, kuandika wala hawajui jambo lolote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani lengo la Serikali liwe mtoto anapomaliza darasa la saba, awe na uwezo japo wa kujitegemea. Tunapowaswaga tu kwamba hakuna mtihani, sisi wenyewe tuna watoto tunaona mitihani inapokaribia wanasoma kwa bidii na walimu wanajibidiisha kuwafundisha watoto kwa ajili ya mitihani. Sasa tukisema mitihani isiwepo, ina maana walale tu waswagwe mpaka wamalize darasa la saba. Taifa hili tunalipeleka wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii, mtihani huo uwepo na wale wanafunzi wanaoshindwa kwa sababu walimu hawatoshi, basi watafutiwe namna nyingine ya kukidhi mahitaji ya kuingia darasa la tano. Tusijidanganye Waheshimiwa Wabunge, robo tatu yetu tuliosoma enzi hizo, tulifanya mtihani wa darasa la saba. Tusiseme kwamba hatukunufaika, tulinufaika na ndiyo maana tupo hapa. Kusema kwamba mtihani wa darasa la nne na mtihani wa kidato cha pili haufai siyo kweli. Watoto wanaokwenda *form one* ni wale ambao hawajui hata kiingereza; kiingereza wanakikutana sekondari. Anapokwenda *form two* apimwe kujua kama ana-*perform* au ha-*perform*; kama hawezi ku-*perform* arudie ili aende vizuri. Wanaomaliza *form four* wawe na mwelekeo na waweze kujitegemea. Wakipata kazi katika ofisi za kawaida tu ya kufagia au yoyote ile waweze kujimudu, lakini tusiwaswage tu kama ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sikubaliani na kuondoa mtihani wa darasa la saba na mtihani wa kidato cha nne. Tunaelewa upungufu wa walimu. Katika Shule za Sekondari hatuna walimu. Sasa hivi tuna Shule za Sekondari za Kata, lakini walimu tulionao ni wale wa leseni waliosoma kwa mwezi mmoja; atamfundisha nini mtoto aliyemaliza darasa la saba jana? Yeye mwenyewe kamaliza kidato cha sita jana tu na leo anatakiwa kumfundisha mtoto wa kidato cha kwanza aelewé; ataelewa nini wakati hata ujuzi hana?

Katika Shule zetu za Sekondari za Kata utakuta walimu watatu ni wa leseni, hao ambao wamekwenda kozi ya muda mfupi na mwalimu mmoja tu (Mwalimu Mkuu), ndiyo mwalimu mwenye ujuzi. Kesho unamwambia mwanafunzi afanye mtihani wa kidato cha pili akifeli aendelee; siyo kweli na wala siyo haki. Hatutakuwa tumewatendea haki watoto wetu na Taifa la kesho. Wanafunzi watakaoshindwa warudie; mwenye nia ya kusoma atasoma na mwenye nia ya kuijendeleza atajijendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tusione kwamba, mtihani huo ni kero kwa wanafunzi. Nadhani walimu pia tutasaidiana nao na wao watatusaidia kujua hili. Mimi nimehojiana na walimu wengi, wanasesma kwamba mtihani huo ukiondolewa, basi wanakuwa na nafasi nzuri ya kupumzika mpaka mtihani utakapokaribia. Sasa tusaidiane wazazi na Waheshimiwa Wabunge, kuhakikisha kwamba watoto wetu wanapata elimu iliyo bora siyo bora elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wetu wa Dodoma, kuna upungufu mkubwa sana wa walimu na mimi nina tathmini hapa kidogo; katika shule za awali mahitaji katika Mkoa wa Dodoma tunahitaji walimu 1,761, lakini walimu waliopo ni walimu 444 tu na upungufu uliopo ni 1,227. Kwa hiyo, tunaona msingi wa watoto kukosa elimu, kwa sababu hatuna walimu wa kutosha. Kwa hiyo, watoto hawapati msingi mzuri tangu wanapoanza elimu ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu angalia katika Mkoa wa Dodoma, shule za msingi tuna mahitaji ya walimu 6,858, lakini walimu waliopo ni 5,913, upungufu walimu 2,745. Unategemea mtoto anapofeli darasa la nne asirudie wakati walimu wenyewe hawapo, aende hivyo hivyo na ujinga wake; siyo kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na upungufu wa walimu, Waheshimiwa Wabunge wamesema kwamba, watoto wengi wanakaa chini. Kwa hiyo, hakuna madawati na madawati hayatoshi. Walimu wengi hawana nyumba, wakitoka wanajiuliza watarudi au wenye nyumba wamekwishatoa *notice*? Walimu wana matatizo chungu nzima, posho zao hawalipwi kwa wakati, nauli za kwenda likizo hawalipwi na wanapoandika barua Wizarani hawajibowi. Walimu wana matatizo chungu nzima, lakini bado wanajitolea kufanya kazi kwa bidii. Naiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, pamoja na kwamba limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge, lakini na mimi napenda kurudia kwamba, Wizara iwakumbuke walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi mwalimu anapoandika barua Wizarani kuomba malipo yake ya kupandishwa daraja, Afisa kujibu barua ya mwalimu inachukua miezi mitatu kweli jamani? Kwa walimu inachukua miezi miwili mpaka mitatu, hawajibowi barua zao walizoandika Wizarani mpaka wafunge safari kwenda Dar es Salaam; watakwenda Dar es Salaam walimu wangapi? Walimu wanapokwenda Dar es Salaam kufuatilia malipo yao, Wizara haiwarudishii nauli zao wala wanapolala huko Dar es Salaam hakuna anayejua wanajua wao wenyewe. Jamani, hebu muwahurumie hao walimu, wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Tukumbuke huko vijijini wanakoishi hakuna umeme, hakuna maji wala hakuna nyumba, lakini bado wanaandika barua Wizarani na bado inachukua muda kujibiwa mpaka wafuatilie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iangalie namna ya kuwashudumia walimu kwa sababu ndiyo kazi ya Wizara. Kama si kazi yao, wangepewa kazi nyingine au watuambie kazi wanazozifanya ni zipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Serikali iangalie namna ya kuwamotisha wale walimu wanaofanya katika mazingira magumu. Kuna walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu na Wizara inajua, Waheshimiwa Wabunge wanajua na hata kwenye Halmashauri wanazotoka, zinajua kwamba kuna walimu wanaotembea hata kilomita 20 mpaka 30 kwa miguu hawajafika kwenye *main road* na bado hawajafuata mishahara yao. Naomba sana, kama inawezekana basi Serikali iangalie namna ya kuwamotisha hao walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilikuwa naomba Wizara iangalie namna ya kuwamotisha wale wanafunzi ambao wanapenda kusoma masomo ya sayansi na kuwa walimu. Hatuna walimu wa sayansi na kwa sababu hatuna walimu wa sayansi, hatuna namna ya kuwapata wanafunzi ambao watakuwa madaktari na *engineers* kesho. Hebu Serikali ione namna ya kuwashawishi wanafunzi ili waweze kusoma masomo ya sayansi waje wawasaidie wanafunzi wetu siku za mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie pia suala la Wizara kugharamia watoto 51,000 tu nchi nzima, wanaoishi katika familia duni na yatima. Yatima ni wengi mno katika Tanzania na wanaoishi katika familia duni pia wapo wengi. Watoto 51,000; angeniambia ni kwa Dodoma tu Mheshimiwa Waziri ningemwelewa, lakini Tanzania nzima; siyo kweli amebana sana matumizi. Naomba awasaidie hao watoto wanaoishi katika mazingira magumu na wale ambao ni yatima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee sasa kuhusu Baraza la Mitihani. Hakuna watu wanaoniudhi kama hawa wa Baraza la Mitihani; mtoto anapokwenda kufuata *results slip* au cheti chake, mimi mwezi wa tano nilifanya ziara nilimkuta mtoto aliyemaliza *form six* mwaka 2004 hajapata cheti chake anaambiwa akafuate Posta. Naomba Wizara ituambie huko Posta wana mtumishi wa Wizara ya Elimu, anayehakikisha kwamba vyeti hivi vinatoka kwa wakati, kwa nini wanawatesa watoto wa wakulima mpaka waende Posta kusubiria? Kama hawamwamini, kila mtoto anayefanya mtihani ana picha kwenye fomu; kwa nini asiaminike akishajaza fomu pale Baraza la Mitihani apate *results slip* yake au cheti mpaka asubiri Posta?

Mheshimiwa Waziri, atuambie kama huko Posta kamewekwa mtumishi wa Wizara yake anayehakikisha kwamba watoto wanapata *results slip* na vyeti vyao kwa wakati, basi huyo awajibishwe kwa sababu hafanyi kazi yake inavyotakiwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kusema kwamba, Wizara isi-create madeni; kila mwaka kuna madeni ya walimu ya likizo. Hawa wanaofanya kazi ya kushughulikia madeni ya walimu, hebu wajifikirie na wao pia kwa sababu unamtendea mwenzio hebu angalia na wewe ukitendewa utajisikiaje? Mkoaa wa Dodoma kwa Manispaa ya Dodoma tu kuna walimu 1450, lakini fedha zilizoletwa ni milioni 30 tu kwa ajili ya malipo ya likizo; haisaidii kitu tena ni madeni ya nyuma wala siyo ya mwezi wa saba, wala wa sita. Mimi naomba Wizara ya Elimu waangalie namna ya kushughulikia mahitaji ya walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

MHE. PROF. IDRIS ALI MTULIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kama mse maji wa mwisho katika hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake wawili, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kutuletea hotuba nzuri, yenye kutia matumaini. Kwa sababu hiyo, naiunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, moja kwa moja. (*Makof*)

Vilevile nilikuwa naomba nitoe sauti ya kuishukuru Wizara, kwa mwaka jana kuipatia gari Wilaya ya Rufiji kwa ajili ya ukaguzi. Ninaomba waendelee na moyo huo ili baadaye tupate zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ndiyo ufunguo wa maisha, ukiwa na elimu utakuwa na afya nzuri, ukiwa na elimu kilimo chako kitakuwa cha kisasa, utaendesha biashara vizuri, viwanda vizuri na utakuwa na hadhi katika jamii. Mimi ninavyoona ni lazima tuchukue mfano wa Mtume Suleiman, ambaye alipewa mambo matatu na Mwenyezi Mungu achague moja; akaambiwa Suleiman nakupa wewe mali nyingi, ninakupa ufalme, ninakupa elimu unachagua nini, Suleiman alichagua elimu na baada ya kupata elimu kubwa akawa mfalme na akawa tajiri sana. Kwa hiyo, elimu ni jambo kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani changamoto kubwa ya elimu inaweza ikagawiwa katika mafungu manne. Changamoto ya kwanza ni suala la ufinyu wa bajeti; ufinyu wa bajeti katika elimu imekuwa donda ndugu haliponi na kila mwaka kuna upungufu wa fedha zinazoingia katika elimu. Wahisani wengi sana wametusaidia tangu baada ya uhuru mpaka sasa, bado mahitaji yetu ni makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nadhani sasa tukubali tu kutumia Mpango wa *Sovereign Guarantee Process* ili tuweze kujenga miundombinu ya elimu kwa kui panga hiyo *Sovereign Guarantee Process*. Namna hiyo ndiyo tu tunaweza kutoka hapa tulipo tukaenda mbele, kuliko kungojea bajeti hii ambayo kila siku haikidhi haja. (*Makof*)

Suala la pili, ni changamoto ya uwangi wa wanafunzi katika nchi yetu. Tunao wanafunzi wengi sana. Sijui ndugu zangu Watanzania, hii nyota ya kijani hatuitazami vizuri na mpaka sasa wanafunzi ni wengi. Nia yetu ni kwamba, tuwe na wanafunzi wachache, tuwape elimu kubwa ili nchi iwe na watumishi bora. Changamoto nyingine ni upungufu mkubwa wa walimu bora. Kule Rufiji usiseme, lakini kila mahali hiki ndiyo kilio na nitalirudia jambo hili baadaye. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya nne ninayoiona mimi kwa nchi nzima ni uhalali wa ugawaji wa rasilimali na kutokuwa na ugawaji bora wa rasilimali. Yaani *inequity or lack of equity* na *equality in the distribution of financial resources for education*. Jambo hili ni jambo la kihistoria, nchi yetu baada ya kupata uhuru ilijiona kabisa ina matabaka makubwa ya sehemu ya nchi iliopata elimu kubwa, sehemu ya *community* iliopata elimu kubwa na wengine hawana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wenye umri wangu, watakumbuka kulikuwa na *Goan Schools, Aghakhan Schools, Indian Schools, East African Muslim Welfare Society Schools, Catholic Schools, Protestant Schools* na Shule za Serikali. Hii ilikuwa changamoto kubwa na tumshukuru Marehemu Baba wa Taifa, alipoona kwamba hakuna njia nyingine ya kuwasawazisha Watanzania kuwagawia rasilimali ya elimu sawa ni kutaifisha shule zote. Mwanaume yule akataifisha shule zote na watu wote akawaambia waingie shule hizo. Hiyo haikutosha, akafuta *school fees* yote kutoka *primary, secondary* hadi *University*. Kwa hiyo, pale sasa elimu ikapata nafasi kwa watu ambao hawakutoka katika nyumba zenye mali nyingi kupata elimu ya juu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile huu mpango wa kugawa kwa mfano *per capita* ya *dollar* 10 ukiwa na sehemu ya nchi ina shule nyingi sana na wanafunzi wengi kama ilivyo na ukiwa na sehemu ya nchi *marginalized*, kwa mfano, kule Rufiji kuna shule chache za sekondari. Kwa hiyo, wanafunzi wachache, unapogawa *per capita* kwamba kila mwanafunzi apate *dollar* 10, utakuta *dollar* hizi zote zitakwenda sehemu moja ya nchi yetu. Kwa hiyo, hapa utaona mgao huu ni halali, lakini hauna haki, kwa sababu wapo wengi wamekosa nafasi katika sehemu ile ya nchi yetu. Hali hii iliendelea mpaka kwenye miaka ya 70 na 80, Benki ya Dunia ikajitosa katika kusaidia elimu baada ya kutanabahi kwamba elimu italeta maendeleo haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliona nini? Waliona Dunia ya Tatu ina matatizo ya *inequity*, yaani watu hawapati mgao sawa wa rasilimali za elimu katika nchi zao. Wakatengeneza *computer program* inaitwa *GINI Coefficient*. *GINI coefficient* ukiitumia inakuonyesha waziwazi katika nchi yako rasilimali za elimu zimegawanywa vipi. *GINI Coefficient* ukiitumia inakuonyesha vilevile uongeze kiasi gani cha ziada kwa wale *marginalized groups* ili na wao waweze kunyanyuka na baada ya muda unaweza kabisa ukatumia *GINI Coefficient* kucheki kama umefanya vizuri kiasi gani kuondoa hizi *inequalities* na *inequities* katika ugawaji wa rasilimali ya elimu. Kwa maana hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri na Wizara yako, hebu tutumie *GNI Coefficient* tuone kiasi gani cha marekebisho kinaweza kufanyika katika ugawaji wa rasilimali ya elimu katika nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine lilikuwa suala la walimu wetu. Yameshazungumzwa na hakuna mtu anayepinga walimu wanapata kipato duni, wanaishi maisha magumu, wana tabu, inaonekana hatujalali vizuri, lakini nia yetu ni kwamba lazima tuwajali, lazima tuwapatie *promotions*, lazima tufanye mishahara yao iwe mizuri, lazima tuwape *housing*, hiyo inawezekana kama ukiwa na watumishi bora katika Wizara. Nadhani watumishi wa Wizara hiyo, wakiongozwa na ndugu yangu, Profesa Hamisi Dihenga, kutakuwa hakuna matatizo na naomba aendelee kuwa mtumishi bora, kuwanyanya walimu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la TEHAMA na *distant learning* kwa kutumia *television*. Hili jambo ni zuri lakini tatizo lake ni kwamba, iliyahi kutumika katika nchi ya *Ivory Coast* ikaonekana kabisa ina gharama kubwa sana. Kama ukiweza kununua *television* zikae katika kila sekondari, nchi hii utakuta *television* zaidi ya nusu zitakaa katika Mikoa miwili hivi, kwa sababu wale wenye shule nyingi ndiyo watapata

hizi *television* na kwa vyovoyote vile naikubali *program* hii, lakini iwe ni hatua ya mpito. Hatua ya kudumu tusomeshe vijana wetu, tupanue shule nyingi na tutumie njia tuliyokwishatumia huko nyuma; tulipokuwa hatuna watumishi wengi katika elimu tulitumia *peace corps recruitments* na tukafanya *recruitments aggressively abroad* tukapata wana sayansi wengi. Hawa watu wakisomeshwa watakuwa na msaada mkubwa kuendesha nchi hii kwa miaka zaidi ya 30. Hivi leo fedha utakayotumia kununua *television, television is a consumable* mara nyingi haiwezi kuishi zaidi ya miaka 10. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwafahamishe kuwa, kuna Wilaya *marginalised* inaitwa Rufiji. Namwomba Mheshimiwa Waziri, aitupie macho kwa sababu kule tunayo matatizo ya upungufu wa madarasa, madawati, vitabu, nyumba za walimu, hosteli na maabara. Itakuwa si jambo muafaka kufikiria Wilaya hizi ziweze kufanya mambo haya bila ya kusaidiwa. Ninaomba kwamba Wizara isaidie Wilaya ambazo ni *marginalized* na ni rahisi kabisa tumieni GINI *Coefficient*, mtajua kiasi gani cha rasilimali cha kuwasaidia na kwa muda gani ili waweze na wao kufikia katika hatua nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naisihi sana Serikali kwamba, ikubali tu Wanasyansi watazamwe kwa jicho la huruma. Wanafunzi wafutiwe ada tangu sekondari mpaka Vyuo Vikuu, mishahara iwe bora na kuwe na vivutio vingine. Mheshimiwa Waziri, mkono mtupu haulambwi sharti utie senti pale ndio watu watakaa kitako kusoma sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nataka kusema kwamba, Serikali yetu vilevile ikubali kufundisha *arts*; asilimia 40 ya *University Students* wanachukua fedha nyingi wanachukua wanafunzi wa *arts* na sayansi nimeona hapa ni asilimia 24 tu. Hii *trend* lazima ibadilike kwa sababu *arts* haijengi, inapanua mawazo tu lakini ukitaka kujenga nchi lazima uwe na sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, ninaomba sana Serikali ikubali kuonea huruma Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı ili mwaka ujao, bajeti yao izidishwe ili tuweze kupata shule nyingi na tuweze kupata wataalam wengi. Baada ya kusema haya, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Mtulia. Sasa naomba nimwite mchangiaji wetu wa mwisho, naye atakuwa Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa.

MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nizungumze machache kwa muda uliobakia. Mwaka jana katika kutaka ufanuzi kuhusu ujenzi wa Taasisi ya Sayansi ya Viumbe Baharini Chuo Kikuu Dar es Salaam, kwa kule Zanzibar Mheshimiwa Waziri aliye kuwa wa Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia alisema kwamba, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilikuwa na mazungumzo na CRDB ili kupata fedha kwa ajili ya

kukamilisha ujenzi ule. Baada ya kulifuatilia jambo hilo, limeonekana kwamba, *CRDB* walikubali lakini Serikali ilikataa kudhamini, kwa maana hiyo fedha hazikupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi ule unagharimu zaidi ya shilingi bilioni sita na ulianza Machi, 2006 na kwa mujibu wa mkataba ulikuwa umalizike Mei, 2008. Hali ya *material* ya ujenzi imepanda mara mbili zaidi na niliambiwa kuna kifungu ambacho walikubaliana kwamba, wavumiliane ambavyo sikuridhika navyo kwa sababu sidhani kama *International Contractor* atakupa wewe nafuu ya kustahimili mpaka upate fedha ndio yeche aendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, ujenzi ule nina wasiwasi nao; mwaka huu tumetengewa shilingi bilioni mbili kwa chuo hicho kumalizia ujenzi huo, lakini kama *uta-review* gharama hizo zitakuwa karibu bilioni nane mpaka kumi. Sasa nataka kumwuliza Mheshimiwa Waziri, hizo fedha za kumalizia ujenzi wa Taasisi hizo zitapatikana na kama hazipatikani kuna mikakati gani ya kuweza kuzipata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumze kuhusu swalii la *Tanzania Commission for Universities (TCU)*. Kama alivyozungumza Mheshimiwa Dr. Mahenge ni kweli kwamba, *TCU* pamoja na *NACTE* zote zina majukumu ya kusimamia kazi za elimu, lakini pia tumezipitisha katika Bunge japokuwa sisi hatukuwepo. Kuna malalamiko upande mwingine ya ushirikishwaji kwamba, *NACTE* wanalamika hasa kwa vile Vyuo vya Elimu ambavyo siyo Vyuo Vikuu wanasema hawajashirikishwa katika *proposal* hiyo. Kwa upande mwingine, Wizara ya Elimu kwa upande wa Zanzibar nao hawajashirikishwa. Utaratibu uliopo ni mzuri, mimi nauafiki kutokana na matatizo ya kuchagua wanafunzi watakaopata mikopo ya Bodi, lakini ushirikishwaji haukuwa umefikiwa. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, alisimamie jambo hilo ili wadau wote washirikishwe.

Ukiangalia katika *proposal*, moja nililoliona ni kwamba, wanafunzi wanapokuwa wanamaliza Kidato cha Sita kabla hawajakaa kwenye mitihani yao inabidi wajaze fomu kwa ajili ya *option* wanataka nini kabla ya matokeo, lakini juu ya hapo walipe na mchango kama wa shilingi 20,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi 20,000 unazotoa lakini hujui matokeo yatakuwaje, zitarejeshwa au hazirejeshwi? Nafikiri utaratibu huo ni mzuri lakini Tume iangalie upya kwamba, shilingi 20,000 zile watakotoa basi watakaofaulu wataendelea lakini ambao watakuwa hawaja-*qualify* warejeshewe zile fedha au njia nyinginezo. Vinginevyo, tutakuwa tunawaonea Watanzania ambao uwezo wao ni mdogo, tutakuwa tunawaibia. Najua wana programu ambayo wanataka *ku-centralise data base* kwa ajili ya wanafunzi, lakini sidhani kama Baraza la Mitihani limesha-*centralise data base* za wanafunzi wote.

Sasa inakuwaje tena Tume iwe na *data base* zake tofauti badala ya kushirikiana tu na *National Examination Council* ili kupunguza gharama hizo? Mimi naomba sana Mheshimiwa Waziri, alisimamie hilo; wadau washirikishwe na waangalie upande wa mchango wa wanafunzi shilingi 20,000 ni nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie kuhusu matatizo katika Vyuo Vikuu vyetu. Tangu mwaka jana, tulikuwa tukisikia wanafunzi wetu wakilalamika na wengine wakiandamana kwenye Vyuo Vikuu kama Dar es Salaam kwa kuzuiwa matokeo yao kwa sababu ya kutolipa ada. Pato la Mtanzania kama tulivyoona safari hii ni shilingi laki tano; *is it laki tano?* Laki tano kwa mwaka si kweli, hiyo ni nadharia tu lakini ukienda hasa kwa Mtanzania mmoja mmoja sidhani kama anaweza kufikia hata shilingi laki mbili kwa mwaka na watoto walio wengi ni maskini na ndio wanaosoma kwenye vyuo vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mwanafunzi ambaye unamzuia matokeo yake na wengine wameshapewa barua; unamwambia bwana usipolipa hurudi, kama utarudi utafanya *semester* utamaliza lakini mwaka wa pili usije. Sisi tunasema tunawahitaji Watalaam wa Sayansi, tena wanafunzi hao ni katika Vyuo Vikuu vya Ardhi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na vingine ambavyo sina taarifa zaidi lakini wanachukua sayansi. Sisi tunasema tunawa-*encourage* vijana wetu katika masomo ya sayansi, sasa unapofika kule unaanza kuwa-*harass*; tutapata kweli wanasayansi hao? Watapata wapi fedha hizo?

Mtu anadaiwa laki mbili mpaka milioni, mtoto wa mkulima! Sasa kwa nini Serikali isiwashubiri kwanza wakamaliza, kwa sababu ni mkopo wakishamaliza digrii zao wataajiriwa; ukimzuia mwaka wa pili au wa tatu usimpe *result* atapata wapi kazi, hapati ajira. Wapewe wamalize wakiajiriwa watalipa. Kuna Wabunge humu tulikopa tunakatwa. Wakishaajiriwa Serikali itapata fedha zake, lakini tutakuwa tumemsaidia kijana yule Mtanzania, mtoto wa maskini na yeye kujikwamua. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, aliangalie hilo na apitie kwenye vyuo awasikilize wanafunzi wana malalamiko mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni *allowances* wanazopata (*meal allowance*). Ukiangalia mwaka 2005/2006 ni shilingi 2,500, mwaka 2006/2007 shilingi 3,500, mwaka 2007/2008 shilingi 5,000, mwaka huu sijui. Ukichukua kipengele tu hicho cha *meal allowance* na *accommodation* shilingi 5,000; Mheshimiwa Mbunge wewe upewe shilingi 5,000 utaishi kweli jamani? Mafuta yamepanda, vyakula vimepanda kila kitu kimepanda, hicho ni kipengele kidogo sana nimekizungumzia, lakini kuna *field*, mambo ya *project write-up* kule ndio kiama, mtu unampa shilingi 195,000 kukamilisha *project* yake, *project* inagharimu shilingi 400,000, 500,000 mpaka 900,000; inategemea *material* yake na kitu gani ame-*propose*!

Kweli tunawaandaa wanafunzi au tunawatesa tu jamani? Matokeo yake ndio tunasema elimu Tanzania imeshuka, isishuke vipi kwa sababu hatuwawezeshi. Sasa mimi ninetaka kupendekeza kwamba, jamani pamoja na hilo, kama tumeamua elimu yetu iwe nzuri, bora basi Serikali isikwepe gharama. Mwanafunzi akila ndio akili zitachaji, lakini usipokula vizuri kweli wewe Mwanasayansi unaweza kubuni kitu kikawa kizuri? Namwomba Mheshimiwa Waziri, a-review hizi *allowances* zote wanazopewa wanafunzi wetu kwa sababu hazitoshelezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niende kwenye *item* nyingine kuhusiana na hizo posho wanazopewa. Sehemu ya *research* kama nilivyozungumza, wana pewa shilingi 195,000 lakini kulingana na *breakdown* zao za haraka haraka na kutegemeana na *project* anayotaka mwenyewe, basi utakuta ya chini kabisa ni shilingi 360,000 na ya juu 800,000. *This is engineering* na *engineering* maana yake mambo ya sayansi yanataka utafiti wa kina, huwezi ukamaliza wewe ukaitwa Mwanasayansi wakati hata *project write-up* hujaikamilisha. Hatutaweza kupata wataalam wazuri katika kipindi ambacho sisi tunajidai kuingia kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, ikiwa vijana wetu hatuwa-*support* hivi sasa.

Kwa hiyo, Serikali isione gharama kubwa na Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi ni Profesa, amesoma kwenye Vyuo hivyo anajua, kwa hiyo, jamani shida ulizozipata ndizo hizo hizo na wenzako wanazipata, wasaidie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nikizungumza sana naweza nikalia sana, kwa sababu inasikitisha na sisi tumepita humo humo. Inasikitisha sana, vijana wetu wanapoandamana tusitumie nguvu za Polisi na kuwapiga na nini; tuwasikilize wana matatizo gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Masolwa. Waheshimiwa Wabunge, huyo alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho, lakini napenda niwatangaze wachangiaji watano wa kesho asubuhi. Kwanza kabisa, atakuwa Mheshimiwa Meryce Mussa Emmanuel, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa na baadaye atafuatia Mheshimiwa Dr. Luka Jelas Siyame.

Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo napenda kuahirisha kikao cha leo mpaka kesho Jumanne, tarehe 15 Julai, 2008 saa tatu asubuhi.

(*Saa 01.45 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,
Tarehe 15 Julai, 2008 Saa Tatu Asubuhi*)